

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 16 Aprili, 2019**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. ATHUMAN B. HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA (MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu

wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA (MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA - MHE. ALLY SALEH ALLY):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. ATHUMAN B. HUSSEIN – KATIBU MEZANI:** Maswali.

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tutaanza na Ofisi, ya Waziri Mkuu swali la Mheshimiwa Paschal Yohana Haonga.

Na. 88

**Madai ya Wastaafu Waliokuwa Wanachama wa PSPF**

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA** aliuliza:-

Kuna watumishi katika Halmashauri nyingi za Wilaya nchini walikuwa wanachama wa *PSPF* wamestaafu zaidi ya

mwaka mmoja na hawajalipwa fedha zao za kiunua mgongo (*pension*) na kwa sasa wanaishi maisha ya taabu na mateso makali:-

(a) Je, ni lini sasa Serikali itawalipa wastaafu hawa?

(b) Inasemekana kwamba Serikali imetumia vibaya fedha za *PSPF* ikiwa ni pamoja na kukopesha baadhi ya watu na taasisi: Je, Serikali haioni kwamba hii inaweza kuwa sababu mojawapo ya kucheleweshwa mafao kwa wastaafu?

(c) Fedha za kiunua mgongo ni mali ya Mtumishi anayestaafu: Je, kwa nini Mifuko ya Pensheni isiwakopeshe wastaafu watarajiwa angalau 40% ya fedha hizo bila riba pale inapobaki miaka 10 kabla ya kustaafu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kufikia tarehe 28 Februari, 2019 Mfuko mpya wa *PSSF* ulikuwa umekamilisha kulipa malimbikizo ya deni la wastaafu liliorithiwa kutoka Mfuko wa *PSPF* ambapo jumla ya wastaafu 9,971 wamelipwa stahiki zao zilizofikia kiasi cha shilingi bilioni 888.39. Aidha, Mfuko umekamilisha mfumo wa ulipaji mafao utakaowezesha kufanya malipo katika ngazi ya mkoa na hivyo kuwezesha mfuko kulipa mafao ndani ya muda uliowekwa kisheria wa siku 60 tangu mwanachama anapowasilisha madai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge iliyoanzisha mfuko husika. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine inasimamia muundo wa utawala na mfumo wa maamuzi na usimamizi wa uwekaji wa fedha za mifuko. Aidha, sheria

inaipa Bodi ya Wadhamini ya mfuko jukumu la kusimamia uwekezaji wa fedha za mfuko kwa uhuru. Hivyo basi, siyo kweli kwamba Serikali inaweza kuingilia uendeshaji wa mifuko au kufanya maamuzi ya uwekezaji ikiwemo kukopesha taasisi au watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, imekuwa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanachama wake kupitia vikundi vya kuweka na kukopa (SACCOS) katika maeneo ya kazi. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2015, Mifuko inaweza kutoa mikopo kwa SACCOS hadi asilimia 10 ya rasilimali za mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii zinaruhusu wanachama kutumia sehemu ya mafao yao kama dhamana kwa ajili ya kujipatia mkopo wa nyumba kutoka katika mabenki na taasisi za fedha nchini ili kuwawezesha kuboresha makazi wakati wa kipindi cha utumishi wao.

Aidha, Kanuni Na. 24 na 25 ya kanuni mpya za Mafao ya Hifadhi ya Jamii za mwaka 2018 zimetoa wigo mpana zaidi kwa wanachama waliochangia kwa miaka isiyopungua 10 kuweza kupata huduma hii tofauti na hapo awali ambapo ni wanachama waliokuwa wametimiza umri kuanzia miaka 55 ndio waliweza kupatiwa mikopo ya kujenga vyumba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa mtumishi anapokuwa anaajiriwa, mara ya kwanza na kwenye *salary slip* yake inaonesha muda atakaostaafu, hivyo inakuwa siyo suala ambalo ni la ghafla, lakini Serikali imekuwa ikichelewa sana kuwalipa watumishi hawa: Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka inapokuwa wamesababisha ucheleweshwaji wa mafao kwa watumishi wa Umma inataikiwa walipe kwa riba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Halmashauri ya Mbozi kuna watumishi 35 wamestaafu toka Septemba, 2018, hadi sasa hawajalipwa fedha zao na wanaidai Serikali na wanaishi maisha magumu sana: Je, ni lini sasa Serikali itaacha kuwatesa watumishi hawa wanaoishi maisha ya taabu sana kwa sababu ya ucheleweshaji wa fedha zao? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza Mheshimiwa Haonga amezungumza kuhusu ucheleweshwaji wa ulipaji wa mafao. Kwa mujibu wa sheria ambayo tumeipitisha hapa ndani Bungeni hivi sasa, inautaka mfuko kulipa mafao ya mstaafu ndani ya siku 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zilikuwepo changamoto nyingi hapo awali, nyingi sio kwambwa zinasababishwa na mfuko husika lakini pia wale wastaafu katika namna moja ama nyingine katika uandaaji wa nyaraka na kufuatilia taarifa zao imekuwa pia ikileta changamoto. Baada ya kuunganisha mifuko hii na kwa kutumia sheria mpya, hivi sasa *PSSF* wameweka utaratibu na *motto* wao ni kwamba wanalipa mafao tangu jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa zoezi la ulipaji wa mafao kwa wastaafu linafanyika kwa kiwango kikubwa sana na kwa idadi ambayo nimesema tayari imeshalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu watumishi katika Jimbo lake la Mbozi, kwa sababu hii inakwenda *case by case*, nisiliseme kwa ujumla, lakini nichukue tu fursa hii kumwambia Mheshimiwa Haonga kwamba ofisi yetu iko wazi, kama kuna madai ya watumishi ambao mpaka hivi sasa bado hawajalipwa mafao yao, basi anaweza kuyasilisha ili sisi Ofisi ya Waziri Mkuu tuweze kufuatilia mkoa husika tujue

changamoto ni nini na baada ya hapo tuweze kutatua changamoto yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kulipa mafao yao kwa wakati kabisa ili kuwafanya watumishi hawa waishi katika maisha ya amani.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

Na. 89

### **Hitaji la Masoko la Segerea**

**MHE. BONNAH M. KALUWA** aliuliza:-

Wananchi wa Kata za Kinyerezi, Bonyokwa, Segerea Liwiti, Kipawa, Kimanga, Kisukulu na Tabata wamekuwa wakitumia fedha na muda mwingi kwenda kutafuta bidhaa na huduma katika masoko ya Buguruni na Kariakoo kutokana na kukosa huduma hizo katika maeneo yao:-

(a) Je, kwa nini Serikali isijenge soko kubwa katika eneo mbadala lililo katikati na linaloweza kufikiwa na wananchi hao kwa wakati?

(b) Je, kwa nini Soko la Kinyerezi lililozinduliwa na Mwenge mwaka 2017 lisifunguliwe ili kutoa huduma kwa wananchi wanaozunguka soko hilo na maeneo ya karibu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Kamoli, Mbunge wa Segerea, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala iliweka kipaumbele cha kutekeleza mradi wa kimkakati wa ujenzi wa Soko la Kisutu utakaogharimu takribani shilingi bilioni 12.17. Mpaka sasa mradi huo umepatiwa jumla ya shilingi bilioni 3.92 na ujenzi unaendelea. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujenga masoko mengine ndani ya Manispaa ya Ilala. Halmashauri inashauriwa kutumia fursa ya miradi ya kimkakati na kuandaa andiko la mradi wa kujenga masoko katika Kata ya Kinyerezi, Bonyokwa, Segerea, Liwiti Kipawa, Kimanga, Kisukulu na Tabata ili kupata fedha za utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Kinyerezi lililoinduliwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 limepangwa kuanza kutumika Mei, 2019 baada ya matengenezo ya choo ambacho kilikuwa hakijakamilika kwa wakati huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kamoli.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ambayo ameyajibu Mheshimiwa Naibu Waziri; kwa kuwa Serikali imeanzisha miradi ya kimkakati katika mikoa mingine na ukizingatia katika Jimbo la Segerea kuna wananchi wengi sana ambao wanakaribia 1,300,000; je, Serikali ina mpango gani kujenga masoko ambayo yatakuwa yanawasaidia wananchi ili wasiweze kwenda mbali kama hivyo alivyosema Kisutu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, nimemsikia Mheshimiwa Waziri anaongelea kuhusiana na Soko la Kinyerezi. Kutokana na kwamba nilifanya ziara mwezi uliopita, hilo soko mpaka sasa hivi kwanza linavuja, halafu pia halijamaliziwa vizuri. Kwa hiyo, haliwezi kuzinduliwa mwaka 2019 kama anavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna Kata nyingi ambazo hazina masoko kama Kata ya Kisukulu, Kata ya Kipawa na Kata nyingine: Je, Serikali ina mpango gani

kuhusiana na hizo Kata nyingine kuhakikisha kwamba zinapata masoko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Soko la Kisutu mwongeze hela.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuelewa, nakushukuru. Swali la kwanza ningeomba niseme tu kwamba utaratibu unaotumika kuibua miradi ya kimkakati ni Halmashauri husika, inakaa na wataalam wake, wanaandika andiko, wanaliwasilisha Ofisi ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha; wataalam wa Wizara ya Fedha wanaenda kufanya tathimini ya andiko lenyewe, gharama zake na mrejesho kwa maana ya faida itakayopatikana na baada ya hapo wataruhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ya kuwa na masoko ya Kinyerezi na maeneo mengine, itategemea Halmashauri ya Manispaa ya Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nilitaka tu niseme kwamba inawezekana ni kweli Mheshimiwa Mbunge anasema, sasa nimwelekeze Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala aende akafanye utaratibu wa kukarabati na kurekebisha soko hilo ili liendane na ambavyo nimejibu katika swali langu la msingi, kwamba Kinyerezi ilizinduliwa mwaka 2017 na Mbio za Mwenge wa Uhuru lakini Mei mwaka huu linatakiwa lianze kufanya kazi. Mkurugenzi aweke pesa pale ili liweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoizungumza Mheshimiwa Mbunge hapa, soko la Kisutu ni kweli lipo kwenye mkakati, limesharuhusiwa na Serikali na fedha imeshatolewa. Naomba nimhakikishie, kwa kadri anavyojua kwamba lazima lisimamiwe; na Mheshimiwa Mbunge nimridhishe kwamba yeye katika Manispaa ya Ilala ana ujenzi wa machinjio ya kisasa kabisa ya Vingunguti ambayo ipo pia kwenye mpango mkakati katika eneo hilo. Ahsante.



**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mji wa Karatu ni Mji wa Kitalii na hauna soko la uhakika. Hivi sasa wananchi wa Karatu kwa kutumia mapato yao ya ndani wameanza kujenga soko lenye hadhi ya Mji huo: Je, Serikali iko tayari sasa kuunga mkono jitihada za wananchi hao ili soko hilo likamilike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana. Mheshimiwa Mlinga na Mheshimiwa Catherine wajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Mkoa wa Manyara tayari tuna mradi wa kimkakati katika Wilaya ya Hanang'. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, fedha zipo, Serikali ipo tayari kutoa ushirikiano. Cha muhimu, Halmashauri husika ikae na kutoa andiko, likija hapa kwenye tathmini hili jambo litafanyika. Sisi tunakusudia kuweka masoko, stendi na majengo mbalimbali ya kimkakati ili baada ya kuwekeza katika maeneo hayo, Halmashauri zetu zipate mapato ya kutosha ili kuweze kuendeleza na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pesa zipo, andikeni maandiko. Pelekeni maandiko TAMISEMI, mtajengewa miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Mlinga halafu Mheshimiwa Catherine.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kata yangu ya Mahenge Mjini ambapo ndiyo Mji wenyewe ulipo, kuna shida kubwa ya soko. Wananchi walijitolea wakajenga soko, Serikali ikatia hela zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 Mwenge ulikuja ukafungua hilo soko, lakini mpaka leo hii soko hilo halijaanza kutumika. Kwa hiyo, Mwenge umedanganywa, Mbunge kadangaywa, wananchi wamedanganywa. Je, lini Serikali itasimamia ufunguaji wa soko hilo ili wananchi wapate kulitumia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, anataka kujua ni lini soko litafunguliwa? Mwenge haujapita kwako?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhsukuru. Hili jambo tumelipokea, tutalifanyia kazi tuone tatizo liko sehemu gani ili liweze kufanya kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa imekuwa ni ahadi ya muda mrefu ya Serikali kujenga Soko la Mto wa Mbu Wilayani Monduli Mkoani Arusha, lakini mpaka sasa hakuna chochote kinachoendelea na wananchi wa Mto wa Mbu wamekuwa wakipata taabu: Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Soko la Mto wa Mbu Mkoani Arusha? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli hili suala hata Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Monduli, Mheshimiwa Julius Kalanga ameniuliza jana. Kama nilivyosema, namwomba Mheshimiwa Mbunge wakae na Halmashauri yao, fedha zipo kama ulivyosema. Ni kuandika andiko na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tupo tayari kusaidia utaalaam na namna ya kuboresha pamoja na Hazina ili andiko likamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuna wapiga kura wengi sana pale Mto wa Mbu, tungependa wapate soko zuri, wapate kipato, pia wachangie kodi katika maendeleo

ya Watanzania wenzetu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane hili jambo liweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mbunge wa Fuoni, kwa niaba yake Mheshimiwa Khadija.

Na. 90

### Changamoto za Muungano

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD (K.n.y. MHE. ABBAS A. H. MWINYI)** aliuliza:-

Changamoto za Muungano wetu bado zipo licha ya vikao vya Kamati za pamoja kati ya SMT na SMZ kukutana mara kwa mara:-

(a) Je, ni changamoto zipi zilizopata ufumbuzi tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani?

(b) Je, changamoto hizo ni ngapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2015 mpaka 2019 Serikali ya Awamu ya Tano iliyoingia madarakani, changamoto mbili zimepatiwa ufumbuzi. Hoja zilizopatiwa ufumbuzi katika kipindi cha Serikali Awamu ya Tano ni utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na kutoa VAT kwa asilimia sifuri kwa umeme unaouzwa na

TENESCO kwa ZECO ikiwa ni pamoja na kufuta deni la kodi ya VAT lililofikia shilingi bilioni 22.9 kwa umeme uliouzwa kwa ZECO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizo, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuitisha vikao vya kisekta, kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizobakia na zinazoendelea kujitokeza. Sekta hizo ni Sekta ya Fedha, Uchukuzi, Biashara, Mifugo, Uvuvi na Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizojadiliwa ni pamoja na Taarifa ya Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha, hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa mapato yanayotokana na faida ya Benki Kuu, usajili wa vyombo vya moto, upatikanaji wa fursa za masoko Tanzania Bara, ushirikiano kati ya Taasisi ya Viwango na Zanzibar (ZBS) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Zanzibar (ZFDA), ZBS kupatiwa nakala ya usaili kiwango cha Afrika Mashariki ili kurahisisha usaili wa kiwango hicho kwa wakati; Leseni za viwanda, Zanzibar kuwa *designated member country* wa mashirika ya *African Regional Intellectual Property Organization (ARIPO)* na *World Intellectual Property Organisation (WIPO)* na upatikanaji wa fursa za miradi inayohusisha maendeleo ya viwango na ubora wa bidhaa kwa maendeleo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo miradi inayohusu maendeleo ya wajasiriamali na kuzuiwa kwa bidhaa ya maji ya kunywa inayozalishwa Zanzibar kuingia Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali zote mbili za SMZ na SMT zimeendelea kuhakikisha kuwa makubaliano yaliyofikiwa na pande mbili yanatekelezwa na kuhakikisha kuwa changamoto zinazojitokeza zinashughulikiwa ipasavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Aboud.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na hayo napenda kuchukua

nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kutatua baadhi ya changamoto muhimu ambazo zilikuwa zinazikumba Serikali zetu hizi mbili, ikiwemo ya kuondosha VAT kwenye suala la umeme, naipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina swali la nyongeza, isipokuwa naendelea kuishauri Serikali kila inapooa inafaa kwa wakati muafaka kuendelea kutatua changamoto hizi za Muungano. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hamna swali la nyongeza. Ahsante kwa ushauri mzuri, Serikali imepokea.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Mbarouk Salum Ali, swali namba 91.

Na. 91

### **Elimu Juu ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD (K.n.y. MHE. MBAROUK SALUM ALI)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa Watanzania hususan kizazi kipya, kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ili kutoa uelewa wa pamoja na dhamira njema za Muungano huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Salum Ali, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba, karibu asilimia 80 ya kizazi cha sasa kimezaliwa baada ya

Muungano na hivyo kuna haja ya kutoa elimu ya Muungano kwa wananchi wote, hususan vijana wa Kitanzania. Elimu hii ni muhimu kwa mustakabali wa Muungano kwani inaongeza ari ya uraia, uzalendo na kujenga undugu wa Kitaifa kati ya wananchi wa pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2018/2019, ofisi imetoa elimu ya Muungano kupitia vipindi vya redio na *television*, ili kuhakikisha makundi mbalimbali yanapata elimu ya Muungano, hususan vijana. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, shughuli za elimu ya Muungano, hususan kwa vijana, zilitolewa kupitia kongamanko la vijana, hususan fursa zilizopo katika Muungano ambapo ilifanyika Zanzibar tarehe 22 Oktoba, 2017. Wanafunzi wa shule za msingi zilizopo Dodoma ilifanyika tarehe 18 Aprili, 2018 na Kongamano la Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyopo Dodoma, itafanyika tarehe 21 Aprili, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ofisi ilishiriki katika maonesho ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani iliyofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja kuanzia tarehe 31 hadi tarehe 6 Juni, 2018, ambapo wananchi walipata fursa za kujulishwa kuhusu masuala ya Muungano. Pamoja na kazi hizo, ofisi ilishiriki katika vipindi vya redio, *television* na magazeti katika kutoa elimu ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua faida zitakazopatikana kwa kutoa elimu ya Muungano, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, itaendelea kutoa vipaumbele katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na imetenga fedha kwa ajili ya kutoa elimu ya Muungano kwa vijana kupitia makongamano na warsha, ambayo yamelenga wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu Tanzania Bara na Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara kadhaa maafisa mbalimbali ambao wanatumia magari ambayo yamekuwa na namba za Zanzibar

wamekuwa wakikumbana na vikwazo vya *TRA* pamoja na Polisi kwamba, namba hizo ni namba za kigeni wakati anapotembea Tanzania Bara. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, yupo tayari sasa kutenga muda mahususi kuwapa taaluma Polisi pamoja na *TRA* kuona kwamba, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuambatana na sisi au na mimi kwenda kuangalia namna Maafisa wa *TRA* wanavyofanya kazi pale bandarini kwamba, unapokuja tu na kilo tano za sukari kutoka Zanzibar au *Tvya* nchi 21 unatakiwa ulipe kodi? Je, hili yupo tayari kwenda kulishuhudia Bandari ya Zanzibar ili kutoa mwongozo na taaluma kwa ajili ya shughuli hizo za kibiashara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbarouk, kwa niaba yake Mheshimiwa Juma ameuliza vizuri sana:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza niko tayari kwa yote mawili, lakini kwa ufafanuzi zaidi hili la vyombo vya moto kwa sababu, bado lipo tayari kwenye majadiliano na vikao vinaendelea, nadhani baada ya hivyo vikao sasa nitakuwa tayari kwa ajili ya kutoa hiyo elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, niko tayari kuambatana na wewe na Wabunge wengine ambao wanatoka Zanzibar kwenda kushiriki kwa pamoja kuhakikisha kwamba, eneo hili tunalifanyia ufumbuzi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuuliza swali dogo la

nyongeza. Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais watumishi wengi wanakaimu.

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha watumishi hawa sasa, wale wanaokaimu wanapandishwa madaraja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru. Nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali ina dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha maeneo yote ambayo watumishi wanakaimu waweze kufanya kazi yao kwa ukamilifu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari ofisi yetu imeshafanya utaratibu wa kuomba kibali kwa ajili ya kuhakikisha watumishi wote wale au maeneo yote, *position* zote ambazo zinakaimiwa ziweze kupata watalaam ambao wako kamili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri, Utawala Bora.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ili nami niweze kufafanua swali la Mheshimiwa Mbunge, Maryam Msabaha. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba nifafanue kidogo juu ya suala zima la kuhusu watumishi kukaimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli watumishi wamekuwa wakikaimu kwa muda mrefu sana na nimekuwa nikilizungumza hili kwamba, hii ni kutokana na watumishi wengi wamekuwa wakikaimishwa na waajiri wao kienyeji na nafasi za kukaimu ni kukaimu tu sio kwamba, ni nafasi ya kuthibitishwa au ni kwamba, umeshapewa ile kazi.



Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi nafasi za kukaimu ziko katika uwezo wa madaraka kwa maana ya *superlative substantive post*. Kwa maana hiyo, sisi kama Serikali, tumetoa waraka kwamba, kukaimu mwisho miezi sita. Kwa maana hiyo waajiri wote nchini wanapaswa kuomba kibali na kama unataka mtumishi aendelee kukaimu basi tuandikie tena barua. Kukaimu lazima iwe kulingana na *level* ya ile nafasi ambayo unastahili kukaimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi.

Na. 92

### **Serikali Kuwekeza kwenye Vyuo vya Ufundi**

**MHE. JANETH M. MASABURI** aliuliza:-

Nchi za China na Singapore zinefanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa Vyuo vya Ufundi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga bajeti ya kutosha ili kuwekeza kwenye Vyuo vya Ufundi ambavyo vitasaidia vijana wengi kupata ujuzi na kujajiri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa nchi kuwekeza katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kufikia azma ya uchumi wa kati unaotegemea

viwanda ifikapo mwaka 2025. Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa mitano katika Mikoa ya Geita, Rukwa, Njombe, Simiyu na Kagera, pamoja na vyuo vya ufundi stadi vya wilaya 13. Aidha, kupitia mradi wa *Education Skills for Productive Jobs (ESPJ)* vyuo vyote 54 vya Maendeleo ya Wananchi vinakarabatiwa ambapo awamu ya kwanza vyuo 20 vitakarabatiwa na ukarabati upo katika hatua za umaliziaji. Vilevile kupitia mradi huu Chuo cha Ufundi wa Kati (*Technical College*) kitajengwa katika Mkoa wa Dodoma kuanzia Mwaka wa Fedha 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kupitia mradi wa *East African Skills for Transformation and Regional Intergration Project* Serikali inatarajia kuzijengea uwezo taasisi za Chuo Cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia Dar-es-Salaam (*DIT*) tawi la Dar-es-Salaam na Mwanza, pamoja na Chuo Cha Taifa Cha Usafirishaji (*NIT*), ili kuwa vivutio vya umahiri katika sekta za nishati, teknolojia ya habari na mawasiliano, usafirishaji na uchakataji wa mazao ya ngozi. Serikali itaendelea kuwekeza katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kadri uchumi utakavyoruhusu, ili kuongeza fursa na ubora wa elimu na mafunzo hayo nchini kwa lengo la kuleta tija zaidi na manufaa kwa Taifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masaburi.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Natambua Serikali imefanya vizuri sana katika sekta hii ya elimu, lakini nina maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa, hivi sasa kwa wastani kwa wahitimu wa vyuo vikuu ni kati ya 10 kwa mmoja kwa wahitimu wanaohitimu vyuo vya ufundi, yaani wasimamizi 10 kwa mtendaji kazi mmoja badala ya msimamizi mmoja kwa watendaji kazi 10. Je, Serikali inasema nini juu ya hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika umuhimu huo wa vyuo vya ufundi ambako ndiko kunakozalisha kundi kubwa la watenda kazi ambalo kundi hili ndilo linajijari lenyewe. Je, Serikali inasema nini juu ya kuweka uwekezaji mkubwa katika vyuo vya ufundi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Janeth Masaburi kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukweli kwamba, kwa sasa hakuna uwiano mzuri kati ya watendaji au wafanyakazi katika sekta ya ufundi katika ile maana ya kwamba, wale watendaji wa kada ya kati pamoja na kada ya chini na wale wa ngazi za juu. Serikali ndio maana imechukua maamuzi ya kuongeza udahili katika vyuo vyetu ili tuendelee kuwapata wataalam wengi ambao baadae watatusaidia kujaza ombwe hili na hivyo kurekebisha hali hiyo, ili tuwe na uwiano mzuri katika wafanyakazi wetu katika sekta ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili kwamba, Serikali inafanya nini kuwekeza katika vyuo vya ufundi. Kama nilivyosema kwenye jibu langu katika swali la msingi, Serikali inachukua hatua kadhaa za makusudi kuhakikisha kwamba, tunaongeza, sio tunaongeza vyuo vingi, lakini vilevile tunaongeza udahili pamoja na ubora wa vyuo hivyo ambavyo vinatoa fani mbalimbali za ufundi. Ndio maana tunapozungumza sasa tunajenga vyuo 13 vya wilaya, lakini tutajenga vyuo vitano vya mikoa, ambavyo vile vya mikoa vyenyewe vinagharimu shilingi bilioni 118, lakini pia hatujaishia hapo, tunakarabati Vyuo vyote 54 vya Wananchi vile tunaviita *FDCs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuweza kuwa na vyuo vingi vyenye ubora mzuri, ili tuongeze udahili, ili tuendelee kuwapata mafundi wengi kwa sababu, watatusaidia katika azma yetu ya kujenga uchumi wa viwanda, lakini vilevile kuongeza fursa za ajira. Kwa sababu, kama mnavyofahamu ni rahisi vijana wengi kujiajiri wakisoma ufundi; lakini pia, tunaendelea kujenga vyuo vya ufundi wa kati na ndio maana tumewekeza katika kujenga chuo kikubwa Dodoma, chuo ambacho kina hadhi kama ilivyo *DIT* na *Arusha Technical College*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dau, Mheshimiwa Shekilindi ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Wananchi wa Mafia kwa kushirikiana na Mbunge wao wamejenga chuo cha kisasa kabisa cha *VETA* na kukamilisha taratibu zote, lakini mpaka leo Wizara hajitoe usajili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri sasa atakuwa tayari kutoa usajili kwa ajili ya *VETA* ya Mafia?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dau amekuwa akifuatilia sana suala la *VETA* ya Mafia. Kwa kweli, kuna wakati hata mimi na yeye kidogo tulitofautiana kwa sababu, aliona kwamba, hatufanyi kazi kwa kasi ambayo anaitaka kwa hiyo, nampongeza sana kwa sababu, amekuwa akifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* ya Mafia imekuwa na changamoto mbili kubwa ambayo ni changamoto ya vifaa, hasa kwenye fani za ushonaji, lakini vilevile Walimu ambao wana viwango vinavyohitajika, ili *VETA* iweze kusajiliwa. Nimemwahidi Mheshimiwa Mbunge na ninaendelea vilevile kumwahidi kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu iko tayari kusaidiana na yeye pamoja na wananchi wake wa Mafia ili changamoto hizo tuweze kuziondoa na tuweze kutoa usajili mapema kwa ajili ya chuo chake.

**MWENYEKITI:** Ahsante, ameshakuelewa. Mheshimiwa Shekilindi, jiandae Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SHAABAN O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wilaya ya Lushoto ni wilaya kongwe na bahati nzuri Waziri Mheshimiwa Ndalichako alitembelea Wilayani ya Lushoto na akaona hali halisi ilivyo. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri utatuma wataalam wake

kwenda kuona majengo yale ya Halmashauri, ili ikimpendeza tuweze kuanza sasa kukarabati majengo yale na watoto wetu waanze kusoma masomo ya VETA?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana, anataka kujua ni lini tu, mwambie.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, leo hii tukitoka mimi na yeye tutapanga ni lini tutawapeleka hao watendaji kule.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu sahihi. Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri anapojibu anaelezea suala zima la kujenga vyuo kila wilaya na mkoa, lakini hawajazungumzia changamoto kubwa ya tatizo kubwa la Walimu wa ufundi stadi. Je, wanapojenga hivi vyuo kila mkoa na kila wilaya wana Walimu kwa sababu, wana Chuo kimoja tu cha Ualimu wa Ufundi Stadi kule Morogoro, ni lini wataongeza au waapanua chuo kile au kujenga chuo kingine, ili tupate Walimu bora ambao wataweza kuhimili au kwenda kwenye hivi vyuo ambavyo vinajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, ni lini? Jiandae Mheshimiwa Hongoli.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kuna upungufu huo na Serikali inatambua na tumeanza hatua za makusudi kuhakikisha kwamba, tunaongeza upatikanaji wa Walimu katika vyuo vyetu vya ufundi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Zamani tulikuwa na shule za msingi ambazo zilikuwa zinatoa mafunzo ya ufundi, lakini pia, tulikuwa na sekondari za ufundi. Je, ni kwa nini sasa Wizara isizifufue zile shule angalau kila kata iwe na shule moja ambayo inatoa mafunzo ya ufundi, ili kuwawezesha vijana ambao hawajafanikiwa kwenda sekondari kupata stadi na mwisho wakaweza kujajiri na vilevile tukateua sekondari katika kila tarafa sekondari moja iwe sekondari ya ufundi, ili vijana wanaokosa kuendelea na kidato cha tano waweze kujajiri?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri. Jiandae Mheshimiwa Mwamoto.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hongoli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kuna haja ya kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi katika ngazi mbalimbali na ndio maana Serikali inajaribu kwa kuanzia kujenga vyuo, lakini badaye tutaangalia uwezekano wa kurudi kwenye shule za sekondari na shule za msingi ambazo ni za ufundi. Kwa sasa zipo shule baadhi za sekondari ambazo zinatoa ufundi vilevile.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamoto, ajiandae Mheshimiwa Magereli.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu limeshaulizwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Magereli.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri aliyoyatoa kuhusu umuhimu wa elimu ya ufundi na Halmashauri ya

Wilaya ya Kigamboni ni wilaya mpya ambayo ina fursa nyingi sana zinaweza kuwasaidia vijana kujajiri wenyewe. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga chuo cha ufundi katika Halmashauri ya Kigamboni, ili kuwaepusha vijana wetu na gharama kubwa ya nauli wanayolipa katika kivuko kuvuka kwenda mjini kutafuta huduma hiyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magereli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Serikali ina mpango wa kujenga vyo vya ufundi vya wilaya katika Wilaya zote ikiwemo na Wilaya ya Kigamboni. Naomba nimshauri vilevile Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote kwamba, pale ambapo wao wenyewe na wananchi wao watakuwa wameanzisha jitihada ya kujenga chuo inakuwa ni rahisi sisi kuja kuongezea kuliko tunapoendelea kusubiri nchi nzima tujenge.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Kilimo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Martin Alexander Msuha.

Na. 93

### **Vyama vya Ushirika vya Msingi**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali ilibadilisha mfumo wa ununuzi na uuzaji kahawa kwamba ni lazima kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi:-

Je, ni Vyama vingapi vya Msingi vya Ushirika (AMCOs) vimeundwa Wilayani Mbinga kufuatia kubadilishwa kwa mfumo huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Martin Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika huanzishwa na wananchi kutokana na mahitaji yao, hivyo, kupelekea kuwepo kwa aina mbalimbali za Vyama vya Ushirika kama vile vyama vya ushirika vya mazao ya kilimo na masoko, mifugo, uvuvi, viwanda, nyumba, fedha na madini kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imeelekeza biashara ya zao la kahawa na mazao mengine ya biashara kufanyika kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi (*AMCOS*) badala ya wanunuzi binafsi kwenda kwa wakulima moja kwa moja. Utaratibu huu utawawezesha wakulima kunufaika na kilimo cha kahawa kwa kuzalisha kahawa yenye ubora na kuzwa kupitia minada ambapo wanunuzi watashindanisha na hivyo kupelekea mkulima kupata bei nzuri na yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Kahawa 67 na Chama Kikuu cha Ushirika kimoja (*MBIFACU*) ambavyo vimeansihwa na wakulima wa kahawa katika Mkoa wa Ruvuma. Aidha, Wilaya ya Mbinga ina jumla ya Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Kahawa 58 ambavyo ndivyo vitasimamia na kuendesha biashara ya kahawa katika Wilaya ya Mbinga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msuha.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini pia



nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa kupeleka mnada wa kahawa Wilayani Mbinga kuanzia msimu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kumetokea changamoto kadhaa katika mfumo huu mpya ikiwemo kuchelewesha malipo kwa wakulima, wakulima kulipwa bei tofauti lakini pia kukosekana kwa uaminifu kwa baadhi ya watendaji wa *AMCOS*. Je, Serikali imejipangaje kutatua kero hizi kwenye msimu ujao wa kahawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kumekuwepo mabadiliko ya bei msimu kwa msimu, je, Serikali inajipangaje ama ina mpango gani wa kuanzisha Mfuko wa Kuimarisha Bei ya Kahawa *(Price Stabilization Fund)* ili kuondokana na tatizo hili la mabadiliko ya mara kwa mara ya bei ya kahawa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martin Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita hasa ya kuchelewesha malipo kwa wakulima pamoja na wakulima kulipwa bei tofauti na bei ambayo ilitangazwa na Serikali ama iliyouzwa mnadani. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Msuha kwa ufuatiliaji wa wakulima wa kahawa nchi nzima kupitia wakulima hawa wa Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujibu swali lake napenda kusema kwamba madai yake ni ya kweli, mimi mwenyewe nilifika katika Mkoa wa Ruvuma na tuliongea na wakulima walithibitisha hilo. Kilichotokea mwaka jana kama unavyokumbuka, ndiyo ulikuwa mwaka wa kwanza kutumia

mfumo huu wakulima wenyewe kwenda kuuza kahawa yao Moshi kupitia vyama vyao vya ushirika. Kwa hiyo, kahawa ile walivyokoboa na kuipeleka mnadani ilichelewa sana kuuzika kutokana na anguko kubwa la bei katika soko la dunia na katika soko la mnada hapa nchini. Kwa sababu walienda kuuza wenyewe, ilikuwa hamna namna nyingine lazima wasubiri mpaka kahawa iuzwe ndipo walipwe. Hata hivyo, kadiri watakavyoendelea kuuza kwenye mnada ndivyo hivyo wakulima wataweza kulipwa pesa zao kwa kuzingatia na mauzo kwenye mnada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili amesema kwamba tumejipangaje. Mwaka huu tumejipanga kupeleka minada hiyo katika kanda zao lakini pili ni kuruhusu wakulima wenyewe kupitia vyama vyao vya ushirika kama wakipata soko la moja kwa moja kuuza nje ya nchi tutatoa vibali hivyo ili wauze moja kwa moja. Kwa taarifa tu ni kwamba mpaka sasa tumeshapata wanunuzi ambao wapo tayari kuingia mkataba na Serikali kwa ajili ya kuuza kahawa hiyo kupitia mnada wa moja kwa moja (*direct export market*) kwa ajili ya kahawa hiyo na tayari mahitaji ya wanunuzi wale ni makubwa kuliko uzalishaji uliopo nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Zao la kahawa lina matatizo makubwa sana nchi nzima na matatizo yanayolikabili ni pamoja na pembejeo na bei yenyewe ya kahawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa Dodoma tulikuwa na kikao cha wadau na Mheshimiwa Waziri uliongea vizuri sana, uzalishaji unapungua kila mara na maeneo mengine kwa mfano kwangu kule Rombo wanaamua kung'oa kahawa ile ya zamani wanapanda ndizi na kabichi. Je, ni mkakati gani ambao Serikali inao kuwasaidia wakulima ili kunyanyua kiwango cha uzalishaji wa kahawa yetu ambayo katika soko la dunia inasemekana ni kahawa tamu sana ukilinganisha na kahawa kutoka maeneo mengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi ajiandae Mheshimiwa Nape, Mheshimiwa Bulembo na Mheshimiwa Maftaha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, anataka kujua Serikali tuna mkakati gani wa kuongeza tija na uzalishaji wa zao la kahawa ili kuvutia bei nzuri kwa wakulima. Mkakati wa kwanza ni kwamba sasa hivi tupo kwenye mazungumzo ya makampuni ambayo yanatengeneza mbolea kama *OCP* kutoka Morocco ili kujenga kiwanda kikubwa cha mbolea hapa nchini ili kurahisisha upatikanaji wa mbolea na pembejeo zingine kwa ajili ya kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia Shirika letu la Maendeleo la Taifa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo, tunawawezesha wakulima kwa kuwapa mikopo na Serikali inadhamini zaidi ya asilimia 80 ya matrekta na nyenzo zingine za kilimo kwa ajili ya kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima. Lengo ni kuongeza tija na uzalishaji, kama alivyosema tuna miaka zaidi ya kumi hatujaweza kuongeza uzalishaji wa kahawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi sana, Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na kupongeza ziara nzuri ya Mheshimiwa Rais Magufuli kwa baadhi ya Mikoa ya Kusini ambayo inalima korosho, Serikali itakubaliana na mimi kama ilivyotokea kwenye kahawa mabadiliko ya mfumo wa ununuzi wa korosho yameathiri mapato ya Halmashauri ambazo zilikuwa zinategemea ushuru wa korosho. Halmashauri nyingi kwa asilimia 70 mpaka 80 zilikuwa zinategemea mapato haya. Serikali ipo tayari kufanya tathmini ya madhara

yatakayojitokeza baada ya maagizo ya Mheshimiwa Rais kwamba pesa hizi zisidaiwe na hivyo kuangalia namna ya kufidia ili hizi Halmashauri zisiathirike zaidi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nape, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la msingi anasema kwamba, je, Serikali ipo tayari kufanya tathmini ya athari zilizopatikana kwa kushuka mapato ya Serikali ya Halmashauri? Kwanza nichukue nafasi hii kusema kwamba Serikali haijabadili mfumo wa ununuzi wa korosho hapa nchi. Kama mnavyofahamu tuliingia kwenye mfumo huo baada ya wakulima wenyewe kukataa kuuza katika mnada uliokuwa halali kwa wanunuzi wale kutokana na bei ambayo haikuwavutia zaidi ya minada mitatu minne. Kama Serikali tusingeweza kuangalia hali ile iendelee ndiyo maana tuli-*intervene* ili kuhakikisha wakulima hawa wanapata bei nzuri wanayostahili. Wakati ule tunaingia tulikuwa tunafahamu bei ni ndogo lakini tulienda kuwalipa wakulima bei ya Sh.3,300 ambayo ilikuwa huwezi kuipata mahali popote duniani zaidi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali lake la kama tupo tayari kufanya tathmini, napenda kusema kwamba tupo tayari na tumeshaanza kufanya tathmini hiyo lakini mapato yale ya Halmashauri ni ya Serikali na iliyolipa ni Serikali, kwa hiyo, Serikali haiwezi kumlipa Serikali mwenzie. Msimu ujao tutajipanga vizuri na mfumo utakuwa kama ulivyokuwa, mapato ya Halmashauri watayapata kupitia mfumo utakaokuwepo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kutokana na swali la msingi,

niipongeze Wizara ya Kilimo na Waziri Mkuu kwa kazi waliyoifanya Kagera. Wakulima wa kahawa Mkoa wa Kagera wa Muleba, Misenyi na Bukoba Vijijini kupitia *KDCU* na *KCU* mpaka leo kuna ambao hawajalipwa malipo yao ya kupeleka kahawa *KDCU* na *KCU*. La pili, bado kuna wakulima ndani wana kahawa...

**MWENYEKITI:** Swali ni moja tu Mheshimiwa.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe tamko kwa wale wakulima ambao hawajalipwa haki yao, ni lini watalipwa haki yao? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna baadhi ya wakulima waliouza kupitia Vyama vya Ushirika vya *KCU* na *KDCU* hawajalipwa malipo yao mpaka sasa hata wale wa Tarime Vijijini katika Mkoa wa Musoma. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, walioenda kuuza kahawa ile ni wakulima wenyewe kupitia vyama vyao vya ushirika kwenye mnada wa Moshi, kwa hiyo watalipwa baada ya kahawa yao kuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea katika msimu wa mwaka jana kahawa ilianguka sana sokoni kwa hiyo wakulima wale waliona siyo busara kuuza kwa bei ya chini kuliko gharama za uzalishaji walizoingia. Pia, kahawa hii ambayo ikikobolewa inatoka madaraja zaidi ya matano, wakati mwingine inachelewa kwa sababu imeuzwa daraja moja, madaraja mengine hayajauzwa. Kwa hiyo, wanasubiri ili kuuza kahawa yote na kwenda kuwalipa wakulima na wanachama wao. Kwa hiyo, naomba waendeleo kuwa na subira kwa sababu kahawa hiyo wameuza wenyewe kila wanapouza watalipwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bulembo kuwa na subira, Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kumekuwa na utaratibu wa hizi *AMCOS* zetu kuajiri ama kutokuwa na vigezo vya wale ambao wanaajiriwa kwamba hawawekewi elimu ni kiwango gani na kwa kiasi kikubwa wahasibu ndiyo wanakuwa ni watu pekee wenye elimu kiasi ambacho kinapeleka kufanya hujuma nyingi sana kwenye hizi *AMCOS*. Naomba kujua Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba wale ambao wanafanyia kazi hizi *AMCOS* wanawekewa vigezo vya kielimu ili wakulima wasiweze kuibiwa kama ilivyo hivi sasa? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu yako ni mazuri sana lakini fanya kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali tulishaanza mpango huo tangu msimu uliopita kwa mfano Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru tulianza kuajiri Wahasibu wenye *degree* moja na kuendelea kwa ajili ya kuongoza vile vyama vya ushirika. Utaratibu ule tutaendeleza nchi nzima kupitia vyama vyote vya ushirika ili tupate Wahasibu wenye weledi ili kuweza kuwahudumia wakulima wetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza.

Na. 94

### **Ujenzi wa Masoko ya Nkwenda na Murongo**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Serikali ilikuwa na mradi wa kujenga masoko katika eneo la Nkwenda na Murongo katika Wilaya ya Kyerwa lakini

masoko hayo hayajakamilika na yametelekezwa. Je, Serikali ilikuwa na malengo gani kujenga masoko hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya Nkwenda na Murungo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ni kati ya masoko matano ya kimkakati yaliyopangwa kujengwa kupitia Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agricultural Sector Investment Project – DASIP*) na ujenzi ulianza kutekelezwa mwaka 2006/2007 hadi mwaka Desemba, 2013. Masoko mengine yapo katika Halmashauri za Busoka (Kahama), Kabanga (Ngara) na Sirari (Tarime). Mradi huo uligharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la ujenzi wa masoko hayo ya kimkakati ilikuwa ni kuanzisha mfumo thabiti wa masoko utakaoongeza tija na pato kwa wakulima ndani ya Wilaya husika. Mfumo huu ulijenga mazingira wezeshi kibiashara katika maeneo ya mpakani ili kurahisisha biashara na majirani zetu na kuinua hali za kiuchumi za wananchi wa maeneo hayo na uchumi wa taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mradi wa *DASIP* unafungwa Desemba 2013/2014, kazi ya ujenzi wa masoko hayo ilikuwa haijakamilika na yalikuwa katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kwa kuzingatia umuhimu wa masoko hayo ya kimkakati katika Halmashauri husika, Serikali imepanga kukamilisha ujenzi wa masoko hayo na mengine nchini kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*). Katika bajeti ya mwaka 2019/2020

Serikali imetenga shilingi bilioni 2.9 kuendelea na ujenzi wa masoko hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mhandisi aliyekuwa anasimamia kujenga Soko la Nkwenda alikuja na Fuso mbili akahamisha nondo, mabati na saruji akidai anapeleka vifaa hivyo vya ujenzi katika Soko la Sirari katika Mkoa wa Mara na Serikali ina taarifa ya tuhuma za huyu Mhandishi. Je, ni hatua zipi zilichukuliwa dhidi ya Mhandisi huyu ambaye kwa kweli alikuwa kikwazo katika ukamilishaji wa soko hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa katika majibu ya Serikali imesemwa kwamba masoko haya yalijengwa kimkakati ili kuweza kusaidia wananchi kufanya biashara na nchi zilizo jirani na maeneo ambayo yamejengwa masoko hayo. Je, sasa ni lini Serikali itayakamilisha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi na ajiandae Mheshimiwa Gekul.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anasema kwamba huyu Mhandisi alipeleka magari kuhamisha vitu hivyo na kwamba Serikali tunayo taarifa na anataka kujua kwamba tumechukua hatua gani. Mpaka sasa tulishavielekeza vyombo vyetu vya ulinzi na kiuchunguzi kuendelea kuchunguza tuhuma na jinai hiyo ili ikithibitika amefanya jambo hili hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.



Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni lini masoko hayo yatakamilika, kama nilivyojibu kwenye swali lake la msingi, kwenye bajeti hii tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 2.9, Waheshimiwa Wabunge mkitupitishia haraka iwezekanavyo kuanzia Julai 1, tutaanza kutekeleza ujenzi wa masoko hayo yote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali na niishukuru kwa moyo wa dhati kwa kutusaidia kutujengea jengo kubwa la *NFRA* pale Babati kwa ajili ya kununua mahindi na kuyachakata. Bahati mbaya mwaka huu tangu Januari mvua hazinyeshi Kanda ya Kaskazini na hali si nzuri, hatuna maharage wala mahindi. Naomba nifahamu Serikali imejipanga vipi kwa ajili ya kukabiliana na hali hii ambayo wananchi wanakwenda kukabiliana nayo ya ukosefu wa mahindi na maharage ili wananchi wetu wapate mazao hayo kwa bei rahisi na wasiingie katika baa la njaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, wewe mzoefu jibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Gekul anataka kujua kwamba Serikali tumejipanga vipi katika kukabiliana na tishio la upungufu wa chakula nchini kutokana na ukame uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwanza tumetenga shilingi bilioni 15 kupitia Wakala wetu wa Taifa (*NFRA*) kwa kuendelea kununua mahindi kwa ajili ya kuyahifadhi kwa ajili ya kuja kuyasambaza au kupeleka sehemu ambazo zitakuwa na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa hivi tumeshawaelekeza wataalam wetu wamesambaa nchi

nzima kufanya tathmini ya kina kujua athari iliyoletwa na mabadiliko ya tabianchi hususan huu ukame ili kujua athari iko kiasi gani ili tuweze kuongeza mikakati mingine. Pia tumetenga zaidi ya shilingi bilioni tisa kupitia Bodi yetu ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kuendelea kununua mahindi na mazao mengine kukabiliana na hali hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

Na. 95

### **Uchakavu wa Vituo vya Polisi – Unguja na Pemba**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Kumekuwa na kilio cha uchakavu wa vituo vya polisi kwa upande wa Unguja na Pemba:-

(a) Je, ni vituo vingapi vipya vya polisi vilivyojengwa kwa upande wa Unguja na Pemba?

(b) Je, vituo hivyo vimejengwa na kampuni gani na ni vigezo gani vilivyoangaliwa katika ujenzi wa vituo hivyo?

(c) Je, ni lini Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara watafuatana nami kwenda kuviona vituo hivyo vilivyoachakaa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa ya Unguja na Pemba vituo vingi vimejengwa au kukarabatiwa katika miaka tofauti, vikiwemo Vituo vya Mwembe Madafu na Mbweni katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Kituo cha Mchanga Mdogo

Mkoani Kaskazini Pemba, Vituo vya Chwaka na Jambiani Mkoa wa Kusini Unguja na Vituo vya Chakechake na Mtambile Mkoa wa Kusini Pemba. Aidha, kuna ujenzi unaoendelea kwa sasa wa Vituo vya Chukwani, Dunga na Mkokotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo mengi ya vituo hivi vya polisi ujenzi ulikuwa ni wa ushirikiano wa wananchi na Jeshi la Polisi. Hata hivyo, tunatambua mkandarasi aitwaye *Albatina Construction Company Ltd* anayejenga Kituo cha Polisi Mkokotoni ambaye kazi yake bado inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo na uchakavu wa vituo vingi vya polisi katika Mikoa ya Unguja na Pemba kama vile vituo vya Mkoani Pemba, Kengeja, Micheweni, Konde, Mahonda, Nungwi, Kiwengwa na Kiboje ambapo hali ya kifedha ikiruhusu vitakarabatiwa. Viongozi wa Wizara wataambatana na Mheshimiwa Mbunge Jaku Hashim Ayoub tarehe 3/7/2019 kwenda kuviona vituo hivyo vilivyochakaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpe pole sana Mheshimiwa Waziri kwa kuvamiwa Kituo chake cha Polisi cha Madema...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, muda wetu umekwisha. Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tarehe 25 Julai, 2017, naomba kunukuu *Hansard*, "taratibu hizo zilishafanyika kama nilivyokwambia sasa. Tarehe 9 Novemba, "Serikali inatambua deni hilo." Tarehe 8 Novemba, 2017 mwaka wa Fedha 2017, "Jeshi la Polisi limetenga jumla ya shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kupunguza madeni ikiwemo mkandarasi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona ni aibu kwa Serikali yangu kupata aibu na hili deni ni la muda mrefu. Je,

Mheshimiwa Waziri, hesabu hata ulipochaguliwa wewe Jimboni kwako ulianza kwa kura moja ukafika hapa. Kama mimi, Serikali yangu kupata aibu nami ninaipenda niko tayari...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, uliza swali.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** ...niko tayari kuanza kuchangia shilingi milioni moja kwa ajili ya kituo. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuchukua shilingi milioni moja, kupokea mchango huu ili tufuatane kupeleka deni hilo na hizi hapa? Maana yake deni limeshakuwa la muda mrefu. Yuko tayari kupokea shilingi milioni moja kufuatana nami kupeleka hizi fedha za deni? (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, michango ni nje ya Bunge. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani hii ya CCM ujenzi wa vituo vya Polisi na makazi ya Askari tumeweka utaratibu kwamba tutahusisha wadau. Ninashukuru sana wewe Bungeni kujitokeza kuwa mdau kwa mujibu wa ilani hii. Hivyo naomba mchango wako uuwasilishe kwa Inspekta Jenerali wa Polisi ili tuendelee na ujenzi wa vituo vya Polisi hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni kweli kabisa kwamba deni la huyu Mkandarasi limekuwa la siku nyingi. Nimhakikishie Mheshimiwa Jaku, ambaye najua akifuatilia jambo lake ni king'ang'anizi, ni moto wa kuotea mbali; na kwa kweli siku siyo nyingi hatutakubali jambo analolisema kwamba Serikali yetu inatiwa aibu. Ndiyo maana Wakandarasi wengi nchini wanapenda kufanya kazi na Serikali na Serikali yetu inalipa madeni yake na deni lake limeshahakikiwa, awe na subira wakati wowote tutaweza kumlipa Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chemba ni moja kati ya wilaya mpya. Tumeanza kujenga kituo cha Polisi kwa sababu huduma nyingi za Polisi zinapatikana kwenye Wilaya mama ya Kondoa: Je, Serikali ina mchango gani kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi pale Chemba ambao tayari tumeuanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mna mpango gani? Jibu kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mshabiki wa Simba namba moja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi katika muundo wake na utoaji wa huduma, tunayo Mikoa 35 ya Kipolisi, tunazo Wilaya 182 za Kipolisi na pia tunazo Tarafa 610 za Kipolisi na tuna Kata na Shehia 4,410. Kwa hiyo, tunao mpango mkakati kuhakikisha kwamba huduma hizi zinakwenda kwenye maeneo yote hayo; na bado tuna mikoa mipya na wilaya mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Juma Nkamia kwamba Wilaya ya Chemba ni miongoni mwa wilaya ambazo mikakati yetu ndani ya Jeshi la Polisi tunakwenda kujenga kituo cha Polisi katika Wilaya ya Chemba.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu hilo linakwenda kwa Wabunge wote ambao majengo yao hayajajengwa.

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

Na. 96

**Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (Km 123)**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Barabara ya Likuyufusi – Mkenda yenye urefu wa kilometa 123 inayounganisha nchi mbili za Tanzania na Msumbiji, bado haijaanza kujengwa kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Likuyufusi – Mkenda yenye urefu wa kilometa 123 ni barabara kuu inayounganisha nchi mbili za Tanzania na Msumbiji na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii iliamua kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa lengo la kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, kazi ambayo ilikamilika mwaka 2013. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 shilingi bilioni 5.86 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa uchimbaji na usafirishaji wa makaa ya mawe katika Kijiji cha Muhukuru kilicho kilometa 74 kutokea Songea katika barabara hiyo, kumesababisha kuongezeka kwa magari mengi na mazito yanayobeba makaa ya mawe. Kufuatia hali hiyo, Serikali

kupitia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*) imeamua kufanya mapitio ya usanifu wa kina (*Design Review*) ili kukidhi mahitaji halisi yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kazi hiyo kukamilika, Serikali itaendelea kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza pia Mbunge wa Jimbo la Peramiho, dada yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia ujenzi wa barabara hii na hata alipokuja Mheshimiwa Rais, alijaribu kusema pale ili barabara hii iweze kujengwa. (*Makofi*)

(a) Swali langu la kwanza; ni kwa nini Serikali inachukua muda mrefu sana kufanya upembuzi yakinifu lakini pia na usanifu wa kina? Barabara hii imechukua karibu miaka kumi kupitia maneno hayo ya upembuzi na usanifu. Ni lini Serikali itamaliza upembuzi huu na usanifu huu ili barabara hii ianze kujengwa? (*Makofi*)

(b) Swali la pili; licha ya Serikali kuonesha kwamba imetenga shilingi bilioni 5.86, lakini fedha hizi hazikuweza kwenda kwa mwaka 2018/2019: Je, Serikali haioni kwamba kutokupeleka fedha hizi inaendelea kuchelewesha maendeleo kupitia barabara hii kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, hususan Jimbo la Peramiho? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana, muda wetu umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu tu nimpongeze Mheshimiwa Jacqueline, lakini nimpongeze Mbunge wa Peramiho kwa kufuatilia kwa sababu amekuwa akifuatilia sana jambo hili. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge mwuliza swali kwamba inachukua muda mrefu kwa sababu kwanza mtandao wa barabara ni mkubwa, mahitaji ya ujenzi ni makubwa na tunaendelea kutafuta fedha na kutenga fedha. Hata mwaka unaokuja tutaliomba Bunge lako liweke fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha. Tukipata fedha tu mara moja tutatangaza na kuanza kujenga barabara hii. Kwa hiyo, kwa majibu hayo, Mheshimiwa Jacqueline avute subira kidogo, tumejipanga vizuri, mahitaji ni makubwa, tunakuja Peramiho kuhakikisha kwamba tumewaunga wananchi wa...

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kemi.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya *Nyakato Steel*– Igombe, kilometa 18 na Barabara ya Mwaloni – Kirumba, kilometa 1.2 zimekuwa zikisuasua na ujenzi wake kwa muda mrefu sana. Mheshimiwa Angeline Mabula, amekuwa akifuatilia barabara hizi kwa muda mrefu lakini bado hatujapata majibu sahihi ya Serikali. Ni lini sasa barabara hizi zitakamilika na wananchi wa Mkoa wa Mwanza, hususan Wilaya ya Ilemela waweze kupata barabara safi na salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua changamoto za barabara za Ilemela, nami



nimekwenda, nimeona. Nitoe tu maelekezo na wito kwa Mameneja wetu kule kwenye Mkoa wa Mwanza kwamba wasimamie kwa ukaribu nami nitakwenda kuhakikisha kwamba maeneo haya; na yapo maeneo siyo haya tu aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, yapo maeneo mengi kwenye Jimbo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Angeline Mabula kwa sababu amekuwa akifuatilia sana, ilinichukua siku nzima, mtandao ni mkubwa sana kwenye Jimbo lake, mjini lakini...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu mazuri na muhimu, fanya ziara naye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nitakwenda. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niulize swali dogo la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Jiandae Mheshimiwa Mama Salma.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** ...barabara ya kutoka Tabora kwenda Kigoma ambayo inatuunganisha na Tabora bado haijakamilika; na kipande cha kutoka Malagarasi mpaka Uvinza ambacho kilikuwa na Mkandarasi wa *Abu Dhabi Fund* tumesikia kuna matatizo ya kiufundi: Je, Mheshimiwa Waziri unasema nini juu ya jambo hilo? Vinginevyo barabara hii haitakamilika mpaka tufike mwaka 2020. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nsanzugwanko anafahamu, tumezungumza mara nyingi sana juu ya barabara hizi. Niseme tu kwa ufupi, Chagu – Kazilambwa pamoja na barabara ya Malagarasi –

Uvinza zitakamilisha mtandao wa barabara kutoka Tabora kwenda Kigoma tukikamilisha vipande hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutazungumza tu na Mheshimiwa Mbunge tuone kama kuna changamoto, basi tujue nini kinachoendelea. Kwa kifupi tunakwenda kujenga barabara hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mama Salma.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara za lami hugarimu pesa nyingi za Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mara tu barabara hizo zinapojengwa, hubomolewa na kupitishwa miundombinu mingine, hatimaye hazirejeshwi katika ubora wake:-

Je, Serikali inatuambia nini juu ya jambo hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ujenzi wa barabara unachukua fedha nyingi, lakini niseme tu shughuli zozote zitakazohusisha kukata barabara lazima zifanyike kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, kama kuna mtu anakata barabara na kuacha uharibifu ni makosa. Nami nielekeze viongozi wote, Mameneja wote wa Mkoa; mtu ambaye atafanya shughuli za kibinadamu na kuharibu barabara bila kurejesha kwa ubora wake na bila kupata kibali kwa mujibu wa sheria ni makosa, wachukue hatua kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa muda wetu mdogo. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Juma Othman Hija.

Na. 97

**Kushuka kwa Thamani ya Shilingi**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Thamani ya Shilingi ya Tanzania inaendelea kuporomoka kila siku, kuporomoka huko kunachangia kwa kiasi fulani ugumu wa maisha kwa wananchi wa kawaida katika kupanga mipango yao ya kimaisha:-

Je, Serikali ina mkakati gani ya kudhibiti mporomoko huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya shilingi dhidi ya sarafu nyingine hutegemea nguvu za soko, yaani ugavi na mahitaji. Sababu za kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni ni pamoja na tofauti ya mfumuko wa bei kati ya Tanzania na nchi wabia katika biashara, mauzo kidogo nje ya nchi, mahitaji makubwa ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje; kupungua kwa misaada na mikopo kutoka nje; kuimarika kwa fedha za kigeni kutokana na kuimarika kwa uchumi wa nchi wabia katika biashara na kuzuka kwa biashara ya kuhisia na kuotea ya sarafu za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, sababu zote hizi hazikuwepo na hivyo thamani ya shilingi yetu dhidi ya Dola ya Marekani ilikuwa tulivu ikilinganishwa na sarafu nyingine dhidi ya Dola ya Marekani. Kwa mfano, thamani ya shilingi ilipungua kwa wastani wa 2% kwa mwaka 2017/2018 na 2016/2017 ikilinganishwa na wastani wa 22% mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiujumla shilingi ilikuwa imara ikilinganishwa na sarafu nyingine kama vile Franc ya Rwanda iliyopungua kwa wastani wa 5% na shilingi ya Uganda iliyoshuka kwa 3.8% katika kipindi kama hicho. Utulivu wa thamani ya shilingi ulitokana na utekelezaji thabiti wa sera za fedha na bajeti pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni, Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa ongezeko la ujazi wa fedha linaendana na ukuaji wa shughuli za uzalishaji;

(ii) Kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma ndani ya nchi;

(iii) Kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, na;

(iv) Kudhibiti hali ya wasiwasi katika soko la fedha za kigeni inayosababishwa na hisia pamoja na biashara ya kuotea ambapo Benki Kuu hununua na kuuza fedha za kigeni katika soko la jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba jukumu la kuimarisha thamani ya shilingi ni shirikishi na pia lina wadau wengi na hivyo kila mmoja anahitajika kushiriki kwa nafasi yake ili kuleta mafanikio kwa nchi. Aidha, wadau wakuu ni Serikali pamoja na wananchi. Serikali ina majukumu makuu mawili:-

(i) Serikali kupitia Benki Kuu ina jukumu la kutekeleza na kusimamia Sera ya Fedha ili kudhibiti mfumuko wa bei, viwango vya kubadilisha fedha na ujazi wa fedha katika soko; na

(ii) Kuandaa na kusimamia sera thabiti za kibajeti, kuhakikisha nchi inakuwa na amani na utulivu na kujenga miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuchochea uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wananchi ambao ndio wawekezaji, wana jukumu la kuzalisha kwa wingi bidhaa na huduma mbalimbali hususan zile zinazoipatia nchi fedha za kigeni na/au zinazoipunguzia nchi mzigo wa mahitaji ya fedha za kigeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Othman Hija.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutosheleza kabisa, lakini nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imekuwa na zoezi la kuyafungia maduka ya *Bureau De Change* nchi nzima. Je, zoezi hili ni miongoni mwa mikakati ya kuimarisha fedha yetu au ni kwa madhumuni gani? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyouliza je, ulikuwa ni mkakati wa kuhakikisha thamani ya fedha yetu. Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi moja ya kazi za benki kuu ni kuhakikisha kwamba thamani ya fedha yetu inakuwa imara na katika mikakati ya kuhakikisha hilo, ni kuhakikisha kunakuwa na usimamizi imara na madhubuti wa maduka yetu ya kubadilisha fedha na hilo ndilo lilikuwa lengo la zoezi lililofanyika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha, tumeshaongoza dakika ishirini ya maswali na hii tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista, mara nyingi Kiti huwa kinasema majibu ya Serikali ni marefu mno, jaribuni kuyapunguza, mnajibu vizuri *very clear*,

lakini yanakuwa ni marefu mno, jibu moja linachukua dakika nne, kwa hiyo, tunaomba mjaribu kulitazama hilo.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo jukwaa la Spika Wageni 38 wa Mheshimiwa January Makamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ambao ni Mhandisi Joseph Malongo, Katibu Mkuu; Balozi Joseph Sokoine, Naibu Katibu Mkuu; Profesa William Mwegoha, Mkurugenzi Mazingira; Dkt. Gwamaka Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu *NEMC*; Profesa Esnath Chaggu, Mwenyekiti wa Bodi *NEMC*; Ndugu Juma Mkomi, Katibu wa Makamu wa Rais; Ndugu Paul Sangawe, Mkurugenzi – Sera na Mipango; Ndugu Sifuni Msangi, Kaimu Mkurugenzi Muungano; Ndugu Mosoud Balozi, Msaidizi wa Makamu wa Rais, Mambo ya Nje; Ndugu Nehemia Mandia, Msaidizi wa Makamu wa Rais siasa; wameambatana na viongozi wa Maafisa wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni wawili wa Mheshimiwa Angelina Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni Askofu Richard Msingwa kutoka Jijini Mwanza na *Engineer* Marko Kotta, kutoka Jijini Dodoma, Karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Japhary Michael kutoka Mkoani Kilimanjaro, Mchungaji Yohana Mbogo. Karibu. *(Makofi)*

Wageni 79 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Mashaka Mahangi, Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya, Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni kwaya ya ushindi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Bishop Julius Nassary, Karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Zainabu Mndolwa ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam ndugu Ahmed Baabad, Ndugu Ayman Baabad na Ndugu Hairat Sweleh. Karibuni. (*Makofi*)

Wageni 42 wa Mheshimiwa Augustine Vuma ambazo ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wakiongozwa na Ndugu Lutakonya Essau. Karibuni. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambaye ni mjukuu wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, Ndugu Sophia Nyerere. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa ibada ya *Chapel* ya Bunge, Mheshimiwa Anna Lupembe anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, wanatangaziwa kuhudhuria ibada katika *Chapel* ya Pius Msekwa leo siku ya Jumanne, tarehe 16 Aprili, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. Waziri wa Nchi.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Nchi, zimeni *microphone* zenu hizo, kaeni chini, wote zimeni *microphones*.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kutoa hoja ifuatayo:-

KWA KUWA tarehe Mosi Aprili, 2019, Kamati ya Kanuni ilikutana na kufanya marekebisho katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Marekebisho hayo yanalenga kuongeza msukumo, ufanisi na kasi ya kudhibiti ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa kuiwezesha Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuwa na jukumu la kusimamia shughuli za Serikali za kudhibiti ugonjwa wa Kifua Kikuu. Jukumu hilo lilikuwa linatekelezwa na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii;

NA KWA KUWA Kamati ya Masuala ya UKIMWI ni Kamati mahususi yenye jukumu la kusimamia Shughuli za Serikali kuhusu utekelezaji wa masuala ya UKIMWI; na kwakuwa, ushahidi wa kitakwimu umeonesha mahusiano makubwa baina ya ugonjwa wa UKIMWI na ugonjwa wa Kifua Kikuu;

NA KWA KUWA Kamati ya Masuala ya UKIMWI imeonesha ufanisi mkubwa katika kusimamia shughuli za Serikali kuhusu utekelezaji wa sera na mikakati ya kudhibiti ugonjwa wa UKIMWI nchini;

NA KWA KUWA Kamati ya Kanuni baada ya kuzingatia uhusiano baina ya ugonjwa wa UKIMWI na ugonjwa wa Kifua Kikuu, iliona umuhimu wa kufanya marekebisho ya kifungu cha 10 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa lengo la kuwezesha Kamati ya masuala ya UKIMWI kusimamia shughuli za Serikali za kudhibiti ugonjwa wa Kifua Kikuu katika nchi yetu ya Tanzania;

NA KWA KUWA marekebisho haya yalifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 155(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016;

NA KWA KUWA Kanuni 156(1) inakataza marekebisho ya Kanuni kuanza kutumika kabla ya kuchapishwa na kuingizwa kwenye toleo la Kanuni za Bunge linalofuata;

NA KWA KUWA Kanuni ya 156(2) inaelekeza kwamba Spika ataagiza Kanuni zilizofanyiwa marekebisho zichapishwe upya kwenye gazeti la Serikali kwa madhumuni ya kuingiza mabadiliko yaliyofanyika;



NA KWA KUWA mabadiliko yaliyofanywa ni madogo na jambo linalofanya kuwe na uzito mdogo wa kuwa na Toleo jipya la Kanuni;

NA KWA KUWA hata bila kuwepo kwa chapisho jipya upo urahisi wa kufanya rejea ya Kanuni bila ya kuwa na Toleo jipya;

NA KWA KUWA mchakato wa kuandaa na kuchapisha toleo jipya la kanuni utagharimu fedha nyingi ambazo zinaweza kutumika katika mahitaji mengine;

NA KWA KUWA muda si mrefu kamati ya Kanuni ndani ya Bunge letu Tukufu inatarajia kuanza mchakato wa kufanya mapitio ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ambapo inatazamiwa yatakuwepo mabadiliko makubwa ya Kanuni na kwamba Kamati itaandaa mapendekezo ya marekebisho ya kanuni ambayo iwapo yatapitishwa na Bunge yataingizwa kwenye Toleo Jipya na marekebisho hayo yatachapishwa kwenye gazeti la Serikali.

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba Kanuni 156(1) na Kanuni ya 156(2) zinazoweka sharti la kuingiza mabadiliko ya Kanuni kwenye Toleo jipya la Kanuni na sharti la kuzichapa upya kwenye gazeti za Serikali zitenguliwe ili kuwezesha mabadiliko yaliyofanyika katika kifungu cha 10, Nyongeza Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, yaanze kutumika bila kuchapisha Toleo jipya na kulitangaza kwenye gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, Waheshimiwa Wabunge hii Kanuni ni muhimu na hii Kamati ya UKIMWI kwa mara ya kwanza imeonesha kazi nzuri sana ndani ya Bunge hili, sasa nitawaoji kuhusu mabadiliko haya ya Kanuni.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, marekebisho ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 yatakuwa, Kamati ya Masuala ya UKIMWI itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia utekelezaji ya masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;

(ii) Kusimamia shughuli za Serikali za kudhibiti na kutokomeza ugonjwa wa Kifua Kikuu;

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI Kifua Kikuu na udhibiti wa dawa za kulevya;

(iv) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti UKIMWI, Kifua Kikuu na dawa za kulevya; na

(v) Kushughulikia bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Kwa hiyo, sasa Mwenyekiti wa Kamati hiki kitu kinakuja kwenu moja kwa moja, muendeleo nacho.

Mheshimiwa Lubeleje Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma anawaomba Wabunge wote wa Dodoma, kuhudhuria kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM, Mkoa wa Dodoma, saa tano asubuhi.

Mkuu wa Mfuko wa Faraja *Fund* Bunge anawatangazia Wabunge wote Wanafaraja, mnakumbushwa kuchangia Mfuko wa Faraja, tafadhali wasiliana na Joseph Mhagama, Afisa Mtendaji Mkuu. Katibu.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda wetu leo mdogo, haya nitachukua Mheshimiwa Khenani na Mbarouk wawili tu. Mheshimiwa Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI,** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7). katika michango ambayo inaendelea ndani ya Bunge kutoka kwenye hotuba ya Waziri Mkuu upande huu wa Upinzani, michango yetu kwa maandishi inakuja, lakini kwa maana ya *video* hazifiki na zikifika zinakuwa nusu. Sasa linapotokea tatizo kama hilo tumeomba Kiti chako mara kadhaa, nini kinatokea, kama kuna shida ya mitambo ya Bunge tujue kwamba mitambo hiyo inaruka upande wa *Opposition* tu, lakini upande wa CCM haifanyi kazi hiyo. Tunaomba Mwongozo wako nini kinasababisha michango yetu isionekane.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tanzania tuna Majiji matano, lakini kwa bahati mbaya mambo mengi yamekuwa yakianza Dar es Salaam, mfano ni suala la vitambulisho hivi vya wajasiriamali, leo katika vyombo vya habari wametangaza kwamba katika Jiji la Dar es Salaam, Mgambo wa Jiji wamekuwa wanakamata wafanyabiashara wadogo wadogo hawa na kuwasumbua pamoja na kuchukua bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua tu Mwongozo wako wakati huku kuna vitambulisho, lakini hapo hapo sasa Mgambo wa Jiji nao wamekuwa wanawakamata wafanyabiashara na kuwasumbua, sasa tuelekee wapi kwamba umuhimu ni kupata vitambulisho au Halmashauri za Majiji nazo zinakuwa zinang'ang'ania hasa kuwasumbua wafanyabishara kutaka mapato. Naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante nina miongozo miwili, Mwongozo wa kwanza ni wa Mheshimiwa Khenani, hili nitalifuatilia kwa sababu majibu yake sinayo hapa mezani.

Pia jambo la Mheshimiwa Mbarouk kwa mujibu wa Kanuni halijatokea ndani ya Bunge leo. Kwa hiyo sina Mwongozo juu ya hilo.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mazingira Mheshimiwa January Makamba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2018/2019; na Malengo ya Ofisi kwa mwaka 2019/2020, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya, uzima na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii. Napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii na kuendelea kuongoza vizuri nchi yetu na kumpongeza kwa mafanikio yaliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Makamu wa Rais kwa kutupa miongozo na maelekezo yaliyotuwzesha kutekeleza majukumu yetu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Ali

Mohamed Shein Rais wa Zanzibar kwa kazi nzuri anayoifanya kwa hekima na Busara zake zilizoweza Muungano wetu kudumu. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake kwanza aliyoitoa hapa Bunge ambayo imetoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka ujao, lakini pia kwa uongozi wake dhabiti hapa Bungeni na pia katika shughuli za kila siku za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, wewe pamoja na Wenyeviti wenzako kwa kuliongoza Bunge letu vizuri. Napenda vile vile kuwapongeza sana na kuwashukuru Wenyeviti wanaoziongoza wanaotusimamia katika Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote mbili Viwanda, Biashara na Mazingira na Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe wa Kamati hizo kwa kazi nzuri wanazofanya kwa kushirikiana na sisi kwa kutuongoza na kutushauri, lakini zaidi kwa kupokea na kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha uliopita na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijadili kuhusu makusanyo na mapato kwa mwaka wa fedha uliopita. Ofisi ya Makamu wa Rais haina vyanzo vya mapato. Hata hivyo, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu lilikuwa limekusaya mapato ya jumla ya Sh.10,430,060,727.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka unaoisha wa fedha kwa mwaka 2018/2019, kwa Fungu 26, jumla ya Sh.6,485,991,000.00 zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Hadi mwezi Machi pesa zilizopokelewa ni Sh.4,572,810,578.05. Kwa Fungu 31 fedha zilizoidhinishwa na Bunge Sh.15,065,422,523.28. Hadi mwezi Machi, fedha zilizopokelewa zilikuwa ni Sh.7,937,894,492.78 ambayo ni sawa na asilimia 52.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Dira ya Maendeleo ya Nchi yetu kwa mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo Endelevu, Sera ya Taifa ya Mazingira, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na maelekezo na miongozo mbalimbali iliyotolewa na viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, niombe hotuba yetu iliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge iingizwe katika *hansard* kama hotuba rasmi iliyotolewa na Ofisi ya Makamu ya Rais na hapa nasoma muhtasari tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Muungano. Muungano wetu ndiyo utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu, bila Muungano hakuna Tanzania. Ili kuenzi na kuimarisha Muungano wetu, ofisi imetekeleza majukumu ambayo imekabidhiwa kikatiba na kisheria ya kuratibu utekelezaji wa masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali zetu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha kazi zifuatazo zimefanyika. Kwanza, kuratibu vikao vya kamati ya pamoja; kuratibu utekelezaji wa masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa; kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali zetu mbili lakini pia kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Pamoja. Katika mwaka unaokwisha ofisi iliratibu na kufanya kikao cha Kamati ya Pamoja tarehe 9 Februari, 2019 hapa Dodoma. Kikao hicho kilitanguliwa na vikao vya mbalimbali vya Sekretarieti, Makatibu Wakuu pamoja na Mawaziri. Hoja zilizowasilishwa katika kikao hicho ni pamoja na mapendekezo ya utaratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja; Mwongozo wa Ushirikishwaji wa Zanzibar kwenye masuala ya kimataifa; na hoja zinazohusu fedha na biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao hicho kilikuwa na mafanikio mengi lakini kadhaa ni yafuatayo. Kwanza, tulipitisha utaratibu wa mpya wa vikao vya Kamati ya Pamoja Kushughulikia Masuala ya Muungano ambapo tulipitisha mfumo mpya wenye lengo la kuimarisha na kuongeza ufanisi wa vikao hivi ikiwa ni pamoja na uwezo na urahisi wa kufuatilia maagizo na maelekezo yanayotolewa na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu mpya ambao umepitishwa umeanzisha Kamati mbili za Kamati ya Pamoja ambapo ni Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kamati hizi zimepewa majukumu ya kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa changamoto zinazohitaji utatuzi wa haraka badala ya kusubiri mlolongo mrefu wa kikao cha Kamati ya Pamoja. Pia katika utaratibu huu mpya tumeurasimisha na tumewezesha Makatibu Wakuu Viongozi kuwa sehemu ya vikao rasmi vya Kamati ya Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto zilizokuwa zinalalamikiwa na Zanzibar kwenye Muungano ni ushiriki na ushirikishwaji mdogo wa Zanzibar kwenye masuala ya Kimataifa na Kikanda. Katika moja ya mafanikio ya kikao hiki ni kwamba tumepitisha Mwongozo wa Ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile changamoto ya ongezeko la gharama za umeme kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO* lilipatiwa ufumbuzi ambapo imekubalika kuwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) itatozwa kwa kiwango cha asilimia sifuri (0%) kwenye umeme unaouzwa na *TANESCO*. Vilevile, mapendekezo ya deni linalofikia shilingi bilioni 22.9 na lenyewe limefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao cha Kamati ya Pamoja pia kilijadili na kuzipatia ufumbuzi hoja za biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ambazo baadhi yake ni gharama za kushusha mizigo; viwanda vya Zanzibar kupata leseni kutoka *BRELA* na upatikanaji wa fursa za ushiriki katika miradi

ya maendeleo ya viwango na ubora kwa bidhaa na maendeleo ya wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka unaokwisha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kupata gawio la asilimia 4.5 ya fedha za Misaada ya Kibajeti (*General Budget Support - GBS*), faida ya Benki Kuu, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Kodi ya Mapato yatokanayo na Ajira (*PAYE*). Hadi kufikia mwezi Machi, jumla ya shilingi bilioni 36.79 zimepelekwa kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika maeneo yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha Ofisi imefanya ufuatiliaji wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo katika Majimbo 16 kati ya 32 yaliyoko Unguja. Matokeo ya ufuatiliaji huo yanaonesha kuwa miradi mingi ikiwemo ya maji na umeme inakidhi mahitaji kwa kuongeza huduma muhimu za kijamii na hivyo kuboresha maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo. Miradi hiyo imefanikiwa kuinua hali ya wananchi, kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa watu kwa pande zote mbili za Muungano. Miradi hiyo hufadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Baadhi ya Miradi ya hiyo ni pamoja na Miradi ya *TASAF*, *MIVARF*, *MKURABITA*, Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Uzalishaji wa Chakula na Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar imeendelea kuhamasisha Sekta zisizo za Muungano kukutana na kujadili masuala yanayohusu sekta zao na kubadilishana utaalum na wataalam ili kuleta ufanisi na uwiano wa maendeleo kati ya pande zote mbili za



Muungano. Katika kipindi hiki vikao tisa (9) vya sekta zisizo za Muungano vimekaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi imeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu na faida zinazotokana na Muungano kupitia vyombo vya habari ikiwemo televisheni na magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi ya mazingira, ni muhimu itambulike kwamba sekta zote za uzalishaji mali hapa nchini zinategemea hifadhi ya mazingira na hivyo mazingira ni muhimu sana na yanatoa mchango mkubwa sana katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa Watanzania. Hata hivyo, shughuli zisizo endelevu zinazofanywa kwa namna isiyoendelevu zinachangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa mazingira na kusababisha uharibifu wa ardhi; ukosefu wa maji salama kwa wananchi wa mijini na vijijini; uchafuzi wa mazingira; upotevu wa bioanuai na makazi; uharibifu wa mifumo ikolojia; uharibifu wa misitu; mabadiliko ya tabianchi; kuongezeka kwa viumbe vamizi na kuongezeka kwa taka za kielektroniki; kuongezeka kwa taka za kemikali; kuwepo kwa uchafuzi utokanao na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi; na kukosekana kwa udhibiti wa mazao yatokanayo na teknolojia ya uhandisi jeni (*GMOs*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulinda na kuhifadhi mazingira na kukabiliana na changamoto ya mazingira nchini, Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mikakati mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na mikataba ya kimataifa ya mazingira pamoja na utoaji wa elimu kuhusu mazingira. Katika kutekeleza azma hiyo, kwa mwaka wa fedha unaokwisha, yafuatayo yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tumeandaa Sera mpya ya Mazingira. Sera ya Mazingira tuliyonayo ni ya mwaka 1997, ina miaka 22 na imepitwa na wakati, kwa hiyo, tunaandaa sera mpya na bora zaidi itakayoweza kutupa nguvu na uwezo wa kusimamia mazingira kwa ufanisi zaidi. Sera hiyo sasa iko kwenye ngazi ya Kikao cha Makatibu

Wakuu na baadaye itapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Katika kipindi cha utekelezaji wa sheria hii, changamoto kadhaa zimejitokeza ikiwemo kutoandaliwa kwa baadhi ya kanuni; uwezo mdogo wa kitaasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria ya mazingira ikiwemo Wizara za kisekta na Serikali za Mitaa; na uelewa mdogo kuhusu wajibu na majukumu ya wadau katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hizi, juhudi mbalimbali zimechukuliwa na Ofisi yetu ikiwemo pamoja na kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden na ni wa miaka mitatu (3) na una thamani ya dola milioni 3. Mradi huu utatusaidia kufanya kazi mbalimbali katika kusimamia vizuri Sheria ya Mazingira. Hadi kufikia sasa, Ofisi imeratibu uteuzi wa Wakaguzi wa Mazingira wapatao 487 watakaosaidia kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira. Ofisi yetu imekamilisha Mwongozo ambao utaboresha Tuzo hii. Awali Tuzo hii ilihusu maeneo machache ya kutunza miti na vyanzo vya maji, maboresho haya sasa yatatoa mtazamo mpana zaidi kuhusu Tuzo hii na kuanzia mwakani tunaweza kuanza kuitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira nchini. Sheria ya Mazingira inatutaka sisi Ofisi ya Makamu wa Rais kila baada ya miaka miwili kuwasilisha Ripoti ya Hali ya Mazingira nchini, hatujafanya hivyo kwa miaka kadhaa sasa lakini katika mwaka wa fedha ujao tutawasilisha ripoti hiyo kwa sababu imekwishakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira. Katika kipindi cha mwaka

unaokwisha, Ofisi iliainisha mapendekezo ya maeneo ya yanayohitajika kufanyiwa marekebisha ya sheria ili kuwezesha Mfuko huu kuanza kazi kwa ufanisi. Matarajio yetu ni kwamba mabadiliko haya yatapitishwa ili Mfuko huu uweze kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Tumekuwa tunatumia Maadhimisho haya kama fursa ya kutoa elimu kwa umma kuhusu mazingira. Mwaka juzi tulifanya Butiama, mwaka jana tulifanya Dar es Salaam na mwaka ujao tutafanya Mkoani Mwanza. Uteuzi wa Mkoa wa Mwanza umezingatia changamoto mbalimbali zinazolikabili Jiji hili ikiwa ni pamoja na uharibifu wa ardhi katika Bonde la Ziwa Victoria pamoja na uharibifu wa mazingira ya ndani ya Ziwa lenyewe unaosababishwa na shughuli za kijamii na kiuchumi. Kufanyika kwa Maadhimisho haya katika Mkoa wa Mwanza kutatoa fursa kwa wananchi wa Mkoa huo kushiriki na kuelimika zaidi na kuhamasishwa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza matumizi ya mkaa unaotokana na miti. Asilimia 80 ya miti inayokatwa hapa nchini inakatwa kwa ajili ya kutengeneza mkaa. Ofisi yetu katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha imeendelea kushirikiana na taasisi nyingine na Wizara zinazosimamia sekta hii kupunguza matumizi ya mkaa unaotokana na miti. Vilevile, tumeendelea kushirikiana na wadau wengine katika kuandaa maonyesho na mashindano ya teknolojia mbadala. Imani yetu ni kwamba katika mwaka ujao wa fedha basi maonyesho haya na uvumbuzi huu utasaidia kupunguza matumizi ya mkaa nchini ili kuokoa misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya mifuko ya plastiki. Naomba hapa nitumie muda mrefu kidogo kuelezea. Hatimaye Serikali kupitia tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu imeamua kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 1 Juni, 2019. Uamuzi huu ni mkubwa na wa kihistoria na wa kijasiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia tamko hili, Ofisi yetu imeandaa kanuni zitakazochapishwa katika Gazeti la Serikali ambazo zitaainisha utaratibu mzima wa suala hili ikiwemo kuweka adhabu kwa mtu atakayekiuka makatazo haya. Vilevile Ofisi yetu imeunda Kikosi Kazi cha Taifa kinachohusisha taasisi mbalimbali za umma ikiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, NEMC, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania, TFDA, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, TAMISEMI na nyinginezo ili kusimamia na kuratibu kwa pamoja zuio hili la matumizi ya mifuko ya plastiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao na wawekezaji wa mifuko ya plastiki ambacho nilikiongoza jana tarehe 15 Aprili, 2019 tukishirikiana na Mawaziri, Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kairuki, wazalishaji wa mifuko mbadala wameihakikishia Serikali kuwa wana uwezo wa kuzalisha mifuko mbadala itakayokidhi mahitaji ya nchi. Ofisi itaendelea kuhamasisha umma kuhusu jambo hili ili tuweze kufanikiwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono jitihada hizi kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifanue zaidi kwa kusema kwamba uchumi mpana zaidi utakaoshirikisha watu wengi zaidi na ajira nyingi zaidi na mapato mengi zaidi upo kwenye mifuko mbadala kuliko mifuko ya plastiki. Vilevile ili kuhakikisha tunafanikiwa, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais ameelekezwa kuwasiliana na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba kila Halmashauri inapata maelekezo mahsusi kuhusu hatua za kuchukua kuhakikisha kwamba tunafanikiwa katika ngazi zote za utawala katika nchi yetu kuanzia vitongoji, vijiji, mitaa na maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa ufafanuzi zaidi kwamba katika jambo hili vifungashio kadhaa hasa vinavyotumika katika sekta ya ujenzi, kilimo, afya havitahusika katika katazo hili. Pia napenda kutoa wito kwa wale wanaohusika na kuzalisha bidhaa za kwenye chupa za plastiki basi utaratibu utawekwa kuhamasisha ukusanyaji wa

chupa zile na urejelezaji (*recycling*) ili tukiondoa plastiki vilevile tuweze kupunguza matumizi ya chupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Viumbe Vamizi (*Invasive Species*). Viumbe vamizi ni changamoto kubwa na mpya ya mazingira nchini. Viumbe hawa husababisha athari kubwa katika uchumi hususan katika sekta kuu za uzalishaji kama vile kilimo, uvuvi, mifugo, maji, maliasili na utalii na hivyo kuathiri ajira na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Pia huathiri afya za binadamu na mifugo pamoja na mazingira kwa kuharibu mifumo ya kiikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonyesha kwamba hapa nchini kwetu kuna takriban aina 220 ya viumbe vamizi na Tanzania imeathirika zaidi ya nchi nyingine katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Kwa kuzingatia hili, hatua za haraka zisipochukuliwa kuwadhibiti viumbe hawa, uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi utaendelea kuathirika kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na athari hii katika mwaka wa fedha unaokwisha, Ofisi yetu iliunda Kikosi Kazi cha Kitaifa kwa ajili ya kuandaa Mpango Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Viumbe Vamizi. Mpango huo utasaidia kudhibiti kuongezeka na kusambaa kwa viumbe hawa na Mpango huo tayari umepitishwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu na unangoja Baraza la Mawaziri ili uweze kupitishwa na kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa taka zenye madhara. Taka hatarishi zinazozalishwa viwandani, migodini, hospitalini na baadhi ya maeneo ya biashara, Ofisi imeendelea kudhibiti uzalishaji na utupaji wa taka hizi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa. Ofisi yetu inabadilisha kabisa utaratibu wa kutoa vibali vya kuruhusu biashara ya taka zenye madhara ikiwemo vyuma chakavu, pamoja na taka nyinginezo. Lengo ni kupunguza na kuondoa biashara holela ya vyuma chakavu inayochangia kuharibu miundombinu ya nchi yetu. Kwa hiyo, tutaendelea na jambo hili katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa umma kuhusu usimamizi na hifadhi ya mazingira. Ofisi ilikamilisha maandalizi ya Mfumo wa Taarifa kuhusu Mazingira (*Central Environmental Information System*) unaoendana na mfumo wa teknolojia ya simu kuwawezesha watumiaji kupokea na kutoa taarifa zinazohusu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizofanyika katika mwaka unaokwisha ni maandalizi ya kutangaza maeneo ya mazingira lindwa na maeneo na nyeti pamoja na kuandaa orodha, kuunda Kamati ya Kitaifa, kuandaa vigezo na kujadili maeneo yanayopendekezwa. Vilevile tuliendelea na kazi za juhudi za kuokoa Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha na kuandaa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto zinazokabili utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti kwa kushirikiana na sekta husika, hasa sekta ya maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliendelea kutoa tathmini ya mazingira kimkakati; kuratibu na utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda kuhusu Mazingira; kuendelea na kazi ya udhibiti wa taka ngumu nchini hususan kuandaa Mwongozo wa Uwekezaji katika Taka Ngumu ili kuhamasisha uwekezaji na kuongeza jitihada za kuboresha usimamizi wa taka hizo hapa nchini. Katika utekelezaji wa Mwongozo huo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ndiyo ina jukumu muhimu kabisa la kudhibiti taka kwenye masoko na kwenye miji yetu. Hivyo ndiyo ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo huo ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*GEF*) katika mwaka unaokwisha tuliratibu shughuli za Mfuko huo kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi iliyofadhili na Mfuko huo. Vilevile tuliwasilisha kwenye Sekretarieti ya *GEF* kwa ajili ya kupata ufadhili nchini kwa awamu ijayo ya mfuko huo ambapo katika awamu hii Tanzania imetengewa fedha kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kazi za *NEMC*; Baraza la Taifa la Hifadhi la Mazingira ambalo ndiyo msimamizi mkuu wa uzingatiji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira limeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Moja, ni kuhakikisha kwamba Sheria ya Mazingira inazingatiwa ipasavyo. Katika kutekeleza shughuli za maendeleo hapa nchini, Baraza limetekeleza kazi zifuatazo:-

Kwanza, Baraza limefanya ukaguzi katika maeneo yanayostahili kufanyiwa ukaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira. Hata hivyo, ukaguzi huo umebaini kwamba asilimia 40 tu ya miradi ndiyo inayozingatia Sheria ya Mazingira na mingine inakabiliwa na changamoto mbalimbali za uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limechukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira kwa miradi iliyokiuka sheria na kanuni. Hatua hizo ni pamoja na kutoa ushauri, maelekezo, maonyo, amri za katazo, amri za urejeshaji wa mazingira lakini pia tumewafikisha Mahakamani watu ambao hawakuzingatia Sheria za Mazingira na hawakuzingatia maelekezo ya Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka katika mwaka unaokwisha *NEMC* imeendelea kupokea malalamiko yanayohusu uchafuzi wa mazingira na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu tathmini ya athari kwa mazingira (*EAI*), naomba eneo hili nilizungumzie kwa kirefu kidogo kwa sababu ni eneo ambalo limekuwa linalalamikiwa hata na viongozi wetu. Niseme kwamba suala la uchelewashaji na gharama za utoaji wa vyeti vya mazingira tumelishughulikia kwa ukamilifu sana. Tumefanya mambo yafuatayo ili kurahisisha kuharakisha na kupunguza utoaji wa vyeti.

Kwanza, tumeweka kanuni mpya za kupunguza gharama za kufanya *EIA* kwenye miradi kutoka shilingi milioni

10 kwa miradi ya watu wa kawaida hadi kwenda shilingi milioni nne na chini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivi kwa msingi kwamba *EIA* siyo chanzo cha mapato bali ni huduma. Kwa hiyo, kuanzia sasa cheti cha mazingira kitagharimu gharama ya shughuli ya kufanya ile kazi na siyo chanzo cha mapato. Vile vile tumepunguza sana muda wa kupata cheti. Kwenye Sheria ya Mazingira muda uliowekwa kwa kawaida ni siku 149.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba shughuli za kufanya *EIA* zipo ndani ya sheria na ni siku 149, lakini tumeweka utaratibu mpya wa kupunguza sana siku hizo na kuhakikisha kwamba watu wanapata vyeti kwa haraka. Kwa mfano, kwenye sheria, Waziri anapaswa kukaa na cheti hicho kwa siku 30, lakini tumekubaliana kwamba cheti kitakapofika kwenye ofisi yangu hakitachukua siku nne kitakuwa kimeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeamua kuweka utaratibu mpya wa kutoa vyeti vya muda (*Provisional Environmental Clearance - PIC*) ambapo cheti hiki ambapo cheti unakipata ndani ya siku saba na kitakuwezesha kuanza shughuli za uwekezaji wakati mchakato wa *EIA* unaendelea; kwa sababu tunaamini kwamba kuna watu wamezingatia sheria lakini wanahitaji vibali vingine na wanahitaji ku-*mobilize* na kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeweka utaratibu kwamba pale utakapoomba na pale tutakapofanya *checklist* kuhakikisha kwamba kiwanja chako kipo mahali salama, unakimiliki, basi tutakupa cheti uanze uwekezaji wakati mchakato unaendelea. Ingawa cheti hiki cha muda haki-*guarantee* kwamba utapata cheti cha kudumu, lakini kinakuwezesha kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumepitia upya kanuni za tathmini ya athari kwa mazingira ili kuondoa vikwazo vinavyowakwaza wawekezaji katika kuanza kushughuli zao.



Pia tumepitia upya kanuni zinazodhibiti wataalam wanaofanya *EIA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima ifahamike kwamba mchakato huu wa *EAI* unahusu *NEMC* na *consultant* binafsi ambao wakati mwingine wao ndio wanachelewesha wawekezaji lakini lawama zinakuja kwa *NEMC*. Kwa hiyo, tunapitia kanuni zinazowadhibiti ili kuhakikisha kwamba hawacheleweshi wawekezaji na pia wanawatoza gharama ambazo siyo kubwa na vile vile tunaondokana na changamoto za udanganyifu zinazoweza kufanywa na *consultants* hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumewachukulia nidhamu watumishi wa *NEMC* ambao walikuwa wandanganyifu ambao walikuwa wanapaka matope Baraza na kusumbua wawekezaji na kuwalaghai. Hivi tunavyongea, watumishi wanane wa *NEMC* wapo Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumepata uongozi mpya, Mkurugezi Mkuu mpya na Bodi mpya ya *NEMC*. Imani yetu ni kwamba hatua zote hizi zitatusaidia kuhakikisha na kuharakisha mchakato wa kupata vyeti. Malalamiko ya *NEMC* ukiyasikia sasa hivi, basi hayakutokea sasa hivi, ni malalamiko ya nyuma kwa sababu kazi kubwa na nzuri inafanyika sasa hivi na sisi tunaamini kwamba usimamizi wa mazingira katika uwekezaji ni jambo muhimu na la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba mchakato wa miradi wa Kitaifa na Kimataifa unakwenda kwa kasi inayokubalika, Baraza limekuwa linashauriana na wahusika katika kila hatua ya utekelezaji. Kwa mfano, mradi wa bomba la mafuta kutoka Uganda, Baraza limeshapokea tathmini ya athari kwa mazingira na imefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Mpira hapa Dodoma, cheti kimeshatolewa; mradi wa *Striegler's Gorge* na wenyewe umepatiwa cheti. Baraza kwa kushirikiana na *TANESCO* wanaratibu na kusimamia

utekelezaji wa mpango wa utekelezaji wa mazingira wakati wote wa utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ofisi yetu pamoja na *NEMC*, ili kuhakikisha kwamba mchakato *EIA* unafanyika kwa ufanisi, tumeshirikiana na Kituo cha Sayansi na Mazingira cha India ili kuandaa miongozo ya kurahisisha mapitio ya miradi ya majengo na Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaangalia uwezo wa Waziri mwenye dhamana ya mazingira kukasimu kwa mamlaka za Serikali na Wizara za Kisekta, baadhi ya vyeti vingine, kwa mfano, vituo cha mafuta pamoja na miradi midogo midogo ili kuharakisha upatikanaji wa vyeti kwa miradi ya aina hiyo ambapo siyo kila mradi hapa nchini unakuja kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mwaka fedha unaokwisha, Baraza limeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu mazingira kwa kutumia vyombo vya habari na mafunzo kwa wadau mbalimbali. Kazi hiyo bado inaendelea na kazi ya Elimu kwa Umma kuhusu Mazingira bado ni kubwa, kwa hiyo, Baraza litaendelea na kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *NEMC* imeendelea kutekeleza ajenda ya Utafiti katika Mazingira (*National Environmental Research Agenda*) kwa kufanya tafiti mbalimbali hapa nchini. Vile vile Baraza limefanya tathmini ya mmomonyoko wa fukwe za Kigamboni na utafiti wa kina kuhusiana na tatizo la kujaa kwa maji ya mvua katika maeneo ya makazi ya Mlandizi na ripoti za utafiti huo zimeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeangalia kwa kina na kuandaa kikosi kazi kwa ajili ya kuangalia tatizo la upatikani wa mchanga katika Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani na uharibifu wa miundombinu na mito kutokana na uhitaji mkubwa sana wa mchanga ambao unaharibu mazingira. Ripoti ya Kamati hiyo inatolewa na hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira limeendelea kusimamia maeneo, kuratibu shughuli za (*Man And Biospher Reserve*) tano hapa nchini na Baraza limeanza maandalizi ya Kongamano la Kisayansi kuhusu hifadhi hai (*biosphere reserves*). Kongamano hilo linatarajiwa kufanyika mwezi Agosti mwaka huu 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira imetoa nafasi ya kuhifadhi baadhi ya maeneo ambayo yanapaswa kuhifadhiwa kutokana na unyeti wake kimazingira na Ofisi ya Makamu wa Rais ilitembelea maeneo mbalimbali nchi ambayo hayana hifadhi yoyote lakini yanahitaji hifadhi kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na Baraza pamoja na Ofisi zimeendelea kufanya maandalizi kwa ajili ya kuyahifadhi maeneo hayo nyeti. Tunaziomba Halmashuri zote nchini kama kuna maeneo kama kuna maeneo ambayo wanadhani ni nyeti na hayana hifadhi yoyote, basi tupo tayari kufanya nao kazi kuyahifadhi kwa kutumia Sheria za Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uratibu wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za washirika wa maendeleo, kwa mwaka unaokwisha Baraza limeendelea kutekeza miradi mbalimbali kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka fedha unaokwisha Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Baraza tumeendelea kusimamia sheria na kanuni na taratibu za utumishi wa Umma sambamba na kuwezesha watumishi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi hiki, watumishi wamehudhuria mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yetu, ofisi yetu ilikumbana na changamoto kadhaa zikiwemo upatikanaji wa rasilimali zinazoendana na mahitaji halisi ya ofisi; pili, uelewa mdogo wa wadau kuhusu masuala ya Muungano na umuhimu wa hifadhi ya mazingira; nyingine ni upatikanaji wa takwimu sahihi za mazingira; na kutokuwa na wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tulichukua hatua kadhaa katika kukabiliana nazo. Hatua hizo ni pamoja na kuandaa miradi na kuiwasilisha kwa wadau wa maendeleo kwa ajili ya kupata fedha, kuendelea kutoa elimu kwa Umma kupitia vyombo vya habari na maonyesho ya Kitaifa kuhusu masuala ya Muungano na umuhimu wa kuhifadhi mazingira, pamoja na kuhamasisha wadau hususan Serikali za Mitaa na sekta binafsi kushiriki katika masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeandaa taarifa ya hali ya mazingira pamoja na kuandaa maandiko mbalimbali ya kupata ufadhili kwa ajili ya eneo la ukusanyaji takwimu, lakini vile vile tumeendelea kutoa mafunzo kwa wataalam pamoja na kuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni malengo na maombi ya fedha za matumizi kwa mwaka fedha unaokuja. Katika kuimarisha na kuenzi Muungano, Ofisi yetu imepanga kutekeleza majukumu na malengo yafuatayo:-

Kwanza, kuendelea kuratibu vikao vya Kamati ya pamoja; pili, kufuatilia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zinazotekelezwa pande zote mbili za Muungano; tatu, kutoa elimu ya Muungano kwa makundi tofauti ya kijamii ikiwa ni pamoja na kuandaa warsha na mafunzo mbalimbali; nne, kuhamasisha Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana kuendelea kushirikiana katika kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi ya mazingira katika kusimamia na kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho, katika mwaka ujao wa fedha Ofisi imepanga kufanya mambo yafuatayo:-

Kwanza kukamilisha Sera mpya ya Taifa ya Mazingira ambayo ni mapitio ya Sera ya mwaka 1997. Vile vile tumepanga kukamilisha na kuchapisha nakala za ripoti ya Taifa ya hali mazingira nchini na kuiwasilisha Bungeni kwa mujibu wa sheria. Pia tutaendelea kuhamasisha na kutoa elimu ili kuhakikisha kwamba matumizi ya mkaa wa kukatwa

kwa miti kwa kweli yanapungua kwa kiasi kikubwa kwa sababu yanaharibu sana mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, kwa mujibu wa mamlaka niliyopewa katika Sheria ya Mazingira kifungu cha 13, tutaweka utaratibu sasa na tunafanya maandalizi kwamba kila Taasisi ya Umma na binafsi, inayolisha watu wanaozidi 300 itakatazwa kutumia kuni na mkaa wa kukata kwenye misitu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie. Tutaweka utaratibu kwenye kanuni na tangazo la Gazeti la Serikali kwamba kila Taasisi ya Umma au binafsi inayolisha watu zaidi ya 300 kwa siku, italazimika aidha kupata mkaa kwenye shamba lake yenyewe au kutumia nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kama Chuo Kikuu cha Dodoma kuna wanafunzi 30,000, kila siku wanakula mara tatu na kila siku vyakula hivyo mara tatu ni mkaa na kuni unaotoka katika misitu wa asili; kuna Kambi za Jeshi, kuna *hospital*/kuna shule, makambi ya wakimbizi na kadhalika. Kwa hiyo, tutalazimisha; naomba niurudie; kila taasisi inayolisha watu wanaozidi 300, aidha, italazimika kupata mkaa na kuni kwenye shamba lake yenyewe au kutumia nishati mbadala. Mamlaka ya kuandika kanuni hiyo ninaya kupitia Sheria ya Mazingira, kifungu cha 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifuko ya plastiki. Kama nilivyosema hapo awali, tumeanza na imani yetu ni kwamba tutafanikiwa. Kwa hiyo, tunasubiri kanuni zitoke kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili tuzichapishe na tuanze utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira yetu ni kutekeleza zoezi hili bila bugudha, bila usumbufu, bila kupigana virungu, kwa sababu tumefanya maandalizi ya muda mrefu wa kwa wadau wote; na imani yangu ni kwamba Watanzania wote watalipokea jambo hili kama jambo jema kwa ustawi wa nchi yetu. Imani yetu ni kwamba uchumi mpya utakaoibuka wa

mifuko mbadala utasaidia kutoa mapato zaidi kwa wananchi, ajira zaidi na hifadhi ya mazingira vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viumbe vamizi. Hili ni jambo jipya ambalo ofisi yetu imeamua kulishughulika kuanzia mwaka uliopita wa fedha na tumeandaa na kwa kweli ninayo faraja kubwa sana kwa wataalam wetu waliofanya kazi kwa zaidi ya miezi miwili kwenda kila kona ya nchi yetu kuangalia viumbe vamizi kwenye maeneo ya malisho, maeneo ya kilimo, maeneo ya maji na kutengeneza mkakati mkubwa na mzuri wa kupambana na *invasive species*. Tanzania itakuwa ni nchi ya pili Afrika ukiondoa *South Africa* ambayo ina mkakati mahususi wa kupambana na viumbe vamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, imani yetu ni kwamba mkakati huo utapitishwa na utatumika kwa ajili ya kuilinda nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mnafahamu kipindi mvua ikiwa inanyesha, ukipita maeneo Kongwa na Gairo ulikuwa unaona maua mengi mazuri pembeni mwa barabara. Yale maua ni viumbe vamizi, yanaenea na kuondoa kabisa maeneo ya kilimo na hamna shughuli inayoweza kufanyika. maua hayo yamevamia maeneo mengi ya nchi yetu na kuondoa ardhi muhimu kwenye uzalishaji wa chakula na malisho. Kwa hiyo, ni tishio kubwa la mazingira la Kitaifa, nasi ofisi yetu tumeamua kulichukulia kwa uzito huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandaji wa miti, katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi yetu itaendelea kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti. Kwa kweli hapa tutaomba kushirikiana na sekta yenyewe husika yenye dhamana ya miti. *TFS, TAFORI, Tanzania Tree Seed Agency*, vyote vipo chini ya Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili zoezi hili lifanyiike na vifanikiwe vizuri, ushirikiano kati ya Ofisi ya Makamu ya

Rais, Wizara ya Maliasili na *TAMISEMI* ni muhimu. Jukumu la upandaji wa miti siyo la ofisi moja peke yake, nasi tutafanya kazi kwa pamoja kuhakiksha kwamba ile dhamira yetu ya miti milioni moja na nusu kila Halmashauri, inatimia na kuna ufuatiliaji kweli kwamba miti hiyo inapandwa na siyo takwimu tu kwenye karatasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira, katika mwaka ujao wa fedha tutaanza kutoa tuzo rasmi. Naomba nizungumzie sasa suala la mita 60 ambalo limezungumzwa sana na limewagusa watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, yalitoka maelekezo kwamba watu wasizuiwe kufanya shughuli katika maeneo ya ndani ya mita 60 na kwamba tungalie upya sheria hiyo. Sheria ya Mazingira ni kweli imekataza kutofanyika kwa shughuli za kibinadamu za kudumu au ambayo asili yake inaweza kuhatarisha mazingira au kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira ndani ya mita 60 ya mito, kingo za mito, bwawa na miambao ya asili ya ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika kifungu hicho hicho kinachofuatia, kimebaini kwamba kuna uwezekano kukatokea uhitaji wa shughuli za kibinadamu za kutafuta ridhiki kufanyika. Ndiyo maana kifungu hicho kimetoa nafasi kwa Waziri mwenye dhamana ya mazingira kutengeneza mwongozo wa namna na aina ya shughuli zinazoweza kufanyika ndani ya mita 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kutumia kifungu hiki, ofisi yetu sasa inaandaa mwongozo wa aina na namna ya shughuli za riziki zinazoweza kufanyika ndani ya mita 60. Mwongozo huo tutauleta kwa ajili ya kupitishwa. Inawezekana kabisa tukaruhusu kilimo katika mita 60 lakini tukataza matumzi ya mbolea za kemikali au tukakataza kwamba tusiende mita 10 au 20 au tukakataza aina fulani ya mazao, lakini tukaruhusu watu watafute riziki ndani ya mita 60 kwa sababu sheria imetoa nafasi hiyo kwa Waziri mwenye dhamana ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni jirani na Kenya na tuna-*share* baadhi ya rasilimali za mazingira. Baadhi ya rasilimali hizo ni pamoja na Ziwa Chala, Ziwa Jipe, Ziwa Natron na Mto Mara. Nilipoenda Kenya nilikutana na Waziri mwenzangu wa Mazingira, nilimwomba naye mkutano na kuna maneno yalikuwa yanazungumzwa kuhusu Mto Mara na Kenya kujenga miradi kule itakayozuia maji yasitiririke na hivyo kuathiri Hifadhi ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri tuliwekeana mkataba kuhusu usimamizi wa pamoja wa rasilimali hizi. Baadhi ya mambo tuliyokubaliana ni kwamba tutaunda kamati ya pamoja ya ngazi ya wataalam na ngazi ya Mawaziri, tutafanya tathmini ya kina ya rasilimali za mipakani, tutaanda mikataba wa pamoja wa usimamizi wa rasilimali zote ambazo tuna-*share* na vilevile tutandaa mpango wa pamoja wa utafutaji wa fedha na rasilimali hizo. Hadi sasa Kamati ya wataalam kwa upande wa Tanzania imeundwa na tunangoja wenzetu wa Kenya walete wataalam wao ili waweze kuja na tuanze kazi hiyo.

Tunaamini jambo hili litasaidia nchi hizi kufanya kazi kwa pamoja, lakini kuimarisha ujirani mwema na urafiki na undugu uliopo kati yetu na ndugu zetu Wakenya kwa kushirikiana katika jambo hili la kuhifadhi rasilimali za pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu usimamizi wa mazingira katika ngazi za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Sheria ya Mazingira inatoa jukumu kubwa na wajibu mkubwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha uratibu na usimamizi wa mazingira, mazingira yote tunayoyazungumza yapo kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwenye vitongoji, vijiji, mitaa na kata, kwa hiyo tumeamua sasa tufanye kazi na wenzetu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili na wenyewe jambo la mazingira waliweke katika vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa ajili hiyo sasa utekelezaji uratibu na ufuatiliaji wa hifadhi ya mazingira utauhusu uundaji wa Kamati za Mazingira katika ngazi ya jiji,



manispaa, wilaya, miji, kata, vijiji, mtaa na vitongoji pamoja na kuhakikisha kwamba Kamati hizi zinafanya kazi na uandaaji wa utekelezaji wa mipango ya mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haitoi umuhimu kwa mazingira, basi tusahau kabisa kuhusu hifadhi ya mazingira nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine ambazo tunazitekeleza katika hifadhi ya Mazingira kwenye Ofisi yetu ni:-

(i) Kutoa mafunzo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara za Kisekta;

(ii) Kuanzisha mfumo wa utoaji vyeti na leseni za mazingira kwa njia ya mtandao;

(iii) Kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi ili cha kuokoa mfumo wa Ikolojia wa Bonde la Mto Ruaha ambacho tulikiunda na kazi hiyo inaendelea;

(iv) Tutaendelea kuelimisha umma kuhusu hifadhi ya mazingira pamoja na matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa (*GMO*);

(v) Tutaendelea Vilevile, kuandaa na kuchapisha Mkakati wa Mawasiliano ya Elimu ya Umma kuhusu Hifadhi ya Mazingira.

(vi) Tutasimamia na kuratibu na kuendelea kufuatilia Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania ni Mwanachama;

(vii) Tutaendelea kutoa vyeti vya (*EIA*) pamoja na *Strategic Environment Assessment*;

(viii) Tutaendelea kufatilia utekelezaji wa mikakati iliyopo chini ya Mikataba ya Kitaifa tuliyoridhia;

(ix) Tutaendelea kuwezesha mchakato wa kuridhia Mikataba na Itifaki za Kimataifa ambazotumezisaini;

(x) Tutaendelea kutekeleza miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabiachi iliyopo chini ya Mikataba ambayo sisi ni washiriki; na

(xi) Tutaendelea kuandaa miradi ya kuhifadhi mazingira na kuiwasilisha kwa wafadhili kwa ajili ya kutafuta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Baraza la Taifa la Kusimamia Hifadhi ya Mazingira kwa mwaka unaokuja katika kutekeleza utekelezaji wa Sheria ya Mazingira, Baraza limepanga pamoja na mambo mengine kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea na ukaguzi na ufuatiliaji jambo ambalo ni wajibu wake na kuchukua hatua stahiki;

(ii) Kuendelea kufanya mapitio ya nyezo na miongozo mbalimbali;

(iii) Kuboresha mfumo wa kutoa vyeti;

(iv) Kuendelea kusajili miradi ya mazingira;

(v) Kufanya tathimini ya mifumo ya Ikolojia;

(vi) Kuendelea na ajenda ya Taifa ya utafiti;

(vii) Kufanya mapitio ya miradi iliyowasilishwa;

(viii) Kuandaa miongozo ya usimamizi wa mazingira katika maeneo lindwa na nyeti; na

(ix) Kazi nyinginezo ambazo ni wajibu wake kKisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maendeleo kwa mwaka unaokuja tutaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama ilivyoodheshwa katika kitabu chetu ambacho tumewakabidhi, lakini vile vile

tutaendelea kusimamia mikataba mbalimbali ambayo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, nchi yetu ni ya Muungano na Muungano huo, una umuhimu wa kipekee kwa Taifa na umekuwa ni utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano huu sasa unatimiza miaka 55 tangu kuasisiwa kwake na katika kipindi cha miaka 55 maingiliano, mashirikiano, udugu na ujamaa umeendelea kuimarika na hamna namna yoyote ambapo Muungano huu unaweza kurudi nyuma au maingiliano haya yanaweza kurudi nyuma. Natoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuenzi, na kuulinda na kuudumisha Muungano huu ili jitihada za kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa faida ya pande zote mbili yaendele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Muungano huu unaendelea kuimarika na kushamiri. Chini ya uongozi wao, naomba nirudie hakuna changamoto yoyote ya Muungano inayoweza kutufarakanisha, kututenganisha na kuturudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha ujao Ofisi na Serikali kwa ujumla itaendelea kuyafanyia kazi mambo yote yanayoleta changamoto katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Naomba niseme hapa, kwamba tusitumie changamoto za Muungano kuupa jina baya Muungano, tusitumie changamoto za Muungano kuhoji uhalali na umuhimu wa Muungano. Changamoto hizi zilikuwepo, zipo na zitaendelea kuwepo hata zikiisha zote leo, miaka kumi, miaka mitano ijayo zitakuja nyingine. Cha muhimu ni taratibu na mifumo ya kushughulikia changamoto hizi za Muungano na sisi tunaamini kwamba kwa wakati huu

tumeweka mfumo na utaratibu bora zaidi wa kushughulikia changamoto hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa mazingira na mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu, ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kwamba mazingira yanalindwa. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla kuunga mkono jitihada za Serikali katika kulinda na kuhifadhi mazingira. Naomba niseme hapo pia kwamba, hatua zote za maendeleo tunazochukua mambo yote tunayojenga yatakuwa hayana maana kama kutafuta riziki na ustawi kutakuwa hakuwezekani, kwa sababu tumeharibu mazingira yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu tunachofanya tunapolima, tunapofuga, tunapovua, *common denominator* ni mazingira, ndiyo ukweli wenyewe. Kwa hiyo bila hifadhi ya mazingira afya za watu, riziki zetu, na shughuli nyingi zinazoajiri ikiwemo Kilimo zitaathirika, kwa hiyo naomba Bunge hili, wajishike kabisa, kama wadau wakubwa wa hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nimalize kabisa kwa kuwashukuru wote walionisaidia kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu ya Ofisi yetu. Napenda kumshukuru Rais wetu kwa uongozi wake, na dira na mwelekeo aliotupatia kuhusu majukumu yetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, kwa uongozi wake uliotuwezesha kutekeleza na kwa kweli kwa ulezi wake, hasa kwangu mimi binafsi na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, najisikia fahari sana, na kwa kweli nadeka kwamba mtu ambaye naripoti kwake ni mama na Makamu wa Rais ambaye anatulea vizuri na kutufundisha vizuri kuhusu uongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana, ndugu yang una rafiki yangu Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Naibu Waziri, ananisaidia na anafanya kazi nzuri sana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, omba pesa, muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, na Watendaji wote wa Ofisi, Mhandisi Joseph K. Malongo, na Balozi Joseph E. Sokoine na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais; na wa *NEMC* kwa kweli kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Wafadhili wote ambao tumewaorodhesha na washirika wa maendeleo ambao wametusaidia Ofisi yetu katika kufanikisha majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha, ili Ofisi yetu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu 26 Makamu wa Rais naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Sh.7,855,093,000/= fedha za Matumizi ya Kawaida na kiasi hiki kinajumuisha mishahara ya watumishi ambayo ni Sh.1,120,128,000/= na fedha za Matumizi Mengineyo ambayo ni Sh.6,734,965,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, naomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe makadirio ya matumizi ya Sh.29,066,298,442/= kwa Fungu hili. Kiasi hiki kinajumuisha Sh.9,847,374,000/= fedha za Matumizi ya Kawaida na Sh.19,218,915,442/= fedha za Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha Sh.2,759,365,000/= fedha za mishahara na Sh.7,088,009,000/= fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fedha za Matumizi Mengineyo zinajumuisha Sh.2,808,957,000/= Ruzuku ya

Mishahara ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Fedha za Ndani Sh.1,000,000,000/= na Fedha za nje Sh.18,218,915,442/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA  
RAIS MHE. JANUARY Y. MAKAMBA (MB.), WAKATI WA  
KUWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI KWA MWAKA 2019/2020 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. *Mheshimiwa Spika***, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2018/19; na Malengo ya Ofisi ya mwaka 2019/20, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2019/20.

**2. *Mheshimiwa Spika***, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka 2019/20 mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, ninamshukuru kwa dhati **Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira. Pia, ninapenda kutoa pongezi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini na thabiti. Mafanikio hayo yanajidhihirisha katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa ya maendeleo. Mafanikio hayo ni dalili tosha kuwa nchi ipo katika njia sahihi ya kufikia malengo

tuliyojiwekea katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya kuwa nchi yenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

**3. Mheshimiwa Spika**, kwa dhati ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo anayotupa katika kusimamia masuala ya Muungano na kuhifadhi Mazingira. Uongozi wake thabiti unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri inayofanywa ya kuudumisha Muungano wetu pamoja na kuhifadhi na kusimamia Mazingira. Aidha, kwa namna ya pekee ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anayofanya ya kuenzi na kuudumisha Muungano wetu.

**4. Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru na kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2019/20. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Pia ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu ya kusimamia shughuli za Muungano na Mazingira.

**5. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa Bunge lako tukufu kwa kazi nzuri ambayo limeifanya kwa kipindi cha uongozi wako. Aidha, ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa. Ninampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu.

**6. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Viwanda, Biashara na Mazingira Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq (Mb.) na Makamu wake Mhe.Kanali (Mst.) Masoud Ali Khamis (Mb.) na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.) pamoja na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2019/20.

**7. *Mheshimiwa Spika***, kwa masikitiko makubwa, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini, kwa kifo cha Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani aliyekuwa Mbunge wao kilichotokea mwezi Julai, 2018 na Mheshimiwa Kasuku Bilago aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu kilichotokea mwezi Mei, 2018. Aidha, ninatoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla kwa kuwapoteza ndugu zao na mali kutokana na ajali na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Ninaomba Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

**8. *Mheshimiwa Spika***, ninawapongeza wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa kisha kuapishwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Uadilifu wao na tabia ya kujituma na kufanya kazi kwa bidii ndio sababu kubwa ya kuwa sehemu ya wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili tukufu.

**9. *Mheshimiwa Spika***, sasa ninaomba kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka 2018/19 na malengo ya mwaka 2019/20.

## **B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/19**

### **Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka 2018/19**

**10. *Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Makamu wa Rais haina vyanzo vya mapato. Hata hivyo, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira hadi kufikia Machi, 2019 lilikuwa



limekusaya mapato ya jumla ya sh. **10,430,060,727.00** kutokana na tozo na faini.

**Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2018/19**

**11. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, jumla ya Sh. **6,485,991,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, Sh. **5,432,325,578.05** zilikuwa ni ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh. **1,053,666,000.00** zilikuwa za Mishahara. Aidha, Fungu 31 liliidhinishwa Sh. **15,065,422,523.28**. Kati ya fedha hizo Sh. **10,002,082,523.28** ni za Matumizi ya Kawaida na Sh. **5,063,340,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha fedha za mishahara kiasi cha Sh. **2,924,993,000.00** na Sh. **7,077,089,523.28** fedha za Matumizi Mengineyo. Fedha za Matumizi Mengineyo zinajumuisha Sh. **3,017,072,000.00** ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Sh. **4,060,017,523.28** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Fedha Zilizopokelewa na Kutumika Hadi Machi, 2019**

**12. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Machi 2019, jumla ya Sh. **4,572,810,578.05** zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyopo chini ya **Fungu 26**. Kati ya fedha hizo Sh. **3,911,669,578.05** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh. **661,141,000.00** kwa ajili ya Mishahara. Aidha, hadi Machi, 2019, jumla ya Sh **4,365,447,196.20** zilikuwa zimetumika. Kati ya fedha hizo kiasi Sh. **3,704,306,196.20** zilitumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh. **661,141,000.00** kwa ajili ya Mishahara.

**13. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2019 **Fungu 31** lilipokea jumla ya Sh. **7,937,894,492.78** ambayo ni sawa na asilimia 52.7 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo Sh. **5,405,152,561.18** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. **2,400,099,489.50** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kiasi cha Sh. **1,652,371,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara, Sh. **2,331,102,003.28** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Ofisi na kiasi cha Sh. **1,554,322,000.00** ni fedha za ruzuku kwa Baraza

la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC. Aidha, Ofisi imetumia jumla ya Sh. **7,266,452,050.68** sawa na asilimia 91.5 ya fedha zilizopokelewa. Kiasi hiki kinajumuisha fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida Sh. **5,405,152,561.18**. na Fedha za Miradi ya Maendeleo Sh.**1,861,299,489.5**. Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zilizotumika zinajumuisha, Sh. **2,198,459,561.18** za Matumizi Mengineyo ya Ofisi, Sh.**1,652,371,000.00** Mishahara ya Watumishi wa Ofisi na Sh. **1,554,322,000.00** ruzuku ya Mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

**14. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi - CCM (2015 – 2020); Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals – SDG 2030*); Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004; na Maelekezo na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Viongozi Wakuu wa nchi.

## MASUALA YA MUUNGANO

**15. Mheshimiwa Spika**, Muungano wetu ndio utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu. Bila Muungano hakuna Tanzania. Ili Kuenzi na kuimarisha Muungano Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu ambayo imekabidhiwa kikatiba na kisheria ya kuratibu utekelezaji wa masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Katika mwaka 2018/19, kazi zifuatazo zilitekelezwa: - Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano; Kuratibu utekelezaji wa masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa; Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya SMT na SMZ; na Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano.

**Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano**

**16. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Ofisi iliratibu na kufanya kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano tarehe 9 Februari, 2019 Jijini Dodoma. Kikao hiki kilitanguliwa na vikao vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ tarehe 6 Februari, 2019; Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ tarehe 8 Februari, 2019; na Mawaziri wa SMT na SMZ tarehe 9 Februari, 2019.

**17. Mheshimiwa Spika**, hoja zilizojadiliwa katika kikao hicho ni pamoja na: - Mapendekezo ya Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano; Mwongozo wa Ushirikishwaji wa SMZ kwenye Masuala ya Kimataifa na Kikanda; na Hoja za Fedha na Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kikao hicho kilikuwa na mafanikio yafuatayo: - Kupitishwa kwa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia Masuala ya Muungano wenye lengo la kuimarisha na kuongeza ufanisi wa vikao vya Kamati ya Pamoja ikiwa ni pamoja na kufuatilia maagizo na maelekezo yanayotolewa na Kamati hiyo. Utaratibu huo pia, umeainisha Kamati mbili ambazo ni Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala zilizopewa jukumu la kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazohitaji utatuzi wa haraka badala ya kusubiri utaratibu wa kawaida wa vikao vya Kamati ya Pamoja vya SMT na SMZ. Kamati hizo zitawasilisha taarifa za utekelezaji katika vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ.

**18. Mheshimiwa Spika**, katika Kikao hicho pia ulipitishwa Mwongozo Kuhusu Ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda. Mwongozo huo umezingatia maeneo ya mikutano ya kimataifa na kikanda, nafasi za masomo ya elimu ya juu na mafunzo mengine nje ya nchi na utafutaji wa fedha za misaada na mikopo ya kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo.

**19. Mheshimiwa Spika**, changamoto ya ongezeko la Gharama za Umeme kutoka TANESCO kwenda ZECO

ilipatiwa ufumbuzi ambapo imekubalika kuwa, kodi ya ongezeko la thamani (*Value Added Tax-VAT*) itatozwa kwa kiwango cha asilimia sifuri (0%) kwenye umeme unaouzwa na TANESCO. Vilevile, malimbikizo ya deni la VAT lililokuwa limefikia Sh. Bilioni **22.9** kwa shirika la ZECO kwenye umeme uliouzwa na TANESCO limefutwa.

**20. Mheshimiwa Spika**, kikao cha Kamati ya Pamoja pia kilijadili na kuzipatia ufumbuzi hoja za biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ambazo ni: - Gharama za kushusha mizigo (*landing fees*); Viwanda vya Zanzibar kupata leseni kutoka Wakala wa Usajili na Utoaji Leseni za Biashara (*Business Registrations Licensing Agency-BRELA*); na Upatikanaji wa fursa za ushiriki katika miradi ya maendeleo ya viwango na ubora wa bidhaa na maendeleo ya wajasiriamali.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba akihutubia wakati wa kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Februari 9, 2019 katika ukumbi wa Kamarage, jengo la Hazina Square, Dodoma.*

**Uratibu wa Masuala ya Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa**

**i. Gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

**21. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kupata gawio la asilimia 4.5 ya fedha za Misaada ya Kibajeti (*Government Budget Support - GBS*); faida ya Benki Kuu; Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo; na kodi ya mapato yatokanayo na ajira (*Pay As You*

*Earn – PAYE*). Hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya Sh. bilioni **36.79** zimepelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni **14.00** ni *PAYE*, Sh. bilioni **1.4** ni fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Sh. bilioni **5.64** ni fedha za Misaada ya Kibajeti (*GBS*) na Sh. bilioni **15.75** ni gawio la Benki Kuu.

ii. **Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Zanzibar**

**22.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Ofisi imefanya ufuatiliaji wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 16 kati ya 32 yaliyopo Unguja, Zanzibar. Majimbo hayo ni Nungwi, Mkwajuni, Chani, Donge, Mahonda, Bumbwini, Mfenesini, Bububu, Welezo, Mwera, Fuoni, Kijitoupele, Mwanakwerekwe, Kiembesamaki, Paje na Makunduchi. Matokeo ya ufuatiliaji huo yanaonesha kuwa, miradi mingi ikiwemo ya maji na umeme inakidhi mahitaji kwa kuongeza huduma muhimu za kijamii na hivyo kuboresha maisha ya wananchi.



*Ujenzi wa minara minne (4) na matenki manne (4) na mabomba katika maeneo ya Magogoni na Mikarafuni-Unguja*

iii. **Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**23.** *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuwawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi

na programu za maendeleo. Miradi na Programu hizo zimefanikiwa kuinua hali ya wananchi, kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii wa pande zote mbili za Muungano. Miradi hiyo hufadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Katika mwaka 2018/19 utekelezaji wa Miradi na Programu hizo ni kama ifuatavyo: -

**a) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund - TASAF*)**

**24. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, *TASAF III* imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa kunusuru Kaya Maskini Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Programu zilizotekelezwa ni:- kutengeneza na kuboresha Mifumo ya kutambua, kuandikisha na kutunza kumbukumbu za Walengwa; Uhawilishaji ruzuku kwa kaya maskini; Uandikishaji na utoaji ajira za muda ili kuongeza kipato kwa kaya maskini; na uwekezaji wa miradi ya kukuza uchumi wa kaya. Aidha, *TASAF III* imeendelea kujenga uwezo wa viongozi, watendaji na wasimamizi wa Mipango katika maeneo yote ya utekelezaji. Katika mwaka 2018/19 kiasi cha Sh. **305,337,803,999.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza programu za mradi. Hadi kufikia Machi, 2019 Sh. **125,795,098,700.00** zilitumika kwa upande wa Tanzania Bara na Sh. **3,512,043,950.00** kwa Tanzania Zanzibar.

**b) Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (*Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance - MIVARF*)**

**25. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, *MIVARF* imeendelea na mpango wa kupunguza umaskini na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kuwezesha kaya za vijijini kuongeza kipato na usalama wa chakula. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wazalishaji na kuwaunganisha na masoko ya mazao na taasisi za fedha. Katika mwaka 2018/19 Sh. **22,912,124,648.00** ziliidhinishwa na hadi kufikia Machi, 2019 kiasi cha Sh. **10,278,334,000.00**

zilitumika Tanzania Bara na Sh. **1,150,504,026.00** Tanzania Zanzibar.

c) **Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**26. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 kazi mbalimbali za kurasimisha rasilimali ardhi na biashara zinazomilikiwa na wananchi ili waweze kuzitumia kupunguza umaskini na hatimaye kuchangia Pato la Taifa kazi zilifanyika. Kazi hizo ni pamoja na; Kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya kisheria na kitaasisi; Kusimamia na kuratibu shughuli za urasimishaji; Kujenga uwezo wa urasimishaji biashara na uanzishwaji wa vituo vya biashara; Kujenga uwezo wa urasimishaji Ardhi Mjini; Kujenga uwezo wa urasimishaji Ardhi Vijijini; na kukamilisha ujenzi wa Masjala za Ardhi. Jumla ya Sh. **1,411,694,987.00** zilizidhinishwa kwa mwaka 2018/19. Hadi kufikia Machi, 2019 Sh. **288,252,127.00** zilitumika Tanzania Bara na Sh. **69,843,000.00** Tanzania Zanzibar.

d) **Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Uzalishaji wa Chakula (Land Degradation and Food Security- LDFS)**

**27. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environment Facility* - GEF) kupitia Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (*International Fund for Agriculture Development* - IFAD). Thamani ya mradi ni dola za Marekani milioni **50** ambapo dola za Marekani milioni **7.156** zinatoka GEF na mchango wa nchi (*in-kind*) ni kiasi cha dola za Marekani milioni **42.94**. Fedha zinazotolewa na GEF zinalenga kuchangia katika kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, na Hifadhi ya Bioanuai na Usimamizi Endelevu wa Ardhi. Mradi wa LDFS utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia Julai, 2017 hadi Septemba, 2022. Mradi huu utatekelezwa katika maeneo yenye changamoto za ukame katikati ya nchi na pwani ambayo ni Kata ya Haubi katika Halmashauri ya Kondo, Mkoani Dodoma; Kata ya Sigili katika Halmashauri ya Nzega, Mkoani Tabora; Kata ya Mpambala Halmashauri ya Mkalama, Mkoani Singida; Kata ya Sukuma, katika Halmashauri ya Magu Mkoani Mwanza na Shehia 8 katika

Wilaya ya Micheweni, Kaskazini Pemba. Jumla ya Sh. **1,230,033,688.96** ziliidhinishwa katika mwaka 2018/19. Hadi kufikia Machi, 2019 kiasi cha Sh. **667,907,922.17** kilitumika Tanzania Bara na kiasi cha Sh. **158,583,866.70** kwa upande wa Zanzibar.



*Sehemu ya miche ya Mikoko iliyopandwa katika ufukwe wa eneo la Kisiwa-Panza, Mjini Pemba*

e) **Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (Expanded Rice Production Project - ERPP)**

**28. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unachangia utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo Tanzania (Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan - TAFSIP) chini ya Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP). Kwa upande wa Tanzania Bara, mradi unatekelezwa katika Halmashauri za Mvomero, Kilosa na Kilombero Mkoani Morogoro na kwa upande wa Zanzibar unatekelezwa Kibonde Mzungu, Mtwango, Koani, Mchangani, Bandamaji (Unguja); na Machigini, Kwalempona, Ole, Dobi – 1 na Dobi – 2 (Pemba). Katika mwaka 2018/19 jumla ya Sh. **22,731,651,587.00** ziliidhinishwa ili kutekeleza kazi za mradi huu. Hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya Sh. **728,072,250.00** zilitolewa na kutumika Tanzania Bara na kiasi cha Sh. **227,860,253.00** Tanzania Zanzibar.

**Uratibu wa Masuala Yasiyo ya Muungano Kati ya SMT na SMZ**

**29. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar imeendelea kuhamasisha Sekta zisizo za Muungano za SMT



na SMZ kukutana na kujadili masuala yanayohusu Sekta zao, kubadilishana utaalum na wataalam ili kuleta ufanisi na uwiano wa maendeleo kwa pande mbili za Muungano. Katika kipindi hiki vikao tisa (9) vimefanyika katika Sekta ya Serikali za Mitaa, Elimu, Maji, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ardhi, Nishati, Fedha na Mipango na Uchukuzi.

### **Elimu ya Muungano kwa Umma**

**30.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Ofisi imeendelea kuelimisha Umma kuhusu umuhimu na faida zinazotokana na Muungano kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, televisheni na magazeti. Ofisi pia, ilitoa elimu ya Muungano kwa Maafisa Viungo (*Focal Persons*) kutoka Wizara za SMT katika kikao kilichofanyika tarehe 18 Oktoba, 2018, Dodoma.

### **HIFADHI ENDELEU YA MAZINGIRA**

**31.** *Mheshimiwa Spika*, Sekta zote za uzalishaji mali zinategemea mazingira na hivyo kufanya sekta hii kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi. Uwepo wa rasilimali kwa ajili ya mahitaji ya sasa na vizazi vijavyo utategemea namna uhifadhi wa mazingira unavyozingatiwa. Shughuli zisizo endelevu zinachangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa mazingira na kusababisha; Uharibifu wa ardhi; Ukosefu wa maji safi na salama kwa wananchi wa mijini na vijijini; Uchafuzi wa mazingira; Upotevu wa bioanuai na makazi; Uharibifu wa mifumo ikolojia ya majini; Uharibifu wa misitu; Mabadiliko ya tabianchi; Kuongezeka kwa Viumbe Vamizi; Kuongezeka kwa Taka za Kielektroniki; Kuongezeka kwa taka za kemikali; Kuwepo kwa uchafuzi utokanao na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi; na Kukosekana udhibiti wa mazao yatokanayo na Teknolojia ya uhandisi jeni.

**32.** *Mheshimiwa Spika*, katika miaka ya hivi karibuni, imedhihirika kuwa mazingira yetu si salama kutokana na kasi ya uharibifu wa mazingira unaoshuhudiwa katika sehemu mbalimbali za nchi. Ushahidi huo ni pamoja na kuongezeka kwa hali ya jangwa na ukame, mafuriko, kuongezeka kwa

magonjwa ya kuambukiza na mabadiliko ya hali ya hewa, kasi ya ukataji miti, kuongezeka kwa Viumbe Vamizi na kuongezeka kwa matumizi ya zebaki katika Sekta ya madini hususan wachimbaji wadogo wa dhahabu. Maendeleo endelevu hayawezi kupatikana bila kutunza mazingira. Pamoja na Serikali kuchukua jitihada kubwa katika utunzaji na usimamizi wa mazingira, hali ya mazingira nchini bado si ya kuridhisha.

**33. *Mheshimiwa Spika***, hali hiyo inachangiwa na changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii ikiwemo: uhaba wa rasilimali fedha, uhaba wa rasilimali watu wa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 katika ngazi zote; uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu na wajibu wa kuhifadhi mazingira; kutokuwa na takwimu sahihi za mazingira kwa wakati; kutokutengwa kwa maeneo maalum ya kutupa taka; na utegemezi wa nishati ya kuni na mkaa.

**34. *Mheshimiwa Spika***, katika kulinda na kuhifadhi mazingira ya nchi yetu na kukabiliana na changamoto za mazingira nchini, Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na mikataba ya kimataifa ya mazingira pamoja na utoaji wa elimu kuhusu mazingira. Katika kutekeleza azma hiyo kwa mwaka 2018/19 yafuatayo yamefanyika; -

#### **Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na Mkakati wa Utekelezaji**

**35. *Mheshimiwa Spika***, mwaka jana niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi inaendelea na hatua za kuboresha Sera ya Mazingira ya Taifa ya Mwaka 1997 na Mkakati wa utekelezaji. Aidha, katika mwaka 2018/19 rasimu ilijadiliwa katika ngazi ya Sekretariati ya Baraza la Mawaziri. Kwa kuwa Sera hii ni mtambuka pamoja na maoni mengine ushauri uliotolewa na Sekretarieti ilikubaliwa kupata maoni zaidi kutoka kwa wadau. Kazi hiyo imefanyika na baada ya kujiridhisha kuwa maoni ya wadau yamezingatiwa Rasimu ya Sera itajadiliwa katika ngazi inayofuata ambayo ni kikao cha Makatibu Wakuu (*Inter - Ministerial Technical Committee - IMTC*).

### **Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191**

**36.** *Mheshimiwa Spika*, Ofisi inaratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ambayo ilitungwa mwaka 2004. Katika kipindi cha utekelezaji wa Sheria hii changamoto kadhaa zimejitokeza ikiwemo kutoandaliwa kwa baadhi ya Kanuni na Miongozo; uwezo mdogo wa Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria ikiwemo Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na uelewa mdogo kuhusu wajibu na majukumu ya wadau katika utekelezaji wa Sheria hii. Ili kukabiliana na changamoto zipo juhudi mbalimbali ambazo ofisi imepanga kuchukua ikiwa ni pamoja na kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden. Mradi huu una thamani ya Dola za Marekani Milioni tatu (3) na utatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu (2019/20 -2021/22). Baadhi ya shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuandaa Kanuni na Miongozo; kuendesha mafunzo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara za Kisekta; na kuanzisha mfumo wa utoaji vyeti na leseni za mazingira kwa njia ya mtandao. Hadi kufikia sasa, Ofisi imeratibu uteuzi wa Wakaguzi wa Mazingira wapatao 487 watakaosaidia kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya usimamizi wa mazingira katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

### **Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira**

**37.** *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imekamilisha Mwongozo wa kushiriki Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Mazingira. Awali Tuzo hii ilihusu masuala ya kupanda na kutunza miti na kuhifadhi vyanzo vya maji pekee. Maboresho ya tuzo yamefanyika ili kuwa na mtazamo mpana wa hifadhi ya mazingira. Maboresho hayo yameongeza masuala yafuatayo: - Uzalishaji endelevu viwandani, matumizi ya nishati mbadala, uchimbaji madini endelevu, kilimo na ufugaji endelevu, usimamizi wa taka, afya na usafi wa mazingira.

### **Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini**

**38.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi imekamilisha rasimu ya Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira nchini na sasa kinachofanyika ni kupitisha rasimu hiyo katika ngazi mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja

na Kamati ya Mazingira ya Baraza la Mawaziri kabla ya kuwasilishwa Bungeni ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 Kifungu 175 (1).

### **Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira**

**39.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Ofisi ilianisha mapendekezo ya maeneo ya kufanyiwa marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 ili kuwezesha Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa kuwa Sera ya Taifa ya Mazingira (1997) inafanyiwa maboresho, kipaumbele ni kukamilisha Sera ili maeneo yote yatakayohitaji maboresho kwenye Sheria yafanyike kwa pamoja. Ni matarajio yetu kuwa Maboresho ya Sera pamoja na Sheria yatasaidia kwa kiasi kikubwa juhudi za Serikali kusimamia masuala ya mazingira nchini na hivyo kuwa na maendeleo endelevu.

### **Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani**

**40.** *Mheshimiwa Spika*, Dunia huadhimisha Siku ya Mazingira tarehe 5 Juni kila mwaka ili kutoa hamasa kwa watu kutunza mazingira. Kitaifa, maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kwa mwaka 2018 yalifanyika Mkoani Dar es Salaam katika viwanja vya Mnazi mmoja. Serikali iliamua Mkoa wa Dar es Salaam uwe mwenyeji wa Maadhimisho haya kwa lengo la kuwapa fursa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam kuelimishwa na kuhamasishwa kupambana na changamoto za uharibifu wa mazingira unaolikumba Jiji la Dar es Salaam, kama vile: -mafuriko; uchafuzi wa mazingira utokanao na mifuko ya plastiki; kubomoka kwa kuta na kingo za fukwe za bahari ya Hindi; pamoja na utumiaji wa kiasi kikubwa cha nishati ya mkaa.

**41.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka huu Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Kimataifa yatafanyika nchini China katika mji wa Hangzhou kaulimbiu ikiwa ni Uchafuzi wa Hewa (*Air Pollution*). Kitaifa maadhimisho haya yatafanyika Mkoani Mwanza. Uteuzi wa Mkoa wa Mwanza umezingatia changamoto zinazolikabili jiji hili ikiwa ni pamoja na uwepo wa uharibifu wa ardhi katika Bonde la Ziwa Victoria pamoja na uharibifu wa mazingira ya ndani ya Ziwa hilo

unaosababishwa na shughuli za kijamii na kiuchumi. Kufanyika kwa maadhimisho ya kitaifa Mkoani humo kutatoa fursa kwa wananchi wa Mkoa huo na Mikoa jirani kuelimishwa na kuhamasishwa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Victoria pamoja na mazingira yake.

### **Kupunguza Matumizi ya Mkaa Unaotokana na Miti**

**42. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na jitihada za kupunguza matumizi ya mkaa unaotokana na miti kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali kuandaa mipango kazi kwa kila Taasisi ya kupunguza matumizi ya mkaa unaotokana na miti. Aidha, Ofisi imeendelea kushirikiana na wadau wa mazingira kutoa mafunzo kwa washindi wa Tuzo ya Teknolojia ya Mkaa Mbadala kwa lengo la kukuza teknolojia na ubunifu wao ili bidhaa zao ziweze kuwa za kiwango kinachokubalika kitaalam na kibiashara na hatimaye kuwafikia wananchi wengi.



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi Bw. Leonard Kushoka mfano wa hundi yenye thamani ya shilingi za kitanzania milioni 300 mara baada ya kuibuka mshindi wa shindano la teknolojia ya nishati mbadala wa mkaa mwaka 2018***

## Matumizi ya Mifuko ya Plastiki

**43.** *Mheshimiwa Spika*, ili kutimiza azma ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki Ofisi ilihamasisha wajasiriamali na wawekezaji kuwekeza katika uzalishaji wa mifuko mbadala ikiwemo vikapu vya asili, mifuko ya karatasi na nguo ili kutumia fursa hiyo kukidhi mahitaji ya soko. Kampeni za uhamasishaji zilifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza kwa lengo la kuwatambua wadau wanaozalisha mifuko mbadala na kupata maoni kuhusu namna ya kujenga mazingira wezeshi kwa wadau kuwekeza zaidi katika uzalishaji wa mifuko mbadala.

**44.** *Mheshimiwa Spika*, kufuatia tamko la Serikali la kupiga marufuku uzalishaji, uingizaji, uuzaji, usambazaji na utumiaji wa mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 01 Juni, 2019, Ofisi imeandaa kanuni zitakazochapishwa katika Gazeti la Serikali chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na kutoa adhabu kwa kila mtu atakayekiuka matakwa ya Kanuni. Vilevile, Ofisi imeunda Kikosi Kazi cha Taifa kwa ajili ya kusimamia uzingatiaji wa Kanuni. Kikosi kazi hicho kinahusisha wajumbe kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege, Shirika la Viwango Tanzania, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**45.** *Mheshimiwa Spika*, katika kikao na wawekezaji wa mifuko mbadala kilichofanyika tarehe 15 Aprili, 2019 wamenihakikishia kuwa wana uwezo wa kuzalisha mifuko mbadala kukidhi mahitaji ya nchi. Aidha, Ofisi itaendelea kuhamasisha umma juu ya jambo hili ili liweze kuzingatiwa. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono jitihada hizi kwa mustakabali wa nchi yetu.



***Kikao cha Wadau wa Mifuko mbadala ya Plastiki kilichofanyika jijini Mwanza***

**Kuokoa Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu**

**46.** *Mheshimiwa Spika*, katika kunusuru Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu, kwa mwaka 2018/19, Wizara na Mikoa husika imetekeleza majukumu yake ya kulinda ikolojia ya bonde hili ambapo jumla ya vyanzo vya maji 5,373 katika mikoa saba vilitambuliwa na kati ya hivyo, vyanzo 652 viliwekewa mipaka ya kudumu; jumla ya kaya 1,218 kutoka Mikoa ya Iringa na Njombe zilizovamia maeneo ya hifadhi ziliondolewa, baiskeli 18 zilikamatwa na kiasi cha Sh. **98,994,000.00** kilikusanywa kama faini kutokana na makosa ya uharibifu wa mazingira kwa Mkoa wa Tabora. Vilevile, jumla ya mifugo 4,303 ikiwemo ngombe, mbuzi na kondoo kwa Mikoa ya Iringa na Tabora ilikamatwa, mabanio yapatayo 7 yasiyo katika ubora yalivunjwa, madaraja 3 ya kienyeji ya kuchepusha maji yalibomolewa na matanuru makubwa 6 ya mkaa yalibomolewa.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan (katikati), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Mhandisi Joseph Malongo wakipitia taarifa ya maendeleo ya kikosi kazi cha kuokoa mfumo-ikolojia wa bonde la mto Ruaha Mkuu*

**47. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha hifadhi na usimamizi wa ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu, TANAPA imeweka vigingi vikubwa (*beacons*) 52 na vigingi vidogo (*intermediate beacons*) 357 ili kuimarisha mipaka. Aidha, NEMC, Tume ya Umwagiliaji (*NIRC*) na Mamlaka ya Bonde la Rufiji wameainisha mipaka kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 28 la terehe 14 Machi, 2008 na kupokea maoni ya wananchi kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya mipaka kwa GN. Na. 28 la terehe 14 Machi, 2008. Katika Mkoa wa Iringa Vijiji 58 na Mkoa wa Mbeya Vijiji 20 viliwezesha kuandaa na kusimamia Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Aidha, miradi mikubwa nane (8) ya umwagiliaji imebainika kuanzishwa bila kufanya Tathimini ya Athari kwa Mazingira. Miradi hiyo ni MAMCOS, Mwashikamile, Nguvu Kazi, Mnazi, Kapunga Small Holder, Igowole, Bwawa la Lwanyo na Mwendamtitu. Miradi yote imepewa amri ya kufanya Ukaguzi wa Mazingira (*Environmental Audit*); Tathmini imefanyika kwenye Mito ya



Mswiswi na Chimala Wilayani Mbarali na jumla ya vibali 15 vimefanyiwa mapitio; Tathimini ya Mazingira Kimkakati (TMK) ilifanyika kwa Bonde zima la Mto Rufiji; na kazi ya kupitia vibali vya watumia maji 20 katika Mito ya Mbarali na Mswiswi limefanyika na wahusika wote 20 wamepewa notisi ili wajenge miundombinu sahihi kuzuia upotevu wa maji.

### **Kutangaza Maeneo ya Mazingira – Lindwa na Nyeti**

**48. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira hatua za makusudi za kushirikisha wananchi pamoja na viongozi wao katika kujadili na kuamua maeneo yanayopendekezwa kuwa maeneo Lindwa au Nyeti ya Mazingira. Katika mwaka 2018/19 Serikali kwa kushirikiana na wadau hao imeandaa orodha ya maeneo Nyeti hapa nchini; Kutathmini hali ya maeneo hayo na kuandaa taarifa za awali; Kuunda Kamati ya Kitaifa ya kuanzisha Maeneo Lindwa au Nyeti; na Kuandaa vigezo vya kubainisha na kuanzisha maeneo Lindwa ya mazingira nchini. Aidha, Serikali inafanya tathmini ya hali ya Milima na Vilima hapa nchini ili kufuatilia na kutathmini mabadiliko yake. Hatua hii inajumuisha ukusanyaji wa takwimu za mifumo ikolojia.

### **Mpango Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Viumbe Vamizi (Invasive Species)**

**49. Mheshimiwa Spika,** Viumbe Vamizi ni changamoto kubwa na mpya ya mazingira nchini. Viumbe hawa husababisha athari kubwa katika uchumi hususan katika sekta kuu za uzalishaji kama vile, kilimo, uvuvi, mifugo, maji, maliasili na utalii na hivyo kuathiri ajira na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Pia huathiri afya ya binadamu, mifugo pamoja na mazingira kwa kuharibu mifumo ikolojia. Tafiti zinaonesha kuna takriban aina 220 ya Viumbe Vamizi nchini na Tanzania imeathirika zaidi ya nchi nyingine katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Kwa kuzingatia hali hiyo hatua za haraka zisipochukuliwa kuwadhibiti, uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi utaendelea kuathirika kwa kasi kubwa.

**50. Mheshimiwa Spika,** Ili kukabiliana na athari hizo katika mwaka 2018/19, Ofisi iliunda Kikosi Kazi cha Kitaifa kwa ajili ya kuandaa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Viumbe Vamizi.

Mkakati huo utasaidia kudhibiti kuongezeka na kusambaa kwa viumbe hawa nchini ambao ni tishio kubwa kwa bioanuai. Mpango Mkakati huo umebainisha hatua za kuchukua ili kukabiliana na changamoto hii pamoja na kuainisha majukumu ya kila Sekta husika. Mkakati huu utajadiliwa katika kikao cha Kamati ya Mazingira ya Baraza la Mawaziri ili kuwa na uelewa wa pamoja wa majukumu ya Serikali na wadau katika utekelezaji wa mkakati huo.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa kikosi kazi cha Kuandaa Mkakati wa kutatua changamoto za viumbe vamizi nchini mara baada ya uzinduzi uliofanyika kwenye Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam*

### **Kampeni ya Upandaji miti**

**51.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Mkakati wa Taifa wa Upandaji wa Miti ( 2016 – 2021) umeendelea kutekelezwa. Hata hivyo, utekelezaji wake umekumbwa na changamoto ya upatikanaji wa rasilimali fedha. Changamoto nyingine ni pamoja na: uwasilishwaji wa takwimu zisizo akisi hali halisi ya upandaji na utunzaji miti katika Halmashauri za Wilaya; Ufuatiliaji na utunzaji hafifu wa miti

iliyopandwa; na upandaji wa miti isiyo rafiki kuendana na eneo husika. Ili kuimarisha utekelezaji wa Mkakati huo Serikali inaandaa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kutafuta namna bora ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati huo.

### **Udhibiti wa Taka Ngumu Nchini**

**52. *Mheshimiwa Spika***, uchafuzi wa mazingira utokanao na taka ngumu umeendelea kuwa changamoto katika maeneo ya mijini. Hii inachangiwa na uwezo mdogo wa Mamlaka za Serikali za Mtaa na miundombinu hafifu ya usimamizi wa taka za aina hii. Katika mwaka 2018/19, Ofisi imeandaa Mwongozo wa Uwekezaji katika Taka Ngumu ili kuhamasisha uwekezaji na kuongeza jitihada za kuboresha usimamizi wa taka hapa nchini. Mwongozo huo umeainisha fursa za uwekezaji zilizopo na taratibu za kuomba vibali na leseni. Baadhi ya fursa zilizopo ni pamoja na ukusanyaji na usafirishaji wa taka ngumu; urejelezaji wa taka; viwanda vya uzalishaji mboji; uzalishaji wa umeme kutokana na taka ngumu; ujenzi na uendeshaji wa madampo ya kisasa na mitambo ya kutibu majitaka; na uteketezaji wa taka hatarishi.

**53. *Mheshimiwa Spika***, shughuli hizi zinafanyika katika maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, hivyo jukumu la usimamizi na udhibiti wa taka ngumu katika maeneo hayo ni la TAMISEMI. Hivyo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina jukumu la muhimu sana kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo huo ili kuleta ufanisi.



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mussa Sima (mwenye kofia) akikagua dampo la Halmashauri ya Mji wa Njombe katika ziara iliyofanyika katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.*

## **Usimamizi wa Taka Zenye Madhara**

**54. *Mheshimiwa Spika***, taka hatarishi zinazalishwa viwandani, migodini, hospitalini na baadhi ya maeneo ya biashara. Ofisi imeendelea kudhibiti uzalishaji na utupaji wa taka zenye madhara kwa mujibu wa Kanuni za Udhhibiti wa Taka zenye Madhara za mwaka 2009. Aidha, Serikali inapitia utaratibu wa kusimamia taka zenye madhara kwa lengo la kuziboresha ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kudhibiti usafirishaji wa vyuma chakavu nje ya nchi. Vile vile, Serikali imeimarisha udhibiti katika vituo vya forodha pamoja na kuimarisha ushirikiano na Taasisi zenye dhamana. Lengo ni kupunguza na kuondoa biashara holela ya vyuma chakavu inayochangia kuhujumu na kuharibu miundombinu. Aidha, kwa kushirikiana na maafisa mazingira wa Halmashauri na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imeendelea kutoa vibali vya kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha na kurejeleza taka kwa kampuni zilizokidhi vigezo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 vibali 87 kati ya maombi 107 vimetolewa.

## **Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK)**

**55. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Ofisi imeandaa Mwongozo wa ufundishaji kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wadau katika kutumia Mwongozo wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati. Mwongozo huo umetafsiriwa katika lugha ya kiswahili ili kujenga uelewa kwa wadau wengi. Mwongozo huu una lengo la kuwezesha Mipango, Mikakati, Sera, na Miradi Mikubwa kufanyiwa Tathmini ya Mazingira Kimkakati ili kuhakikisha kuwa uchumi wa viwanda unakua katika hali endelevu.

**56. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19 Ofisi imesajili mipango saba (7) ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati ambayo ripoti zake zimekamiliika na nyingine zinaendelea kuandaliwa na ziko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Mipango iliyosajiliwa na kupata idhini ni:- Mradi wa kufua Umeme wa Rufiji (*Rufiji Hydropower Project*); Uboreshaji wa Mpango kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (*Updating National Irrigation Master Plan*); Mpango Kabambe wa Usafiri katika Jiji la Dar es Salaam, (*Dar es Salaam Transport Master Plan*); na Sera, Mikakati, Sheria na kanuni za Uvuvi wa Bahari

Kuu (*Policy for Deep Sea Fisheries; Policy Implementation Strategy; Deep Sea Fishing Authority Act; and Deep Sea Fishing Authority Regulations*); Aidha, Mipango iliyosajiliwa ambayo ipo katika mchakato wa kukamilisha tathimini na kupatiwa idhini ni:- Mpango Kabambe wa Mji wa Serikali (*Government City Master Plan*); Mpango Kabambe wa Mafuta na Gesi (*Oil and Gas Master Plan*); na Mpango Kabambe wa eneo la Viwanda Handeni (*Handeni Industrial Park Limited, Master Plan*).

**Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Environmental Facility*)**

**57. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira wa Dunia hapa nchini kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi mitatu iliyopata ufadhili kutoka GEF ambayo ni Mradi wa Kukabiliana na Ujangili Nchini (*Combating Poaching and Illegal Wildlife Trade in Tanzania Through Integrated Approach*) unaotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii; Mradi wa kuzuia Uharibifu wa Ardhi na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame ya Nyanda za Kati (*Reversing Land Degradation Trends and Increasing Food Security in Degraded Ecosystems of Semi-arid Areas of Central Tanzania*) unaotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais; na Mradi wa Kukuza Matumizi ya *Bio-Ethanol* kama Nishati Mbadala kwa Kupikia (*Promotion of Bio-Ethanol as Alternative Clean Fuel for Cooking in the United Republic of Tanzania*) ambao unatekelezwa na Wizara ya Nishati.

**58. Mheshimiwa Spika**, Ofisi kwa kushirikiana na wadau imeandaa miradi mitano (5) na kuiwasilisha katika Sekretarieti ya GEF kwa ajili ya kupata ufadhili chini ya Awamu ya Saba ya mfuko huo (*GEF – 7th Replenishment Cycle*). Katika awamu hii Tanzania imetengewa fedha kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 24 ambazo zitatumika katika kuandaa na kutekeleza miradi inayolenga kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia vipaumbele vya nchi pamoja na matakwa ya Mikataba ya Kimataifa inayohusu mazingira ambayo nchi yetu ni mwanachama. Miradi iliyowasilishwa ni pamoja na: Programu ya Hifadhi Endelevu ya Ziwa Tanganyika (*The Lake Tanganyika Regional Environmental Programme*); *Integrated Land Use*

*and Restoration Program for Tanzania's Productive Forest Landscape; Integrated Land Cape Management in the Dry Miombo Woodlands in Tanzania; Sustainable Cities Programme; na Programu ya Ufadhili wa Miradi Midogo (GEF Small Grants Programme).*

**Uratibu na Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda ya Mazingira**

**59.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na Wadau wa Maendeleo imeratibu na kutekeleza Mikataba ya mazingira ya Kimataifa na Kikanda. Mikataba hiyo ni:-

**Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto**

**60.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Ofisi imeratibu utekelezaji wa miradi minne mikubwa ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Miradi hiyo ni:- Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi; Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Jiji la Dar es Salaam; Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Hifadhi ya Ikolojia (*Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience*; na Mradi wa Kupunguza Uharibifu wa Ardhi na Kuboresha Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame Nchini (*Reversing Land Degradation Trends and Increasing Food Security in Degraded Ecosystem of Semi Arid Areas of Tanzania-LDCFS*).

**61.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi. Kupitia mradi huu ukuta wa Mto Pangani Tanga umeendelea kujengwa hadi kufikia mita 795 kati ya mita 950 zilizopangwa kujengwa. Lengo la ujenzi huu ni kukabiliana na mmomonyoko wa fukwe utokanao na kuongezeka kwa kina cha bahari (*sea level rise*). Aidha, mikoko imepandwa katika Wilaya ya Kibiti (hekta 208). Vilevile, miundombinu ya kuvuna maji ya mvua imejengwa katika Shule za Sekondari Kingani na Matipwili katika Wilaya ya Bagamoyo. Kazi nyingine zilizofanyika ni ujenzi wa matanki 10 ya kuhifadhi maji ya visima ya ujazo wa lita 15,000 kila moja.

**62. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Ofisi imeendelea kutekeleza mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Jiji la Dar es Salaam. Kupitia mradi huu ujenzi wa mfereji wenye urefu wa mita 550 katika eneo la Mtoni, Temeke, Dar es Salaam uliobomolewa na mvua kubwa mwezi Aprili, 2018 ulijengwa upya na kukamilika; miche ya mikoko ilipandwa kwa ajili ya kuziba mapengo yaliyojitokeza katika eneo la Mbweni na Kigamboni; na Tathmini ya Mwisho ya Mradi na Ukaguzi wa mradi ulifanyika.

**63. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ilianza utekelezaji wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Vijijini kupitia Mfumo Ikolojia (*Ecosystem-Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania*). Mradi huu ni wa miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2018 hadi 2022 na unafadhiliwa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa nchi Masikini (*Least Developed Countries Fund – LDCF*) kupitia Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environment Facility – GEF*). Mradi unatekelezwa katika Wilaya nne (4) Tanzania Bara na Wilaya moja (1) Tanzania Zanzibar. Wilaya hizo na Mikoa yake ni pamoja na: Mpwapwa (Dodoma), Kishapu (Shinyanga), Simanjiro (Manyara), Mvomero (Morogoro) na Kaskazini A Unguja (Kaskazini Unguja).

**64. Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kuongeza uhimilivu wa kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi kupitia mifumo ikolojia katika maeneo ya vijijini. Kufikiwa kwa lengo hili kutachangia katika kupunguza hatari za athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii zinazoishi vijijini. Kupitia uboreshaji wa mifumo ikolojia, mradi utachangia pia katika kuongeza uzalishaji wa chakula, kuboresha ufugaji na kuboresha uhifadhi wa mazingira katika Wilaya husika za mradi. Mradi utawanufaisha wananchi wapatao 1,468,035 katika Kaya 298,631 katika Wilaya zinazotekeleza mradi. Mradi utaongoa hekari 9,200, kati ya hizo hekari 3,000 ni maeneo ya vyanzo vya maji (*watershed*) na maeneo ya misitu yaliyoharibika; hekari 6,000 zitaongolewa na kutumika katika kuboresha nyanda za malisho (*rangeland rehabilitation*) kwa ajili ya mifugo; na hekari 200 zitaongolewa katika maeneo yaliyoko kando ya Mito iliyoharibiwa (*riverbank rehabilitation*).

Aidha, mradi unatarajia kuendesha Kilimo Rafiki kwa Hali ya Hewa (*Climate Smart Agriculture – CSA*) ambacho kitafanyika katika Vijiji vinavyotekeleza kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi.

**Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame**

**65. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu inakabiliwa na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame katika maeneo mengi. Suala hili kwa sasa linachochea zaidi na janga la Mabadiliko ya Tabianchi. Katika kipindi cha mwaka 2018/19, Ofisi imeratibu maandalizi ya Programu ya Kitaifa yenye madhumuni ya kufanya tathmini ya maeneo yaliyoathirika ili kuweka shabaha ya kuzuia uharibifu wa ardhi (*Land Degradation Neutrality Target Setting*) ifikapo mwaka 2030 katika kutekeleza maazimio ya nchi wanachama. Uandaaji wa shabaha hizi ni mojawapo ya utekelezaji wa Makubaliano ya Mkutano wa Kumi na Mbili wa Nchi Wanachama wa Mkataba uliofanyika Jijini Ankara nchini Uturuki mwaka 2015.

**66. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Ofisi ilianza utekelezaji wa Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na Kuongeza Uhakika na Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Pwani ya Tanzania kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Environment Facility - GEF*) kupitia Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (*International Fund for Agricultural Development - IFAD*). Lengo la mradi huu ni kuboresha mifumo ya Ikolojia ya Kilimo ambayo itawezesha kuongeza uzalishaji wa chakula na kuchangia kuboresha Mazingira katika Wilaya husika za mradi. Madi huu unatekelezwa katika Vijiji ishirini na tano (25) katika Kata sita (6) Wilaya tano (5) na Mikoa mitano (5) kama ifuatavyo: - Mkoa wa Tabora ni vijiji vya Lyamalagwa, Sigili, Bulambuka, Iboja na Bulende vilivyoko kata ya Sigili, Wilaya ya Nzega. Mkoa wa Mwanza ni vijiji vya Lumeji, Iseni na Nyang’hanga vilivyoko kata ya Sukuma, Wilaya ya Magu. Mkoa wa Singida ni vijiji vya Mpambala, Nyahaa, Lugongo, Mkiko na Munguli vilivyoko kata ya Mpambala, Wilaya ya Mkalama. Mkoa wa Dodoma ni vijiji vya Ntomoko, Haubi, Mafai na Mwisanga vilivyoko kata ya Haubi, Wilaya ya Kondoa. Katika Mkoa wa



Kaskazini Pemba mradi unatekelezwa katika Wilaya ya Micheweni, Kata ya Micheweni, Shehia za Micheweni Mjini, Micheweni Chamboni, Kwale/Majenzi, Shumba Mjini na Mjini Wingwi. Katika Kata ya Kiuyu mradi unatekelezwa katika Shehia ya Kiuyu Mbuyuni na katika Kata ya Maziwa Ng'ombe unatekelezwa katika Shehia za Maziwa Ng'ombe na Shanaka.

### **Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai**

**67.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Ofisi imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai na Itifaki zake. Ofisi imeandaa Ripoti ya Sita ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai ambayo itawasilishwa katika Sekretarieti ya Mkataba kwa ajili ya kuandaa taarifa ya Hali ya Bioanuai Duniani (*Global Biodiversity Outlook*). Pamoja na mambo mengine ripoti imebainisha hali ya bioanuai nchini; changamoto zinazosababisha upotevu wa bioanuai; hatua na Mikakati iliyochukuliwa kutekeleza Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai nchini (*National Biodiversity Strategy and Action Plan, NBSAP*). Aidha, katika kipindi hiki, Ofisi kwa kutumia wakaguzi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa imeendelea kusimamia na kukagua shughuli za utafiti wa mazao ya kilimo yaliyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Makutupora, Dodoma.

**68.** *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imeendelea kukuza uelewa wa jamii kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa kwa kutumia vyombo vya habari kama radio na luninga. Vilevile, Ofisi imeendesha mafunzo kwa wataalam kutoka Sekta zinazohusika na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa, mafunzo hayo pamoja na mambo mengine yalilusisha maeneo yafuatayo: utambuzi wa mazao yaliyoboreshwa vinasaba (*GMOs Detection*); tathmini ya uwezekano wa kutokea kwa madhara kwa mazingira (*Environmental Risk Assessment*); na tathmini ya usalama wa chakula cha binadamu na wanyama (*Food and Feed Assessment*).

**Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi**

**69. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Nairobi pamoja na Itifaki zake. Katika mwaka 2018/19 Ofisi iliratibu uandaaji wa miradi ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mkataba wa Nairobi wa Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari Magharibi ya Bahari ya Hindi kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu (*The Strategic Action Programme for the Protection of the Western Indian Ocean from Land-Based Sources and Activities - WIOSAP*). Kupitia uratibu huu, Ofisi ilipokea maandiko ya awali ya miradi ya mfano kumi (10) kutoka kwa wadau mbalimbali wanaojihusisha na uhifadhi wa mazingira ya bahari inayolenga kupunguza uchafuzi wa bahari kutokana na maji taka, usimamizi wa maeneo nyeti ya bahari (*Management of critical habitat*) na usimamizi endelevu wa mitiririko ya mito (*Sustainable Management of River Flows*). Maandiko hayo yalipitiwa na timu ya wataalamu katika ngazi ya Kitaifa na kupata maandiko bora matatu (3) ambayo yamewasilishwa Sekretarieti ya Mkataba kwa ajili ya kupitiwa na kuboreshwa katika ngazi ya Kikanda.

**70. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imefanya mapitio ya Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka (2006) na Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka (2008). Mikakati hii imefanyiwa mapitio ya utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano (2019 -2024). Mapitio ya Mikakati hii yamebainisha changamoto mpya ambazo hazikuwa zimebainishwa wakati wa maandalizi ya Mikakati hii mwaka 2006 na 2008. Changamoto mpya zilizobainishwa ni pamoja na: Mabadiliko ya Tabianchi; Viumbe Vamizi; Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Baharini na kwenye Maziwa; na ongezeko la uchafuzi kutokana na Taka za Plastiki. Aidha, Mikakati hii imeainisha hatua na mipango ya utekelezaji ili kutatua changamoto hizo.

**71. Mheshimiwa Spika**, mapitio ya Mikakati hii na maandalizi ya mipango ya utekelezaji katika kipindi cha

mwaka (2019 - 2024) yalishirikisha wadau kutoka Wizara za Kisekta, Vyuo vya Elimu ya Juu na Taasisi za Utafiti, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Ushiriki huu wa wadau ulisaidia katika kutoa mwongozo na kusanifu Mikakati ya utekelezaji inayoendana na utekelezaji wa Sera, Mipango na Mikakati yao pamoja na kujenga uwezo wao katika kuutekeleza Mkakati huu.

### **Mkataba wa Basel Kuhusu Udhhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu Kati ya Nchi na Nchi**

**72. Mheshimiwa Spika**, kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Basel, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa Umma kupitia vyombo vya habari kuhusu taratibu za kukusanya, kusafirisha na kurejeleza taka hatarishi na taratibu zinazotakiwa ili kusafirisha taka nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali ikiwemo kurejelezwa au kuteketezwa. Vilevile, Ofisi imeendelea kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa taka zenye madhara baina ya nchi kupitia Tanzania kwa kuzingatia Kanuni na Matakwa ya Mkataba wa Basel.

### **Mkataba wa Stockholm Kuhusu Udhhibiti wa Kemikali Zinazodumu Katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

**73. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm katika kuzuia madhara ya kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu. Ofisi imeratibu zoezi la kukusanya sampuli za mafuta ya transfoma zinazomilikiwa na TANESCO na ZECO yanayodhaniwa kuwa na kemikali aina ya "*Polychlorinated Biphenyls*" (PCBs) ambayo imethibitika kuwa ina madhara katika mazingira na inapaswa kuondoshwa ifikapo mwaka 2025 kulingana na matakwa ya Mkataba huu. Sampuli hizo zitawasilishwa katika kituo cha *Africa Institute* kilichopo Pretoria, Afrika Kusini kwa ajili ya uchunguzi kabla ya kuondoshwa kwa kemikali hizo. Vilevile, Ofisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika nchi za Kitropiki (*Tropical Pesticides Research Institute* - TPRI) imetoa mafunzo kwa maafisa ugani na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zinazojishughulisha na uchimbaji wa gesi nchini kuhusu udhibiti wa kemikali.

**74. Mheshimiwa Spika,** Ofisi kwa kushirikiana na wadau wengine imeendesha zoezi la ukusanyaji wa taarifa za hali ya uhomaji wa taka kwenye madampo makubwa katika Majiji yote nchini. Lengo la taarifa hizi ni kuandaa Mpango wa kuhamasisha mbinu bora na rafiki kwa mazingira za kupunguza uzalishaji wa kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu zitokanazo na uhomaji wa taka.

### **Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

**75. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba na Itifaki yake inayohusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: Kuendesha mafunzo kwa maafisa forodha na mafundi mchundo 40 kuhusu teknolojia mpya na njia sahihi za kuhudumia vifaa vinavyotumia kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni; Kutoa elimu kwa Umma kuhusu utekelezaji wa Itifaki ya Montreal na kemikali mbadala wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ozoni tarehe 16 Septemba, 2018; na kuendelea kuhamasisha wafanyabiashara, watumiaji na waingizaji wa kemikali nchini kupunguza kiasi cha uingizaji na utumiaji wa kemikali ambazo zitaondolewa katika soko kutokana na kubainika kuongeza joto angani (*Hydrochlorofluorocarbons - HCFCs*). Aidha, Ofisi imeratibu ukusanyaji wa takwimu za uingizaji na matumizi ya kemikali mbadala zinazoharibu Tabaka la Ozoni. Takwimu hizi zinaendelea kutusaidia kupanga mikakati ya kusitisha matumizi ya kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni.

### **Mkataba wa Minamata Kuhusu Udhibiti wa Matumizi ya Zebaki**

**76. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2018/19, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Minamata unaohusu udhibiti wa matumizi ya zebaki kwa ajili ya kulinda afya ya binadamu na mazingira. Aidha, Ofisi imekamilisha Rasimu ya Mpango-Kazi wa Kitaifa wa Kupunguza Matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini pamoja na kuandaa Kanuni za zebaki.

## **Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund – GCF*)**

**77. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Ofisi iliendelea kuhimiza suala la Taasisi za Umma na Sekta binafsi hapa nchini kupata ithibati (*accreditation*) katika Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF). Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya tathmini ya Kitaasisi yenye lengo la kuangalia jinsi mifumo, taratibu, Kanuni na miongozo ya fedha hapa nchini, inavyokidhi mahitaji na vigezo vya usajili vya GCF. Mwezi Januari mwaka 2019, Wizara iliendesha warsha ya wadau kwa ajili ya kupokea, kujadili, na kuhakiki (*validate*) rasimu ya taarifa ya tathmini. Vilevile, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mwezi Februari, 2019 iliwasilisha rasmi maombi ya kupata ithibati kwenye Sekretarieti ya GCF.

**78. Mheshimiwa Spika**, Ofisi iliendelea kuratibu uchambuzi wa miradi chini ya ufadhili wa Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund - GCF*). Katika kipindi hiki uchambuzi wa miradi mitatu ulifanyika. Kati ya miradi hiyo mradi mmoja ambao umekidhi vigezo uliwasilishwa GCF kwa ajili ya kupatiwa fedha za utekelezaji. Aidha, katika kipindi hiki Ofisi iliwezesha ukamilishaji wa Mikataba ya kifedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Simiyu wenye gharama ya kiasi cha Sh. bilioni 250. Ofisi ilisimamia uwekaji saini wa Mkataba wa Kifedha kati ya GCF na KfW. Tukio hilo lilifanyika tarehe 12 Desemba, 2018 huko Katowice, Poland wakati wa Mkutano wa 24 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi.



**Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mussa Sima akihutubia wakati wa Mkutano wa Mabadiliko ya tabia Nchi (COP24/CMP14/CMA1.3) uliofanyika Katowice-Poland.**

## **Itifaki ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Usimamizi Endelevu wa Mazingira**

**79. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na inashiriki katika kutekeleza Mikataba na Itifaki mbalimbali zinazopitishwa na nchi wanachama wa Jumuiya. Katika kipindi cha mwaka 2018/19, Ofisi imeanza utaratibu wa kuridhia Itifaki ya SADC kuhusu Usimamizi Endelevu wa Mazingira ikiwa ni pamoja na kukusanya maoni ya wadau na kuandaa andiko kabla ya kuanza taratibu ya kuridhia itifaki hiyo.

## **Elimu kwa Umma Kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira**

**80. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ilikamilisha maandalizi ya Mfumo wa Taarifa kuhusu Mazingira (*Central Environmental Information System*) utakaoendana na mfumo wa teknolojia ya simu kuwawezesha watumiaji kupokea na kutoa taarifa zinazohusu masuala ya Mazingira.

## **BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

**81. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambalo ndio msimamizi mkuu wa uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 limeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

### **Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira**

**82. Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inazingatiwa ipasavyo katika kutekeleza shughuli za maendeleo hapa nchini, Baraza limetekeleza kazi zifuatazo:-

#### **i) Ukaguzi wa Maeneo ya Uwekezaji na Mazingira**

**83. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19 Baraza limefanya ukaguzi katika viwanda, machinjio ya wanyama, migodi (yakiwemo machimbo ya mchanga na kokoto), hifadhi ya vyanzo vya maji, mashamba, vituo vya mafuta, maghala ya kuhifadhi kemikali na taka hatarishi, madampo, hoteli, mifumo ya maji taka, taasisi za elimu na afya, majengo ya biashara na makazi ili kupima uzingatiaji na usimamizi wa

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira nchini. Katika ukaguzi huo jumla ya miradi 4,853 ilikaguliwa ambapo miradi 1,627 ni ya viwanda sawa na asilimia 34. Ukaguzi huo ulibaini kuwa asilimia 40 ya miradi inazingatia Sheria na baadhi ya miradi kuwa na changamoto za kimazingira kama:- kutiririsha majitaka kwenye vyanzo vya maji na mazingira; Kutumia rasilmali za misitu ya asili kwa ajili ya kuni na majengo; Kutokuwa na mifumo ya kuhifadhi na kusimamia taka ngumu; Uzalishaji wa hewa chafu; Udhibiti na Uhifadhi duni wa taka hatarishi; Upigaji wa kelele na mitetemo zaidi ya viwango vinavyokubalika kimazingira; na baadhi ya viwanda kuanzishwa kwenye makazi ya watu.

**84. Mheshimiwa Spika,** Baraza limechukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, kwa miradi iliyokiuka Sheria na Kanuni zake. Hatua hizo ni pamoja na kutoa ushauri, maelekezo, maonyo, amri za katazo, amri za urejeshaji wa mazingira na kuwafikisha mahakamani

ii) **Kushughulikia Malalamiko ya Kimazingira**

**85. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19 Baraza limeendelea kupokea malalamiko yanayohusu uchafuzi wa mazingira kutoka kwa wananchi na kuyashughulikia kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake. Katika kipindi hiki zaidi ya malalamiko 701 yamepokelewa kutoka maeneo mbalimbali nchini na kuyapatia ufumbuzi. Baadhi ya malalamiko yalihusu:- Kelele kutoka katika karakana; Nyumba za ibada; Kumbi za starehe; Viwanda na utengenezaji wa matofali; Utiririshaji wa majitaka kutoka kwenye maeneo mbalimbali ya uzalishaji; Uchimbaji wa mchanga katika vyanzo vya maji na maeneo mengineyo; na uchafuzi wa mazingira kutokana na uanzishwaji wa machinjio ya wanyama kwenye makazi ya watu.

**Ukaguzi wa Sampuli**

**86. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19, Baraza kwa kushirikiana na Maafisa wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa, lilichukua sampuli thelathini (30) za tope/tabaki kutoka kwenye vijito mbalimbali vya maji vinavyopatikana

kwenye maeneo ambayo ni maarufu kwa uchimbaji mdogo wa madini katika Wilaya ya Chunya. Sampuli hizo zimepelekwa kwenye maabara ya SGS – Mwanza kwa lengo la kuchunguza uwepo wa viambata vya kemikali za sumu (hasa Zebaki). Matokeo ya vipimo hivyo yatatoa majibu sahihi ya hali halisi na taarifa zitatolewa kwa Umma. Aidha, sampuli sita (6) za tabaki na maji zilichukuliwa katika fukwe karibu na eneo la uchakataji wa gesi asilia (Mnazi Bay - Mtwara) kwa ajili ya ufuatiliaji.

### **Mafunzo kwa Wakaguzi wa Mazingira**

**87.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Baraza limetoa mafunzo kwa Wakaguzi wa Mazingira (*Environmental Inspectors*) 194 kutoka Kanda za Mashariki, Kusini, Nyanda za Juu Kusini na Ziwa; Wizara ya Maji; na Wizara ya Mambo ya Ndani. Mafunzo haya yatawawezesha Wakaguzi kusimamia vilivyo Sheria ya mazingira katika maeneo yao ya utendaji.

### **Uteketezaji wa Kemikali/Taka Hatarishi**

**88.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Baraza kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali kama Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Serikali za Mitaa (LGAs), limesimamia uteketezwaji (*incineration*) wa taka hatarishi kiasi cha tani 90. Uteketezaji huo umefanyika kwa kutumia mtambo wa uteketezaji taka (*incinerator*) wa *Safe waste* ulioko Mkuranga na *Tindwa Medical and Health Service* ulioko Kisarawe. Vile vile, makampuni 45 yalipewa miongozo na kusimamiwa katika uteketezwaji wa taka hatarishi hususani kemikali, madawa ya binadamu yaliyomaliza muda wa matumizi na mabati ya *asbestos*. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Taasisi ya Usajili na Utafiti wa Viuatilifu nchini (TPRI) lilifanya ukaguzi wa eneo lenye madawa chakavu ya kilimo (*Obsolete Pesticides*) lililoko Arusha na kuhakikisha madawa hayo yamehifadhiwa (*Safeguarding Obsolete Pesticides Stockpiles*) katika utaratibu maalum na hivyo kuondoa uwezekano wa kusababisha athari za kiafya na kimazingira.



## Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM)

### i) Usajili wa Miradi na Utoaji wa Vyeti vya Mazingira

**89.** *Mheshimiwa Spika*, ili kufanyia kazi changamoto zilizojitokeza katika utoaji wa vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira katika Miradi ya Maendeleo utaratibu wa utoaji wa vyeti hivyo umeboreshwa. Baraza limeweka utaratibu wa kutoa Kibali cha Awali cha Mazingira (*Provisional Environmental Clearance*) ili kuwawezesha wawekezaji kuendelea na maandalizi ya awali ya mradi wakati mchakato wa TAM unaendelea. Kibali hicho kinatumika kwa miradi ya viwanda, kilimo na miradi mingine ya kipaumbele kwa Serikali. Mpaka sasa jumla ya Vibali saba (7) vya Awali vya Mazingira vimetolewa. Utaratibu huu utasaidia kuharakisha uwekezaji katika Sekta ya viwanda nchini. Vilevile Serikali inaandaa utaratibu utakaowezesha kuwa na namba za simu (*hot lines*) zitakazowezesha wawekezaji kutoa taarifa au malalamiko kuhusiana na maombi wanayoyawasilisha ili yaweze kufanyiwa kazi kwa wakati. Utaratibu huu utawezesha Ofisi kufanyia kazi maoni yanayotolewa na hivyo kuboresha taratibu zinazotumika kutoa vyeti hivi kila inapohitajika.

Katika mwaka 2018/19 Baraza limesajili jumla ya miradi 1,254 ya maendeleo kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Ukaguzi wa Mazingira, ambapo jumla ya miradi 455 ilikamilika na kupatiwa vyeti vya mazingira. Vilevile, Ofisi imefanya maboresho ya Kanuni katika mchakato wa TAM na kupunguza idadi ya siku. Miradi yenye athari ndogo kwa mazingira itatumia jumla ya siku 35 tu kupata cheti ambapo siku 21 zitakuwa kwa ajili ya NEMC kukamilisha taratibu husika, na siku 14 ni kwa ajili ya Waziri mwenye dhamana ya mazingira kutoa maamuzi. Aidha, Miradi yenye athari kubwa kwa mazingira itapata kibali cha muda ndani ya siku 14 na sasa mchakato wa TAM utatumia siku 88 kutoka siku 149 zilizokuwa zikitumika awali. Aidha, gharama ya usajili wa miradi ya TAM imepungua na haitozwi kwa kiwango cha asilimia ya gharama ya mradi kama ilivyokwa awali. Kwa sasa gharama za usajili wa mradi zinaanzia Sh. Milioni 4 kwa miradi midogo na kwa miradi mikubwa gharama haizidi Sh. milioni 50.

**90.** *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha mchakato wa miradi ya kitaifa na kimataifa inakwenda kwa kasi inayokubalika, Baraza limekuwa likishauriana na wahusika katika kila hatua ya utekelezaji. Mfano wa miradi hiyo ni: Mradi wa ujenzi wa Bomba la mafuta (*East Africa Crude Oil Pipeline - EACOP*). Baraza limepokea ripoti ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kamati ya kupitia ripoti hii imeteuliwa; Mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Mpira Dodoma (*Dodoma Sports Complex*) ulipewa cheti cha Mazingira tarehe 31 Julai 2018; na Mradi wa kufua Umeme wa Rufiji (*Rufiji Hydropower Project*) umeshapatiwa cheti cha TAM. Baraza kwa kushirikiana na TANESCO litaratibu na kusimamia utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira wakati wote wa utekelezaji wa mradi.

**ii) Kuandaa Miongozo kuhusu TAM**

**91.** *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha mchakato wa TAM unatekelezwa kwa ufanisi, Baraza kwa kushirikiana na Kituo cha Sayansi na Mazingira cha India limeandaa miongozo itakayosaidia kurahisisha mapitio ya miradi ya majengo na Sekta ya ujenzi. Miongozo hii iko katika hatua za mwisho ambapo wadau watashirikishwa kutoa maoni kabla ya kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza.

Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali – Mbeya, Ofisi ya Madini ya Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Chunya, Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Mamlaka ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi (Mbeya) na wawakilishi wa wachimbaji wadogo kutoka Wilaya ya Chunya limeandaa utaratibu wa kurahisisha mchakato wa kuandaa maandiko ya Tathimini ya Athari kwa Mazingira kwa miradi ya wasafishaji wadogo wa dhahabu (*elusion plants*) katika Wilaya ya Chunya. Utaratibu huu utawapunguzia gharama za kufanya TAM wawekezaji hao wadogo katika Sekta ya madini.

**Elimu kwa Umma Kuhusu Hifadhi ya Mazingira**

**92.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19, Baraza limeendelea kutoa elimu kwa Umma kwa kutumia vyombo vya habari na mafunzo kwa wadau kuhusu masuala ya

mazingira ili kujenga uelewa kwa jamii kuhusu masuala ya mazingira. Aidha, Baraza lilishiriki katika maadhimisho mbalimbali na muhimu kimazingira ili kukuza na kukuza uelewa wa jamii kwa lengo la kuboresha uwajibikaji katika kutunza na kuhifadhi Mazingira. Maadhimisho hayo ni pamoja na Siku ya Maonesho ya Viwanda na Biashara na Maonesho ya Nane Nane. Pia Baraza liliendesha warsha ya kuelimisha wadau kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake ambapo jumla ya wachimbaji wadogo 70 wa dhahabu pamoja na wamiliki 23 wa viwanda vya kukoboa mpunga katika Mikoa ya Mbeya na Songwe walielimishwa.

### **Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira (*National Environmental Research Agenda - NERA*)**

**93.** *Mheshimiwa Spika*, Baraza limeendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira (*National Environmental Research Agenda - NERA*) kwa kufanya tathmini ya lindimaji/dakio (*catchment*) la Bonde la Wami-Ruvu. Mkutano wa wadau unaandaliwa ili kutengeneza Mpango wa Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira ya dakio hilo. Vile vile, Baraza limefanya ufuatiliaji wa bomba kuu la mafuta (TAZAMA *pipeline*) ili kupata taarifa ya hali ya mazingira na bioanuai zilizopo na kupendekeza njia bora za uhifadhi.

**94.** *Mheshimiwa Spika*, Baraza pia limefanya tathmini ya mmomonyoko wa fukwe za Kigamboni kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa na wananchi na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kukabiliana na hali hiyo. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Ardhi limefanya utafiti wa kina kuhusiana na tatizo la kujaa kwa maji ya mvua katika makazi eneo la Mlandizi, Halmashauri ya Kibaha. Ripoti ya utafiti huo inaandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa katika Mamlaka husika kwa utekelezaji. Rasimu 85 za maandiko ya miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi zilipokelewa na kupitiwa. Jumla ya miradi mitatu (3) ilipitishwa baada ya kukidhi vigezo. Miradi hiyo imewasilishwa kwenye Sekretarieti ya Bodi ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa ajili ya hatua zaidi.

**Mipango ya Hifadhi ya Mazingira katika Maeneo Maalum**

**95.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Baraza limeendelea kuratibu shughuli zote za Hifadhi Hai (*Man and Biosphere Reserves - BRs*) tano (5) ambazo ni Serengeti, Ngorongoro, Ziwa Manyara, Usambara Mashariki na Jozani Chwaka Bay iliyopo Zanzibar. Aidha, Baraza limeanza maandalizi ya Kongamano la Kisayansi kuhusu Hifadhi Hai (*Biosphere Reserves*) nchini. Kongamano hili linatarajiwa kufanyika mwezi Agosti, 2019.

**96.** *Mheshimiwa Spika*, Baraza lilitembelea Mikoa sita (Singida, Tabora, Geita, Mara, Manyara na Arusha) kuthibitisha taarifa za maeneo yaliyopendekezwa kutengwa kama maeneo Nyeti na Lindwa (*EPA and ESAs*). Maeneo yaliyotembelewa na kuridhiwa na wananchi ili yatangazwe kuwa maeneo Nyeti ni pamoja na Msitu wa Mwalimu Nyerere na Mlima Mkendo yaliyoko Mkoa wa Mara pamoja na Singidani, Kindai na Munang yaliyoko Mkoa wa Singida. Baraza liko katika mchakato wa kuainisha na kuyapima maeneo hayo ili kupata ukubwa na '*geographical coordinates*' kwa ajili ya kuyatambua. Aidha, mazungumzo na wadau muhimu yanaendelea ili kujiridhisha na taarifa zilizopatikana kabla ya kufanya maamuzi ya mwisho ya kuyatangaza maeneo hayo kuwa maeneo Lindwa.

**Uratibu wa Miradi Inayotekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo Nchini**

**97.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Baraza limeendelea kutekeleza na kuratibu miradi miwili (2) kwa kupitia fedha za wafadhili. Miradi hiyo ni:

i. **Mradi wa Kuhifadhi Lindimaji la Bonde la Kihansi pamoja na dakio lake (*Kihansi Catchment Conservation Management Project - KCCMP*)**. Baadhi ya kazi zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na zoezi la uwekaji mipaka katika eneo la Kihansi ambalo linatarajiwa kutangazwa kuwa eneo lindwa la kimazingira (*Environmental Protected Area -EPA*) ; na Kuendesha maabara za vyura, kurejesha na kufuatilia maendeleo ya vyura waliorejeshwa kwenye makazi yao ya asili pamoja na mazingira yake.

ii. **Mradi wa Kujenga Uwezo kwenye Sekta Zinazoshughulika na Nishati (*Energy Sector Capacity Building Project - ESCABP*)**. Baadhi ya kazi zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na kuweka (*installation*) kituo cha taarifa za mazingira (*Environmental Information Centre*) ambacho kitakuwa na maktaba ya vitabu mango (*hard copies*) na nakala tete (*e-library*); na kuboresha maabara ya mazingira kwa ajili ya kufanya vipimo vya mazingira kwa mujibu wa Viwango vya Mazingira (*Environmental Standards*).

## **MASUALA MTAMBUKA, (UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU)**

**98. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma sambamba na kuwawezesha watumishi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi hiki watumishi 33 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kati ya hao 17 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 16 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi.

**99. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imefanikiwa kuajiri watumishi wapya saba (7) wa kada mbalimbali kwa lengo la kujaza nafasi zilizo wazi ili kuongeza nguvukazi na kuwezesha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi zaidi. Watumishi wawili (2) wamebadilishwa vyeo kwa kuzingatia sifa, miundo inayotawala kada zao na Mfumo Wazi wa Utendaji Kazi na Upimaji (OPRAS). Aidha, watumishi nane (8) wamethibitishwa kazini baada ya kumaliza muda wa majaribio. Vilevile, taarifa na kumbukumbu za watumishi zimeboreshwa kwa asilimia mia moja (100%) kupitia mfumo wa taarifa za watumishi na mishahara (*Human Capital Management Information System – HCMIS*).

**100. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 Ofisi imeendelea kuimarisha utawala bora, demokrasia na dhana ya ushirikishwaji watumishi pahala pa kazi katika mipango ya Ofisi kupitia vikao vya Idara na vitengo, vikao vya menejimenti na vya Baraza la wafanyakazi. Aidha, mazingira

ya utendaji kazi yameboreshwa kwa kuwezesha upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha. Vilevile, ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika mji wa Serikali Ihumwa, Dodoma unaendelea.

### **Usimamizi wa Ofisi, Maslahi na Maendeleo ya Watumishi - NEMC**

**101.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Baraza limewapatia watumishi wake vitendea kazi kama kompyuta na samani za Ofisi ili kuboresha utendaji kazi. Pia, Baraza limefanya tathmini ya utendaji kazi wa watumishi wake kwa kupitia mfumo wa OPRAS na kufanya vikao vya wafanyakazi wote ili kujadili na kutatua changamoto zinazowakabili. Vilevile, Baraza limewawezesha wafanyakazi kushiriki katika semina, mikutano na mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo katika masuala ya mazingira. Aidha, Baraza limeboresha mifumo ya kifedha na kujiunga na Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato na Malipo Mtandao (*Government e-Payment Gateway - GePG*).

### **CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO**

**102.** *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yetu Ofisi ilikumbana na changamoto kadha zikiwemo; - Upatikanaji wa rasilimali fedha zinazoendana na mahitaji halisi ya Ofisi; Uelewa mdogo wa wadau kuhusu masuala ya Muungano na umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira; Upatikanaji wa takwimu sahihi za mazingira; na kutokuwa na wataalam wa kutosha. Hata hivyo tulichukua hatua katika kukabiliana nazo ikiwa ni pamoja na ; -Kuandaa miradi na kuiwasilisha kwa Wadau wa Maendeleo kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji; Kuendelea kutoa elimu kwa umma kupitia redio, luinga, magazeti, machapisho, maadhimisho na maonyesho ya kitaifa kuhusu Masuala ya Muungano na umuhimu wa kuhifadhi mazingira, pamoja na kuhamasisha wadau hususan Serikali za Mitaa na sekta binafsi kushiriki katika masuala ya mazingira; Kuandaa taarifa ya Hali ya Mazingira pamoja na kuandaa maandiko ili kupata ufadhili katika eneo la ukusanyaji takwimu; kutoa mafunzo kwa wataalam pamoja na kuajiri.

**C. MALENGO NA MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2019/20**

**Masuala ya Muungano**

**103. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha na kuenzi Muungano katika mwaka 2019/20 Ofisi imepanga kutekeleza majukumu na malengo yafuatayo: -

i) Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na ufuatiliaji wa maelekezo na maagizo yanayotolewa katika vikao;

ii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zinazotekelezwa pande zote za Muungano, kuhakikisha gawio la asilimia 4.5 ya fedha za Misaada ya Kibajeti (GBS), faida ya Benki Kuu, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na PAYE linapelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na ziara za kikazi ili kuimarisha Muungano’;

iii) Kutoa elimu ya Muungano kwa makundi tofauti ya kijamii ikiwa ni pamoja na kuandaa warsha na makongamano ili kuendelea kuamsha ari ya kuenzi, kuulinda na kuimarisha Muungano ambao umedumu miaka 55; na

iv) Kuhamasisha Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana kuendelea kufanya vikao angalau mara mbili kwa mwaka ili kupunguza changamoto za kisékta kwa ustawi wa Muungano wetu.

**Hifadhi ya Mazingira**

**104. Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia na kuhifadhi Mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho katika mwaka 2019/20 Ofisi imepanga kutekeleza majukumu na malengo yafuatayo:-

**Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997**

**105. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Ofisi imepanga kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 na Mkakati wake wa Utekelezaji. Lengo la mapitio hayo ni ni kuboresha Sera ya Taifa ya Mazingira kwa kuhakikisha masuala mapya ya kimazingira yanazingatiwa ili

kujumuishwa katika Mkakati wa utekelezaji. Aidha, kwa kuzingatia maboresho ya Sera Ofisi itakamilisha Marekebisho ya Sheria ikiwa ni pamoja na kuwezesha Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira kusajiliwa na kuanza kufanya kazi kama inavyostahili. Ni matarajio yetu kuwa Maboresho ya Sera pamoja na Sheria yatasaidia kwa kiasi kikubwa juhudi za Serikali kusimamia masuala ya mazingira nchini na hivyo kuwa na maendeleo endelevu.

### **Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini**

**106.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20, Ofisi itachapisha nakala za Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira ya Mwaka 2018 kwa lengo la kuzisambaza kwa wadau na kutoa elimu kwa umma kuhusu hali ya mazingira nchini. Vilevile Ofisi itaandaa Ripoti hiyo katika lugha nyepesi ili kurahisisha utoaji wa elimu. Ripoti hii ina takwimu na taarifa muhimu zitakazosaidia katika Mipango ya kuhifadhi mazingira nchini. Ripoti hiyo itawasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 Kifungu 175 (1).

### **Kuhamasisha Matumizi ya Nishati Mbadala**

**107.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20, Ofisi itaendelea kuelimisha na kuhamasisha umma ili kuhakikisha kuwa, mkaa mbadala unatumiwa na kukubalika na watu wengi ikiwa ni pamoja na kuwa na viwango vinavyokubalika kitaalam. Ofisi kwa kushirikiana na taasisi za elimu na za utafiti, itatumia kazi za washindi kuweka viwango vya ubora wa mkaa mbadala unaozalishwa hii ikiwa ni pamoja na: kiwango cha nishati joto (calorific values); aina ya vifungashio (packaging materials); uzito wa mkaa (density) pamoja na kujua usalama wa kiafya kwa mkaa unaozalishwa kulingana na aina ya viambata (ingredients) vinavyotumika kutengeneza mkaa husika. Pia Taasisi zote za Serikali zitahamasishwa kupunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya mkaa na kuni na kuongeza matumizi ya nishati mbadala hususan gesi ya kwenye mitungi (Liquified Petroleum Gas – LPG).



### **Mifuko ya Plastiki**

**108.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20, Ofisi itaendelea kusimamia uzingatiji wa Kanuni zinazoandaliwa chini ya usimamizi wa Sheria ya Mazingira, kutoa elimu na kuhamasisha wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa viwanda vya mifuko ya plastiki ili kuhakikisha utekelezaji wa tamko la Serikali la kupiga marufuku uingizaji, uuzaji, uzalishaji na utumiaji wa mifuko ya plastiki linatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, nichukue fursa hii kuwahimiza wawekezaji kuendelea kutumia fursa hii kuwekeza katika teknolojia ya uzalishaji wa mifuko mbadala.

### **Viumbe Vamizi**

**109.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20, Ofisi kwa kushirikiana na wadau itaratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Viumbe Vamizi (2019 - 2029). Mkakati huo unalenga kuimarisha juhudi za Serikali kukabiliana na ueneaji wa viumbe hao na athari zake ambazo zinaendelea kuongezeka kwa kasi nchini na hivyo kuathiri sekta kuu za uchumi ambazo ndiyo msingi wa uzalishaji na ajira. Juhudi hizo zitakwenda sambamba na utoaji elimu kwa umma juu ya jambo hili ili kuhakikisha wadau wanaunga mkono juhudi za Serikali katika kupambana na tatizo hili. Nachukua fursa hii kuomba wadau wa mazingira ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo, Mashirika na Asasi zisizo za Serikali kuunga mkono juhudi za Serikali kukabiliana na tatizo hili.

### **Kampeni ya Upandaji Miti**

**110.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20, Ofisi itaendelea kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti kwa kushirikiana na Sekta zinazohusika katika Halmashauri za Wilaya Nchini ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazokwamisha kufikiwa kwa malengo ya kampeni hii. Baadhi ya masuala yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kuhamasisha wananchi kupanda miti ya matunda ambayo pamoja na kuhifadhi mazingira itasaidia kukuza kipato na kuimarisha afya kwa jamii. Juhudi hizo zitakwenda sambamba na kusesitiza juu ya utunzaji wa miti ya asili.

### **Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira**

**111.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20, Serikali itaendesha mashindano ya Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira kwa kutumia Mwongozo wa Tuzo ulioboreshwa. Baadhi ya masuala yalioongezwa katika mwongozo huo ili kuuboresha ni pamoja na uzalishaji endelevu viwandani, matumizi ya nishati mbadala, uchimbaji madini endelevu, kilimo na ufugaji endelevu, usimamizi wa taka, afya na usafi wa mazingira. Aidha washindi wa Tuzo hii wanatarajiwa kupewa Tuzo zao wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, tarehe 5 Juni, 2020;

### **Uzuiaji wa Shughuli za Binadamu katika Baadhi ya Maeneo**

**112.** *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 Kifungu cha 57 (1) kinakataza kutofanyika shughuli yoyote ya kibinadamu ya kudumu au ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira na au utunzaji wa bahari au kingo za mito, bwawa, au miambao ya asili ya ziwa. Hata hivyo, Kifungu 57 (2) kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya mazingira kuweka miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo yaliyoelezwa. Kwa kuzingatia hilo Ofisi inaandaa Miongozo itakayotoa ufafanuzi kuhusu aina ya shughuli zinazoweza kutekelezwa katika maeneo hayo. Lengo ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na uwiano kati ya uongezaji wa kipato cha wananchi pamoja na uzingatiaji wa uhifadhi wa mazingira katika eneo lililolengwa.

### **Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Maji Zinazovuka Mipaka Kati ya Kenya na Tanzania**

**113.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania na Kenya ni nchi jirani zinazomiliki kwa pamoja baadhi ya Maziwa na Mito ikiwemo, Ziwa Chala, Ziwa Jipe, Ziwa Natron na Mto Mara. Kwa muda mrefu nchi hizi mbili zimekuwa kwenye changamoto za matumizi yasiyo endelevu kwa rasilimali hizo na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira unaopelekea upungufu wa utiririshaji maji, kupungua kwa kina cha maji kwa baadhi ya Mito na Maziwa na kuongezeka kwa magugu maji kunakohatarisha bioanuai ya maeneo haya. Ili kukabiliana na changamoto hizo nchi za Kenya na Tanzania

zimekubaliana masuala yafuatayo; Kuunda Kamati ya pamoja katika ngazi ya Wataalam na Mawaziri; Kufanya tathmini ya kina ya rasilimali za mipakani; na Kuandaa Mkataba wa usimamizi wa rasilimali hizo pamoja na Mpango wa utafutaji wa rasilimali fedha. Hadi sasa Kamati ya pamoja ya Wataalam kwa ajili ya kutoa mwongozo wa kitaalam wa usimamizi wa rasilimali za mipakani zinazomilikiwa kwa pamoja imeshaundwa na kuanza kazi.

**114. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Serikali itaendelea kuratibu kazi chini ya Kamati hizi kwa kushirikiana na Serikali ya Kenya.

#### **Uratibu wa Usimamizi wa Mazingira Katika Ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**115. *Mheshimiwa Spika***, katika juhudi za kutekeleza Sheria ya Mazingira, Ofisi itaendelea kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali ya Mitaa ili kuimarisha uratibu wa usimamizi wa Mazingira kwa kuhakikisha uteuzi wa wataalam wa usimamizi wa mazingira katika ngazi za Miji, Wilaya, Manispaa, Jiji na Mikoa unaendelea kufanyika. Maafisa hao ni kiungo katika utekelezaji, usimamiaji na ufuatiliaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 katika maeneo hayo na hivyo wana wajibu wa kushauri Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Sheria hii. Aidha, utekelezaji, uratibu na ufuatiliaji utahusisha uundaji wa Kamati za Usimamizi wa Mazingira za Jiji, Manispaa, Wilaya, Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji pamoja na kuhakikisha kuwa zinafanya kazi na uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Mazingira ya mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**116. *Mheshimiwa Spika***, Kazi nyingine zitakazotekelezwa katika hifadhi ya mazingira ni pamoja na:-

- i) Kuendesha mafunzo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara za Kisekta; na kuanzisha mfumo wa utoaji vyeti na leseni za mazingira kwa njia ya mtandao;
- ii) Kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi ili kuhakikisha hali ya Mfumo Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu inaendelea kuimarika;

- i) Kuelimisha Umma kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira pamoja na matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa (GMO) kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, luninga na magazeti. Vilevile, Ofisi itaandaa na kuchapisha Mkakati wa Mawasiliano na Elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi ya Mazingira;
- ii) Kusimamia, Kuratibu na Kufuatilia Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira ambayo Tanzania ni Mwanachama na kuandaa msimamo wa nchi na kuratibu ushiriki katika mikutano ijayo ya nchi wanachama wa Mikataba ya kimataifa ya hifadhi ya mazingira;
- iii) Kutoa vyeti vya Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) kwa miradi na Tathmini ya Mazingira Kimkakati (SEA) na kufuatilia utekelezaji wa suala hili kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004;
- iv) Kuratibu utekelezaji wa Mikakati iliyopo chini ya Mikataba ya Kimataifa tuliyoridhia;
- v) Kuwezesha mchakato wa kuridhia Mikataba na Itifaki za Mazingira ambazo Tanzania imesaini;
- vi) Kutekeleza miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na Mabadiliko ya Tabiachi iliyopo chini ya Mikataba ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini na ufuatiliaji; na
- vii) Kuandaa miradi ya kuhifadhi mazingira na kuiwasilisha kwa wafadhili kwa ajili ya kupatiwa fedha kutoka kwenye Mifuko na Mashirika yanayohusika na kuhifadhi mazingira.

### **Malengo ya Baraza la Taifa la Kusimamia na Kuhifadhi Mazingira**

**117. *Mheshimiwa Spika***, Baraza katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 limepanga kutekeleza yafuatayo katika mwaka 2019/20: -

- i) Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa Miradi ya Uwekezaji na kuchukua hatua stahiki kwa wataokiuka Sheria pamoja

na kushughulikia malalamiko wa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni zake;

ii) Kuandaa na kufanya mapitio ya nyezo na miongozo mbalimbali inayohusu uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake;

iii) Kuendesha maabara ndogo ya kimazingira kwa ajili ya kupima sampuli kwa hatua za awali katika kubaini uchafuzi katika mazingira;

iv) Kuboresha mfumo na mchakato wa TAM ili kuwezesha upatikanaji wa vyeti kwa haraka zaidi na kuendelea kutoa miongozo kwa wadau ili kuhakikisha TAM inazingatiwa kabla ya uwekezaji kufanyika;

v) Kuendelea kusajili miradi kwa ajili ya mchakato wa TAM, kusajili wataalam wa TAM na Wakaguzi wa Mazingira pamoja na kufanya vikao vya kinidhamu ili kufuatilia mienendo yao katika kutoa ushauri kwenye masuala ya Mazingira;

viii) Kufanya tathmini ya mifumo ikilojia katika bonde la maji la Rufiji katika eneo la mradi wa umeme wa Rufiji;

viii) Kuendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira kwa kufanya tafiti na tathmini mbalimbali za mazingira pamoja na kufuatilia shughuli za Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi;

ix) Kufanya mapitio ya miradi inayowasilishwa na wadau na kuiwasilisha kwenye Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ili iweze kupata ufadhili;

x) Kuandaa miongozo ya usimamizi wa mazingira katika maeneo lindwa na nyeti (Environmental Protected Areas - EPAs and Environmental Sensitive Areas - ESAs);

xi) Kufanya ufuatiliaji wa karibu wa shughuli zinazofanyika katika Mradi wa Uzalishaji Umeme wa Rufiji ili kuhakikisha hifadhi ya mazingira na usalama mahali pa kazi unazingatiwa;

- xii) Kuimarisha Usimamizi wa taka ngumu na kuboresha udhibiti wa utupaji wa taka hatarishi kwa kushirikiana na wadau;
- xiii) Kuongeza wigo wa mapato kwa kupitia utekelezaji wa kanuni ya Tozo pamoja na uandaaji wa Miradi ya Maendeleo;
- xiv) Kuendelea na kampeni za elimu ya mazingira kwa umma na kuifanya NEMC ijulikane zaidi kwa jamii;
- xv) Kuanza ujenzi wa Ofisi za kudumu katika kiwanja cha Baraza kilichopo eneo la Njendengwa, Dodoma; na
- xvi) Kuanzisha Ofisi ya Kanda ya Magharibi na kuimarisha Ofisi za Kanda zilizopo kwa kuongeza watumishi na vitendea kazi ili kuongeza ufanisi.

### **Miradi ya Maendeleo**

**118.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20 miradi mikubwa ifuatayo ya hifadhi na usimamizi wa mazingira imepangwa kutekelezwa: -

#### **i. Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame Tanzania**

**119.** *Mheshimiwa Spika*, katika mradi huu kazi zifuatazo zitatekelezwa:- Kuandaa Mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 17 katika Halmashauri tano ambazo ni Magu (3), Nzega (5), Mkalama (5) na Kondoa (4) na Wilaya ya Micheweni katika Shehia 8; Kuanzisha mashamba darasa kwa wakulima kuhusu kilimo, hifadhi na mbinu bora za kilimo rafiki kwa mazingira; Kutoa mafunzo ya uboreshaji na urutubishaji wa udongo, mbinu za kilimo cha misitu (agro-forest) na kilimo cha makinga maji; Kuchimba, kukarabati na kujenga mabwawa na visima na ununuzi wa matanki ya kuhifadhi maji; Kupanda miti kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi wa vijiji; na Kutambua teknolojia na maeneo yanayofaa kwa uvunaji wa maji ya mvua.

ii. **Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia**

**120.** *Mheshimiwa Spika*, katika mradi huu kazi zifuatazo zitatekelezwa:- Kujenga uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha mifumo ya ikolojia; Kufanya tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi na kutoa mapendekezo ya kukabillana na athari hizo; Kuunda mfumo wa ujuzi kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi (Formulation of Adaptation Knowledge Management System); Kuendesha mafunzo kwa wadau wa mradi kuhusu umuhimu wa Ikolojia katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi; Kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na Kutoa elimu ya matumizi ya majiko banifu na sanifu kwenye maeneo ya utekelezaji wa mradi.

iii. **Mradi wa Kusaidia Utekelezaji na Usimamizi wa Mbinu Jumuishi za Mazingira Katika Kuongoa na Kurejesha Ikolojia Iliyoharibika na Hifadhi ya Bioanuai**

**121.** *Mheshimiwa Spika*, katika mradi huu kazi zifuatazo zitatekelezwa: - Kuhuisha masuala ya hifadhi ya Bioanuai na matumizi endelevu ya huduma za ikolojia katika Sekta za uzalishaji; Kuwezesha matumizi endelevu na usimamizi wa ardhi katika mifumo ya uzalishaji (kilimo, safu, na misitu); na Kuongoa na kurejesha Ikolojia iliyoharibika katika sekta ndogo ya misitu.

iv. **Mradi wa Kusimamia Uhifadhi na Matumizi Endelevu ya Bonde la Ziwa Nyasa**

**122.** *Mheshimiwa Spika*, katika mradi huu kazi zifuatazo zitatekelezwa:- Kuwezesha uzalishaji wa mkaa endelevu pamoja na matumizi ya majiko sanifu na banifu; kutoa mafunzo kwa vikundi kuhusu usimamizi endelevu wa uvuvi pamoja na kuendeleza ujasiliamali; Kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wadogo wa madini na mchanga kuhusu uchimbaji endelevu; Kuanzisha na kujenga uwezo kwa jumua za watumia maji (*Establishment/Strengthening of Water Users Association*) kwa ajili ya usimamizi endelevu wa rasilimali za maji; na Kusaidia utekelezaji wa mipango shirikishi ya usimamizi wa misitu.

**123. Mheshimiwa Spika**, Miradi mingine itakayotekelezwa na Ofisi katika mwaka 2019/20 ni pamoja na:- Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi Kusimamia na Kupunguza Athari za Mazingira kwa Jamii za Vijijini Katika Sehemu zenye Ukame; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Sheria ya Mazingira; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi Kupunguza Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozone; Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Ufuatiliaji na Udhhibiti wa Taka Zinazodumu Katika Mazingira Kwa Muda Mrefu; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kusimamia Kemikali na taka nchini; na Mradi wa Kuhisha Uhusiano Kati ya Afya na Mazingira na Uwezo wa Kisheria na Kitaasisi Katika Udhhibiti wa Kemikali na Taka.

## HITIMISHO NA SHUKRANI

**124. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ni ya Muungano ambao una umuhimu wa pekee kwa Taifa na umekuwa ni utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu katika kudumisha Amani na Usalama wa nchi yetu. Mwaka huu Muungano wetu unatimiza miaka 55 tangu kuasisiwa kwake. Ninatoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano ili jitihada za kusukuma mbele maendeleo kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa faida za pande zote mbili.

**125. Mheshimiwa Spika**, chini ya uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Muungano wetu unaendelea kuimarika na kushamiri. Chini ya uongozi wao hakuna changamoto yoyote inayoweza kutufarakanisha, kututenganisha wala kuturudisha nyuma. Katika mwaka 2019/20 Ofisi na Serikali kwa ujumla itaendelea kuyafanyia kazi mambo yote yanayoleta changamoto katika utekelezaji wa masuala yanayohusu Muungano na kutoa elimu kuhusu Muungano ili uendeleo kuimarika.

**126. Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa mazingira katika mustakabali wetu na maendeleo ya uchumi



wa viwanda, ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira na maliasili za nchi yetu zinalindwa na kuhifadhiwa. Ninapenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla kuunga mkono juhudi za Serikali katika kulinda na kuhifadhi mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**127. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20, Ofisi imejipanga kuipa elimu ya mazingira kipaumbele kwa jamii ili kuhakikisha mazingira yanalindwa na kutunzwa. Aidha, Ofisi itahakikisha masuala yote yanayohusu uharibifu wa mazingira yanapatiwa ufumbuzi. Vilevile, Ofisi itaendelea kutoa miongozo ya hifadhi ya mazingira katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kuhifadhi mazingira kwa kuangalia mifumo ya ikolojia, mifumo ya uzalishaji mali, na mifumo ya uchumi ya matumizi ya rasilimali asili.

**128. Mheshimiwa Spika,** ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Shukrani zangu za dharti na za kipekee ni kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na dira na mwelekeo aliotupatia kuhusu majukumu yetu. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano anaonipa katika utekelezaji wa kazi za Ofisi. Vilevile, ninapenda kuwashukuru Mhandisi Joseph K. Malongo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; *Balozi* Joseph E. Sokoine, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais; Ndugu Ali Mufuruki, Mwenyekiti wa Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira na Wajumbe wa Bodi ya Mfuko huo; Dkt.Samuel Mafwenga Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Wakuu wa Idara na Vitengo; na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza kwa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu. Pia ninawashukuru wale wote waliotwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na

ambao wamesaidia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/20.

**129. Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Ninapenda kuwataja baadhi ya washirika wa maendeleo ambao Ofisi imefanya nao kazi kwa karibu kama ifuatavyo: Serikali ya Norway; Serikali ya Canada; Serikali ya Sweden; Serikali ya Italia; Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea; Umoja wa Nchi za Ulaya (*European Union - EU*); Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*United Nations Development Programme - UNDP*); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization - UNESCO*); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (*UNEP*); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Environment Facility - GEF*); Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma za Miradi (*United Nations Office for Project Services - UNOPS*); Benki ya Dunia (*World Bank - WB*); Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank - AfDB*); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*United Nations Industrial Development Organization - UNIDO*); Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Denmark (*Danish International Development Agency - DANIDA*); *World Wide Fund for Nature - WWF*; Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (*International Fund for Agricultural Development - IFAD*); Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund - GCF*); Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (*Food and Agriculture Organization - FAO*); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (*Gesellschaft fiir Internationale Zusammenarbeit - GiZ*); Kikundi cha Washirika wa Maendeleo kinachoshughulikia Mazingira (*Development Partners Group on Environment - DPGE*); Asasi Zisizo za Kiserikali (*AZISE*); na Sekta binafsi. Aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba washirika wa maendeleo kuendelea kutoa ushirikiano katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika kulinda na kuimarisha Muungano wetu na kulinda na kuhifadhi mazingira yetu.

## MAOMBI YA FEDHA

**130.** *Mheshimiwa Spika*, ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishhe maombi ya fedha kwa mwaka 2019/20, kama ifuatavyo:

### Fungu 26: Makamu wa Rais

**131.** *Mheshimiwa Spika*, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe Makadirio ya Matumizi ya Sh. **7,855,093,000** fedha za Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2019/20. Kiasi hiki kinajumuisha fedha za Mishahara ya watumishi Sh. **1,120,128,000** na fedha za Matumizi Mengineyo Sh. **6,734,965,000**.

### Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais

**132.** *Mheshimiwa Spika*, ninaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishhe makadirio ya matumizi ya Sh. **29,066,298,442** kwa Fungu hili. Kiasi hiki kinajumuisha Sh. **9,847,374,000** fedha za Matumizi ya Kawaida na Sh. **19,218,915,442** fedha za Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha Sh. **2,759,365,000** fedha za Mishahara na Sh. **7,088,009,000** fedha za Matumizi Mengineyo. Fedha za Matumizi Mengineyo zinajumuisha Sh. **2,808,957,000** Ruzuku ya Mishahara ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Fedha za Ndani Sh. **1,000,000,000** na Fedha za Nje Sh. **18,218,915,442**.

**133.** *Mheshimiwa Spika*, ninaomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ajiandae Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. (*Makofi*)

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI  
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kwa upekee kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha katika kila jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni na Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6(2)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano ina Mafungu mawili ya bajeti, ambayo ni Fungu 26 Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne kama yanavyoonekana hapo chini. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, kwa kuzingatia muundo wa majukumu ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais Muungano, hakukuwa na bajeti ya miradi ya maendeleo katika fungu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano katika kutekeleza Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 6309 – Ujenzi wa Ofisi na Nyumba ya Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar yaani (*Construction of Vice President Office and Residence in Zanzibar*), ambao uliidhinishiwa Shilingi Bilioni Moja na Mradi Na. 6389 – Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (*Luthuli II*) (*Construction and Rehabilitation of Vice President Office Luthuli II and State Lodges*), ambao uliidhinishiwa Shilingi milioni mia tano thelathini na nne na laki nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano ya tarehe 20 Machi, 2019, kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Mradi Na. 6389 wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (*Luthuli II*) ulikuwa umepokea fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge, Shilingi milioni mia tano thelathini na nne na laki nane sawa na asilimia 100. Hata hivyo, Mradi Na. 6309 haujapokea kiasi chochote cha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano Kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati Kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati imepokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019; uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili, 2018 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi, 2019 katika Robo ya Tatu ya mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kiasi cha fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia mwezi Machi, 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina; Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Fungu hili lilitengewa Shilingi bilioni sita, milioni mia nne themanini na tano, laki tisa tisini na moja elfu mia tano sabini na nane na senti tano kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni moja na milioni hamsini na tatu, laki sita sitini na sita elfu ilikuwa ni kwa ajili ya mishahara, na Shilingi bilioni tano, milioni mia nne thelathini na mbili, laki tatu ishirini na tano elfu, mia tano sabini na nane na senti tano ilikuwa ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2018 hadi mwezi Machi, 2019, jumla ya Shilingi bilioni nne, milioni mia tano sabini na mbili, laki nane na kumi elfu, mia tano sabini na nane na senti tano zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo. Kiasi hicho cha fedha kilichopokelewa ni sawa na asilimia 70.5% ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika Fungu 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Hazina kwa kutoa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati, hatua ambayo imesaidia Ofisi Binafsi ya Makamu Rais - Muungano kutekeleza Majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais; katika mwaka wa fedha 2018/2019, Fungu hili kwa ujumla lilitengewa Shilingi bilioni kumi na milioni mbili, themanini na mbili elfu, mia tano ishirini na tatu na senti ishirini na nane kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Ofisi hiyo ilipokea Shilingi bilioni tano, milioni mia tano thelathini na saba, laki saba tisini na tano elfu na tatu na senti ishirini na nane, sawa na asilimia 55.4% ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu unaonesha kuwa kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mafungu yote yaani Fungu 26 na Fungu 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa ujumla kwa kutoa fedha za matumizi ya kawaida kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 - Fungu 31; Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano iliidhinishiwa Shilingi bilioni moja, milioni mia tano thelathini na nane na laki nane kwa ajili ya Miradi Miwili ya Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Zanzibar) (Mradi Na.6309) na Mradi wa Kujenga na kukarabati Ofisi ya Makamu wa Rais *Luthuli II* (Dar es Salaam) (Mradi Na. 6389).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Mradi Na. 6389 wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais(Luthuli II) ulikuwa umepokea asilimia 100 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge, ambazo ni Shilingi milioni mia tano thelathini na nane na laki nane. Aidha, Kamati imebaini kuwa, Mradi Na. 6309 haukuwa umepokea kiasi chochote cha fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ni kuwa, Miradi hii imechukua muda mrefu, hivyo, Serikali ihakikishe Mradi Na. 6309 unaanza na kukamilika katika mwaka huu wa fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020; Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa mwaka wa fedha 2019/2020, tarehe 20 Machi, 2019, ambayo imelenga kutekeleza masuala ya Muungano kwa vipaumbele vilivyoainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi mwendelezo wa kuimarisha na kulinda Muungano wetu kwa manufaa ya Watanzania wote na kudumisha udugu, umoja na mshikamano wa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza sana Serikali, ya Awamu ya Tano kwa kuendeleza jitihada za dhati za Awamu ya Nne na zilzotangulia katika kutatua changamoto mbalimbali za Muungano kwa manufaa ya pande zote mbili na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020; Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi hii inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni saba milioni mia nane hamsini na tano na tisini na tatu elfu kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Mengineyo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni moja milioni mia moja ishirini laki moja ishirini na nane elfu ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi bilioni sita milioni mia saba thelathini na nne laki tisa sitini na tano elfu ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti ya Fungu 26 imeongezeka kwa kiasi



cha Sh.1,369,101,422 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 21.11% ya bajeti ya Fungu 26 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya Ofisi hiyo hususan gharama za utoaji huduma kwa Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Makamu wa Rais (Fungu 31) inaomba kuidhinishwa jumla ya Sh.5,357,575,560 kwa ajili ya Matumizi ya Mishahara na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, Sh.1,931,624,000 ni kwa ajili ya Mishahara na Sh.3,425,951,560 ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Fungu 31 imeongezeka kwa asilimia 4.5% ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kama ilivyoelezwa hapo juu, ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na uratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na uanzishwaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 (Fungu 31). Kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, Mradi mmoja wa Maendeleo unaendelea kuombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mradi huo ni Mradi Na.6309 wa Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar ambao unaombewa Sh.1,000,000,000. Kamati inapendekeza fedha hizo zitolewe kwa wakati kwa mwaka huu wa fedha 2019/2020 ili kurahisisha ukamilishaji wa mradi huo muhimu. Aidha, kuhusu kuanza utekelezaji wa Mradi huo kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha, Kamati inashauri Serikali itoe fedha*

*zilizopangwa na kuidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-*

*(i) Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika mwaka wa fedha 2018/2019, ikiwa ni pamoja na kuendelea na ukarabati wa magari na mitambo yote inayotumiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kununua magari mapya kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali chini ya Ofisi hii muhimu. (Makofi)*

*(ii) Kamati inaipongeza juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa kushirikiana na Mamlaka husika za pande mbili za Muungano katika kuendelea kutatua changamoto mbalimbali katika sekta ya biashara baina ya pande mbili za Muungano, hatua ambayo itachochea ukuaji uchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.*

*(iii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuratibu utekelezaji wa Waraka wa Mgao wa Muda wa Ajira (Quota) ambapo Taasisi za Muungano zinatakiwa kuzingatia matakwa ya Waraka huo pindi fursa za ajira zinapatikana.*

*(iv) Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuongeza na kuboresha vitendea kazi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa lengo kurahisisha utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.*

*(v) Kwa upande wa fedha za maendeleo kuhusu Mradi Na.6309, Kamati inashauri kuwa, fedha hizo kiasi cha Sh.1,000,000,000 kwa mradi huo zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu, zitolewe zote kwa wakati kwa mwaka*

*wa fedha 2019/2020 ili kurahisisha ukamilishaji wa mradi huo muhimu.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kukupongeza wewe mwenyewe kwanza binafsi kwa kasi ya kuliendesha Bunge hili. Pia napenda nitumie fursa hii kumpongeza Spika, Mheshimiwa Job Ndugai na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa weledi na umahiri wao katika kuliongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayofanya ya kushauri na kusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja nawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu tuliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Januari Makamba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano. Naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Angelina L. Sanga, Katibu wa Kamati hii, Ndugu Stanslaus Kagisa na Msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji

wote wa Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kwa kuhakikisha Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA  
SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA  
MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) KWA MWAKA WA FEDHA  
2018/2019; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6 (2) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rias - Muungano.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kinatoa Jukumu kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazosisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti

linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ina Mafungu 2 ya Bajeti ambayo ni:-

- i) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, na
- ii) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais,

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na;

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati

## **TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

***Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.***

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Muundo na Majukumu ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Muungano), hakukuwa na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo katika Fungu hili.

***Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano;***

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano. Orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

i) **Mradi Na. 6309** – Ujenzi wa Ofisi na Nyumba ya Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar (*Construction of Vice President Office and Residence in Zanzibar*), ambao uliidhinishiwa **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000/=)**, na

ii) **Mradi Na. 6389** – Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Luthuli II) (*Construction and Rehabilitation of Vice President Office Luthuli II and State Lodges*), ambao uliidhinishiwa **Shilingi Milioni Mia Tano Thelathini na Nne na Laki Nane (538,800,000/=)**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano ya tarehe 20 Machi, 2019, kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, **Mradi Na.6389** wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais(Luthuli II) ulikuwa umepokea fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge, **Shilingi Milioni Mia Tano Thelathini na Nne na Laki Nane (538,800,000/=)** sawa na asilimia 100%. Hata hivyo, **Mradi Na. 6309** haujapokea kiasi chochote cha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

#### **UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 20 Machi, 2019. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

#### ***Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya

Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2018 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2019 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa Fedha 2018/2019. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

***Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina***

**FUNGU 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 **Fungu 26** la Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais **lilitengewa Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Nne Themanini na Tano, Laki Tisa Tisini na Moja Eflu Mia Tano Sabini na Nane na Senti Tano (6,485,991,578.05/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Moja na Milioni Hamsini na Tatu, Laki Sita Sitini na Sita Eflu (1,053,666,000/=)** ilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nne Thelathini na Mbili, Laki Tatu Ishirini na Tano Eflu, Mia Tano Sabini na Nane na Senti Tano (5,432,325,578.05/=)** ilikuwa ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2018 hadi mwezi Machi 2019, **Jumla ya Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tano Sabini na Mbili, Laki Nane na Kumi Eflu, Mia Tano Sabini na Nane na Senti Tano(4,572,810,578,.05)**, zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo. Kiasi hicho cha Fedha kilichopokelewa ni sawa na **asilimia 70.5%** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika **Fungu 26**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Hazina kwa kutoa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati, hatua ambayo imesaidia Ofisi Binafsi ya Makamu Rais-Muungano kutekeleza Majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa.

**FUNGU 31: Ofisi ya Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 **Fungu 31** la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla lilitengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Milioni Mbili, Themanini na Mbili Eflu, Mia Tano Ishirini na Tatu na Senti Ishirini na Nane (10,002,082, 523.28/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Ofisi hiyo ilipokea **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tano Thelathini na Saba, Laki Saba Tisini na Tano Eflu na Tatu na Senti Ishirini na Nane (5,537,795,003.28)** sawa na **asilimia 55.4%** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, kwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mafungu yote (**Fungu 26 na Fungu 31**).

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa wakati.

***Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - FUNGU 31***

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano iliidhinishiwa **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Thelathini na Nane na Laki Nane (1,538,800,000/=)** kwa ajili ya Miradi Miwili ya Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Zanzibar) (**Mradi Na.6309**) na Mradi wa Kujenga na kukarabati Ofisi ya Makamu wa Rais *Luthuli II* (Dar es Salaam) (**Mradi Na.6389**).



**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha Juai, 2018 hadi Machi, 2019, **Mradi Na.6389** wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais(Luthuli II) ulikuwa umepokea **asilimia 100%** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge, ambazo ni **Shilingi Milioni Mia Tano Thelathini na Nane na Laki Nane (538,800,000/=)**. Aidha, Kamati imebaini kuwa, **Mradi Na. 6309** haujapokea kiasi chochote cha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, Miradi hii imechukua muda mrefu, hivyo, Serikali ihakikishe Mradi Na.6309 unaanza na Kukamilika katika mwaka huu wa Fedha, 2019/2020.

#### **UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 tarehe 20 Machi 2019, ambayo imelenga kutekeleza masuala ya Muungano kwa vipaumbele vifuatavyo:-

- i) Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) vya Kushughulikia masuala ya Muungano,
- ii) Kuratibu masuala ya kijamii na kiuchumi pamoja na kufuatilia utekelezaji wa program na Miradi ya Maendeleo kwa pande mbili za Muungano,
- iii) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Muungano kwa makundi mbalimbali ya kijamii, na
- iv) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zenye majukumu yanayoshabihiana.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi mwendelezo wa kuimarisha na kuulinda Muungano wetu kwa manufaa ya Watanzania wote na kudumisha Udugu, Umoja na Mshikamano wa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuendeleza jitihada za dhati za Awamu Nne zilizotangulia, katika kutatua changamoto mbalimbali za Muungano, hususan, kuendelea kurahisisha mwingiliano wa kibiashara baina ya Pande mbili za Muungano kwa kuzitafutia ufumbuzi kero mbalimbali za kikodi na kisheria kwa manufaa ya pande zote mbili na wananchi wake kwa ujumla.

### ***Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020***

#### **Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (**Fungu 26**) inaomba kuidhinishwa jumla ya **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Nane Hamsini na Tano na Tisini na Tatu Eflu (7,855,093,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Ishirini, Laki Moja Ishirini na Nane Eflu (1, 120,128,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Thelathini na Nne, Laki Tisa Sitini na Tano Eflu (6,734,965,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, Bajeti ya **Fungu 26** imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Sitini na Tisa, Laki Moja na Moja Eflu, Mia Nne Ishirini na Mbili (1,369,101,422)** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ongezeko hilo ni sawa na **asilimia 21.11%** ya Bajeti ya **Fungu 26** kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya Ofisi Ofisi hiyo hususan gharama za utoaji huduma kwa Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

### **Fungu 31; Ofisi ya Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Makamu wa Rais (**Fungu 31**) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Hamsini na Saba, Laki Tano Sabini na Tano Eflu, Mia Tano Sitini (5,357,575,560/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Mishahara na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Thelathini na Moja, Laki Sita Ishirini na Nne Eflu (1,931,624,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nne Ishirini na Tano, Laki Tisa Hamsini na Moja Eflu, Mia Tano Sitini, (3,425,951,560/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa **Fungu 31** imeongezeka kwa **asilimia 4.5%** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya Fungu hili kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kama ilivyoelezwa hapo juu, Ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na uratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania(SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na uanzishwaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar.

### ***Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 (FUNGU 31).***

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano, Mradi mmoja wa Maendeleo unaendelea kuombewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Mradi huo ni **Mradi Na. 6309** wa Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar ambao unaombewa **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000/=)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza Fedha hizo zitolewe kwa wakati kwa Mwaka huu wa Fedha 2019/2020 ili kurahisisha ukamilishaji wa mradi huo muhimu. Aidha, kuhusu kuanza utekelezaji wa Mradi huo kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha, Kamati inashauri Serikali itoe fedha zilizopangwa na kuidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kama ifuatavyo:-

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, ikiwa ni pamoja na kuendelea na ukarabati wa Magari na Mitambo yote inayotumiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kununua Magari mapya kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa Majukumu mbalimbali chini ya Ofisi hii muhimu.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa kushirikiana na Mamlaka husika za pande mbili za Muungano katika kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya biashara baina ya Pande mbili za Muungano, hatua ambayo itachochea ukuaji Uchumi kwa Mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuratibu utekelezaji wa Waraka wa Mgao wa Muda wa Ajira (*Quota*) ambapo Taasisi za Muungano zinatakiwa kuzingatia matakwa ya Waraka huo pindi fursa za Ajira zinapatikana.

iv) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuongeza na kuboresha vitendea kazi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa lengo kurahisisha utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.

v) **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fedha za Mandeleo kuhusu **Mradi Na.6309**, Kamati inashauri kuwa, Fedha hizo kiasi cha **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000/=)** kwa

Mradi huo zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu, zitolewe zote kwa wakati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kurahisisha ukamilishaji wa mradi huo muhimu.

### HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda nikupongeze kwa umahiri wako katika kasi ya kullendesha Bunge hili katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania, pia, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaomba afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhe. Januari Makamba, (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Mussa Ramadhan Sima,(Mb), Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano. **NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI YA BUNGE (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengera, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;

6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe;
22. Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb - Mjumbe;
23. Mhe. Dkt. Suzan Alphonse Kolimba, Mb - Mjumbe;

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) kwa kuhakikisha Taarifa hii inatoka wa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais -Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.  
**MWENYEKITI,**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**  
16 APRILI, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

**MHE. KANALI MST. MASOUD ALI KHAMIS - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi wa Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai kuweza kufikia siku ya leo ambapo tumekutana kwa ajili ya kujadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira. Kwa kuzingatia umuhimu wa yaliyomo kwenye taarifa hii pamoja na muda wa kutoa maoni, naomba taarifa yote ya Kamati kama ilivyo katika kitabu iingie katika kumbukumbu za taarifa za Bunge yaani *Hansard*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Fungu 31 kwa

mwaka 2018/2019 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilizingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambapo ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019, kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na kuchambua Mpango na Bajeti kwa mwaka fedha wa 2019/2020 kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha maombi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi ili kuboresha shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo yafuatayo. Moja, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mbili, matokeo ya ukaguzi ya miradi ya maendeleo. Tatu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira mwaka wa fedha 2018/2019. Nne, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/2020. Tano, maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa mwaka 2018/2019. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Katika uchambuzi huo, Kamati ilitumia mapitio ya taarifa



zilizowasilishwa, matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya mazingira pamoja na mahojiano wakati wa vikao. Lengo la njia hizo lilikuwa ni kujiridhisha kuhusu ukusanyaji wa mapato, utekelezaji wa malengo/kazi na upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 17 Aprili, 2018, Bunge lako Tukufu lilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira – *NEMC* lilipanga kukusanya Sh.18,877,446,995 kutoka vyanzo vya ndani vya Baraza. Lengo hili la makusanyo lilikuwa limezidi lengo la mwaka wa fedha 2017/2018 kwa asilimia 20.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2019, *NEMC* ilikuwa imekusanya SH.10,430,060,727 kiasi ambacho ni pungufu ya lengo kwa asilimia 44.8 ya kiasi kilichopangwa kukusanywa kwa mwaka huu wa fedha. Takwimu hizo zinaonesha kuwa katika robo moja ya kipindi cha utekelezaji, *NEMC* itakusanya asilimia 44.8 ya lengo la makusanyo jambo ambalo si la kawaida/uhalisia. Aidha, Takwimu hizi zinaashiria kuwa lengo hili lilipangwa bila kuzingatia uhalisia wa uwezo wa *NEMC* wa kukusanya na upungufu huu unaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya *NEMC* kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kutokana na uwezekano mdogo wa kukusanya asilimia 44.8 iliyobaki kwa mwaka wa fedha unaoishia, Kamati imeishauri *NEMC* kupanga lengo la makusanyo kwa kuzingatia uwezo wake wa kukusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira iliidhinishwa jumla ya Sh.8,118,494,000.00 kwa ajili ya matumizi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2019, Ofisi hii ilikuwa imepokea Sh.4,167,969,635.79 tu, sawa na asilimia 51.3 ya fedha zote zilizokuwa zimeidinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kiasi kilichopokelewa ni pungufu kwa asilimia 48.7. Kwa kipindi hiki cha robo ya nne ya mwaka wa Fedha 2018/2019 ilitarajiwa zaidi ya asilimia 75 ya fedha

zilizoidhinishwa na Bunge ziwe zimepokelewa tofauti na ilivyo sasa ambapo ni asilimia 51.3 tu ndiyo ilikuwa imepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya Sh.3,524,540,000.00 ya fedha za Miradi ya Maendeleo ni Sh.1,861,299,489.50 tu ndizo zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, kiasi hicho ni fedha za nje. Vilevile, Kamati ilibaini kuwa katika fedha za maendeleo kulikuwa na fedha za ndani ambazo ni Sh.1,461,200,000.00 lakini hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019 zilikuwa hazijapokelewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu unadhihirisha kuwa baadhi ya majukumu ya usimamizi wa mazingira yameshindwa kutekelezwa ipasavyo hususani miradi ya maendeleo. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za hifadhi ya mazingira si wa kuridhisha kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo hususani fedha za ndani. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati na msisitizo katika kuwezesha shughuli za usimamizi wa mazingira kwa kutenga fedha za kutosha zikiwepo fedha za ndani na kuzipeleka kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kazi zilizopangwa kuhusiana na hifadhi na usimamizi wa mazingira zilitekelezwa. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuongeza juhudi katika majukumu sita kama ilivyooneshwa katika taarifa hii.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Jumla kuhusu utekelezaji wa bajeti. Matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – mazingira kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira yanaonesha kuwa upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa shughuli za Idara ya Mazingira (fedha za matumizi ya kawaida) umekuwa mzuri ukilinganisha na upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo hususani fedha za ndani ambapo hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2019, kati ya fedha zote za Miradi ya*

*Maendeleo ni fedha za nje tu ndizo zilikuwa zimepokelewa jambo ambalo halitoi picha nzuri kwa wahisani wetu. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Fungu 31, iliidhinishiwa Sh.3,524,540,000.00 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh.1,461,200,000.00 ni fedha za ndani na Sh.2,063,340,000.00 fedha za nje. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi - Bagamoyo (Mradi Namba 5301); Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za NEMC (Mradi Namba 6507) na shughuli za uhifadhi mazingira katika Ziwa Manyara. Ufafanuzi wa miradi ya maendeleo na shughuli za mazingira zilizotembelewa na kukaguliwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kama ilivyoonekana katika taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembelea hifadhi ya mazingira Manyara kwa lengo la kujionea hali ya mazingira katika eneo la hifadhi ambayo inahusisha na Ziwa Manyara na kuangalia changamoto na mkakati wa Serikali katika kukabiliana na athari za kimazingira katika eneo hilo la hifadhi. Shughuli za hifadhi na mazingira katika Ziwa Manyara zinatekelezwa na TANAPA na zinahusisha kutoa elimu ya mazingira na sheria, usimamizi wa mazingira katika ngazi za Wilaya na Halmashauri ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa Mazingira katika Ziwa Manyara unakumbana na changamoto ya ukosefu wa fedha za kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika eneo la hifadhi, jambo linalopelekea athari za uharibifu unaofanywa kuendelea na kupelekea kuhatarisha eneo la hifadhi hususani Ziwa Manyara. Pia Shughuli za binadamu (kilimo kisichofuata kanuni za kitaalamu, uwepo wa mifugo mingi) katika maeneo ya karibu na Ziwa Manyara zinazopelekea mmomony'oko wa udongo na kupelekea tope jingi kuelekea ziwani na kupunguza kina cha maji kupelekea kukauka kwa ziwa. Takwimu zinasema katika kipindi cha miaka 35 ya karibuni

(1980-2015) hali imezidi kuwa mbaya ambapo matukio ya kukauka Ziwa yalikuwa 7 wakati kati ya mwaka (1920-1970) ziwa liliripotiwa kukauka mara tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni mabadiliko ya tabianchi ambayo hupelekea ukame na kukauka kwa vyanzo vya maji yatirikayo kwenda ziwani na kupelekea kukauka kwa Ziwa manyara. Vilevile, shughuli za kibinadamu katika eneo la hifadhi zisizolenga matumizi endelevu ya rasilimali za asili jambo linalopelekea kuharibu mfumo ikolojia ya Tarangire na Ziwa Manyara na kuviweka katika hatari ya kutoweka na mimea vamizi/wageni katika baadhi ya vyanzo vya maji vya Ziwa Manyara ambavyo hupelekea maji kushindwa kufika ziwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ziara katika Ziwa Manyara Kamati ilikuwa na maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kwa kuwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya kusimamia mazingira kuliingiza katika orodha ya maeneo lindwa eneo lolote linaloonekana lipo katika hatihati za kutowekea, Serikali ifanye haraka kuanza mchakato wa kuliingiza Ziwa Manyara katika maeneo lindwa. Hatua hii ichukuliwe kwa maziwa yote ambayo yapo katika hatari ya namna hii likiwepo ziwa Jipe na Chala.

(ii) Serikali kuangalia namna ya kuwasaidia na kuwasimamia wakulima na wafugaji kufanya shughuli zao mbali na miinuko. Shughuli hizi zimekuwa zikiporomosha udongo na tope katika Ziwa Manyara.

(iii) Ziwa Manyara na Bioanuai zipatikanazo katika ziwa hili ni moja ya kivutio kikubwa kinachovuta utalii katika Hifadhi ya Manyara, changamoto zinazopelekea kukauka kwa Ziwa Manyara kunahatarisha na kupelekea kupungua kwa shughuli za utalii katika Hifadhi ya Manyara. Serikali ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha wanalinusuru Ziwa Manyara.

(iv) Kuna udhaifu katika kusimamia Sheria za Mazingira na Sheria ndogondogo za Vijiji na Halmashauri jambo linalotoa mianya kwa baadhi ya watu kuendelea shughuli zao katika eneo la hifadhi. Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya kufutilia na kusimamia matakwu ya sheria ili kuzuia shughuli zisizo endelevu katika eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya mwaka 2018/2019, Kamati ilikuwa na maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo na inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali kulipa uzito suala la hifadhi ya mazingira kwa kutenga fedha za maendeleo na kuzipeleka kwa wakati. Kwa sasa asilimia kubwa ya Miradi ya Maendeleo ya Mazingira inatekelezwa kwa kutumia fedha za wafadhili jambo ambalo si sahihi sana.

(ii) Sekta asili (kilimo, ufugaji na uvuvi) kwa kiasi kikubwa ndiyo zinategemewa katika uchumi wa nchi yetu na maendeleo ya sekta hizi kwa kiasi kikubwa yanategemea uhifadhi wa mazingira. Jambo la kushangaza shughuli hizi hizi zimekuwa zikiendeshwa bila kuzingatia taratibu za kitaalamu. Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira, pia kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za asili hususani misitu na vyanzo vya maji.

(iii) Sheria ya Mazingira inayotekelezwa sasa ni ya mwaka 2004 lakini inatekelezwa kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997. Sera hii ni ya zamani takribani miaka 22 na haijahusisha mabadiliko mengi ambayo yameendelea kutokea katika mazingira mfano mabadiliko ya tabianchi na viumbe vamizi. Kamati inashauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuandaa Sera mpya itakayoendana na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilifuatilia uzingatiaji wa ushauri iliyoutoa wakati wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira mwaka

wa fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali na kutoa maagizo kumi na mbili (12). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati na kutekeleza maagizo hayo. Hata hivyo, kuna maeneo manne ambayo serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; kabla ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi katika jukumu la kuhifadhi na kusimamia mazingira, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2019/2020. Lengo lilikuwa ni kufuatilia tija inayoweza kupatikana kutokana na malengo yaliyopangwa na ofisi hii kwa fedha zinazoombwa katika kifungu 5003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ililinganisha malengo ya mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020 na katika ulinganisho huo Kamati ilibaini yafuatayo:-

Moja, malengo yote yaliyozingatia hati idhini ya Serikali iliyoainishwa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

Pili, lengo Na.2 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na lengo la 12 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 yanaendana na kwamba yote yanajielekeza kwenye udhibiti wa utupaji taka ngumu na hatarishi.

Tatu, lengo linahususha udhibiti wa taka ngumu kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ni mwelekeo wa uzingatiaji wa ushauri uliowahi kutolewa na Kamati hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa wenyekiti, aidha, agizo la Waziri Mkuu alilolitoa akihitimisha hoja Bungeni tarehe 9/4/2019, linatoa nguvu ya msisitizo kama ilivyotolewa na Kamati ya mwaka

2017/2018. Kwa uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupokea ushauri uliotolewa na Kamati na kutoa muda wa kutosha kwa wawekezaji hao kuanzia Agosti, 2017 hadi Mei, 2019 na ni matumaini ya Kamati kuwa wawekezaji hao watakuwa wametumia vizuri muda uliotolewa na Serikali, hivyo kuweza kutumia teknolojia nyingine na kuwezesha kuzalisha mifuko mbadala.

Aidha, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kufuatilia utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu na kuhakikisha ifikapo tarehe 30 Mei, 2019 matumizi ya mifuko ya plastiki yatakuwa yamefika mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya mapato. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Makamu wa Rais chini ya Fungu 31 inalenga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 18.2 kutoka katika vyanzo vya ndani vya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) ambayo ni ada, faini zitokanazo na shughuli za usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kiasi kinachotengwa kukusanywa kinakaribiana kabisa na malengo ya mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo yalitekelezwa kwa asilimia 55.2 tu hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha, kipindi ambacho walipaswa kukusanya asilimia 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huu, Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

Moja, kupanga lengo la makusanyo kwa kuzingatia kasi na uwezo wake wa kukusanya; pili, wakati wa kupanga lengo la makusanyo, izingatie changamoto zilizokwamisha kufikia lengo la makusanyo la mwaka wa fedha uliotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa wingi wa mapato yatokanayo na shughuli za mazingira ni mkubwa, lakini kasi ya ukusanyaji bado ni ndogo. Kamati inashauri Serikali kuiongezea *NEMC* uwezo kwa kuwapatia

matumizi na vitendea kazi ili waweze kuongeza kasi ya ukaguzi na hatua ambayo itaongeza mapato kwa Baraza pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uchambuzi wa bajeti ya matumizi. Bajeti ya matumizi kwa ajili ya shughuli za Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira hutengwa katika Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais. Kamati ilijulishwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 22.7 zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu muhimu. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 179.71 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa ongezeko la bajeti ya shughuli za Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lina athari katika fedha za miradi ya maendeleo ambayo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 3.52 mwaka 2018/2019 mpaka shilingi bilioni 18.2 mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni maoni ya jumla kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Tanzania ni nchi mwanachama wa mikataba mingi ya Kimataifa inayohusishwa na mambo ya Mazingira. Kupitia mikataba hiyo, nchi hii ina fursa ya kupata fedha za maendeleo kwa kuandika maandiko ya miradi na kuyawasilisha katika Taasisi za Mazingira Duniani. Kamati imebaini kuwa kama nchi, haijatumia fursa hiyo ipasavyo, kwa kuwa hatujaandika maandiko ya kutosha ambayo yanawezesha upatikanaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira siyo wa kuridhisha, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) na wadau wengine wa mazingira kuchangamkia fursa hii kwa kuongeza kasi na kuandaa maandiko ya kutosha yenye uhalisia na kuyawasilisha katika taasisi za Kimataifa kila fursa inapotokea. Juhudi hizo zitapelekea kuongezeka kwa fedha za uhifadhi na utunzaji wa mazingira nchini.



Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuwatambua wadau wote wa mazingira hususan *NGO's* ambao wanatumia fursa hii kupata fedha za miradi. Umuhimu wa kuwatambua wadau hawa ni kuwawezesha Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuweza kuwafuatilia na kuhakikisha fedha wanazozipata zinatumika kutekeleza miradi inayokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati: Hali ya Mazingira nchini siyo ya kuridhisha. Tafiti zimeonesha kuwa tafiti zilizofanyika na kubainisha hali mbalimbali zinaashiria jambo hili. Kamati ilipata fursa wakati wa ziara zake za ukaguzi wa miradi, kutembelea na kushuhudia hali isiyo ya kuridhisha ya mazingira katika baadhi ya maeneo nchini. Kamati imebainisha maeneo machache tu ambayo yanadhihirisha hali mbaya ya mazingira kwa lengo la kutoa picha ya kuathirika kwa mazingira ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo ni pamoja na:-

Moja, athari za mabadiliko ya tabia nchi, ambazo zimeshadhihirika katika maeneo mbalimbali nchini. Athari hizo ni pamoja na ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, kuongezeka kwa ujazo wa maji baharini, kuharibu kingo za bahari na fukwe, kumezwa kwa visiwa vidogo kwenye bahari na kuathiri *water table*, kuyeyuka kwa barafu katika vilele vya milima kama vile Mlima Kilimanjaro, uharibifu wa madaraja, barabara, reli na makazi kutokana na mafuriko,

Pili, hali ya ukame na jangwa nchini; tafiti zinaonesha kuwa asilimia 61 ya nchi ipo hatarini kugeuka jangwa. Baadhi ya Mikoa iliyoathirika zaidi na hali ya ukame nchini ni pamoja na Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Manyara na baadhi ya maeneo ya Mikoa wa Kilimanjaro. Kwa kiasi kikubwa hali hii inatokana na matumizi ya yasiyo endelevu ya rasilimali asili nchini.

Tatu, takwimu za ukataji wa misitu zinaonesha kuwa, msitu wenye ukubwa wa kiwanja cha mpira hufyekwa kila baada ya dakika moja. Takwimu hizi zimepelekea Tanzania kuwa katika ya nchi tano za juu (*top five*) zinazoongoza kwa ukataji wa misitu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeingia katika orodha ya nchi zenye upungufu wa maji ikilinganishwa na mahitaji, hali hiyo ni moja ya kiashiria cha uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maziwa yaliyopo kwenye hatari ya kupotea ni Ziwa Manyara, Jipe na Chala. Kupotea kwa maziwa haya kwa kiasi kikubwa kimechangiwa na shughuli za kibinadamu zinazoendeshwa katika maeneo ya ziwa ambapo hupelekea uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni baadhi tu ya maeneo ambayo yameonekana kuwa hali ya mazingira nchini siyo ya kuridhisha. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada za kimakusudi kwa lengo la kunusuru nchi kutokana na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira mwaka 2018/2019, pamoja na mapendekezo na mapato ya mwaka wa fedha 2019/2020 ya ofisi hii, Kamati imekuwa na maoni na ushauri kadhaa kwa Serikali. Ni imani ya Kamati kuwa, maoni na ushauri huu yatafanyiwa kazi hivyo kupelekea kuboresha shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka kadhaa tumeshuhudia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira imeendelea kutengewa bajeti ndogo ukilinganisha na ukubwa wa jukumu walilionalo la uhifadhi wa Mazingira. Kuna vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo vinatokana na mazingira lakini vyanzo hivi vinaingia katika mfuko ambao haurudishi katika shughuli za hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuwa vyanzo hivi vimeshaainishwa na kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri. Kamati inasisitiza Serikali kuhakikisha katika mwaka wa fedha 2019/2020, kwa kuanzia na angalau na vyanzo vitano tu vichangie katika Mfuko wa Mazingira kwa asilimia tano. Hatua hii itasaidia kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali katika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwa, baada ya kupitisha vyanzo hivi vya mapato ya Mfuko, ifanye maboresho katika Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 Sura ya 191 ili iwezeshe kutambua na kusimamia utekelezaji wa sekta zote zinazotakiwa kuchangiwa na mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira imemtambua na kumpa majukumu makubwa Afisa Mazingira. Pamoja na kuwa Afisa Mazingira anapewa majukumu na Sheria ya Mazingira na analengwa kumsaidia Mkurugenzi wa Mazingira, lakini ni mwajiriwa wa Halmashauri na anaripoti kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Aidha, taarifa ya kazi anazozifanya Afisa wa Mazingira ili zimfikie Mkurugenzi wa Mazingira ni lazima zipitie TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wamewezesha kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali katika kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa January Makamba; Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, , Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutoa maelekezo mbalimbali ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati hii. Aidha,

napenda kukushukuru wewe mwenyewe kwa kutupa nafasi ya kutoa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Fedha na Uchumi Bwana Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni kiasi cha shilingi 22,708,713,882.00 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA AZINGIRA CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) FUNGU 31 KWA MWAKA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya hifadhi na usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Fungu 31 kwa Mwaka 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambapo ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019, kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na kuchambua Mpango na Bajeti kwa Mwaka Fedha wa 2019/2020 kama inavyoelekeza na Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi yatasidia kuboresha shughuli za hifadhi na usimamizi wa Mazingira.

## **2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/2019 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

### **2.1 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilichambua Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Katika uchambuzi huo, Kamati ilitumia mapitio ya taarifa zilizowasilishwa, matokeo ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Mazingira pamoja na mahojiano wakati wa vikao. Lengo la njia hizo lilikuwa ni kujiridhisha kuhusu ukusanyaji wa mapato, utekelezaji wa malengo/kazi na upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

### 2.1.1 Makusanyo ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 17 Aprili, 2018 Bunge lako tukufu lilijulishwa kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira – *NEMC* lilipanga kukusanya Shilingi **18,877,446,995** kutoka vyanzo vya ndani vya Baraza. Lengo hili la Makusanyo lilikuwa limezidi lengo la Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa asilimia 20.4.

Uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2019, *NEMC* ilikuwa imekusanya Shilingi **10,430,060,727** kiasi ambacho ni pungufu ya lengo kwa asilimia **44.8** ya kiasi kilichopangwa kukusanywa kwa mwaka huu wa fedha. Takwimu hizo zinaonesha kuwa katika robo moja ya kipindi cha utekelezaji, *NEMC* itakusanya asilimia **44.8** ya lengo la makusanyo jambo ambalo si la kawaida/uhalisia. Aidha, Takwimu hizi zinaashiria kuwa;-

i) Lengo hili lilipangwa bila kuzingatia uhalisia wa uwezo wa *NEMC* wa kukusanya;

ii) Upungufu huu unaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya *NEMC* kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uwezekano mdogo wa kukusanya asilimia **44.8** iliyobaki kwa Mwaka unaoishia wa fedha, Kamati imeishauri *NEMC* kupanga lengo la makusanyo kwa kuzingatia uwezo wake wa kukusanya.

### 2.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **8,118,494,000.00** kwa ajili ya matumizi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2019 Ofisi hii ilikuwa imepokea shilingi **4,167,969,635.79** tu, sawa na asilimia **51.3** ya fedha zote zilizokuwa zimeidinishwa na Bunge.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kiasi kilichopokelewa pungufu kwa asilimia **48.7**. Kwa kipindi hiki cha robo ya nne

ya Mwaka wa Fedha **2018/2019** ilitarajiwa zaidi ya asilimia **75** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge ziwe zimepokelewa tofauti na ilivyo sasa ambapo ni asilimia **51.3** tu ndio ilikuwa imepokelewa.

Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya shilingi **3,524,540,000.00** ya fedha za Miradi ya Maendeleo ni shilingi **1,861,299,489.50** tu ndizo zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, kiasi hicho ni fedha za nje.

Vilevile, Kamati ilibaini kuwa katika fedha za maendeleo kulikuwa na fedha za ndani ambazo ni shilingi **1,461,200,000.00** lakini hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha **2018/2019** zilikuwa hazijapokelewa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huu unadhihirisha kuwa baadhi ya majukumu ya usimamizi wa mazingira yameshindwa kutekelezwa ipasavyo hususani miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za hifadhi ya mazingira si wa kuridhisha kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo hususani fedha za ndani. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati na msisitizo katika kuwezesha shughuli za usimamizi wa mazingira kwa kutenga fedha za kutosha zikiwepo fedha za ndani na kuzipeleka kwa wakati.

### **2.1.3 Utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuiwezesha Kamati kujiridhisha na dhamira ya Bunge kuiidhinisha Bajeti kwa ajili ya Shughuli za Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira, Kamati ilijulishwa kuhusu utekelezaji wa kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha **2018/2019**. Jumla ya kazi Kumi na Sita (16) zilipangwa kutekelezwa na taarifa ya Waziri ilibainisha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji huo.

Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa mwaka wa fedha **2018/2019**, kazi zilizopangwa kuhusiana na Hifadhi na usimamizi wa mazingira zilitekelezwa. Hata hivyo, Kamati inaendela kuisisitiza Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuongeza juhudi katika majukumu yafuatayo:-

i) Kukamilisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira 1997 na mkakati wa utekelezaji wake kwa lengo la kuihuisha iweze kuendana na mazingira halisi ya sasa ya mazingira (ihusishe mabadiliko yote yaliyotokea katika mazingira ambayo hayakuwepo miaka ya 1997) ili iweze kuboresha usimamizi wa shughuli za mazingira;

ii) Kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa kudhibiti Viumbe vamizi (Invasive Alien Species) kwa lengo la kuokoa maisha ya binadamu, mazingira na bioanuai zote na athari za viumbe vamizi ambazo miaka ya hivi karibuni zimeendelea kushamiri;

iii) Kukamilisha Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira Nchini na kuiwasilisha Bungeni kama inavyoelekezwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Mwaka 2004. Sheria ya Mazingira inaelekeza kuwa Ripoti ya Hali ya Mazingira Nchini iwasilishwe Bungeni kila baada ya miaka miwili lakini kwa kipindi kirefu sasa haijawasilishwa;

iv) Kukamilisha mchakato wa kuokoa Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kulinusuru kwa kuwa lipo hatarini kupotea kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu zinazoendeshwa katika eneo la bonde bila kuzingatia taratibu na sheria;

v) Kuendelea kulisimamia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira – NEMC kuhakikisha wanaongeza kasi ya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na kanuni zake kwa lengo la kudhibiti na kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira;

vi) Kuongeza jitihada katika kutekeleza kampeni za Upandaji miti hususani katika maeneo ambayo yameathirika



sana na ukame, sambamba na hili Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira iweke utaratibu wa ufuatiliaji wa miti iliyopanda katika kampeni mbalimbali za upandaji miti na zawadi zitolewe kwa maeneo ambayo kampeni hizo zimefanikiwa (wahasika wameitunza mpaka kukua); na

vii) Kundelea kusimamia utekelezaji wa masharti ya mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Ofisi hii imeridhia kwa niaba ya nchi, kwa kuwa mikataba hii imekuwa ya manufaa sana kwa Tanzania na kwa kiasi kikubwa kwani inasaidia kupata fedha za kupambana na athari za uharibifu wa mazingira.

## **2.2 Maoni ya Jumla kuhusu utekelezaji wa Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuhusu hifadhi na Usimamizi wa Mazingira yanaonesha kuwa Upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa shughuli za Idara ya Mazingira (fedha za matumizi ya kawaida) umekuwa mzuri ukilinganisha na upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo hususani fedha za ndani ambapo hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2019, kati ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo ni fedha za nje tu ndizo zilikuwa zimepokelewa jambo ambalo halitoi picha nzuri kwa wahisani wetu.

### **2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

#### **2.3.1 Mapitio ya Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inazitaka Kamati za Sekta, kutumia siku zisizozidi saba kwa kutembelea na kukagua miradi ya Maendeleo. Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira Fungu **31**, iliidhinishiwa shilingi

**3,524,540,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kati ya fedha hizo Shilingi **1,461,200,000.00** ni Fedha za ndani na Shilingi **2,063,340,000.00** fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi - Bagamoyo (**Mradi Namba 5301**), Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za NEMC (**Mradi Namba 6507**) na shughuli za Uhifadhi mazingira katika Ziwa Manyara, maelezo ya utekelezaji wa miradi hiyo ni kama yanavyoonekana katika taarifa hii.

**a) Mradi wa Mabadaliko ya Tabianchi Bagamoyo (Mradi Namba 5301)**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 18 Machi, 2019 Kamati ilitembelea **Mradi Namba 5301** wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa eneo la Bagamoyo. Lengo la Kamati kutembelea Mradi huu ni kubaini namna Mabadiliko ya tabianchi yameathiri mazingira yetu na kwa namna Serikali inakabiliana na athari zake.

**Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya tabianchi ni jambo dhahiri na athari zake zimeendelea kuonekana katika maeneo mbalimbali Duniani. Ongezeko la usawa wa bahari (sea level rise) kwa sentemita **19** katika kipindi cha miaka **50** iliyopita ni moja za athari za mabadiliko ya Tabiachi. Kwa Tanzania ongezeko la usawa wa bahari limechangia uharibifu wa mwambao wa Pwani hususani katika maeneo ya Kisiwa Panza Zanzibar, Mto Pangani, Fungu la Nyani Rufuji, na baadhi ya visima vya maji baridi katika maeneo ya Bagamoyo kuharibiwa na maji chumvi. Katika kutambua hilo, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inatekeleza Miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (**Mradi namba 5301**).

**Mheshimiwa Spika**, kama nilivyokwisha eleza kuwa athari ya Mabadiliko ya Tabianchi katika Pwani ya Bagamoyo imeathiri visima vya asili baada ya kina cha maji ya bahari kuongezeka na kufikia usawa wa meza ya maji (water table) na kupelekea maji hayo ya bahari kuingia katika visima vya asili na kuleta madhara kwa watumiaji wa maji ya visima hivyo. Kwa

Bagamoyo mradi huu umehusisha ujenzi wa visima vikubwa vya maji masafi na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji maji ya mvua.

Mradi unatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira chini ya ufadhili wa *Least Development Countries Fund-LDCF* na umegharimu takriban jumla ya Shilingi **1,171,668,189/=**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ziara ya Kamati Mradi ulikuwa umekamilika na kazi zifuatazo zilikuwa zimatekelezwa:-

i) Ujenzi wa miundombinu ya uvunaji maji ya mvua katika shule ya Sekondari ya Kingani Matipwili;

ii) Uchimbaji wa visima na ujenzi wa matanki kumi (10) katika maeneo ya Ukanda wa Pwani wa Bagamoyo; na

iii) Mafunzo ya ufahamu wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi na athari zake kwa wakazi wa Ukanda wa Pwani wa Bagamoyo.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa katika utekelezaji wa Mradi ilikuwa ni ufinyu wa Bajeti, jambo lililopelekea malengo ya kuchimba visima 17 na miundombinu mitatu (3) ya kuvuna maji ya mvua kutofikiwa na badala yake kuchimba visima 10 na miundombinu ya kuvuna maji ya mvua miwili (2) tu. Pia Mradi ulikabiliwa na Mvua nyingi za masika zilizopelekea baadhi ya maeneo ya miradi kushindwa kufikika na kupelekea kuchelewa kukamilika. Vilevile, kuwepo na changamoto ya nguvu ndogo ya umeme (Low voltage) wa TANESCO katika maeneo matatu ya visima hali iliyopelekea miradi ya eneo hilo kuchelewa kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa **Mradi Namba 5301, Fungu 31** unaohusu Mabadiliko ya Tabianchi Wilayani Bagamoyo ni:-

i) Serikali itumie mradi huu kama mfano, na kwa kupitia Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira Serikali ijipange kutafuta miradi mingine mingi ya aina hii ili kupunguza

changamoto ya maji, lakini pia kuwaokoa wananchi kuendelea kutumia maji yasiyo salama; (kwa sasa mradi umetekelezwa katika maeneo machache tu wakati athari mabadiliko ya tabianchi imeharibu visima vingi vya asili na kusababisha upungufu wa maji kwa wakazi wa eneo lote la Ukanda wa Pwani ya Bagamoyo.)

ii) Kamati za maji zianganalie namna ya kuyatibu (treat) maji ya mvua yanayovunwa na kuhifadhiwa katika matanki kwa muda mrefu, kwa lengo la kulinda afya za watumiaji. Kama inavyofahamika maji ya mvua baada ya muda mfupi huota ukungu na kuzalisha vijidudu;

iii) Kwa maeneo ambayo mradi unatekelezwa, wananchi wapatiwe elimu ya kutosha juu ya mradi huo ikihusianishwa na mabadiliko ya Tabianchi na waelimishwe jinsi ya kutunza mradi huo ili uweze kuwa mradi endelevu;

iv) Kwa mradi ya namna hii ambayo inatekelezwa katika halmashauri zetu ni vema tukatumia wahandisi wa halmashauri kwa lengo la kupunguza gharama, kutokana na ukweli kwamba fedha zinazotumika kumlipa mhandisi mshauri ni nyingi na kupelekea kuongezeka kwa gharama za mradi; na

v) Kamati ya Maji ya vijiji husika kuangalia namna nzuri ya kuendesha mradi ili wananchi wapate maji kwa gharama nafuu na vilevile kupunguza urasimu wa upatikanaji wa maji.

**b) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za NEMC (Mradi Namba 6507);**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea **Mradi Namba 6507** ujulikanao kama Ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – *NEMC*. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za NEMC ulianzishwa kwa lengo la kupunguza gharama ya Baraza itokanayo na kodi ya pango.

Tangu kuundwa kwa Baraza mwaka 1983 halikuwahi kupatiwa ofisi za Serikali na ilikuwa ikipanga katika majengo

mbalimbali, juhudi za NEMC kupatiwa ofisi za Serikali zilishindikana na mnamo mwaka 2009 Katibu Mkuu Kiongozi aliilagiza Bodi ya NEMC kutafuta ofisi za kudumu na ndipo Baraza lilipochukua uamuzi wa kununua kiwanja na kujenga jengo lake katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Ujenzi wa mradi huo ulipewa **Namba 6507**, mradi umetekelezwa kupitia ruzuku kutoka Serikalini pamoja na makusanyo ya ndani Baraza. Mradi umehusisha ununuzi wa viwanja vinne (vitatu Dar es salaam Mikocheni na kimoja Dodoma) pamoja na ujenzi wa jengo la ghorofa mbili katika viwanja vya Mikocheni- Dar es Salaam. Mradi umegharimu jumla ya shilingi **5,564,364,893.00** ambazo shilingi **1,650,000,000.00** ni ruzuku kutoka Serikalini na shilingi **3,253,464,893.00** ni fedha za ndani za Baraza na **660,900,000.00** ni Msaada kutoka Benki ya Dunia.

Mchanganuo wa fedha za Mradi ni shilingi **660,900,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa jengo, shilingi **4,903,464,893.00** kwa ajili ya viwanja vinne ambapo viwanja vitatu vipo Dar es Salaam Mikocheni na kiwanja kimoja kipo Dodoma.

### **Hali ya Mradi wakati wa Ziara ya Kamati;-**

Wakati wa ziara ya Kamati ilikuta mradi umekamilika ambapo

- i) Jengo la ghorofa mbili likukuwa limejengwa;
- ii) Mashine za kisasa kwa ajili ya utafiti zilikuwa zikiendelea kufungwa katika jengo hilo; na
- iii) Baadhi ya watumishi walikuwa wameanza kuhamia katika jengo jipya kitendo kilichopunguza msongamano uliokuwepo katika majengo yaliyokuwa yakitumika awali.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto katika utekelezaji wa Mradi huu ilikuwa ni mabadiliko ya mpango wa awali wa ujenzi wa jengo ambalo lililengwa kutumika upande mmoja kwa ajili ya ofisi na upande mwingine kwa ajili ya Biashara. Mabadiliko haya yalipelekea kuchelewesha utekelezaji wa mradi sababu

Baraza lililazimika kuanza upya mchakato wa upatikanaji wa mchoro wa jengo jipya;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilifahamishwa changamoto za Baraza katika utekelezaji wa Majukumu ya Baraza ambapo moja ya changamoto kubwa ni upungufu wa watumishi ambao ni wataalamu wa masuala ya mazingira jambo linalopelekea kushindwa kutekeleza jukumu la ukaguzi wa masuala ya mazingira kwa ufanisi. Makadirio ya Baraza ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi wanahitaji angala wafanyakazi 2000 na lakini kwa sasa wana wafanyakazi 250. Kamati iliielekeza Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuongeza kazi ya ufwatilaji wa maombi ya vibali waliyoyapeleka Utumishi, kwa kuwa Baraza limepewa majukumu makubwa sana na Sheria ya Mazingira lakini bila kuwa na watumishi wa kutosha hawataweza tekeleza majukumu hayo kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepongeza Serekali na Baraza kwa kutekeleza wa mradi huu, kwa kuwa jengo hili limeipa Baraza sehemu ya kufanyia kazi lakini pia imelipa Baraza hadhi inayostahili. Hapo awali Ofisi za Baraza hazikuwa na hadhi ya ofisi, walikuwa wanatumia nyumba walizozikuta wakati wananunua viwanja na kupelekea baadhi ya ofisi kuwa katika stoo ya nyumba hizo. Hatua hii ilikuwa ikipelekea baadhi ya wawekezaji hususani kutoka nje ya nchi kukosa imani na huduma za Baraza.

Aidha, kwa kuwa Serikali imejipanga kuhamia Dodoma na imezielekeza Taasisi zake kuhamia Dodoma pia, Kamati inaishauri Serikali kuziwezesha taasisi hizi kifedha ili ziweze kujenga ofisi zake kama ilivyofanya kwa Wizara. Hatua hii itaondoa gharama za kodi.

**c) Shughuli za Uhifadhi mazingira katika Ziwa Manyara;**

Kamati ilipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Ziwa Manyara kwa Lengo la kujionea Hali ya Mazingira katika eneo la hifadhi ambayo inahusisha na ziwa manyara, changamoto na mkakati wa Serikali katika kukabiliana na athari za kimazingira katika eneo hilo la hifadhi.

Shughuli za Uhifadhi wa Mazingira katika Ziwa Manyara zinatekelezwa na TANAPA na zinahusisha Kutoa elimu ya mazingira na sheria ya usimamizi wa mazingira katika ngazi ya wilaya na Halmashauri za Mkoa wa Manyara; Kufanya ufuatiliaji wa wachimbaji wadogo na wakubwa ili waweze kufanya uchimbaji kwa kufuata taratibu na sheria zilizopo; na Kutengeneza mabwawa (makingia maji) kuzunguka eneo la ziwa ya kupokea maji ya mvua yanayotoka katika maeneo ya miinuko kwa lengo la kuchuja tope, kwa lengo la kupunguza uingiaji wa tope katika ziwa;

**Shughuli za uhifadhi wa Mazingira katika Ziwa Manyara zinakumbana na Changamoto zifuatazo;-**

i) Ukosefu wa fedha za kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika eneo la Hifadhi, jambo linalopelekea athari za uharibifu unaofanywa kuendelea na kupelekea kuhatarisha eneo la hifadhi hususani ziwa Manyara;-

ii) Shughuli za binadamu (kilimo kisichofuata kanuni za kitaalamu, uwepo wa mifugo mingi) katika maeneo ya karibu na Ziwa Manyara zinazopelekea mmomony'oko wa udongo na kupelekea tope jingi kuelekea ziwani na kupunguza kina cha maji kupelekea kukauka kwa ziwa. Takwimu zinasema katika kipindi cha miaka **35** ya karibuni (**1980-2015**) hali imezidi kuwa mbaya ambapo matukio ya kukauka Ziwa yalikuwa **7** wakati kati ya mwaka (**1920-1970**) ziwa liliripotiwa kukauka mara tatu tu;

iii) Mabadiliko ya Tabianchi ambayo hupelekea ukame na kukauka kwa vyanzo vya maji yatiririkayo kwenda ziwani na kupelekea kukauka kwa ziwa manyara;

iv) Shughuli za kibinadamu katika eneo la hifadhi zisizolenga matumizi endelevu ya rasilimali za asili jambo linalopelekea kuharibu mfumo Ikolojia ya Tarangire na Ziwa Manyara na kuviweka katika hatari ya kutoweka. Pia kuharibika maeneo ya shoroba na maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori; na

v) Mimea vamizi/wageni katika baadhi ya vyanzo vya maji vya ziwa manyara ambavyo hupelekea maji kushindwa kufika ziwani; hali hii pia hupunguza vyanzo na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mazingira, wanyamapori na mahitaji ya jamii zinazozunguka hifadhi (mfano wa mimeo hiyo ni Mikaratusi, Misanduku).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya ziara katika Ziwa Manyara Kamati ilikuwa na maoni na ushauri ufuatao;-

i) Kwa kuwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya kusimamia mazingira kuliingiza katika orodha ya maeneo Lindwa eneo lolote linaloonekana lipo katika hatihati za kutowekea. Serikali ifanye haraka kuanza mchakato wa kuliingiza ziwa manyara katika maeneo Lindwa kwa lengo la kuliweka katika usimamizi maalumu na kulitoa katika hatari ya kupotea. Hatua hii ichukuliwe kwa maziwa yote ambayo yapo katika hatari ya namna hii likiwepo ziwa Jipe na Chala

ii) Serikali kuangalia namna ya kuwasaidia na kuwasimamia wakulima na wafugaji kufanya shughuli zao mbali na miinuko. Shughuli hizi zimekuwa zikiporomosha udongo na tope katika Ziwa Manyara na hivyo kupelekea kupungua kwa kina cha ziwa na kuliondolea uwezo wa kutunza maji kwa muda mrefu.

iii) Ziwa Manyara na Bioanuai zipatikanazo katika ziwa hili ni moja ya kivutio kikubwa kinachovuta utalii katika Hifadhi ya Manyara, changamoto zinazopelekea kukauka kwa ziwa Manyara kunahatarisha na kupelekea kungua kwa shughuli za utalii katika Hifadhi ya Manyara. Serikali ichukue jitihada za makusudi kuhakikisha wanalinusuru Ziwa Manyara na Bioanuai zote zinazopatikana katika ziwa hili;

vi) Kuna udhaifu katika kusimamia Sheria za Mazingira na Sheria ndogondogo za Vijiji na Halmashauri jambo linalotoa mianya kwa baadhi ya watu kuendelea shughuli zao katika eneo la hifadhi; Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kufutilia na kusimamia matakwa ya sheria ili kuzuia shughuli zisizo endelevu katika eneo la hifadhi.



### **2.3.2 Maoni ya Jumla kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

i) Serikali kulipa uzito suala la hifadhi ya Mazingira kwa kutenga fedha za maendeleo na kuzipeleka kwa wakati, kwa sasa asilimia kubwa ya Miradi ya Maendeleo ya Mazingira inatekelezwa kwa kutumia fedha za wafadhili jambo ambalo si sahihi sana. Kwa mfano katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka, fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo zilikuwa hazijatolewa kabisa.

ii) Sekta asili (kilimo, ufugaji na uvuvi) kwa kiasi kikubwa ndio zinategemewa katika uchumi wa nchi yetu, na maendeleo ya sekta hizi kwa kiasi kikubwa yanategemea uhifadhi wa mazingira, jambo la kushangaza shughuli hizi hizi zimekuwa zikiendeshwa bila kuzingatia taratibu za kitaalamu. Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza Mazingira, pia kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za asili hususani misitu na vyanzo vya maji;

iii) Sheria ya Mazingira inayotekelezwa sasa ni ya Mwaka 2004 lakini inatekelezwa kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997. Sera hii ni ya zamani takribani miaka 22, na haijahusisha mabadiliko mengi ambayo yameendelea kutokea katika mazingira mfano mabadiliko ya Tabia nchi na viumbe vamizi. Kamati inasishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuandaa Sera mpya itakayoendana na mazingira ya sasa.

### **3.0 UZINGATIAJI WA USHAURI WA KAMATI KUHUSU BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kamati ilitoa ushauri kwenye

maeneo mbalimbali na kutoa maagizo Kumi na Mbili (12). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati na kutekeleza maagizo hayo, hata hivyo kuna maeneo ambayo serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii;-

i) ***Serikali ifanye Tathimini ya Athari kwa Mazingira- EIA katika maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wachimaji wadogo wa madini kabla ya kuwakabidhi ili kuepusha athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza.*** Maelezo ya Serikali kuhusu utekezaji wa agizo hili ni kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kwa kushirikiana na NEMC wanaendeleo kusimamia Sheria ya Mazingira na kuhakikisha kila mradi unaotaka kutekelezwa unafanyiwa EIA na unafuata masharti ya EIA. Maelezo haya hayaendani na agizo la Kamati, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali juu utekezaji wa agizo hili kwa lengo la kuepusha athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza katika maeneo ya wachimbaji wadogo (wachimbaji wadogo hawana uwezo wa kufanya EIA ni vema Serikali ikafanya ukaguzi huo)

ii) ***Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii kukusu athari za kuharibu vyanzo vya maji ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu, na kuliingiza bonde hilo katika orodha ya maeneo lindwa kwa kutumia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.*** Kamati inaendelea kusisitiza kuhusu utekezaji wa agizo hili hususani katika kipengele cha kuliingiza Bonde lote la Mto Ruaha Mkuu katika orodha ya maeneo lindwa kwa sasa kipande kilichopita katika hifadhi tu ndio kinalindwa sehemu iliyobaki haijahifadhiwa. Sheria ya Mazingira inampa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira mamlaka ya kuliingiza eneo lolote katika orodha ya maeneo lindwa pale eneo hilo linapoonekana kuwa katika hatihati ya kupotea. Kutokana na changamoto zilizopo katika maeneo ya bonde hili, Kamati inaishauri Serikali kutumia Sheria hii na kuliweka bonde lote katika maeneo lindwa lakini pia kuunda chombo cha usimamizi wa bonde ambacho ni Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Hatua hii itasaidia kulinda bonde letu lakini pia itatoa uhakika wa maji katika Mradi Mkubwa wa Umeme unaoenda kutekelezwa (Stigler's Gorge).

iii) ***Serikali ihakikishe kuwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mfuko wa Mazingira unawezeshwa na kuanza kufanya kazi kikamilifu.*** Maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa agizo hili hayaridhishi, Kamati inatambua kuwa changamoto kubwa ya Mfuko wa si marekebisho ya Sheria pekee ball kuna changamoto ya vyanzo vya mapato ya mfuko pia. Kwa kuwa mchakato wa maboresho ya sheria unaendelea. Kamati inaishauri Serikali kutatua nah ii changamoto ya vyanzo vya mapato kwa kupitisha vyanzo vyote vya Mapato yatokanayo na shughuliza uchafuzi wa mazingira kuchangia walau kwa asilimia tano katika mfuko wa Mazingira kwa lengo la kuuwezesha mfuko kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

iv) ***Machinjio yahamishwe kutoka kwenye makazi ya watu na ukaguzi wa mara kwa mara ufanyike ili kuhakikisha wanaozindesha wanafuata Sheria inayosimamia machinjio hayo na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya kulinda afya za walaji.*** Kamati inaendeleo kusisitiza juu ya utekelezaji wa agizo hili na kuongeza kasi ya ukaguzi kwani kuna baadhi ya maeneo bado mazingira za machinjio si yakuridhisha.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

##### **4.1 Uchambuzi wa malengo/mpango**

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuchambua makadirio ya Mapato na Matumizi katika jukumu la kuhifadhi na kusimamia mazingira, Kamati ilipitia maelezo ya Waziri kuhusu kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Lengo lilikuwa ni kufatilia tija inayoweza kupatikana kutokana na malengo yaliyopangwa na Ofisi hii kwa fedha zinazoombwa katika kifungu **5003**. Kamati ililinganisha malengo ya Mwaka wa Fedha **2018/2019** na **2019/2020** na katika ulinganisho huo kamati ilibaini yafuatayo:-

i. Malengo yote yalizingatia hati idhini ya serikali iliyoainisha majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais- mazingira.

ii. Lengo namba mbili (ii) kwa mwaka wa fedha **2018/2019** na lengo namba kumi na mbili (xii) kwa mwaka wa fedha **2019/2020** yanaendana na kwamba yote yanajielekeza kwenye udhibiti wa utupaji wa taka ngumu na hatarishi.

iii. Lengo linalohusu udhibiti wa taka ngumu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni muendelezo wa uzingatiaji wa ushauri uliowahi kutolewa na Kamati hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, agizo la Waziri Mkuu alipokuwa akihitimisha hoja yake bungeni tarehe 9/4/2019, Linatoa nguvu na msisitizo kama ilivyotolewa na Kamati 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo Kamati inaipongeza Serikali kwa kupokea ushauri uliotolewa na Kamati na kutoa muda wa kutosha kwa wawekezaji hao, kuanzia Agosti, 2017 hadi Mei, 2019, na ni matumaini ya Kamati kuwa wawekezaji hao watakuwa wametumia vizuri muda uliotolewa na Serikali. Hivyo, kuweza kutumia teknolojia nyingine na kuweza kuzalisha mifuko mbadala.

Aidha, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kufuatilia utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu na kuhakikisha ifikapo tarehe 30 Mei, 2019 matumizi ya mifuko ya plastiki yatakuwa yamefikia mwisho.

#### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya mapato

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira chini ya **Fungu 31** inalenga kukusanya jumla ya Shilingi **18,218,915,442.00** kutoka katika vyanzo vya ndani vya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – *NEMC* ambavyo ni ada na faini zitokanazo na shughuli za usimamizi wa mazingira.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kiasi kinacholengwa kukusanywa kinakaribiana na kabisa na malengo ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambalo yalitekelezwa kwa asilimia **55.2** tu hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha, kipindi ambacho walipashwa kukusanya asilimia **75**. Kutokana na uchambuzi huu kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

i) kupanga lengo la makusanyo kwa kuzingatia kasi na uwezo wake wa kukusanya.

ii) Wakati wa kupanga lengo la makushanyo izingatie changamoto zilizokwamisha kufikia lengo la makusanyo la Mwaka wa Fedha uliotangulia na kuzitatua.

Vilevile, Kamati inatambua kuwa wigo wa mapato yatokanayo na shughuli za Mazingira ni mkubwa lakini kasi ya ukusanyaji bado ni ndogo. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea NEMC uwezo kwa kuwapatia watumishi na vitendea kazi ili waweze kuongeza kasi ya ukaguzi na hatua ambayo itaongeza mapato ya Baraza pia.

### **4.3 Uchambuzi wa Bajeti ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya matumizi kwa ajili ya shughuli za Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira hutengwa katika Fungu 31 Ofisi ya Makamu wa Rais. Kamati ilijulishwa kuwa jumla ya shilingi **22,708,713,882.00** zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu hili muhimu, Kiasi hicho ni ongezeko kwa asilimia **179.71** ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa ongezeko la Bajeti ya shughuli za Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 linaathari katika fedha za miradi ya maendeleo ambayo imeongezeka kutoka **3,524,540,000.00** Mwaka 2018/2019 mpaka shilingi **18,218,915,442.00** Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### **4.4 Maoni ya jumla kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania Nchi mwanachama wa mikataba mingi ya kimataifa inayohusiana na mambo ya Mazingira. Na kupitia mikataba hiyo nchi ina fursa ya kupata fedha za maendeleo kwa kuandika maandiko ya miradi na kuyawasilisha katika taasisi za mazingira duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kama nchi hatujaitumia fursa hiyo ipasavyo, kwa kuwa hatujaandika

maandiko yakutosha ambayo yanawezesha upatikanaji wa fedha hizo.

**Kwa kuwa**, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira si wa kuridhisha. **Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira – NEMC na wadau wengine wa mazingira kuchangamkia fursa hii kwa kuongeza kasi na kuandaa maandiko ya kutosha yenye uhalisia na kuyawasilisha katika taasisi za kimataifa kila fursa inapotokea. Juhudi hizo zitapelekea kuongezeka kwa fedha za uhifadhi na utunzaji wa mazingira nchini.

Sambamba na hilo Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuwatambua wadau wote wa mazingira (hususani NGO's) ambao wanatumia fursa hii na kupata fedha za miradi. Umuhimu wa kuwatambua wadau hao ni kuiwezesha Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuweze kuwafuatilia na kuhakikisha fedha wanazozipata zinatumika kutekeleza miradi/shughuli zilizokusudiwa.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 Hali ya Mazingira

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya Mazingira nchini si ya kuridhisha, tafiti zimefanyika na kubainisha hali mbalimbali zinazodhihirisha jambo hili. Kamati ilipata fursa wakati wa ziara zake za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kutembelea na kushuhudia hali isiyo ya kuridhisha ya mazingira katika baadhi ya maeneo nchini. Kamati imebainisha maeneo machache tu ambayo yanadhihirisha hali mbaya ya mazingira kwa lengo la kutoa picha ya kuathirika kwa mazingira ya Nchi. Maeneo hayo ni pamoja na;-

i) Athari za Mabadiliko ya Tabianchi, ambazo zimekwisha dhihirika katika maeneo mbalimbali nchini. Athari hizo ni pamoja na ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, kuongezeka kwa ujazo wa maji ya bahari (kuharibu kingo za bahari na fukwe; kumezwa kwa visiwa

vidogo kwenye bahari; na kuathiri *wáter table*), kuyeyuka kwa barafu katika vilele vya milima mirefu kama vile Mlima Kilimanjaro, uharibifu wa madaraja, barabara, reli na makazi kutokana na mafuriko;

ii) Hali ya ukame na jangwa nchini, tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 61 ya nchi ipo hatarini kugeuka jangwa. Baadhi ya Mikoa iliyoathirika zaidi na hali ya ukame nchini ni pamoja na Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Manyara na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa kiasi kikubwa hali hii inatokana na matumizi ya yasiyoendelevu ya rasilimali asili nchini.

iii) Takwimu za ukataji wa misitu zinaonesha kuwa, msitu wenye ukubwa wa kiwanja cha mpira hufyekwa kila baada ya dakika moja, takwimu hizi zimeipelekea Tanzania kuwa katika ya nchi tano za juu (top five) zinazoongoza kwa ukataji wa misitu (*deforestation*) Duniani;

iv) Hali ya rasilimali maji, Tanzania imeingia katika orodha ya nchi zenye upunguvu wa maji ukilinganisha na mahitaji (water stressed country). Hali hiyo ni moja ya kiashiria cha uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji;

vii) Hatari ya kupotea kwa baadhi ya maziwa nchini, baadhi ya maziwa yaliyopo kwenye hatari ya kupotea ni Ziwa Manyara, Jipe na Chala. Kupotea kwa maziwa haya kwa kiasi kikubwa kumechongiwa na shughuli za kibinadamu zinazoendeshwa katika maeneo ya ziwa ambazo hupelekea uharibifu wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, hayo ni baadhi tu ya maeneo ambayo yanaonesha kuwa hali ya mazingira nchini si ya kuridhisha. Hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada za makusudi kwa lengo la kuinusuru nchi kutokana na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira.

## 5.2 Maoni na Ushauri

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira 2018/2019, pamoja na mapendekezo ya Mapato kwa Mwaka wa fedha 2019/2020 ya Ofisi hii Kamati imekuwa na Maoni na Ushauri kadhaa kwa Serikali. Ni imani ya Kamati kuwa maoni na ushauri huu utafanyiwa kazi hivyo kutapelekea kuboresha shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

### i) Mfuko wa Mazingira

**Mheshimiwa Spika**, kwa miaka kadhaa tumeshuhudia Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira imeendelea kutengewa bajeti ndogo ukilinganisha na ukubwa wa jukumu walilionalo la uhifadhi na usimamizi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, dhana ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Mazingira ilikuwa ni kuisaidia Serikali kuisimamia Sekta Binafsi kuchangia katika shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Mfuko huu umeanzishwa tangu mwaka 2007 lakini unashindwa tekeleza majukumu yake mpaka sasa.

**Mheshimiwa Spika**, kuna vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo vinatokana na mazingira lakini vyanzo hivi vinaingia katika mifuko ambayo hairudishi katika shughuli ya hifadhi ya mazingira. Kamati ilifahamishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuwa vyanzo hivi vimekwisha ainishwa na kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri. Kamati inaisisitiza Serikali kuhakikisha katika mwaka wa fedha 2019/2020, kwa kuanzia walau vyanzo vitano tu vichangie katika Mfuko wa Mazingira kwa asilimia tano (5). Hatua hii itasaidia kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali katika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwa baada ya kupitisha vyanzo hivi vya mapato ya Mfuko, ifanye maboresho katika Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 Sura ya 191 ili iweze



kutambua na kusimamia utekelezaji Sekta zote zinazotakiwa kuchangia katika mfuko.

ii) **Afisa Mazingira**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Mazingira imemtambua na kumpa majukumu makubwa Afisa Mazingira. Pamoja na kuwa Afisa Mazingira anapewa majukumu na Sheria ya Mazingira na analengwa kumsaidia Mkurugenzi wa Mazingira lakini ni muajiriwa wa Halmashauri na anaripoti kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Aidha, taarifa ya kazi anazofanya Afisa Mazingira ili zimfikie Mkurugenzi wa Mazingira ni lazima zipitie TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, mlolongo huu unapelekea ucheleweshaji wa taarifa lakini pia unakwamisha utekelezaji wa shughuli za mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuondoa mlolongo huo mrefu na badala yake Afisa Mazingira awe anaripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Mazingira kwa masuala yote yanayohusu mazingira. Jambo hili si jipya limekuwa likitekelzwa na Maafisa Maji wa Halmashauri zote, wao wanaripoti moja kwa moja Wizara ya Maji.

Pia, Kamati inashauri Serikali kwa siku za usoni kuangalia namna ya kuwahamisha maafisa mazingira wote kuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira. Hatua hii itasaidia uratibu wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

iii) **Elimu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**Mheshimiwa Spika**, katika suala la uhifadhi na usimamizi wa mazingira asilimia sabini (70) ya jukumu lao ni kutoa elimu ili kujenga uelewa kwa jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira na athari za kuharibu mazingira; na asilimia thelathini (30) iliyobaki ni kutekeleza miradi/shughuli za kupambana na mabadiliko ya Tabianchi kama vile ujenzi wa ukuta kwenye kingo za bahari na mito, kampeni za upandaji wa miti n.k. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kusambaza elimu ya uhifadhi wa mazingira. Elimu hii iende sambamba na aina ya shughuli za kijamii zinazofanyika katika maeneo husika kwa

kuwa aina ya uharibifu wa mazingira inategemea aina ya shughuli za binadamu katika eneo husika. Mfano aina ya uharibifu unaofanywa na wakulima ni tofauti na uharibifu unaofanywa na wafugaji.

iv) **Utekelezaji wa Sheria ya Namba 20 ya Mazingira kuhusu Mita 60**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu namba **57** cha Sheria ya Mazingira ya Mwaka **2004** kinampa Waziri mwenye dhamana na masuala ya Mazingira, mamlaka ya kutunga Kanuni na miongozo mbalimbali ambayo itasaidia katika kusimamia shughuli za usimamizi wa mazingira katika maeneo ya owevu yani bahari, mito na mabwawa. Kamati imebaini kuwa kuna upungufu katika Kanuni na Miongozo zilizotungwa kwa lengo la kusimamia maeneo hayo jambo linaloleta changamoto katika utekelezaji wa sheria hii na kupelekea migogoro na malalamiko kwa baadhi ya maeneo. Kamati inaishauri Serikali kupitia kwa Waziri mwenye dhamna ya mazingira kurekebisha kanuni na miongozo hii ili iweze kuelekeza kwa uwazi ni kwa jinsi gani wananchi wanaokaa pembezoni mwa bahari, mito na mabwawa wanaweza kufanya shughuli zao bila ya kuharibu mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Pia Kamati inaishauri Serikali kuzielekeza Halmashauri zote ambazo zina maeneo owevu, kuainisha maeneo yote na kuorodhesha shughuli zinazoweza kufanyika katika eneo husika, kisha kuwasilisha maombi kwa Waziri mwenye dhamna ya Mazingira ili waweze kutumia maeneo hayo. Sambamba na hilo Halmashauri hizo ziwajibike kusimamia maeneo hayo.

v) **Utekelezaji wa Majukumu ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira- NEMC.**

**Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu juu ya utendaji wa NEMC. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa malalamiko haya yametokana na uzamani wa kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Baraza hususani uendeshaji wa Tathimini ya Athari za Mazingira – EIA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika Baraza, kuanzia Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza na inamatumaini kuwa uendeshaji wa Baraza utaimarika na malalamiko yatafika mwisho. Pamoja na mabadiliko hayo Kamati inaishauri Serikali kulisimamia Baraza kufanya mapitio ya kanuni na taratibu za utekelezaji wa shughuli zake na kuziboresha kuhakikisha zinaendana na mazingira halisi ya sasa.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya eneo ambalo linahitaji sana maboresho ni hatua zinazofuatwa wakati wa kuomba cheti cha Tathimini ya Athari za Mazingira – EIA. Baadhi ya hatua zilizowekwa si za lazima na haziendani na wakati kwani dunia ya sasa ni ya kidigitali.

vi) **Vibali vya Tathimini ya Athari za Mazingira – EIA**

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu NEMC imekuwa ikilalamikiwa juu ya ucheleweshaji wa vibali vya Tathimini ya Athari za Mazingira – EIA. Kamati inatambua kuwa kupata kibali cha EIA ni mchakato na unachukua muda, lakini inatambua pia kuwa si muda mrefu kama unaolalamikiwa na baadhi ya wadau (mpaka miaka mitatu). Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaisimamia NEMC kupunguza urasimu katika kutoa vibali na EIA kwa lengo la kuisaidia Serikali kujenga mazingira mazuri ya Uwekezaji ukizingatia kuwa **Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli** ameelekeza kuwa Mwaka 2019 ni Mwaka wa Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa nchi inajielekeza kwenye uwekezaji, kuna haja kubwa ya kuangalia upya gharama za EIA katika miradi mikubwa ya uwekezaji. Gharama za Tathimini ya Athari za Mazingira - EIA kwa miradi mikubwa ya uwekezaji ni kubwa na zinalipwa kwa wakati mmoja. Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kupitia upya gharama hizo na kuziboresha. Pia, Kamati inashauri kwamba wajaribu kugawanya gharama ambazo mteja anapaswa kulipa, ili aweze kulipa kwa awamu, jambo hilo linaweza kutekelezwa kwa kuangalia hatua za uwekezaji kama vile

hatua za awali, kati na mwisho. Hatua hii itatoa unafuu kwa wawekezaji wetu kwa kuwa gharama za awali za kuanza uwekezaji zitakuwa zimepungua.

vii) **Nguvu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 imejipambanua vizuri na imegawa majukumu/wajibu kwa kila mtu kuanzia ngazi ya Serikali mpaka kufikia kwa wananchi. Kamati imebaini kuwa changamoto ipo katika usimamizi wa utekelezaji wa Sheria hii. Wahusika waliotajwa na Sheria tena hususani mamlaka za Serikali hazichukui nafasi zao na kutekeleza majukumu yao. Kamati inaishauri Serikali kupitia kwa Waziri mwenye dhamana kutumia mamlaka yake ya kisheria kuwawajibisha wale wanaopuuzia majukumu yao.

viii) **Taarifa ya Hali ya Mazingira Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu 175 cha Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 kinamuelekeza Mkurugenzi wa Mazingira kuandaa na kutoa taarifa kuhusu hali ya usimamizi wa mazingira nchini kila baada ya miaka miwili na taarifa hiyo inapaswa kuwasilishwa Bungeni. Takribani miaka mitano (5) sasa kuanzai mwaka 2014 hadi 2019, taarifa hii haijaandaliwa wala kuwasilishwa Bungeni. Kamati inaishauri Serikali kusimamia taarifa hii kuhakikisha inakamilika na kuwasilishwa Bungeni kabla ya Mwaka wa fedha 2019/2020 haujaisha kwa lengo la kutoa picha ya hali ya mazingira nchini, lakini pia kuwapa Wabunge nafasi ya kujadili na kuishauri Serikali.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali katika kukamilisha taarifa hii. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini.

i. Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb

**Mwenyekiti**

ii. Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb

**M/Mwenyekiti**

iii. Mhe. David Cecil Mwambe, Mb

**Mjumbe**

iv. Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
v. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb	Mjumbe
vi. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
vii. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
viii. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb	Mjumbe
ix. Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
x. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
xi. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe
xii. Mhe. Kmamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe
xiii. Mhe. Zainabu Mndolwa Amiri, Mb	Mjumbe
xiv. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
xv. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
xvi. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
xvii. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
xviii. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb	Mjumbe
xix. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb	Mjumbe
xx. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb	Mjumbe
xxi. Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
xxii. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu Rais-Muungano na Mazingira, Mhe. January Y. Makamba, Mb, Naibu waziri wa wizara hiyo Mhe. Mussa Ramadhan Sima, Mb, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kutoa ufafanuzi mzuri wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein, Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto, makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba na Bi Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato

na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira **Fungu 31** kwa **Mwaka wa Fedha 2019/2020** ambayo ni kiasi cha Shilingi **22,708,713,882.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Suleiman Ahmad Sadiq, (Mb)  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA,**  
**BIASHARA NA MAZINGIRA**

16 Machi, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Msemaji wa Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE K.n.y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, napenda kuwasilisha hotuba kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia sote kuwa hapa kwenye Mkutano huu wa bajeti katika Bunge hili la Kumi na Moja. Pamoja na hujuma na njama zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa kwa kuwarubuni baadhi ya Wabunge wenzetu kuhamia upande wa pili, bado Upinzani kwa ujumla na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iko imara na inachapa kazi kwa weledi mkubwa zaidi. Kwani tunaamini, kesho yetu ni bora kuliko jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniadini na

kunipa fursa hii ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Ofisi hii ya Makamu wa Rais na hivyo kusimama hapa na kutoa mtazamo wa Kambi kwa hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naushukuru pia uongozi mzima wa Kambi Rasmi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wote kwa msaada wao na ushirikiano wao katika matayarisho ya wasilisho hili. Aidha, nawashukuru Watanzania wenzangu na wadau wa mazingira kutoka pande zote mbili za Muungano kwa kunipa hoja ambazo zimenisaidia sana katika kukamilisha hotuba hii ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo wa kazi nikiwa ndani ya Bunge na nje ya Bunge. Pia kwa Ofisi ya Spika, shukrani zangu haziwezi kuwa na ukomo, naitukuza kila fursa niliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya Muungano; ukweli ni kuwa masuala ya Muungano yameelezwa vizuri katika Ibara ya (4)(3) na kuorodheshwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba. Kuna hoja ambazo kwa miaka yote imekuwa ni kilio kutoka upande wa pili wa Muungano na kupelekea kuundwa kwa Tume kadhaa ili kutatua kero hizo za Muungano. Kero hizo ambazo zimekuwa zinapigiwa kelele miaka yote ni mafuta na gesi asilia, mambo ya Muungano, ajira za Wazanzibar katika Taasisi za Muungano, uwezo wa Zanzibar kukopa nje, gawio la Zanzibar katika mali za Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, Mfuko wa Pamoja wa Fedha, utozwaji kodi mara mbili kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar peke yake ama kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano, zimechukua hatua kadhaa za kutafuta ufumbuzi wa kero za Muungano. Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, miongoni mwa hatua ilizochukua na ambazo zinajulikana ni pamoja na kuunda Kamati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa Kamati zilizoundwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kushughulikia kero za Muungano kati ya mwaka 1990 na 2003 ni pamoja na zifuatazo: Kamati ya Baraza la Mapinduzi (Kamati ya Amina) ya 1992; Kamati ya Rais ya Kupambana na Kasoro za Muungano (Kamati ya Shamhuna, 1997; Kamati ya Rais Kuchambua Ripoti ya Kisanga (Kamati ya Salim Juma); Kamati ya Rais ya Kuandaa Mapendekezo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar juu ya Kero za Muungano (Kamati ya Ramia ya mwaka 2000); Kamati ya Baraza la Muungano juu ya Sera ya Mambo ya Nje; Kamati ya Rais ya Wataalamu juu ya Kero za Muungano ya mwaka 2001; Kamati ya Baraza la Muungano ya Jamuiya ya Afrika Mashariki; Kamati ya Mafuta; Kamati ya Madeni baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kamati ya suala la *Exclusive Economic Zone*, Kamati ya masuala ya Fedha na Benki Kuu na Kamati ya Masuala ya Simu ya mwaka 1996 hadi mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pia imewahi kuajiri mtaalamu wa mambo ya fedha, Dkt. Courtrey Blackman na mtaalam wa masuala ya mafuta katika kutafuta suluhu ya mambo hayo yanayoyumbisha Muungano wetu, lakini kamati zote hizo hazikuzaa matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa tatizo kubwa liko kwenye Muundo wa Muungano na suluhu ya tatizo hilo ni kubadilisha muundo ili Muungano wetu uimarike zaidi na kuwa wenye manufaa kwa pande zote washirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na baadhi ya Kamati hizo za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar peke yake, Serikali ya Muungano Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimeunda Tume, Kamati na kuajiri wataalamu mbalimbali ili kutafuta suluhisho la kero mbalimbali za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa Tume na Kamati hizo ni kama zifuatazo: Kamati ya Mtei, Tume ya Nyalali, Kamati ya Shellukindo, Kamati ya Bomani, Kamati ya



Shellukindo ya pili ya kuandaa muafaka juu ya mambo ya Muungano baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano Tanzania, Kamati ya *Harmonisation*, Kamati ya masuala ya simu ambayo ilikuwa ni Kamati ya Kusila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano Tanzania zimefanya vikao vya pamoja visivyopungua 80 katika ngazi mbalimbali ili kuzungumzia kero za Muungano. Aidha, Serikali hizi mbili mwaka 1994 ziliomba msaada wa *IMF* ili kuzishauri kuhusiana na Benki Kuu, mgawanyo wa misaada na uhusiano wa kifedha (*intergovernmental fiscal relationship*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya juhudi zote hizo, tarehe 14 Novemba, 2000 wakati Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa alipokuwa akizundua Bunge aliahidi kuzipatia ufumbuzi kero za Muungano ndani ya siku 60. Tokea ahadi ilipotolewa hadi leo ni miaka 19 imepita, Serikali zinazoongoza ni zile zile za Chama cha Mapinduzi. Kuchelewa huko kutatua kero hizo, kunaonesha dhahiri kwamba Serikali za CCM hazijatoa kipaumbele kwa Muungano huu kuendelea kuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*) ni asasi ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, sura 140 ya mwaka 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*), ni asasi ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Sura 140 ya mwaka 1996). Tume ilizinduliwa rasmi tarehe 5 Juni, 2003, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteua Makamishna saba. Aidha, Tume ina Sekretarieti ambayo ni chombo kikuu kiutendaji. Tume hii ilikuwa njia mojawapo ya kutatua kero za kifedha kati ya zile kero kuu za Muungano, lakini kwa

masikitiko makubwa hata Tume hiyo ambayo ni chombo cha kiutendaji kimeshindwa kutimiza azma ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba, Tume ya Pamoja ya Fedha ina majukumu yafuatayo:-

(a) Kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao wa kila mojawapo ya Serikali hizo;

(b) Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili;

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ibara ya 133 ya Katiba inaeleza kuwa:

*“Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti maalum itakayoitwa “Akaunti ya Fedha ya Pamoja” na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge, kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi hapa ya kuomba majibu kutoka Serikalini ni je, hiyo Akaunti ya Pamoja imeshafunguliwa? Kwa kuwa toka uwepo wa Tume imeshindwa kutatua kero za kifedha zinazohusiana na Muungano na hivyo malalamiko kuzidi kurundikana, ni wazi kuwa chombo hiki licha ya kuwa ni chombo cha kikatiba kimekosa uhalali kwa wananchi wa kuendelea kutengewa fedha za walipa kodi katika kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka sasa kama ambavyo wanazuoni mbalimbali wa masuala haya ya Muungano walivyo na wanavyozidi kushauri kuwa tatizo ni muundo wa Muungano, hivyo vyombo vyote

vitakavyoundwa kwa nia njema ya kuleta suluhu vitashindwa kufanya kazi iliyopo na inayokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kuwa ili matatizo au kero za Muungano zishe hatuna budi kurejea kwenye mapendekezo yaliyotolewa katika rasimu ya pili ya Katiba iliyotolewa na Tume ya Marekebisho ya Katiba iliyokuwa chini ya Uenyekiti wa Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba kuhusiana na Muundo wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi naomba kunukuu "Ibara ya 60(1) ya Rasimu ya Pili ya Katiba kama wananchi walivyohitaji muundo wa Muungano wetu utakavyokuwa: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na muundo wa shirikisho lenye Serikali tatu ambazo zitakuwa ni:

- (a) Serikali ya Muungano;
- (b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na
- (c) Serikali ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia sera yake ukurasa wa 13 na 14, Sura ya 2.4 inaeleza wazi aina na muundo wa Muungano na kueleza malengo yatakayofikiwa kuwa ni kila nchi mshirika wa Muungano itakuwa na mamlaka kamili katika kumiliki na kutumia rasilimali na maliasili zake; isipokuwa masuala yote ya msingi ya jumla kama vile Katiba ya Shirikisho la Jamhuri ya Muungano, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ulinzi na Usalama, Uraia, Sarafu ya Benki Kuu, Mfumo wa Elimu, Mahakama ya Katiba na Bunge la Shirikisho yatashughulikiwa na Serikali ya Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini juu ya kuurudisha Muungano karibu zaidi na wananchi kwa kuwashirikisha kwa njia mbali mbali, kuchagua na kuyatambua yale wanayoyataka katika Muungano wao ili yaheshimiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na uhifadhi na uendelevu wa mazingira. Mazingira ni dhana pana inayojumuisha vitu vyote vinavyotuzunguka, iwe ni sekta ya maji (maziwa, bahari, mito, mabwawa aina na mbinu za kupata rasilimali ziishizo kwenye maji - aina ya uvuvi na kadhalika), sekta ya kilimo(matumizi bora ya uhifadhi wa ardhi - aina za mitambo ya kilimo inayotumika, matumizi ya mbolea, matumizi ya dawa), sekta ya misitu, sekta ya viwandani (jinsi mabaki ya viwandani yanavyohifadhiwa na aina ya teknolojia inayotumika katika uzalishaji), sekta ya afya (taka zinavyotunzwa na kuteketezwa) na kadhalika. Maisha ya binadamu na viumbe vingine yanategemea sana hali ya mazingira, ndiyo maana nimeyaita mazingira kuwa kitalu cha maisha. Kutokana na umuhimu huo usio na shaka, mazingira ni miongoni mwa masuala mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Serikali kutambua umuhimu wa mazingira; na kuweka sheria, kanuni na miongozo ya ulinzi na uhifadhi wa mazingira kama vile Sera ya Mazingira ya mwaka 1997, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, Mpango Kazi wa Taifa wa Mazingira (*National Environmental Action Plan, 2013*), MKUKUTA awamu ya pili wa mwaka 2010; Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 pamoja na kuridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa kuhusu uhifadhi na utunzaji wa mazingira; bado suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira halijapewa umuhimu na uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba shughuli yoyote inayofanywa na binadamu katika uso wa dunia, ina athari za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja katika mazingira. Athari hizo zinazosababishwa na binadamu katika mazingira, baadaye hugeuka na kuathiri tena maisha ya binadamu na viumbe vingine pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ilidhani kwamba jambo hili ambalo linagusa karibu kila sekta ambayo binadamu anafanya shughuli za kuendesha maisha yake lingepewa uzito angalau hata wa kujadiliwa siku mbili lakini limepewa siku moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la aibu kwa Serikali hii kutegemea fedha za nje kukabiliana na majanga yanayotokana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa mfano, kipindi hiki cha mvua ambapo mafuriko yamebomoa nyumba nyingi za wananchi; mazao mashambani yameharibiwa vibaya na miundombinu ya barabara na madaraja yameharibiwa vibaya, wananchi wamepoteza maisha kwa kusombwa na maji tusbiri fedha za nje ambazo hatujui zitatolewa lini kukabiliana na majanga hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, mazingira ni suala mtambuka (*cross cutting issue*); lipo kila mahali na madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira yanagusa karibu sekta zote, hivyo ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali, kutenga fedha za kutosha kutunza na kuhifadhi mazingira yetu; lakini pia kwa ajili ya kukabiliana na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya jumla ya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwenye utanzaji na uhifadhi wa mazingira ni kama ifuatavyo:-

Jumla ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilikuwa shilingi bilioni 6.788, lakini fedha iliyotolewa na kutumika (ambayo ni ya nje tu) hadi kufikia tarehe 8 Machi, 2018 ilikuwa ni shilingi bilioni 1.7, sawa na asilimia 25 tu ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utekelezaji huo duni wa bajeti, ni wazi kwamba Serikali haiko makini kabisa katika suala hili la mazingira. Tafsiri ndogo ya takwimu nilizozitoa ni kwamba Serikali imeweka rehani maisha ya wananchi kwa wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kuzungumzia kuhusiana na uchumi wa kijani. Uchumi wa kijani ni uboreshaji wa uchumi na ustawi wa jamii unaozingatia

uzalishaji na matumizi yasiyoharibu mazingira. Ukiangalia hati idhini inaonesha kuwa moja ya kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais ni *"Promotion of Cleaner Production and Green Economy"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imethibitika kuwa Tanzania inapoteza zaidi ya hekta 372,000 kila mwaka eneo linalokadiriwa kuwa sawa na ukubwa wa nchi ya Rwanda, kutokana na ukataji miti kwa matumizi ya nishati ya kuni na mkaa, uchomaji wa misitu unaofanywa na baadhi ya raia wasio waaminifu kwenye hifadhi mbalimbali nchini. Jambo hilo lina athari kubwa katika mkakati wa nchi yetu wa kujikita katika uchumi wa kijani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba zaidi ya asilimia 90 ya nishati inayotumika katika familia za Tanzania wanategemea nishati inayotokana na miti na mabaki ya mazao ya shambani au taka zingine zaidi ya zile za plastiki kwa matumizi ya kila siku ya majumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vijijini asilimia mbili kutoka kwenye umeme na asilima nane inayotokana na bidhaa za petroli. Kati ya nishati hiyo kuni na mkaa ndio chanzo kikuu cha nishati kwa wananchi waishio mijini na vijijini. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza uchumi wa gesi tulioaminishwa kuwa upo na ndio mwarobaini wa kututoa hapa kwenye matumizi makubwa ya nishati itokanayo na miti upo au umeondoka katika Awamu hii ya Tano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi unaozingatia matumizi yasiyo endelevu ya maliasili hauna manufaa katika dunia ya leo. Watu wanapaswa kuachana na mbinu za kizamani za ukuaji wa uchumi wa matumizi shinikizi ya rasilimali, ambapo maendeleo yamekuwa yakigharimu mazingira; badala yake, wanapaswa kufuata mbinu mpya ambazo tija huongezwa kwa kutumia na kusimamia maliasili kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za kiuchumi lazima zizingatie athari za muda mrefu kwa mazingira na haja ya

kuhifadhi urithi wetu wa pamoja kwa faida ya vizazi vijavyo. Uchumi wa kijani huchochea ukuaji wa uchumi, mapato, na ajira. Tena husaidia kuimarisha mazingira na kuongeza tija kwa wananchi. Aidha, aina hii ya uchumi huleta maendeleo ya kiuchumi ya muda mrefu na yanayotoa fursa kwa watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya sekta muhimu kama vile kilimo, ujenzi, misitu na usafiri, uchumi wa kijani hutengeneza ajira nyingi zaidi kuliko ambazo zipo katika hali ya kawaida. Katika sekta kama vile uvuvi; uchumi wa kijani utalazimisha kushuka kwa mapato na ajira katika muda mfupi na wa kati ili kujazia hifadhi asilia, lakini hali hii hubakia ya muda mfupi na baadaye sekta hukua na kutoa tija kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za maendeleo nchini Tanzania lazima zifanywe kwa kuzingatia uhalisia wa mambo. Kwanza, zaidi ya asilimia 75 ya wananchi wa nchi hii huishi vijijini. Hivyo, jitihada madhubuti za kupunguza umaskini na kuleta maendeleo lazima zilenge wakazi na uchumi wa vijijini ili kuwa na matokeo mazuri. Kuna uhusiano mkubwa kati ya watu maskini hasa wa vijijini na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwa muktadha huo wa uchumi wa kijani, ni kweli uwekezaji wa mradi wa kuzalisha umeme unaotokana na nguvu za maji (*Stiegler's Gorge*) uliophelekea kufyekwa kwa misitu kwenye eneo ambalo ni sawa na ukubwa wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ofisi hii ya Makamu wa Rais inatoa kauli gani kuhusiana na utekelezaji wa mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa kijani sio kama unaishia kwenye kufyeka misitu tu bali pia matumizi sahihi na endelevu ya pembejeo za kilimo kama vile (mbolea na madawa) yanayotumiwa kwenye kilimo ili ardhi isiharibike na hivyo kushindwa kuhimili uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya

mfumo wa hali ya hewa yanayosababishwa na kazi za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja za binadamu, ambazo zinaongeza gesi joto (*greenhouse gases*) na kubadilisha mchanganyiko wa viwango vya gesi katika angahewa la dunia, ambayo pia ni nyongeza ya mabadiliko ya asili ya mfumo wa hali ya hewa yaliyotathminiwa na kulinganishwa kwa muda mrefu (usiopungua miaka thelatini na zaidi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi kwa kiasi kikubwa (zaidi ya 95%) yanasababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwemo uzalishaji wa viwanda unaotoa gesi ukaa (*carbon dioxide*) kwa kiwango kikubwa sana. Matokeo au athari za mabadiliko ya tabianchi ni kuongezeka kwa joto, mvua kubwa na za muda mfupi, mafuriko, mvua ya mawe ikiambatana na upepo mkali, mvua fupi zisizo za msimu na ukame wa muda mrefu na unaojirudia mara kwa mara. Tabia hizi zote zimeshajitokeza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi ni jambo linalohusu sekta zote za uchumi katika nchi, iwe kwenye kilimo, mifugo, uvuvi, miundombinu ya barabara, misitu, afya kwa kuzuka magonjwa mapya, sekta ya wanyapori na kadhalika, hivyo jambo hili ni jambo kubwa sana kuliko ambavyo Serikali inavyolichukulia kwa urahisi sana. Uwekezaji unaofanywa unaweza kuwa kazi bure kama hatutawekeza vya kutosha katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi, ambayo pia huchangiwa na uharibifu mkubwa wa mazingira umeleta athari kubwa katika sekta mbalimbali za maendeleo ya jamii na sekta zingine ziko katika hatari ya kuathirika pia. Sekta hizi ni nishati, kilimo na usalama wa chakula, maji, mifugo (kwa kuzuka kwa magonjwa ya milipuko, ukosaji wa malisho na maji), uvuvi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nenda kwenye maombi ya pesa.



**MHE. LATHIFAH H. CHANDE – K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA :** Kambi Rasmi inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini kila mara inashindwa kutenga kutoa fedha za ndani ikiwa kulikuwa na Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Mabadiliko ya Tabia Nchi au ndio kusema Mkakati huo haukuwa na kipengele cha bajeti kwa ajili ya kuutekeleza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kuwepo kwa uwazi zaidi katika hatua za utatuzi wa changamoto za Muungano na pia hatua shirikishi katika viwango mbalimbali ili kuondosha dhana kuwa Muungano huu ni wa viongozi zaidi na sio wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi zaidi ingepaswa kubuniwa ambayo ni ile Tanzania kuwa na uchumi endelevu na wenye kutoa ajira kwa wananchi wengi (Uchumi wa kijani ni uboreshaji wa uchumi na ustawi wa jamii unaozingatia uzalishaji na matumizi yasiyoharibu mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Tanzania bado ina fursa nyingi katika kuifanya nchi yetu kuwa kwenye uchumi wa kijani na fursa hiyo ilikuwa ni kuifanya Tanzania kutumia rasilimali gesi kwa kiwango kikubwa ili kudhibiti matumizi ya nishati itokanayo na miti hapa nchini ili juhudi zinazofanywa na Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Kiserikali matunda yake kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha hii hotuba yot eiliyoko hapa mbele yangu na imeikabidhi kwenu. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**HOTUBA YA MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI  
BUNGENI, ALLY SALEHE ALLY (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
MUUNGANO NA MAZINGIRA KWA MWAKA WA 2019/2020 -  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Inatolewa chini ya kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge,  
Toleo la mwaka 2016)

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia sote kuwa hapa kwenye mkutano huu wa bajeti katika Bunge hili la 11. Pamoja na hujuma na njama zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa za kuwarubuni baadhi ya wabunge wenzetu kuhamia upande wa pili bado Upinzani kwa ujumla na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni imara na inachapa kazi kwa weledi mkubwa zaidi, kwani tunaamini Kesho yetu ni bora kuliko jana.

2. **Mheshimiwa Spika**,Natoa shukrani za dhati kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniadini na kunipa fursa hii kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Ofisi hii ya Makamu wa Rais na hivyo kusimama hapa na kutoa mtazamo wa Kambi kwa hoja iliyopo mbele yetu. Naushukuru pia uongozi mzima wa Kambi Rasmi ya Upinzani na waheshimiwa wabunge wote kwa msaada wao na ushirikiano wao katika matayarisho ya wasilisho hili. Aidha, nawashukuru Watanzania wenzangu na wadau wa mazingira kutoka pande zote mbili za Muungano kwa kunipa hoja ambazo zimenisaidia sana katika kukamilisha hotuba hii ya wananchi.

3. **Mheshimiwa Spika**,Mwisho lakini si kwa umuhimu niishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo wa kazi nikiwa ndani ya Bunge na nje ya Bunge, pia na kwa ofisi ya Spika, shukrani zangu haziwezi kuwa na ukomo. Naitukuza kila fursa niliyopewa.

**B. MASUALA YA MUUNGANO**

**4. Mheshimiwa Spika,**Ukweli ni kuwa masuala ya Muungano yameelezwa vizuri katika Ibara ya (4)(3) na kuorodheshwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba. Kuna hoja ambazo kwa miaka yote imekuwa ni kilio kutoka upande wa pili wa Muungano na kupelekea kuundwa kwa tume kadhaa ili kutatua kero hizo za Muungano. Kero hizo ambazo zimekuwa zinapigiwa kelele miaka yote ni;

- Mafuta na Gesi Asilia
- Mambo ya Muungano
- Ajira za Wazanzibari katika Taasisi za Muungano
- Uwezo wa Zanzibar Kukopa Nje
- Gawio la Zanzibar katika Mali za Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (EACB)
- Mfuko wa Pamoja wa Fedha
- Utozwaji Kodi mara mbili kwa Wafanyabiashara wa Zanzibar

**5. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) peke yake ama kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano, zimechukua hatua kadhaa za kutafuta ufumbuzi wa Kero za Muungano. Kwa upande wa SMZ, miongoni mwa hatua ilizochukua na ambazo zinajulikana ni pamoja na kuunda Kamati mbali mbali. Miongoni mwa Kamati zilizoundwa na SMZ kushughulikia Kero za Muungano kati ya mwaka 1990 na 2003 ni pamoja na zifuatazo:

- (a) Kamati ya Baraza la Mapinduzi (Kamati ya Amina) ya 1992.
- (b) Kamati ya Rais ya Kupambana na Kasoro za Muungano (Kamati ya Shamhuna, 1997).
- (c) Kamati ya Rais Kuchambua Ripoti ya Kisanga (Kamati ya Salim Juma).
- (d) Kamati ya Rais ya Kuandaa Mapendekezo ya SMZ juu ya Kero za Muungano. (Kamati ya Ramia, 2000).
- (e) Kamati ya BLM juu ya Sera ya Mambo ya Nje.
- (f) Kamati ya Rais ya Wataalamu juu ya Kero za Muungano (2001).
- (g) Kamati ya BLM ya Jamuiya ya Afrika Mashariki.
- (h) Kamati ya Mafuta

- (i) Kamati ya Madeni baina ya SMZ na SMT.
- (j) Kamati ya Suala la Exclusive Economic Zone (EEZ)
- (k) Kamati ya Masuala ya Fedha na Benki Kuu.
- (l) Kamati ya Rais ya Masuala ya Simu – (1996 – 1999)

Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pia imewahi kuajiri mtaalamu wa mambo ya fedha, Dr. Courtrey Blackman na Mtaalam wa masuala ya mafuta katika kutafuta suluhu ya mambo hayo yanayoyumbisha Muungano wetu, lakini kamati zote hizo hazikuzaa matunda.

**6. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa tatizo kubwa liko kwenye Muundo wa Muungano na suluhu ya tatizo hilo ni kubadilisha Muundo ili Muungano wetu uimarike zaidi na kuwa wenye manufaa kwa pande zote washirika.

**7. Mheshimiwa Spika**, Mbali na baadhi ya Kamati hizo za SMZ peke yake, SMT na SMZ zimeunda Tume, Kamati na Kuajiri Wataalamu mbali mbali ili kutafuta suluhisho la Kero mbali mbali za Muungano. Miongoni mwa Tume na Kamati hizo ni kama zifuatazo:

- (a) Kamati ya Mtei
- (b) Tume ya Nyalali
- (c) Kamati ya Shellukindo
- (d) Kamati ya Bomani
- (e) Kamati ya Shellukindo 2, ya kuandaa Muafaka juu ya Mambo ya Muungano baina ya SMZ na SMT.
- (f) Kamati ya Harmonisation.
- (g) Kamati ya Masuala ya Simu (Kamati ya Kusila)

Aidha SMZ na SMT zimefanya vikao vya pamoja visivyopungua 80 katika ngazi mbali mbali ili kuzungumzia Kero za Muungano. Aidha Serikali hizi mbili mwaka 1994 ziliomba msaada wa IMF ili kuzishauri kuhusiana na Benki Kuu, mgawano wa misaada na uhusiano wa kifedha (intergovernmental fiscal relationship). Mbali ya juhudi zote hizo, tarehe 14 Novemba, 2000 wakati Rais Benjamin Mkapa alipokuwa akizundua Bunge aliahidi kuzipatia ufumbuzi Kero

za Muungano ndani ya siku 60!! Tokea ahadi ilipotolewa hadi leo ni ni miaka 19 imepita. Serikali zinazoongoza ni zile zile za Chama cha Mapinduzi. Kuchelewa huko kutatua kero hizo kunaonesha dhahiri kwamba Serikali za CCM hazijatoa kipaumbele kwa muungano huu kuendelea kuwepo.

**a. TUME YA PAMOJA YA FEDHA -Joint Finance Commission-JFC**

**8. Mheshimiwa Spika,**Tume ya Pamoja ya Fedha (Joint Finance Commission – JFC) ni asasi ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (ya mwaka 1977) na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Sura 140 ya mwaka 1996). Tume ilizinduliwa rasmi tarehe 5 Juni, 2003, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteua Makamishna saba. Aidha Tume ina Sekretarieti ambayo ni chombo kikuu kiutendaji. Tume hii ilikuwa ni njia mojawapo ya kutatua kero za kifedha kati ya zile kero kuu za Muungano lakini kwa masikitiko makubwa hata Tume hiyo ambayo ni chombo cha kiutendaji kimeshindwa kutimiza azma ya uanzishwaji wake.

**9. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Katiba, Tume ya Pamoja ya Fedha ina majukumu yafuatayo:

a) Kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao wa kila mojawapo ya Serikali hizo;

b) Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili;

**10. Mheshimiwa Spika,** aidha, Ibara ya 133 ya Katiba inaeleza kuwa; *“Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti maalum itakayoitwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali Mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu*

*wa Sheria iliyotungwa na Bunge, kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano”.*

11. **Mheshimiwa Spika**, hoja ya msingi hapa ya kuomba majibu kutoka Serikalini ni je hiyo Akaunti ya Pamoja imeshafunguliwa?

12. **Mheshimiwa Spika**,kwa kuwa toka uwepo wa Tume imeshindwa kutatua kero za kifedha zinazohusiana na Muungano na hivyo malalamiko kuzidi kurundikana, ni wazi kuwa chombo hiki licha ya kuwa ni chombo cha kikatiba kimekosa uhalali kwa wananchi wa kuendelea kutengewa fedha za walipa kodi katika kufanya kazi zake.

13. **Mheshimiwa Spika**, ni muda mwafaka sasa kama ambavyo wanazuoni mbalimbali wa masuala haya ya muungano walivyo na wanavyozidi kushauri kuwa tatizo ni muundo wa Muungano, hivyo vyombo vyote vitakavyoundwa kwa nia njema ya kuleta suluhu vitashindwa kufanyakazi iliyopo na inayokusudiwa.

14. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kuwa ili matatizo au kero za Muungano ziishe hatuna budi kurejea kwenye mapendekezo yaliyotolewa katika rasimu ya pili ya KATIBA iliyotolewa na Tume ya Marekebisho ya Katiba iliyokuwa chini ya Uenyekiti wa Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba kuhusiana na Muundo wa Muungano.

15. **Mheshimiwa Spika**,Kwa ufupi naomba kunukuu “Ibara ya 60(1) ya Rasimu ya Pili ya Katiba kama wananchi walivyohitaji Muundo wa Muungano wetu utakavyokuwa: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na Muundo wa shirikisho lenye Serikali tatu ambazo ni;-

- a. Serikali ya Muungano
- b. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na;
- c. Serikali ya Tanganyika.

**16. Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia sera yake uk. 13 &14 Sura ya 2.4 inaeleza wazi aina na Muundo wa Muungano na kueleza malengo yatakayofikiwa kuwa ni kila nchi mshirika wa Muungano itakuwa na mamlaka kamili katika kumiliki na kutumia rasilimali na maliasili zake; isipokuwa masuala yote ya msingi ya jumla kama vile Katiba ya Shirikisho la Jamhuri ya Muungano, Mambo ya nje na ushirikiano wa Kimataifa, Ulinzi na Usalama, Uraia, Sarafu ya Benki Kuu, Mfumo wa Elimu, Mahakama ya Katiba na Bunge la Shirikisho yatashughulikiwa na Serikali ya Shirikisho.

**17. Mheshimiwa Spikia,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini juu ya kuurudisha Muungano karibu zaidi na wananchi kwa kuwashirikisha kwa njia mbali mbali, kuchagua na kuyatambua yale wanayoyataka katika Muungano wao ili yaheshimiwe.

**C. UHIFADHI NA UENDELEU WA MAZINGIRA**

**18. Mheshimiwa Spika,** mazingira ni dhana pana inayojumuisha vitu vyote vinavyotuzunguka, iwe ni sekta ya maji (maziwa, bahari, mito, mabwawa aina na mbinu za kupata rasilimali ziishizo kwenye maji-aina ya uvuvi n.k), sekta ya kilimo(matumizi bora ya uhifadhi wa ardhi-aina za mitambo ya kilimo inayotumika, matumizi ya mbolea, matumizi ya madawa), sekta ya misitu(upandaji wa miti na ukataji wa misitu) sekta ya viwandani (Jinsi mabaki ya viwandani yanavyohifadhiwa na aina ya teknolojia inayotumika katika uzalishaji), sekta ya afya (Taka zinavyotunzwa na kuteketezwa) n.k. Maisha ya binadamu na viumbe vingine yanategemea sana hali ya mazingira, ndiyo maana nimeyaita mazingira kuwa kitalu cha maisha. Kutokana na umuhimu huo usio na shaka, mazingira ni miongoni mwa masuala mtambuka.

**19. Mheshimiwa Spika,** licha ya Serikali kutambua umuhimu wa mazingira; na kuweka sheria, kanuni na miongozo ya ulinzi na uhifadhi wa mazingira kama vile Sera ya Mazingira ya mwaka 1997, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, Mpango Kazi wa Taifa wa Mazingira (National Environmental Action Plan 2013), MKUKUTA awamu ya Pili

mwaka 2010; Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 pamoja na kuridhia mikataba mbali mbali ya kimataifa kuhusu uhifadhi na utunzaji wa mazingira; bado suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira halijapewa umuhimu na uzito unaostahili.

**20. Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kwamba shughuli yoyote inayofanywa na binadamu katika uso wa dunia, ina athari za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja katika mazingira. Athari hizo zinazosababishwa na binadamu katika mazingira, baadaye hugeuka na kuathiri tena maisha ya binadamu na viumbe vingine pia.

**21. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ilidhani kwamba jambo hili ambalo linagusa karibu kila sekta ambayo binadamu anafanya shughuli za kuendesha maisha yake lingepewa uzito angalau hata wa kujadiliwa siku mbili lakini limepewa siku moja tu.

**22. Mheshimiwa Spika**, ni jambo la aibu kwa Serikali hii kutegemea fedha za nje kukabiliana na majanga yanayotokana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa mfano, kipindi hiki cha mvua ambapo mafuriko yamebomoa nyumba nyingi za wananchi; mazao mashambani yameharibiwa vibaya miundombinu ya barabara na madaraja yameharibiwa vibaya, wananchi wamepoteza maisha kwa kusombwa na maji tsubiri fedha za nje ambazo hatujui zitatolewa lini kukabiliana na majanga hayo?

**23. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, mazingira ni suala mtambuka (cross cutting issue); lipo kila mahali na madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira yanagusa karibu sekta zote, hivyo ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali ,kutenga fedha za kutosha kutunza na kuhifadhi mazingira yetu; lakini pia kwa ajili ya kukabiliana na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira.

**24. Mheshimiwa Spika**, tathmini ya jumla ya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwenye utunzaji na uhifadhi wa



mazingira ni kama ifuatavyo:- Jumla ya fedha iliyodhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/18 ilikuwa shilingi bilioni 6.788, lakini fedha iliyotolewa na kutumika (ambayo ni ya nje tu) hadi kufikia tarehe 8 Machi, 2018 ilikuwa ni shilingi bilioni 1.7 sawa na asilimia 25 tu ya bajeti ya maendeleo iliyodhinishwa na Bunge.

**25. Mheshimiwa Spika**, kwa utekelezaji huo duni wa bajeti, ni wazi kwamba Serikali haiko makini kabisa katika suala hili la mazingira. Tafsiri ndogo ya takwimu nilizozitoa ni kwamba Serikali imeweka rehani maisha ya wananchi kwa wahisani.

**D. UCHUMI WA KIJANI (Green economy)**

**26. Mheshimiwa Spika**, Uchumi wa kijani ni uboreshaji wa uchumi na ustawi wa jamii unaozingatia uzalishaji na matumizi yasiyoharibu mazingira. Ukiangalia hati idhini inaonesha kuwa moja ya kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais ni “Promotion of Cleaner Production and Green Economy”

**27. Mheshimiwa Spika**, imethibitika kuwa Tanzania inapoteza zaidi ya hekta 372,000 kila mwaka eneo linalokadiriwa kuwa sawa na ukubwa wa nchi ya Rwanda, kutokana na ukataji miti kwa matumizi ya nishati ya kuni na mkaa, uchomaji wa misitu unaofanywa na baadhi ya Raia wasio waaminifu kwenye hifadhi mbalimbali nchini. Jambo hilo linaathari kubwa katika mkakati wa nchi yetu wa kujikita katika uchumi wa kijani.

**28. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kwamba zaidi ya asilimia 90 ya nishati inayotumika katika familia za Tanzania wanategemea nishati inayotokana na miti na mabaki ya mazao ya shambani au taka zingine zaidi ya zile za plastiki kwa matumizi ya kila siku ya majumbani kwao.

**29. Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa vijijini asilimia 2 kutoka kwenye umeme na asilima 8 inatokana na bidhaa za petroli<sup>1</sup>. Kati ya nishati hiyo kuni na mkaa ndio chanzo kikuu cha nishati kwa wananchi waishio mijini na Vijijini. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza uchumi wa gesi tulioaminishwa kuwa upo

na ndio muharobaini wa kututoa hapa kwenye matumizi makubwa ya nishati itokanayo na miti upo au umeondoka katika awamu hii ya Tano?

**30. Mheshimiwa Spika**, ukuaji wa uchumi unaozingatia matumizi yasiyo endelevu ya maliasili hauna manufaa katika dunia ya leo. Watu wanapaswa kuachana na mbinu za kizamani za ukuaji wa uchumi wa matumizi shinikizi ya rasilimali, ambapo maendeleo yamekuwa yakigharimu mazingira; badala yake, wanapaswa kufuata mbinu mpya ambazo tija huongezwa kwa kutumia na kusimamia maliasili kwa ufanisi zaidi.

**31. Mheshimiwa Spika**, shughuli za kiuchumi lazima zizingatie athari za muda mrefu kwa mazingira na haja ya kuhifadhi urithi wetu wa pamoja kwa faida ya vizazi vijavyo<sup>22</sup>Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uzinduzi wa jukwaa la uchumi wa kijani mjini iringa tarehe 08 mei, 2012

. Uchumi wa kijani huchochea ukuaji wa uchumi, mapato, na ajira. Tena husaidia kuimarisha mazingira na kuongeza tija kwa wananchi. Aidha aina hii ya uchumi huleta maendeleo ya kiuchumi ya muda mrefu na yanayotoa fursa kwa watu wengi.

**32. Mheshimiwa Spika**,Katika baadhi ya sekta muhimu kama vile kilimo, ujenzi, misitu, na usafiri, uchumi wa kijani hutengeneza ajira nyingi zaidi kuliko ambazo zipo katika hali ya kawaida. Katika sekta kama vile uvuvi; uchumi wa kijani utalazimisha kushuka kwa mapato na ajira katika muda mfupi na wa kati ili kujazia hifadhi asilia, lakini hali hii hubakia ya muda mfupi na baadaye sekta hukua na kutoa tija kubwa kwa wananchi.

**33. Mheshimiwa Spika**,Jitihada za maendeleo nchini Tanzania lazima zifanywe kwa kuzingatia uhalisia wa mambo. Kwanza, zaidi ya asilimia 75 ya wananchi wa nchi hii huishi vijijini. Hivyo, jitihada madhubuti za kupunguza umaskini na

kuleta maendeleo lazima zilenge wakazi na uchumi wa vijijini ili kuwa na matokeo mazuri. Kuna uhusiano mkubwa kati ya watu maskini hasa wa vijijini na mazingira.

**34. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwa muktadha huo wa uchumi wa kijani, ni kweli uwekezaji wa mradi wa kuzalisha umeme unaotokana na nguvu za maji (Stigler's Gorge) uliophelekea kufyekwa kwa misitu kwenye eneo ambalo ni sawa na ukubwa wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ofisi hii ya Makamu wa Rais inatoa kauli gani kuhusiana na utekelezaji wa mradi huo?

**35. Mheshimiwa Spika,** uchumi wa kijani sio kama unaishia kwenye kufyeka misitu tu bali pia matumizi sahihi na endelevu ya pembejeo za kilimo kama vile (mbolea na madawa) yanayotumiwa kwenye kilimo ili ardhi isiharibike na hivyo kushindwa kuhimili uzalishaji wa mazao.

#### **E. MABADILIKO YA TABIANCHI**

**36. Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya mfumo wa hali ya hewa yanayosababishwa na kazi za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja za binadamu, ambazo zinaongeza gesi joto (Greenhouse Gases) na kubadilisha mchanganyiko wa viwango vya gesi katika angahewa la dunia, ambayo pia ni nyongeza ya mabadiliko ya asili ya mfumo wa hali ya hewa yaliyotathminiwa na kulinganishwa kwa muda mrefu (usiopungua miaka thelatini na zaidi).

**37. Aidha, Mheshimiwa Spika,** Mabadiliko ya tabianchi kwa kiasi kikubwa (zaidi ya 95%) yanasababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwemo uzalishaji wa viwanda unaotoa gesi ukaa (carbon dioxide) kwa kiwango kikubwa sana. Matokeo au athari za mabadiliko ya tabianchi ni:

- kuongezeka kwa joto
- mvua kubwa na za muda mfupi
- mafuriko
- mvua ya mawe ikiambatana na upepo mkali
- mvua fupi zisizo za msimu

- ukame wa muda mrefu na unaojirudia mara kwa mara.

Tabia hizi zote zimeshajitokeza hapa nchini.

**38. Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya tabianchi ni jambo linalohusu sekta zote za uchumi katika nchi, iwe kwenye kilimo, mifugo, uvuvi, miundombinu ya barabara, misitu, afya kwa kuzuka magonjwa mapya, sekta ya wanyapori n.k. hivyo jambo hili ni jambo kubwa sana kuliko ambavyo Serikali inalichukulia kwa urahisi sana. Uwekezaji unaofanywa unaweza kuwa kazi bure kama hatukuwekeza vya kutosha katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**39. Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya tabianchi, ambayo pia huchangiwa na uharibifu mkubwa wa mazingira umeleta athari kubwa katika sekta mbalimbali za maendeleo ya jamii na sekta zingine ziko katika hatari ya kuathirika pia. Sekta hizi ni nishati, kilimo na usalama wa chakula, maji, mifugo (kwa kuzuka kwa magonjwa ya milipuko, ukosaji wa malisho na maji), uvuvi, misitu, wanyapori, afya, miundombinu, utalii, n.k.

**40. Mheshimiwa Spika**, Tanzania tayari imeshuhudia madhara ya mabadiliko ya tabianchi, Mabadiliko ya misimu ya uzalishaji kwa wananchi yanachangia kwa kiasi kikubwa katika shughuli za kiuchumi. Kila mabadiliko ya tabianchi yanayotokea kila mwaka yanapelekea gharama za uchumi kuongezeka kwa asilimia 1 ya pato la Taifa. Na kadri madhara yanavyozidi, inazidi kupunguza ukuaji wa uchumi na hivyo kuendelea kuathiri maisha ya mamilioni ya watanzania<sup>3</sup>. Athari za mabadiliko ya tabianchi ni zaidi ya uharibifu wa mazingira; huathiri na kurudisha nyuma juhudi za maendeleo ya nchi hususani zinazotegemea maliasili kama Tanzania.

**41. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba mabadiliko ya Tabianchi sio nadharia za kwenye vitabu tu kama ambavyo watu wengi pamoja na Serikali inavyoamini, bali ni jambo la uhalisia usiokuwa na hata chembe ya mashaka kama ripoti mbalimbali za kisayansi zinavyothibitisha.

**42. Mheshimiwa Spika**, wakati nchi yetu imeridhia mikataba ya kimataifa kuhusu namna ya kukabiliana na athari za kimazingira na mabadiliko ya tabia nchi; lakini kinachofanyika ndani hasa suala la kutenga na kutekeleza bajeti kuhusu masuala hayo bado, tuko nyuma sana.

**43. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kwamba Tanzania imekuwa inachukua hatua mbalimbali katika kuelezea mabadiliko ya tabianchi kwa muktadha wanchi yetu na hivyo kutayarisha nyaraka muhimu za mkakati kama vile "The National Climate Change Strategy (2012) and the Zanzibar Climate Change Strategy (2014)" ambazo zinaeleza kwa kina hatua za kuchukua katika kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

**Kambi Rasmi inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini kila mara inashindwa kutenga kutoa fedha za ndani ikiwa kulikuwa na Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Mabadiliko ya Tabia Nchi. Au ndio kusema Mkakati huo haukuwa na kipegele cha bajeti kwa ajili ya kuutekeleza?**

#### **F. MAPITIO YA BAJETI ZA UTEKELEZAJI MIRADI YA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI 2018/19-2020**

**44. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa mabadiliko ya Tabianchi nisuala mtambuka na sio tu linaathiri sekta moja, ili kukabiliana na suala hili nguvu toka pande zote inatakiwa kutumika. Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37 miradi inayohusu kujiandaa kwa majanga na mabadiliko ya Tabianchi haikupata hata senti moja;

I. Mradi wa kujenga uwezo wa kujiandaa na kukabili maafa ambao ulitengewa jumla ya shilingi 176,530,200 za kutoka nje, lakini hadi Febr 2019 hakuna hata shilingi iliypokelewa na kutolewa.

II. Mradi wa kuimarisha upatikanaji wa taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi na mifumo ya Tahadhari, uliokuwa umetengewa jumla ya shilingi 286,923,269 fedha za nje, lakini fedha hizo hazikupatikana.

45. **Mheshimiwa Spika**, kwa bahati mbaya sana ukiangalia mpango wa maendeleo kwa fungu hilo 37 miradi ni hiyo hiyo ya toka mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 kwa Kasma 5306 na Kasma 6575 inaombewa kuidhinishiwa fedha za nje shilingi 36,577,565,737. Fedha za ndani kwa kasma zote za Miradi ya Maendeleo hakuna hata shilingi moja ya fedha za ndani.

46. **Mheshimiwa Spika**, miradi hii kwa kiwango kikubwa inahusu usalama wa wananchi na mali zao, lakini kitendo cha Serikali kutegemea fedha za utekelezaji wa miradi hii kutoka nje, maana yake ni kuweka rehani usalama wa watanzania na mali zao. Jambo hili kwa kweli halikubali na linatakiwa kukemewa kwa nguvu zote.

47. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira fedha za maendeleo zilizotengwa zilikuwa ni shilingi 5,063,340,000 lakini hadi mwezi Machi 2019 zilitolewa ni shilingi 2,400,099,489.50 zikiwa ni fedha za nje. Bajeti hiyo ya shilingi bilioni 5.063, asilimia 69.6 zilikuwa ni fedha za mazingira na tabianchi lakini hadi Februari 2019 hakuna hata senti moja ya fedha za ndani iliyotolewa.

48. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka huu wa fedha miradi hiyo inayohusu mazingira na mabadiliko ya Tabianchi inaombewa jumla ya shilingi 18,218,915,441.73. Katika fedha hizo zinazombwa hakuna hata shilingi moja ya fedha za ndani inayoombwa, hili nalo ni jambo la kujjuliza kama kweli Serikali yetu inaona umuhimu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi? Tukumbuke kuwa miradi yote inayojengwa kama hatukuwa na mpango mahususi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi inaweza kuwa ni kazi bure kwa muda mfupi sana.

#### **G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2019**

49. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 7.86 kwa Fungu 26, na shilingi bilioni 29.07 kwa fungu 31 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa angalizo tu, kwani mwaka wa bajeti unaomalizika

Fungu 26 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 6.5 na kwa fungu 31 iliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 15.065.

**50. Mheshimiwa Spika**, kati ya hizo zilizoombwa walipewa kwa fungu 31 walipokea asilimia 52.7 hadi mwezi Februari, 2019. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni kwa nini muombe kubwa zaidi wakati mnaona uwezo ni mdogo au kipaumbele cha Serikali sio Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi?

**H. HITIMISHO**

**51. Mheshimiwa Spika**, Ofisi hii ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ndiyo yenye mamlaka kama kutakuwa na dhamira na nia njema ya kuhakikisha kwamba Kero na malalamiko ya Muungano zinamalizika. Pili ndiyo yenye mamlaka ya kuhakikisha kuwa Tanzania tunaingia kwenye uchumi wa kijani, kama ambavyo imeelezwa hapo awali.

**52. Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa ni kwamba ofisi hii inashindwa kusimama kwa miguu yake na kuhakikisha yale yote yaliyomo kwenye Hati Idhini inayasimamia kwa ukamilifu wake na badala yake malalamiko ya Muungano bado ni kitendawili japokuwa tunaambiwa vikao vya pamoja vinakaa, lakini matunda ya vikao hivyo hayaonekani kwa wananchi.

**53. Mheshimiwa Spika**, tumepokea taarifa kuwa vile vinavyoitwa vikao vya kutatua kero za Muungano kupitia Kamati ya Pamoja vinaelekea kurasimishwa zaidi kwa kutengenezewa ratiba yake na kuundiwa kamati mbili yaani ile ya Uchumi na Fedha na ile ya Sheria na Utawala katika nia ya kutekeleza maamuzi kadri yanavyofikiwa.

**54. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kuwepo kwa uwazi zaidi katika hatua za utatuzi wa changamoto za Muungano na pia hatua shirikishi katika viwango mbali mbali ili kuondosha dhana kuwa Muungano huu ni wa viongozi zaidi na sio wananchi

55. **Mheshimiwa Spika**, Miradi zaidi ingepaswa kubuniwa ambayo ni ile Tanzania kuwa na uchumi endelevu na wenye kutoa ajira kwa wananchi wengi (Uchumi wa kijani ni uboreshaji wa uchumi na ustawi wa jamii unaozingatia uzalishaji na matumizi yasiyoharibu mazingira).

56. **Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kwamba Tanzania bado ina fursa nyingi katika kuifanya nchi yetu kuwa kwenye uchumi wa kijani, na fursa hiyo ilikuwa ni kuifanya TANZANIA kutumia rasilimali gesi kwa kiwango kikubwa ili kudhibiti matumizi ya nishati itokanayo na miti (kuni na Mkaa) hapa nchini ili juhudu zinazofanywa na Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Kiserikali matunda yake kuonekana.

57. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
Latifah H.Chande (Mb)

**K.N.Y MSEMAJI MKUU – KAMBI RASMI YA UPINZANI-OFISI YA  
MAKAMU WA RAIS  
MUUNGANO NA MAZINGIRA  
16 Aprili, 2019**

**MWENYEKITI:** Sasa tunaanza na uchangiaji, tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Sware dakika tano, anakuja Mheshimiwa Hawa dakika tano halafu atakuja Mheshimiwa Najma nae dakika tano.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Nitaanza kwa kutafakari kwa pamoja. Ni dhahiri kwamba Taifa letu bado halijatambua thamani ya mazingira na afya ya mazingira na hili lipo linajionesha dhahiri ndani ya Serikali baina yetu sisi hapa Wabunge hata na jamii inayotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu ukiangalia tu kwa Wizara zilizopita humu ndani Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tunagombania nafasi za kuchangia kama



ni TAMISEMI au ni Utawala Bora au ni Ofisi ya Waziri Mkuu na vitengo vyake lakini sasa kama tulikuwa tunakimbilia kutetea shule, barabara, vyakula, afya na kadhalika tulitakiw atujue kwamba kiini kinachotubeba sisi kama Taifa na afya na uchumi wa Taifa, ni mazingira. Mazingira ndiyo kiini cha maendeleo. Tungelitambua hilo tukaisimamia Serikali ipasavyo tungetoka kwenye huu umaskini, kwa sababu hali ya umaskini inajengwa na vitu vikuu vitatu, uchumi duni, utawala bora na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania mazingira ndiyo yanayotubeba, kwa sababu hata hao wananchi wetu huku vijijini asilimia 96 wanategemea maliasili, zaidi ya asilimia 90 wanategemea nishati kutoka kwenye maliasili. Kama tunaongelea viwanda, maji safi na salama inategemea na hali ya mazingira iliyopo. Kama mazingira yanachechemea hatutakaa tukote katika dimbwi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitunga Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 kama Mheshimiwa Waziri husika alivyosema na ilianisha mambo sita makuu ya uharibifu wa mazingira. Tuliainisha changamoto za uharibifu za vyanzo vya maji, hii tunaangalia mito, mabwawa, bahari na kadhalika; tuliainisha uharibifu mkubwa wa maji safi ambayo yanaenda kujenga uchumi kwa sababu kusipokuwa na wananchi wanaopata maji safi inaenda kuharibu afya yao binafsi, mifugo au na chochote kinachotegemea maji safi; tuliainisha uharibifu wa ardhi, ardhi ndiyo iliyobeba miundombinu ambayo tunaitegemea sisi aidha sekta za kilimo na vinavyobebwa na kilimo au ni shughuli za madini na kadhalika; na tuliainisha kwamba kuna upotevu mkubwa wa makazi ya viumbepori na bioanuwai. Hivi vyote kwa ujumla wake ni nguzo hizo sita ambazo zinabeba shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 22 iliyopita Mheshimiwa Waziri umesema haya na sasa hivi tunachanganua hii sera kwa upya wake, ardhi inasemaje, uharibifu wa ardhi upo katika *percent* ngapi na una-*reflect* vipi hali ya uchumi? Kwa sababu unapoharibu ardhi

inamaana unaharibu na uzalishaji ambao unategemeana na ile ardhi. Kama unaharibu vyanzo vya maji hupati maji safi au maji yanayotakiwa unaenda kuwa *reflected* kwenye shughuli za kiuchumi. Tunalia kila siku kuhusu bajeti ya maji haitoshi, sasa tungeweza ku-*link* kuhusu upatikanaji wa maji, *budget wise* na upatikanaji maji kwenye kutunza vyanzo vya maji na njia za maji basi tungeweza kwenda sambamba na kukuza uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera yetu imeainisha mambo sita makubwa ambayo bado hayana ufumbuzi kwa sababu bado tunaharibu mazingira, sasa nayo yanakuwa *reflected* kwenye uchumi wetu. Uchumi wa mtu mmoja mmoja unategemea na hayo mazingira kwa sababu kila mtu anategemea mazingira hayo. Mfano tu mfupi, usipokuwa na maji safi kwanza ukinywa maji machafu au maji hayako salama jamii hiyo husika inapata maradhi, kwa hiyo, inaenda ku-*reflect* bajeti ya afya, bdo tunazidi kuididiza. Kama hupati maji kwa ajili ya kilimo chako cha umwagiliaji unategemea mvua na sasa hivi kuna mabadiliko ya tabianchi ina maana uzalishaji wako utakuwa wa wasiwasi hutakaa utoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuipa nguvu Sheria yetu ya Mazingira ambayo imeainisha mambo makuu manne, kuna utafiti, uelimishaji na kadhalika, hii sekta inaweza ikatutoa hapa kwenye dimbwi la umaskini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. (*Makofi*)

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwape bajeti inayotakiwa, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Ofisi ya

Makamu wa Rais na nitajikita zaidi kwenye suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe masikitiko yangu makubwa sana kuhusiana na bajeti ya Wizara hii. Kama ambavyo hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imesema imekuwa ni mazoea kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kutokutengewa bajeti ya kutosha na hata hiyo kidogo ambayo inawekwa haifiki kama ilivyokusudiwa, hivyo kupelekea ufanyaji kazi katika hii kuwa mgumu kuliko ambavyo tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tunafahamu suala zima la mazingira ndiyo roho za sisi Watanzania. Tunapodharau mazingira tutegemee tutapata elimu na afya tunajidanganya. Bila mazingira hakuna afya, elimu na miundombinu vinginevyo tunajisumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wakizungumzia kuhusiana na sula zima la ukatazaji wa matumizi ya mifuko ya plastiki. Bahati nzuri niko kwenye Kamati ya Mazingira, suala hili lilianza muda mrefu na sisi kama Kamati tulijaribu sana kuishauri Serikali na kuangalia ni kwa namna gani wanaweza wakafanya ili kusaidia hawa wenye viwanda ambao wanatengeneza mifuko ya plastiki waweze kutengeneza kwa teknolojia ya kisasa. Teknolojia za kisasa zipo ambapo mifuko hii mingine watu wanatengeneza na inaoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama Serikali imejiandaaje baada kuzuia matumizi haya kwa nchi jirani ambazo zinazalisha kwa wingi kuliko tunavyozalisha Tanzania mifuko ya plastiki kuingia nchini kwetu? Kwa sababu ni ukweli usiopingika Tanzania tunazalisha mifuko ya plastiki kwa asilimia 30 peke yake lakini asilimia 70 ya mifuko ya plastiki inayoingia nchini kwetu ni mifuko inayotoka nje ya nchi. Je, Serikali imejipanga namna gani kuhakikisha kwamba mifuko hii haiwezi kuingia nchini Tanzania na matumizi ya mifuko ya plastiki yakaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati tunakataza mifuko ya plastiki tumejiandaa na vifungashio vya aina gani? Kwa sababu nachokiona hapa ni makatazo tu lakini hatujaambiwa kwamba tunakwenda kutumia mifuko ya aina gani, leo tutakuwa tunabeba mikononi bidhaa ama tutakuwa tunafanyaje? Kwa hiyo, tungeomba sana Waziri anapokuja hapa atuambie ili Watanzania wajue baada ya mifuko ya plastiki kukatazwa tarehe 1 siji Mei au Julai, nini ambacho kitatumika mbadala badala ya mifuko hii ya plastiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ya mazingira ni mtambuka kama nilivyosema, kwa hiyo lisiishie kwenye masuala ya mifuko ya plastiki peke yake, je, suala la mkaa limefikia wapi mpaka sasa? Kwa sababu ya kupata mkaa watu wanakata sana miti. Leo tunaambiwa nchi inakwenda kuwa jangwa kwa asilimia 61, hii ni asilimia kubwa sana kwa nchi ya Tanzania, tunapoelekea vizazi vyetu vitakuja kukuta nchi imeshakuwa jangwa, hali ni mbaya kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapofikiria zaidi mifuko ya plastiki, mimi huwa nasema vitu vidogo vidogo Mheshimiwa Waziri anajua, tusing'ang'anie na vitu vidogo vidogo kama mifuko ya plastiki tuangalie uhalisia wa mazingira, vitu vingi zaidi vinategemea mazingira yetu. Kama mazingira hayataboreshwa tusije tukategemea hivi vyote ambavyo tunavifanya vitaendelea kuwepo kwa sababu ni lazima vitapotea kutokana na kwamba mazingira siyo rafiki, tunakwenda kuingia kwenye ukame wa hali ya juu. Kama ambavyo mmeshuhudia kuna maeneo ambayo mvua hazijanyesha kabisa, kuna maeneo kama kwenye Mikoa yetu ya Tabora tulikuwa tunapata mvua misimu miwili, leo Tabora ukienda ni msimu mmoja tu ndiyo mnapata mvua na mvua zenyewe siyo za zinatoshleza, hali ni mbaya kweli kweli kila maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali iangalie upya kuhakikisha kwamba bajeti inayotakiwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais inapelekwa kama ilivyokusudiwa kuliko kutegemea bajeti za wafadhili. Hawa wafadhili leo

umeomba bajeti ya asilimia 40 unaletewa bajeti asilimia 10, mwisho wa siku mambo yanakuwa hayaendi ama hawaleti kabisa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Najma, ajiandae Mheshimiwa Josephine Genzabuke, wote dakika tano tano.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa dakika hizo tano. Kwanza kabisa, naanza kwa kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Muungano. Nitumie fursa hii kumuunga mkono sana na kuwapongeza Waziri wa Muungano, Mheshimiwa January Makamba na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mussa, kwa kazi nzuri wanayofanya lazima niwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natumia fursa kwa kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameondoa changamoto iliyokuwa inatukabili muda mrefu ya deni la *ZECO*. Hilo lazima tushukuru sana na kupongeza na hii inathibitisha kwamba Mheshimiwa Rais ni muumini wa kweli wa Muungano wetu. Hilo lazima tulioneshe na Watanzania lazima waelewe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mazuri yanayofanywa na Mheshimiwa January na timu nzima, napenda kusema kwamba sote tunaupenda Muungano, mimi ndiyo muumini wa kwanza wa Muungano. Katika kuupenda Muungano tunaomba hayo ambayo mmeyakusudia na kuyaendeleza muyafanyie kazi inavyostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize maeneo matatu kwa haraka haraka. Fursa za kiuchumi Zanzibar ni jambo linalopigiwa makelele siku zote. Miaka ya 1985 mpaka tunakwenda 2000 wenzetu wa Tanzania Bara walikuwa wanakuja kufanya biashara Zanzibar, wanabeba mali kule

na wanatunufaisha Wazanzibari. Sijui kimetokea nini hapa katikati, ndugu zetu wa Tanzania Bara mnamia Rwanda, Burundi, Kenya na Uganda mnatuacha jirani zenu, hebu angalieni hapo tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwenye masuala ambayo tunaungana, nakwenda kwenye Balaza la Mitihani la Taifa, hapo bado hapajakaa vizuri. Kuna *communication, coordination* na *cooperation* ndogo, tuweke sawa hapo. Balaza la Mitihani lile na chombo maalum kinachotambulika kisheria ili ku-*coordinate, cooperate* na ku-*communicate* baina ya Wizara zetu mbili, tutakwenda vizuri, tunaupenda Muungano. Pia *NACTE* kwenye elimu ya juu, tuangalie kinachotambulika Tanzania Bara na Zanzibar kitambulike. Tunaomba tufanye hayo kwani tutakwenda vizuri na Muungano wetu Mheshimiwa January na timu yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine zuri kabisa, naomba niliseme kwa Watanzania wote kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejenga misingi imara ambayo inaweza kulidumisha Taifa letu miaka mia ijayo. Kwa hiyo, yale marekebisho madogo madogo ambayo tunaomba yanaendelea kufanyika siku zote isiwe ni neno la kuleta mjadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na marekebisho madogo madogo, Katiba yetu iko vizuri na tutakwenda nayo vizuri hata miaka mia ijayo kwa sababu kila kilicho ndani ya Katiba ile kinatafsirika vizuri. Hiyo *implementation* ni jambo lingine wala siingilii lakini Katiba yenyewe kama Katiba inatufaa na ndiyo maana ikatufikisha miaka 55 hii na tukiwa tunasifiwa na mataifa yote ulimwenguni kwa Muungano ambao tunao, kwa nini tusiringe? Lazima turinge na Taifa letu kwa sababu Muungano wetu ni mzuri, uko *very unique*, inatakiwa na mataifa yote waige kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kuendeleza haya, hizo changamoto tuzimalize kwa muda unastahiki ili

tuweze kujivunia zaidi Muungano wetu na kuupenda zaidi Muungano wetu. Mimi naipenda Zanzibar, naipenda Tanzania Bara lakini nakupenda Muungano zaidi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Genzabuke, dakika tano na ajiandae Mheshimiwa Saada Mkuya, dakika tano.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza napenda niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa jinsi inavyofanya kazi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa January Makamba, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba waliyotuletea leo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia kuhusu mazingira. Kuanzia 1995, Mkoa wa Kigoma ulipata na wimbi kubwa la wakimbizi lakini pamoja na Mikoa ya jirani ikiwemo Kagera na Rukwa. Kutokana na wimbi kubwa la wakimbizi kufika katika mikoa hiyo ni ukweli usiopingika yametokea madhara makubwa ya uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipoingia watu kutoka Burundi kwa mara ya kwanza katika Wilaya ya Kasulu walifikia katika Kambi moja ya Mtabila, wakati huo mazingira yaliharibika kwani miti mingi ilikatwa. Kwa hiyo, unaweza kuona ni jinsi gani mazingira yalivyoweza kuharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata waliporudishwa walienda tena kwenye Kambi moja ya Nyarugusu ambayo ni kubwa, ina wakimbizi wa kutoka DRC na Warundi. Kwa hiyo, ni jinsi gani unaweza kuona mazingira katika Mkoa wa Kigoma yalivyoharibika na kule Kibondo vilevile ipo Kambi ya Nduta lakini Kakonko iko Kambi ya Mtendeli. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *UNHCR* kuangalia ni jinsi gani zinaletwa pesa kwa ajili ya kunusuru

mazingira katika mikoa hiyo ambayo ilipokea wakimbizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali iweze kuipatia Ofisi ya Makamu wa Rais pesa za kutosha kwa ajili ya kuweza kufanya ziara katika mikoa hiyo lakini kuweza kupeleka pesa kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hili la mazingira. Ukienda kuangalia jinsi misitu ilivyoteketea, kwa kweli ni kilio kikubwa sana na wakati mwingine uharibifu wa mazingira unaendelea siyo kwamba eti mazingira yanahifadhiwa, hapana. Bado tuna kila sababu ya kuhakikisha Wizara hiyo inapatiwa pesa ili kwenda kunusuru mikoa ile ambayo imeathirika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muungano, naomba wanafunzi waendeleo kufundishwa umuhimu wa Muungano kuanzia darasa la kwanza mpaka vyo viko. Kwa sababu watoto wakianza kufundishwa wakiwa bado ni watoto wataendelea kuupenda tangu mwanzo mpaka watakapoendelea kuwa wakubwa na wataendelea kuulinda kwa nguvu zao zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada, dakika tano.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na naunga mkono hoja na nazipongeza Serikali zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona kuna nia ya dhati kabisa ya kutatua changamoto za Muungano. Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri tunawapongeza pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni dakika tano, itabidi niende haraka haraka. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 14 ameelezea kuhusiana changamoto ya ongezeko na gharama za umeme ambapo Serikali ya Awamu ya Tano imehakikisha kwamba changamoto hii



inaondoka na tunaipongeza sana kwa hilo. Hata hivyo, changamoto hii ya VAT si kwamba inakwenda moja kwa moja kuondoa gharama za umeme kwa mwananchi wa kawaida wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa ukiwa mwenye dhamana ya kuratibu masuala ya Muungano, Wizara ya Nishati ihakikishe kwamba yule *Consultant* ambaye amepewa kazi ya kuangalia gharama za umeme anamaliza kazi hii mapema zaidi ili wananchi sasa waweze kunufaika kutokana na kupungua kwa gharama hizo. Hii VATimeondoka lakini haijaondoa hizo gharama kama vile ambavyo tulitarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Waziri amejikita zaidi sasa kuendelea kutoa elimu. Mchangiaji aliyemaliza kuongea Mheshimiwa Genzabuke amesisitiza jinsi gani Wizara iangalie hii elimu inapelekwa katika shule za msingi, sekondari na vyo vikiu. Naamini Mheshimiwa Waziri wakati hilo linaendelea mimi nadhani elimu kuhusu Muungano ianzie humu ndani katika Bunge letu Tukufu kwa sababu bado tunaona hata baadhi ya Wabunge ile *concept* ya Muungano haijatuungia sawasawa. Ndiyo maana hata baadhi tu ya kauli zinaweza zikawa zinatoka ambazo unahisi kwamba huyu mtu bado hajafahamu hasa nini maana ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo hata katika ngazi ya watendaji linatokea. Changamoto zinazoonekana ni kwa sababu ya *issue* za Muungano hazijawa *mainstreamed*. Kama tumeweza ku-*mainstream issue* za HIV, gender na mazingira, Muungano ni *issue* ambayo inatakiwa kuwa *mainstreamed*, *wether* iko kwenye eneo ambalo taasisi zetu zinafanya kazi kwenye Muungano au katika taasisi ambazo siyo za Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaloliona sasa hivi Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na Muungano yeye ndiye anakuwa *responsible* kuangalia masuala ya Muungano lakini Wizara ambazo tunazona tu kikawaida kwamba siyo

Wizara za Muungano lakini moja kwa moja lolote linalofanyika katika Wizara zile linaathiri upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, Muungano huu siyo Muungano ambao anausimamia Mheshimiwa January Makamba ni Muungano ambao sote tunakiwa tusimamie katika maeneo yetu tunayofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na utaratibu Mawaziri ambao wanachaguliwa katika Taasisi za Muungano mara moja wanakwenda Zanzibar, wanamwona Mheshimiwa Rais na viongozi wengine lakini *I do hope* hilo haliishii kwenye kwenda kumuona Mheshimiwa Rais, linatakiwa liwe katika kazi zetu za kila siku. Bahati mbaya wale ambao wameji-*term* kwamba Wizara zao siyo za Muungano hatuwaoni kwenda Zanzibar labda siku ya Sherehe za Mapinduzi, tunaomba sana hii nchi yetu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 16 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza mambo mengi yaliyopatikana ikiwa ni pamoja na gawio la Benki Kuu. Tunashukuru sana Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutoa gawio. Hii ni taasisi ya Muungano na inasimamia fedha za Serikali lakini bado Mheshimiwa Waziri kuna taasisi za Muungano na gawio halitolewi. Kuna taasisi ambazo zina *operate* katika Muungano lakini hatuoni gawio kwenda Zanzibar. Kwa mfano, Mashirika yetu kama *TCRA, AICC, NIC, TTCL*, bado gawio haliendi Zanzibar. Hizi ni taasisi za Muungano na inatakiwa gawio linatolewa kwa Serikali ya Jamhuri na Zanzibar ipate.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Khenani kuhusu kutopata *clip*

zake na hii nafikiri wengi wanalalamika lakini tarehe 9 Mei, 2019, Kiti kilitoa *ruling* hapa, haki ya Mbunge ni *Hansard*, *clip* na vitu vingine ni *privilege* tu basi. Kwa hiyo, tumieni *PR* kuzipata hizo *clip* mnazoziomba, haki yako ni *Hansard*, ukikosa *Hansard* una haki ya kulalamika.

Waheshimiwa Wabunge, vilevile kulikuwa na Mwongozo mwingine, Mheshimiwa Mkuchika inakuhusu hii, kuhusu ustaarabu wa michango inayochangishwa ndani ya Bunge kutangazwa. Kuna michango hapa imekusanywa na timu moja huko nje na Wabunge wengi wametoa lakini taarifa rasmi ya mchango ile mpaka leo hamna.

**WABUNGE FULANI:** Eeeh.

**MWENYEKITI:** Sasa tunaomba wahusika wa michango ile...

**WABUNGE FULANI:** Ya nani?

**MWENYEKITI:** Anajua huyu, *Club* ya Yanga waliomba michango kwa Wabunge humu, kwa hiyo, Wabunge wanataka kupata taarifa ya michango yao. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya Bunge hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza na Mheshimiwa Jaku Hashim ajiandae Mheshimiwa Khamis Mtumwa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, nianze kwa ni-*declare interest* kwamba mimi ni mmoja wa wanaohitaji Muungano na Wazanzibar wengi wanauhitaji, lakini ni formula tu ya kuuendesha muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nichukue fursa hii kuwashukuru sana viongozi wetu wawili wakubwa; Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushirikiano mkubwa wa kutatua tatizo la mazingira ya hali ya VAT ya umeme na tumefikia mahali muafaka; mwezi huu wa Aprili, aliwahi kuzungumza Mheshimiwa Najma hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa January Makamba, pamoja na kuambiwa na Mawaziri wenzake ni Mzanzibar, akubali hivyo hivyo. Ameonesha uwezo mkubwa sana katika Mawaziri ambao wameitwa Zanzibar wakafika kwa wakati, mmojawapo ni yeye. Haya ndiyo malezi mazuri binadamu anatakiwa kulelewa. Ameonyesha ushirikiano kwa hali na mali bila kujali mvua wala jua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitamfanyia haki Mheshimiwa Naibu Waziri wake tumemshuhudia sana katika kutatua matatizo hayo. Pia nitakuwa sijamfanyia haki ndugu yangu, jirani yangu Mheshimiwa Keissy. Nakushukuru sana kwa utulivu wake alioonesha kwa kipindi kirefu baada ya kero hizi

za Muungano. Ametulia sana Mheshimiwa Keissy, namshukuru sana na huu ndiyo uungwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** ...nataka kuuliza...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** ...nini Muungano?...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** ...maana ya *formula* ya Muungano?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nataka nimpe taarifa huyu.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** ...umuhimu wa kuungana ni watu kuwa pamoja, kushirikiana katika nyanja mbalimbali katika kuungana kiuchumi...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** ...ulinzi,...

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** ...maendeleo

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji, anasema mimi nimetulia muda mrefu. Mimi sikuwa napinga Muungano, nilikuwa napinga habari ya bidhaa kutoka Zanzibar ambazo hazilipiwi ushuru, ndiyo nilikuwa napinga. Mambo mengine mimi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba afute kauli yake. Kule Wazanzibar wanalipa ushuru, vinginevyo kwa vyovyote vile kungekuwa hakuna Serikali pale bila kulipa ushuru. Naomba umruhusu afute kauli yake kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Siyo kauli ya kiungwana aliyoitumia. Hiyo siyo kauli ya kiungwana, yeye atetee mambo yake kule Nkasi; maji hakuna, barabara ndiyo vya kutetea. Wazanzibar wapo wenyewe wasemaji. Wakuu wa Dunia walishirikiana katika Jumuiya za Afrika Mashariki waliomba *European Union* kwa mashirikiano makubwa sana, lakini jambo la kushangaza na la kusikitisha, niye katika bidhaa za biashara hasa kutoka upande wa Zanzibar kuja kutafuta soko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni geti kubwa la Bandari ya Tanzania Bara na ndiyo soko kubwa lenye walaji wengi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kati. Hili suala limekuwa ni la muda mrefu, vinginevyo labda ifutwe hii kauli. Kuna mahali Kenya inataka kwenda, Rwanda inataka kwenda na Burundi inataka kwenda, lazima ipite katika *gateway* kubwa hii ya Bandari ya Dar es Salaam. Sasa patafutwe njia. Hili suala limekuwa la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar wapo katika Jukuiya ya Afrika Mashariki, vinginevyo, watumwe Wabunge wetu wa Afrika Mashariki na Kati wapeleke hoja binafsi Zanzibar itolewe katika hili. Hili ni soko lenye walaji karibu milioni mbili na kuendelea. Hili ni jambo la kufikiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango lilitokea tatizo la Kenya, bidhaa za Kenya kuja huku ilikuwa maziwa sijui na *cigarette* na bidhaa za hapa kwenda kule, tatizo likatatuliwa mara moja. Sisi ndugu wa damu. Mheshimiwa January utapa kazi kubwa sana haya mambo, lazima ufuatilie; na yote utakuwa *masuuli* hata kwa Mwenyezi Mungu. Haya ni mambo ya kuyafikiria. Mmetatua kero za mbali za karibu mmeziacha! Lah, hii siyo halali, mlifikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, Mheshimiwa Dada yangu Mheshimiwa Saada aliyazungumza Mashirika ya Muungano. Kwanza naipongeza sana Benki Kuu. Katika Shirika linalotoa pesa wakati, BoT; 4.5 ile inapatikana kwake tofauti na Mashirika mengine. Mheshimiwa Naibu Waziri yupo, Waziri wako hayupo, hii 4.5 tulikuwanayo ya mkataba tu, ni ya muda. Zanzibar imekua, *population* imekua, *IMF* walitumia kutokana na kigezo cha watu lakini mlifikirie. Mheshimiwa January lifuatilie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapato ya *NBC*, Zanzibar imo. Kuna Benki ya *NMB*, Zanzibar imo; kuna *Postal Bank*, Zanzibar imo; kuna *TTCL*, Zanzibar imo; kuna *TCRA*, Zanzibar imo; kuna *TCAA*, Zanzibar imo; imepata nini? Haya ni matatizo. Zanzibar imepata lini? Haielekei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira za mambo ya Muungano Mheshimiwa January; kuna *Jeshi*, kuna *migration*, kuna Polisi, kuna Mambo ya Nje. Mnapogawa hizi kazi mfikirie mtapeleka namna gani Zanzibar, zinahitajika, Ajira imekuwa *issue*. Muungano wetu keshokutwa Mungu akijaalia unatimiza miaka 55, twende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uchumi siyo suala la Muungano, ndiyo hoja yangu ilipo; Zanzibar ina haki yake ya kutumikia Wazanzibar wake na Tanzania Bara ina haki ya kutumikia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khamis Mtumwa, jiandae Mheshimiwa Juma Kombo.

**MHE. KHAMIS MTUMWA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Wizara hii ya Muungano na Mazingira. Pia naomba nichukue fursa hi kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuhakikisha kwamba wanaulinda, kuuhifadhi na kuutetea muungano wetu huu mpaka sasa unafika miaka 55. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu na Makamu wa Rais kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba wanazikusanya kero hizi za Muungano na kuweza kuzifanyiakazi hatua baada ya hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu kwa kuweza kuzichanganua na kuzitafuta kero hizi na hatimaye tunaona matokeo yake ya kuweza kutatuliwa moja hadi moja kwa kadri ya siku zinayokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze sasa kwenye suala zima la umuhimu wa Muungano wetu. Muungano wetu huu ni wa historia na unatusaidia sana pande zote mbili ya Tanzania Bara na ya Zanzibar na hasa kwenye suala zima la kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mambo mbalimbali ya kibiashara yanafanyika pande mbili hizi na watu hunufaika, lakini bado kuna kikwazo kikubwa cha kufanya *double taxation* ambayo inafanyika Zanzibar ukipeleka kitu ukileta Tanzania Bara ulipie tena ushuru mara ya pili. Hii bado ni kero na tunaipigia kelele sana na Wabunge wengi wa Zanzibar wanaipigia kelele hii kwa sababu bado



inaonekana haitendi haki kwa pande zote mbili za Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumza kuhusiana na suala la ushiriki na ushirikiano mdogo kuhusu masuala ya Kitaifa na kikanda. Kama Mheshimiwa Waziri alivyoelezea katika kitabu chake hiki, amefanya juhudi za kuunda Kamati ya kuweza kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinafanyiwa kazi za kielimu, nafasi za masomo na vilevile amezungumza kuhusiana na suala la utafutaji wa fedha kwa masuala ya mambo ya nje ya misaada na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ametuambia masuala mbalimbali yameundiwa Kamati ambayo atahakikisha kwamba *soon* tunaona matokeo yake. Napenda sana kumshauri Mheshimiwa Waziri tutakapokuja kwenye bajeti ya mwakani, changamoto hizi tusiwe tunazirejea tena kila siku katika Bunge letu hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nizungumzie kuhusiana na suala la Elimu ya Muungano. Wenzangu wametangulia kusema kwamba ipo haja ya kutoa taaluma kwa yale ambayo yanatatuliwa katika Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusiana na zile kero za Muungano, kwa sababu vijana wanaoamkia sasa hivi bado wana *mentality* kichwani kwamba Muungano siyo mzuri, au unatunyonya sana kule Zanzibar. Kiukweli Muungano una faida kubwa sana za kiuchumi, kisiasa na kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kukiwa na utoaji wa elimu katika maeneo mbalimbali hasa kule Zanzibar juu ya changamoto ambazo zinatatuliwa na umuhimu wa Muungano wetu, mimi nina imani kwamba muungano huu utazidi kudumu zaidi ya miaka 100 badala ya miaka 55 hii tuliyofikia sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia suala la ushirikiano kuhusiana na masuala mbalimbali ya Muungano hasa katika Taasisi hizi za ukaguzi. Tumeshuhudia kwamba Ofisi ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu (CAG) hufanya

ukaguzi katika Taasisi mbalimbali au katika Taasisi za Ubalози bila kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar. Suala hili tumeshalzungumza sana kwamba wale wenzao ni vyema kwamba wakashirikiana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhali hili suala siyo la Muungano lakini ni vyema zaidi wakaenda kukagua katika Taasisi za Muungano ambazo zipo nje hasa Ubalози wawashirikishe na wenzetu kule ili wapate *exposure* na mambo mengine ambayo wataweza kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliniahidi siku moja kwamba tutafuatana mimi naye twende kule Zanzibar, tuone, tukae na Taasisi ambayo inahusiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi kuangalia zile changamoto zao ambazo zinawakabili, lakini alitingwa na kazi. Naamini baada ya Bunge hili au baada ya kujibu hoja zetu hizi tutafuatana ili tuone tatizo hili pia linatatuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri; baada ya kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kusema kwamba ikifiuka tarehe 1 Juni, 2019 suala la mifuko ya *plastic* ni marukufu, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Katibu Mkuu wake wamefanya jitihada ya haraka kuonana na wadau na kuweza kuzungumzia mambo mbalimbali ambayo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Juma Kombo, ajiandae Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. KHAMIS MTUMWA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nami nafasi hii ya kuchangia mawili, matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametupa afya, bado tupo na tunaendelea na pia nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na msemo wa Kiswahili, watu wa Pwani tunakuwa na msemo tunasema kwamba, "ukipenda boga, basi upende na mti wake." Siyo sahihi kwamba unapenda boga, lakini mti wake unautia moto. Hii itakuwa siyo sahihi na wala haikubaliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia udugu siku zote ni kufaana na siyo kufanana. Kama kufanana, miaka 50 tumefanana vya kutosha, lakini sasa tunatakiwa tuwe na mwelekeo mpya kabisa wa kufaana hususan katika masuala mazima ya kiuchumi. Kama tutajaribu kuimba na kusifu tu masuala ya Muungano lakini bila kusaidiana kiuchumi, bila kupeana fursa zaidi za kiuchumi, kwa kweli Muungano huu utakuwa hauna mwendo mwema na hauna afya kwa Watanzania hususan wale walioko Zanzibar kwa maana ya Wazanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kimsingi ni ukweli usiopingika kwamba Muungano kama Muungano ni muhimu na hakuna anayekataa hata mmoja. Siyo kweli kwamba kuna Wazanzibar fulani hawataki Muungano, siyo kweli kabisa. Wazanzibar wanataka Muungano. Kama alivyosema Kaka yangu Mheshimiwa Jaku tunahitaji Muungano ambao utakuwa na maslahi kwa pande zote mbili. Hatuhitaji Muungano ambao umejikita maslahi ya upande mmoja hii itakuwa siyo muungano. Naomba Mawaziri watakapokuja ku-*wind up* kwanza waje wanijibu masuala mawili ambayo tumekuwa tukiyazungumza mara kwa mara pale tunapopata fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusiana na vyombo vya moto. Kwa kweli tumekuwa tukipata taabu sana Wazanzibar, hasa sisi Wabunge, tumekuwa tukibughudhiwa sana na *TRA* na Polisi kwa sababu tu tuna magari yamesajiliwa kwa namba za Zanzibar. Hii siyo halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kwenye mchezo ule wa Simba na Mazembe ya Congo, tuliwakuta Wakongo wanahojiwa kwenye vyombo vya habari. Walikuja hapa na magari yao na wakafanya shughuli zao Dar es Salaam, Tanzania hii hii na halafu wakaondoka na magari yao. Leo hakuna Mzanzibar anayethubutu kuja Tanzania Bara na gari yake akatumia, hii siyo haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi na-*declare* kwamba ipo siku nilifukuzwa na *TRA* na Polisi usiku Dar es Salaam. Nasimama, wananiambia tuna wasiwasi na gari yako. Kwa nini? Unatumia namba za kigeni. Aah, nikashangaa, nikamwuliza wewe nani? Mimi Afisa wa *TRA*. Hii namba ya wapi? Namba ya Zanzibar. Hivi Zanzibar leo ni nchi ya kigeni na Dar es Salaam? Ananiambia kwani Zanzibar ni Tanzania Bara. Nikataka kujua kumbe hivi kuna nchi inaitwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni vitu ambavyo vinahitaji majibu. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja anipe jibu sahihi juu ya suala hili kwamba ni lini sasa bughudha hii na adhabu hii itaondoka kwa Wazanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka Mheshimiwa Waziri aje anijibu kwa kina ni suala la uwepo wa *Account* ya Pamoja ya Fedha ambayo imetajwa wenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 133. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, mwaka juzi 2017 tulizungumza suala hili akaahidi kwamba linakwenda kutatuliwa; mwaka jana 2018, tulizungumza suala hili akaahidi kwamba linakwenda kutatuliwa. Leo tunataka *commitment* ya Serikali kwamba ni lini sasa suala hili linakwenda kumalizwa na tuone *Account* ya Pamoja ya Fedha ambayo itashughulika na mgawanyo sahihi wa mapato ya Muungano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara au Tanganyika unakwenda sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya yanakuja kwa sababu moja; hakuna siku Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa na nia njema na Muungano huu. Hiyo ndiyo kauli *simple* kabisa, ndiyo kauli rahisi. Siku Muungano huu unaundwa uliundwa kwa siku mbili baina ya Mwalimu Nyerere na Karume, lakini tunazungumzia kero ya Muungano tena ambayo iko ndani ya Katiba inachukua miaka 50, nia njema iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuimba tu kwamba tuna nia njema, tunataka kutatua kero za Muungano, sijui tunafanyeje, wakati nia njema hakuna. Vijana wetu hao, wote vijana; Mheshimiwa Makamba na Mheshimiwa Mussa, wote wana utashi wa kuona kero za Muungano zinatatuliwa. Tena hata ukizungumza nao unahisi kwamba wanaumia na wako tayari kuona kero za Muungano zinatatuliwa. Ushirikiano wanaopata bila shaka ni tatizo, Serikali haiko tayari kuona kero hizi zinatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano limekuwa na shida na ndiyo maana zipo taarifa zinasema na ni sahihi kabisa, hata mgogoro uliokuwepo katika miaka ya 1970 baina ya Mwalimu Nyerere na Karume sababu ilikuwa ni Muungano. Hata mgogoro uliomwondoa Jumbe kwenye madaraka kama Rais wa Zanzibar akafukuzwa Urais, akafukuzwa nafasi zote sababu ilikuwa ni Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mashehe ambao leo wako jela kwa mwaka wa sita sasa; siyo ugaidi, wala siyo suala la uanaharakati, wala siyo suala lolote, ni kwa sababu walisimama na Wazanzibar kudai maslahi zaidi...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** ...ya kiuchumi kwa ajili...

**MWENYEKITI:** Taarifa. Mheshimiwa Kombo kaa chini kwanza.

## T A A R I F A

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji, anaposema kwamba Chama cha Mapinduzi hawana nia njema na Muungano huu na Chama cha Mapinduzi sasa hivi kina umri wa zaidi ya miaka 51 na Chama cha Wananchi *CUF* walipojaribu kuja na Muungano wa Shirikisho, Chama cha Mapinduzi ndiyo kilisimama imara kupinga Muungano ule wa shirikisho. Kwa hiyo, suala la kusema Chama cha Mapinduzi hakina nia njema na Muungano huu, siyo sawa sawa. (Makofi)

**MWENYEMITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kombo, taarifa hiyo.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuchauka ndugu yangu wewe umekwenda juzi CCM...

**MWENYEKITI:** Jibu taarifa yake. Mengine yaache.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** ...hayo mapenzi yako na CCM yamekuja lini? Au kwa sababu Mbunge! Subiri kesho kutwa CCM wakuangushe halafu uanze kuimba imba huko. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba nia njema ndiyo itakayodumisha Muungano. Naomba niseme moja na katika hili naomba Mheshimiwa Jenista anisikilize vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa ya mazungumzo ambayo ipo sasa kwenda kutatua changamoto hizi za Muungano, baada ya muda hazitakuwepo tena na tutakuja kushuhudia mambo mengine ambayo hayastahili. Kwa sababu unapobana fursa za kiuchumi za Zanzibar, vizazi vinavyokuja havitakubali kuona kwamba wao hawa-*enjoy* fursa za kiuchumi kama zile ambazo wenzao Watanzania Bara wanazipata ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hili hawatalikubali. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba tutumie fursa ambayo ipo, tutumie nafasi ambayo sasa hivi tunayo ili kutatua changamoto hizi tukiwa na nia njema ya

kwenda kwenye Muungano ambao utadumu na utadumisha usawa na haki kwa pande hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie mchango wangu kwa kusema kwamba, suala la mazingira Wizara hii bahati mbaya sana hakuna fedha ya ndani ambayo imetengwa katika kuendeleza suala la mazingira ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Fedha yote inayotegemewa ni ya misaada kutoka nje. Hii inadhihirisha au inaonyesha kwamba ni kiasi gani Serikali haiko *serious* na kuendeleza suala la mazingira katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wakati wa kupitisha bajeti na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na *Cabinet* iwe *serious* na suala la mazingira kwa sababu ni muhimu na ni suala ambalo linagusa binadamu na viumbe vyote vilivyomo ndani ya Tanzania yetu. Bila mazingira sahihi na bila kudumisha mazingira, Taifa hili litatupotea na tutakuja kujutia nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Mtolea. Jiandae Mheshimiwa Mattar

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Dakika 10 eh?

**MWENYEKITI:** Dakika tano.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niwapongeze sana Mawaziri wanaosimamia Wizara hii kwa namna ambavyo wanajitoa kuhakikisha wanasimamia Muungano, lakini pia upande wa mazingira. Waendeleo kufanya ziara nyingi kwa sababu mazingira kwa kweli yameharibika kwa kiasi kikubwa na Muungano unahitaji kusemewa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu kuna tatizo moja; kuna mtaro mmoja unatiriri nafikiri ni maji ya sumu, nimeshawahi kulizungumza hili hapa Bungeni na leo ni mara ya pili. Kwenye Kata ya Sandari kule Temeke Mikoroshini, kuna mtaro wa mfereji wa Mpogo, yake maji yanaoneka yanatoka kwenye moja kati ya viwanda vilivyoko Vingunguti, nyumba zilizokuwa pembeni bati zinaharibika na matofali yanamung'unyuka. Hali hii inaonesha kabisa kwamba pale kuna sumu inatembea na kama matofali yanamung'unyuka maana yake afya za watu wanaoishi pale ziko kwenye hii changamoto kubwa. Kwa hiyo, naomba hili jambo walichukue na walifanyie kazi kwa haraka. Sisi kama Halmashauri tumeshatenga fedha ya kuujenga ule mfereji, lakini haiondoi ukweli kwamba maji yanayotiririka yanakuwa na sumu. Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naitaka Wizara wawe wanatupa taarifa za mara kwa mara za uchafuzi wa mazingira katika Jiji la Dar es Salaam. Tunapata taarifa ambazo zinaleta sintofahamu kidogo, kuna wakati tunaambiwa kwamba mabonde yale hayafai hata kwa kulima mbogamboga za majani, kuna wakati tunaambiwa *water table* ya Dar es Salaam yote imechafuka hata maji ya visima tunayoyatumia si mazuri. Sasa ni vizuri wakawa wanatuandalia taarifa za wazi na za kina ili tujue kitu kipi tufanye na kitu kipi tusifanye. Maana yake sasa tukienda sokoni tunaogopa michicha tunaogopa matembele, tunahisi yamelimwa kwenye yale maeneo ambayo yana sumu. Ikiwezekana waweke hata mabango tujue kwamba eneo hili linastahili, eneo hili halistahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, sheria ambazo zinatumiwa na *NEMC* kwa kuwaadhibu wanaochafua mazingira, ziingaliwe upya, inawezekana ni za Ulaya sana. Kwa mfano, mtu mwenye *garage* anatakiwa awe amesakafia na kuwe na *system* ya kutofautisha maji na *oil*. *Garage* zetu nyingi hazijasakafiwa, kwa hiyo kinachofanyika ni kama tumetengeneza mwanya wa watu kupiga fedha. Leo mtu anapelekewa *notice* kwamba hii *garage* uisakafie ndani ya siku 14, jambo ambalo haliwezekani. Akija siku ya



pili, yule mtu atakachofanya ili asitozwe faini ya milioni tano, atamuona tu pembeni huyu mtu, kwamba bwana usiniandikie, chukua hii milioni moja, chukua hii laki mbili, sasa watu wataishi hivi mpaka lini? Lazima tuwe na sheria ambazo zinaendana na mazingira yetu, je tuna uwezo kwenye kila *car wash* kuwa na hiyo *system* ya kuchuja maji na *oil*. Magari yetu yenyewe ya mitumba, likisimama tu hapo linavuwa *oil*, mtu anatakiwa awe na *system* ya kuchuja hiyo kitu, hii inawezekana vipi? Kwa hiyo, tuziangalie hizi sheria kama kweli ni rafiki na zinaweza kutekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni la Muungano; nimeshtushwa sana, mtu aliyesimama hapa kusema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haiutaki Muungano tena na yeye anasimama akitoka *CUF*. *CUF* wanaamini kwenye madaraka kamili, mamlaka kamili, mamlaka kamili maana yake Zanzibar isimame kama nchi tofauti na Tanzania Bara isimame kama nchi tofauti, sasa hapa ni nani asiyeupenda Muungano? Kwa hiyo, nafikiri kwenye jambo hili la Muungano, ni vizuri tukawa wakweli, kwamba hizi nchi mbili, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, zinahitajiana sana *whether* tuko ndani au nje ya Muungano. (*Makofi*)

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumekubali tuko ndani ya muungano ni vizuri....

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mamlaka ya Zanzibar ambayo ni kupata fursa zaidi za kiuchumi hususan katika nyanja za kimataifa, haliharamishi kutokuwepo Muungano. Tuna mifano mingi, tuna *European Union*, ni Muungano una nchi kadhaa, lakini kila nchi si ina mamlaka yake! Kwa hiyo, suala la kujadili, Mheshimiwa Mtolea, suala la kusema kwamba eti kwa sababu kuna watu wanazungumzia suala la kwamba Zanzibar iwe na mamlaka

kamili, hawataki Muungano, hii siyo sahihi. Suala la mamlaka kamili ni suala la kuwepo kwa Serikali tatu....

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea endelea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siipokei hiyo taarifa yake. Tunapozungumzia Muungano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, tunazungumzia kitu tofauti sana. Huwezi kufananisha na miungano mingine hiyo sijui ya *European Union* na sehemu nyingine. Huu ni muungano wa kipekee, una historia ya kipekee na mazingira yake ni ya kipekee. Sasa ukianza kusema kwamba tunakosa fursa, si kweli na wakati mwingine eti mtu anasema kwamba tumechoka kubebwa kwenye koti la Muungano, hivi aliyebewa anaweza akaanza kuchoka kabla ya aliyembeba? Maana yake aliyekubeba anavumilia kwa sababu anafahamu thamani ya anachokifanya. Mama akimbeba mtoto, si kwamba eti mtoto aanze kuchoka eti mama hajachoka, lakini Mama anaendelea kumbeba kwa sababu anajua ni jukumu lake na ndicho Tanzania Bara wanachokifanya... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsate. Mheshimiwa Mattar hayupo enh?

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Januari Yusuph Makamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Mussa Sima bila kuwasahau wafanyakazi wa Wizara hii kwa kusimamia na kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa mazingira naishauri Serikali itenge fedha za ndani katika bajeti

ili kuweza kutekeleza majukumu yake na sio kutenga fedha za wahisani kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri katika kampeni ya upandaji miti Serikali ione haja sasa ya kupanda miti yenye faida zaidi ya moja, nashauri ipandwe miti mingi ya matunda kwanza tutahifadhi mazingira pia yatapatikana matunda ambayo ni muhimu kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko ya plastiki si vizuri kwa mazingira na naunga mkono usitishwaji wake. Ushauri maelekezo ya awali ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kutumia Kiwanda cha Mgololo kutengeneza mifuko mbadala na kiwanda hicho hutumia malighafi ya misitu (miti).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihamasishe wananchi kila mkoa kuanza kulima kilimo cha miti ambayo itatumika katika viwanda vitakavyotengeneza mifuko hiyo kikiwemo Kiwanda cha Mgololo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya mita 60 ipitiwe upya maana kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi maeneo ikiwemo mito maziwa (Victoria) na kadhalika na kusababisha migongano isiyo ya lazima katika ya Serikali na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utupwaji hovyoyote wa chupa za maji, *juice* pembezoni mwa barabara kuu ziendazo mikoani. Serikali ifanye utaratibu wa kutoa elimu hususan kwa wafanyakazi wa magari ya abiria licha ya kuwa na vyombo ndani ya mabasi vya kuhifadhi taka, lakini bado utupwaji upo na unaharibu mazingira. Hivyo, wafanyakazi hao wa magari ya abiria wapewe elimu ya kutosha ya uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Wizara ya Nishati ili kupunguza ukatwaji wa miti ambayo hutumika kusambaza umeme mijini na vijijini na Wizara ya Nishati ianze mara moja utumiaji wa nguzo za zege ambazo kila mara imeahidi

kutumia ili sasa kuepuka kukata miti mingi ambayo itapelekea nchi kugeuka jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Mungu ampe Mheshimiwa Waziri umri mrefu na afya njema katika kuyatekeleza majukumu yako ya kila siku.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ndiyo uliozaa jina Tanzania na ni wa kihistoria Afrika na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi zinataka kufanya Muungano kama huu lakini zimeshindwa na pia zipo nchi ziliungana na baadaye muungano huo ulivunjika na sasa zinafanyika bidii za kujiunga upya na mfano ni Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977 na sasa bidii na juhudi zinafanyika kuunda upya muungano huo (*East Africa Community*) kwa nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Southern Sudan. Ni mategemeo yangu Muungano wa watu wa pande hizi (Tanganyika na Zanzibar) utadumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida, changamoto na mustakabali; Watanzania kwa miaka mingi wamekuwa na umoja na mshikamano katika nyanja mbalimbali ambapo kwa kutekeleza haya ndiyo tunapata neno Muungano. Kihistoria tokea miaka mingi iliyopita tangu dunia iumbwe, makabila na watu wa maeneo mbalimbali katika Tanganyika, wamekuwa na ushirikiano na mahusiano ya karibu. Mfano ni katika harakati za kuondoa uonevu, ukandamizaji na ubaguzi uliokuwa ukifanywa na Wakoloni Wajerumani mnamo mwaka 1905 hadi mwaka 1907.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Vita ya Minonge katika maeneo ya Ukanda wa Pwani Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Zanzibar, mikoa hii makabila yake yalishirikiana kuondoa uonevu hali iliyopelekea kutokea Vita ya Kwanza ya Dunia (*1<sup>st</sup> World War 1914-1918*). Hii yote ni kuonesha namna muungano ulivyokuwa na umuhimu na faida kwa jamii. Hivyo, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulianza

miaka mingi na hadi katika Mapinduzi ya Zanzibar 1964. Mchango mkubwa ulitokea Tanganyika (Tanzania Bara) na kufanikiwa kuondoa ukandamizaji uliokuwa ukifanywa na Wakoloni wa Kiarabu katika Visiwa vya Unguja na Pemba (Zanzibar).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi na ushauri; Serikali izifanye kazi kero zote za Muungano na kuzipatia ufumbuzi wa haraka; Sera ya kulinda viwanda vya ndani ifanye kazi pande zote za Muungano, mfano Kiwanda cha Sukari Mahonda kiruhusiwe kupata soko la sukari na bidhaa zake upande wa Tanzania Bara. Magari yaliyosajiliwa Zanzibar yaruhusiwe kutumika Tanzania Bara bila vikwazo vyovyote; kero na changamoto zinazofanyiwa kazi, taarifa zake ziwekwe wazi na isiwe siri; gawio la Pato la Taifa, deni la *TANESCO*, suala la *FIFA*, *Exclusive Zone* katika Bahari Kuu yafanyiwe kazi na yaishe; suala la mafuta ya gesi, zote hizi ni sekta ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi na kupata ufumbuzi. Mfumo wa Serikali tatu (Serikali ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Shirikisho ndio ufumbuzi wa kudumu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni neno lenye maana pana sana ambalo bado Watanzania wengi hawajalielewa maana yake na bahati mbaya bado Serikali hajatoa elimu ya kutosha kwa kutumia vyombo vya habari, vipeperushi na Taasisi zake katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira katika Tanzania yanaingiliana sana na shughuli za uzalishaji mali (kutafuta riziki) kwa wananchi wake kama vile kilimo, uvuvi, ufugaji na shughuli za viwandani. Sheria nyingi na Kanuni zinatungwa bila kuwashirikisha wananchi ili wazielewe na kuzifanyia kazi, badala yake Sheria zinatumika kuwakandamiza wananchi na pale wawakilishi wao tunapotetea (Wabunge, Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa) tunajibiwa *ignorance of laws is not a defence* na inaonekana Serikali inatumia makosa yanayofanywa na wananchi kujipatia faini (fedha) na kuwa chanzo cha mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji, wakulima na wawindaji wamekuwa wahanga wakubwa katika suala zima la mazingira, hivyo Serikali katika hili ifanye kazi ya ziada kwa kutoa elimu ya kutosha. Sheria ya kuacha mita 60 ya vyanzo vya maji katika shughuli za uzalishaji mali ni mpya, iwekwe vizuri na itolewe elimu ya kutosha ili kuondoa mkanganyiko ullopo hususan pale ambapo sheria imekuta mwananchi ameshaanza kufanya kazi (kabla Sheria kuanzishwa), Serikali imfidie kwa eneo litakalotwaliwa na sheria hii katika ngazi za Serikali za Vijiji, Serikali za Mitaa, Halmashauri za Manispaa na Halmashauri za Majiji kwa thamani ya fedha katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inatengewa fedha ndogo sana na mfano katika bajeti ya 2018/2019, bajeti iliyotengwa hadi mwaka wa fedha unaoishia ni shilingi bilioni 1.7 tu ndiyo iliyopokelewa hali inayoonesha Serikali haitilii maanani suala la Mazingira.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata muda huu kuweza kuchangia kwa maandishi. Namshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri na Makamu wa Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Viumbe Vamizi. Kuhusu hasa gugu la Kongwa ambalo linaharibu malisho ya mifugo ni la muda mrefu sasa ingawaje Serikali inajitahidi kukabiliana nalo, lakini bado ni tatizo. Mheshimiwa Waziri nashauri jitihada zaidi zitumike ili kutokomeza kabisa gugu hili la Kongwa. Naomba maelezo zaidi kwa niaba ya wafugaji na Serikali na hasa kuhusu gugu hili lililoenea katika *Ranch* ya Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gugu karoti ambalo linaenea kwa kasi hasa Mikoa ya Kaskazini. Gugu hili ni hatari, Mheshimiwa Waziri anafahamu gugu hili linahatarisha na hasa katika kilimo mazao na malisho. Mheshimiwa Waziri

ningependa kujua kwa niaba ya wakulima na wafugaji mikakati inayoendelea ya haraka ili kutokomezwa gugu karoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyanzo vya maji na upandaji miti rafiki ya vyanzo vya maji. Natoa pongezi za jitihada zinazoendelea kunusuru vyanzo vya maji. Nashauri elimu izidi kutolewa kuhusu vyanzo vya maji na kupanda miti rafiki ili kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro tuna matatizo ya maji na hasa Halmashauri ya Morogoro Manispaa. Sababu mojawapo ikiwa ni uharibifu wa vyanzo vya maji na ukataji miti katika Milima ya Uluguru. Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake za kulinda mazingira, naomba akaliangalie tatizo hili, ili kunusuru vyanzo vya maji milima ya Uluguru (Morogoro) kwa madhumuni ya upatikanaji wa maji na uhai wa mito kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri kwa kulisimamia suala hili la mifuko ya karatasi. Kama Mheshimiwa Waziri alivyoelekeza kupitia kwenye mkutano (15/04/2019) na kwenye hotuba yake ya bajeti. Nashauri Mheshimiwa Waziri na watalaam wake walisimamie kwa ukamilifu ili tuweze kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukataji miti na uchomaji mkaa bado ni tatizo. Elimu zaidi inatakiwa kwa wananchi kuhusu faida na hasara za kutunza mazingira, hasa kwa kupanda miti na kukata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gunduzi kuhusu nishati mbadala na hasa zinazooneshwa wakati wa maonesho ya Siku ya Wakulima – Nane Nane zipewe kipaumbele kwa kuwaendeleza na kuwawezesha wagunduzi hawa wa nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la fedha katika ofisi hii ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Nashauri fedha zote zilizoombwa wakati wa bajeti hii zitolewe kwa wakati ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri wanazozifanya za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC*; naomba Serikali waangalie utendaji wa *NEMC* kwani washauri wanachukua fedha nyingi kuliko Serikali. Waangalie mradi gani unahitaji upembuzi wa muda mrefu na mengine kama imeshapitishwa na Halmashauri *NEMC* wapitishwa kwa haraka. *NEMC* na taasisi nyingine kama *EWURA* na wengine wakae pamoja na kutafuta njia nyepesi ya kuwasaidia wawekezaji wa mafuta (naweka maslahi wazi ni mdau). Badala ya kulipa malipo makubwa mara moja, nashauri katika kukuza na kuendeleza uwekezaji waweke tozo ambazo zinaweza kulipwa kila mwaka, hii itasaidia hata wawekezaji wadogo kuweza kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko ya *plastic*; naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kupiga marufuku kwani mazingira yetu yaliharibika vibaya kutokana na mifuko kujaa ardhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano; naipongeza Serikali kwa kujitahidi kutatua kero za Muungano kwa kiasi tulichofikia inatia moyo sana. Tudumishe Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Matumizi ya mifuko ya *plastic*; ni jambo jema kwa Serikali kutoa tamko mwisho



wa kutumia mifuko ya *plastic* ni 1/6/2019. Tamko pekee halitoshi, ni vizuri Waziri atueleze ni lini suala hili litatumika kisheria ili yeyote anayetumia mifuko hiyo ajue kuna faini ya kulipa au anaweza kufungwa jela. Bila sheria kuna baadhi ya watu wataendelea kutumia mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kabisa mwaka huu mvua mfano kaskazini bado hazijanyesha lakini kwa kisingizio cha mabadiliko ya tabianchi, lakini ni wazi kuwa miti imekuwa ikikatwa ovyo kwa matumizi ya mkaa, wengine kwa ajili ya kilimo. Siku zilizopita vijijini (Serikali za Vijiji) ilikuwa ni lazima kupanda miti na ilikuwa hairuhusiwi kulima kando ya mito, lakini sasa hivi ni jambo la kawaida kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri shule zote za msingi na sekondari katika kila vijiji wawe na vitalu vya kupanda miti na iwe kabisa ni elimu kuanzia shule za awali kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira kwa kupanda miti na wajue ukikata mti lazima uwe umepanda mti mwingine. Wazee wetu walisomesha vijana wao kwa kukata mti na kuuza mbao lakini walihakikisha kuna mti mwingine pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kila halmashauri ziwe na vitalu vya miti ikiwezekana ya matunda pia ambayo yatatumika kujenga afya na kuongeza kipato kwa wananchi na uuzwe kwa bei nafuu ili kila mwananchi aweze kununua.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii ya Waziri. Hata hivyo, ninayo machache ya kushauri; ni dhahiri bila kutunza mazingira nchi yetu itapata matatizo mengi na makubwa. Mkoa wa Kigoma na hasa Halmashauri ya Mji Kasulu ulibahatika kutembelewa na timu ya wataalam wa mazingira na vyanzo vya maji. Timu hii ilimaliza kazi na kutoa ripoti yake mwaka 2017. Kazi kubwa iliyofanyika ni pamoja na kutembelea vyanzo vya maji vilivyopo Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Vyanzo kadhaa vilifanyiwa tathmini na utafiti wa kina baada ya taarifa ile ya kitaalam niliamini kwamba hatua za utekelezaji zimechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hotuba yako ya Bajeti 2019/2020, ukurasa wa 83 (xi) kwamba moja ya kazi zitakazotekelezwa mwaka huu ni kupitia miradi iliyowasilishwa na wadau ili ipate wafadhili wa Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je mradi wa ulinzi wa vyanzo vya maji zaidi ya 25 katika Halimashauri ya Kasulu Mjini ni sehemu ya mkakati huu? Naomba Wizara yako ifahamu kwamba maji yanayotiririka kutoka uwanda wa juu wa Heru Juu, Buhigwe maji hayo hatimaye hutiririka hadi Ziwa Tanganyika. Ulinzi wa vyanzo hivi si tu kwamba ni muhimu ni jambo la lazima, tafadhali hatua sasa zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa ardhi oevu ya Malagarasi; eneo hili maarufu Malagarasi *wetland* linahitaji kulindwa. Eneo hili kwa kiasi kikubwa linakumbwa na uvamizi wa ng'ombe wengi kutoka baadhi ya maeneo ya nchi yetu na wakati fulani nchi jirani. Eneo hili la *Ramsar Site* litapotea, urithi wetu utapotea na rasilimali hii itaangamia pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Wizara ya Maliasili na Utalii, TAMISEMI, Mambo ya Ndani na Wizara hii waje na mpango mkakati wa kulinda eneo hili, lisipolindwa ndani ya miaka mitano mpaka saba shida itakuwa haiwezi kurekebishika tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatakie Wizara hii kazi njema katika kulinda mazingira ambayo ni uhai wa Taifa letu.

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii kwa kazi wanazozifanya katika mazingira mazuri kutokana na kutokuwa na rasilimali za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni suala la kufa na kupona kutokana na umuhimu wake kwa viumbe vyote duniani ikiwa ni pamoja na sisi binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haijatoa uzito unaostahili kibajeti kwa eneo hili. Nichukue fursa hii kuiomba Wizara kufuatilia maombi yangu ya mara kwa mara ya kuja Jimboni kwangu kuona athari mbalimbali zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ukanda wa tambarare katika Kata za Arusha Chini, Mabogini, Old Moshi Magharibi na Kahe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yetu imefanya jitihada na kupata mshirika toka Ujerumani Jiji la Kiel ambalo linatusaidia sana kufanikisha mradi wa mazingira wenye lengo la kurejesha miti ya asili ambayo ni rafiki wa mazingira katika eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Waziri aje aone jitihada hii, aitambue na Serikali ione jinsi ya kuchangia na kupanua mradi huu kuhusu manufaa ya maeneo mengine katika Taifa.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote kwa kazi wanazozifanya, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Urambo ina Mto Ugalla. Mto huu ni muhimu sana kwa uhai wa wananchi lakini pia uhai wa Mto Malagalasi ambao unapata maji kutoka Mto Ugalla. Serikali ina mpango gani wa kuondoa magugu yaliyovamia Mto Ugalla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Urambo, naomba Serikali yetu isome tena barua rasmi iliyotumwa Wizarani kuhusu magugu yaliyovamia Mto Ugalla na kuchukua hatua za kuokoa mto huo haraka iwezekanavyo. Aidha, tunaomba semina za kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira na kuacha kukata miti hovy.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri na

wataalamu wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi yao ya uhibiti wa uharibifu wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa dhati na weledi pamoja na kutopelekewa fedha kama zilivyopitishwa na kuidhinishwa na Bunge kutoka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu eneo kubwa limeathiriwa na uharibifu wa mazingira na tabianchi na kupelekea vipindi vyetu vya masika (mvua) kubadilika na mvua kuwa ndogo na mazao ya mahindi, mpunga na kadhalika kukosa maji (mvua) na kufanya uzalishaji kuwa mdogo. Mfano mwaka huu mazao yamekubwa na ukame, hivyo nashauri Serikali ijipange namna ya kukabiliana na ukosefu wa chakula nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kila Halmashauri kubaini miinuko (milima) iliyokuwa kipara yaani hakuna miti kuweka mkakati wa kupanda miti na kuweka kanuni za kulinda miinuko hiyo. Pia, kwa vile athari ni kubwa kwa nchi, ni vema bajeti ya Wizara hii katika Fungu 31 na 26, zikatolewa kwa asilimia zaidi ya 85 kwani hali ya mazingira yetu ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yasipoboreshwa kwa uharaka zaidi, lengo la maendeleo ya uchumi wa viwanda halitakuwa lenye mafanikio na endelevu kwa vizazi vijavyo. Tufanye jitihada za kufufua na kuboresha mazingira ili tupate mvua za kutosha na kupunguza athari za upepo (kuezuliwa na kubomoa majengo) ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri tupate Maafisa wa Mazingira wa kutosha ili watoe elimu na iwe elimu endelevu kwa wananchi wetu na tuwe na ushindani kwenye Halmashauri zetu. Wataalam hawa wasiwe na urasimu mkubwa wa kufikisha mapendekezo kwa Mkurugenzi wa Mazingira kutokana na waliyoyaona katika utekelezaji wao wa majukumu ili kusaidia kutatua changamoto za mazingira katika maeneo yao. Tuwe na kanuni na miongozo ya kurejesha hali ya mazingira yetu kwa haraka tusiwe na urasimu? Chelewa chelewa tutakuta mazingira

yameharibika kwa kiasi kikubwa na kuwa jangwa na gharama ya kuyarejesha itatushinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali tushughulikie haraka suala hili, hali ni mbaya sana. Naomba tuone umuhimu wa kuongeza bajeti yetu ndani. Pia tuweke mikakati maalum ya kupanda miti rafiki ya kulinda mazingira na vyanzo vya mito, maziwa na bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Rukwa nalo limejazwa na udongo unaotemka kwenye milima na kushuka kwenye Bonde la Rukwa hadi kuingia Ziwa Rukwa. Hivyo nalo liko mbioni kina chake kutoweka. Naomba nalo lipewe kipaumbele ili kulinusuru na hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, suala la mazingira tuliangalie upya na kuliwekea mikakati kwani tunahitaji mazingira kwa ajili ya urithi wa vijana wetu. Naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa napenda kuchangia zaidi katika suala la mazingira hasa juu ya uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti hovyoo kwa matumizi mbalimbali ikiwemo uchomaji wa mkaa, kuni, utayarishaji wa mashamba na kadhalika. Uharibifu huu unafanyika bila ya kuwepo hatua madhubuti za kuhakikisha nchi yetu haiwi jangwa. Watanzania walio wengi hawana destruli ya kupanda miti ni mabingwa wa kukata miti na hawaelewi kuhusu uharibifu wa mazingira. Ifike mahali Serikali ichukue hatua kali kabisa dhidi ya Watanzania wenzetu wanaoharibu mazingira kwa kukata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri zitungwe sheria za kumtaka kila Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 kupangiwa utaratibu wa kupanda miti angalau 10 kwa mwaka kwa kuwa miti ndiyo chanzo cha mvua na hifadhi ya

mazingira. Bila kuchukua hatua za makusudi, Tanzania inakwenda kugeuka jangwa ndani ya kipindi kifupi. Hivyo basi ni wajibu wa Serikali kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko kubwa la watu na wanyama wafugwao kunachangia kwa kiwango kikubwa uharibifu wa mazingira. Kuna umuhimu mkubwa kuingiza masomo yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira katika mitaala ya elimu nchini kuanzia chekechea hadi chuo kikuu. Madhara ya uharibifu wa mazingira ni pamoja na ukame, mafuriko na mmomonyoko wa ardhi. Ipo sababu ya msingi kabisa kwa Serikali kusisitiza umuhimu wa kuwataka Watanzania kujenga tabia ya kupenda mazingira kwa kuzuia ukataji miti badala yake wawe wanapanda miti katika mashamba yao na kwenye makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri ufuatao:-

- (i) Uzazi wa mpango upewe kipaumbele;
- (ii) Idadi ya mifugo inayohamahama ipunguzwe;
- (iii) Watanzania wanaofanya biashara ya mkaa wapewe masharti ya kuwa na mashamba ya kupandwa kwa ajili ya ukataji miti ya kuchoma mkaa; na
- (iv) Kila Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 apewe malengo ya kupanda angalau miti 10 au zaidi katika mashamba na kwenye viwanja vya makazi, maeneo ya biashara na makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi ni suala mtambuka na siyo tu linaathiri sekta moja. Ili kukabiliana na suala hili, nguvu toka pande zote inatakiwa kutumika. Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37, miradi inayohusu kujiandaa kwa majanga na mabadiliko ya tabianchi haikupata hata senti moja. Kwa

maana hii, nchi yetu ya Tanzania hatuoni kama hili ni tatizo na kama tunaona ni tatizo kwa nini basi tusione ni wakati kama Taifa kuyalinda mambo ya mazingira kwa kutumia fedha zetu ili kuondokana na tatizo la ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchafuzi wa mazingira kutokana na taka ngumu ni changamoto katika maeneo ya mijini kutokana na uwezo mdogo wa Mamlaka za Serikali za Mtaa na miundombinu hafifu ya usimamizi wa taka za aina hii hasa mifuko ya plastiki au rambo. Nchi yetu Tanzania ina Kiwanda cha Karatasi Nyororo Mkoani Iringa, Wilaya ya Mufindi, kinatoa karatasi za kiwango cha juu ambazo zinasafirishwa nchi jirani. Kwa nini Serikali isichukue maamuzi magumu kuwekeza katika utengenezaji wa mifuko ya kaki katika kiwanda hicho na kwa kufanya hivyo mapato ya Serikali yataongezeka, wakati huo matumizi ya mifuko ya plastiki itakoma na hali ya mazingira itakuwa salama. Ni mipango ambayo kama nchi hatupaswi kulialia, hapa ni uamuzi mgumu ambao unatakiwa kufanyika kulinusuru Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria ya utunzaji wa vyanzo vya maji ambayo inaelekeza shughuli za kibinadamu zisifanyike kandokando na mito, nashauri sheria hii isimamiwe kwa umakini kwani kuna maeneo mengine wanaambiwa wafanye shughuli zao ndani ya mita 60 na maeneo mengine mita 100. Nashauri watu wote waelekezwe umbali ufanane kama ni mita 60 au mita 100, kauli iwe moja tu kwa kuwa nchi ni moja na watu ni wamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukauka kwa Mto Ruaha Mkoani Iringa kunasababishwa na wakulima wa mpunga Mbarali ambao baada ya kumwagilia mashamba yao wanaacha maji yanatiririka ambapo kungekuwa na usiamamizi mkali wa kuhakikisha kila mwenye shamba baada ya kumaliza kumwagilia maji wanayarudisha kwenye mto. Kadri Mto Ruaha Mkuu unavyozidi kukauka wanyama wa Mbuga ya Ruaha, Mkoani Iringa watahama na mbuga hii ndiyo mbuga kubwa kuliko mbuga zote Tanzania. Nini kauli

ya Serikali kuhusu hatma ya mbuga hiyo? Nataka kauli ya Serikali wakati wa kuhitimisha.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii na naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza mtoa hoja Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho zuri. Nianze kuchangia hotuba hii kwa kurejea kitabu cha hotuba ukurasa wa 50 juu ya mkataba wa Nairobi kuhusu hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi. Mkataba huu unataka kuhakikisha tunalinda na kupambana na uchafuzi wa mazingira ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonesha ifikapo mwaka 2035 eneo la pwani ya bahari ya Tanzania litakuwa na mifuko mingi ya plastiki na takataka nyingine kuliko samaki baharini. Nashukuru sana tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu na leo Mheshimiwa Waziri wa Mazingira kwa kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki. Hatua hii imekuja wakati muafaka kwani hali ya mazingira ya pwani yetu ni mbaya na inaathiri wananchi hususani sisi tunaoshi kwenye visiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni matumizi ya mkaa, kama lilivyoelezwa kwa uzuri kwenye kitabu cha hotuba ukurasa wa 29, kasi ya ukataji miti kwa uchomaji wa mkaa imekuwa ikiongezeka siku hata siku. Nashauri bei ya gesi ipungue ili wananchi waweze kuacha matumizi ya mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji wa miti kama lilivyojadiliwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 37 ni jambo jema. Naishauri Serikali yangu iongeze fedha kwenye kampeni za upandaji miti. Ni ukweli usio na shaka kasi ya ukataji miti imekuwa kubwa sana hivyo ipo haja ya kuongeza fedha kwa ajili ya kampeni za upandaji miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuharibika kwa ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu kama lilivyoelezwa kwenye kitabu cha hotuba ukurasa wa 50.



Ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu ndiyo inayotiririsha maji kwenye Mto Rufiji na hatimaye maji hayo ndiyo tegemeo kwenye uzalishaji wa umeme kwenye mradi wa Rufiji *Hydro Project*. Kwa msingi huu, ni muhimu ikolojia hii kutunzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika hoja hii, kama ifuatavyo. Kwanza, ni matumizi ya mifuko ya plasitiki. Baada ya katazo la mifuko ya plasitiki, naomba Serikali itoe njia mbadala ya mifuko hii ya plasitiki. Serikali itoe maelekezo ya vifaa vitakavyotumika badala ya plasitiki. Mfano, vitengenezwe vifungashio kwa kutumia karatasi za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa kuna ukataji mkubwa sana wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa. Niombe Serikali ipunguze bei ya gesi ili wananchi waweze kutumia gesi badala ya kuni na mkaa ambao unasababisha uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Muungano, naomba wananchi waendeleo kupata elimu juu ya Muungano huu. Hata wanafunzi wafundishwe masuala ya Muungano ili kuendelea kuenzi juhudi za waasisi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kunipa fursa hii ili nitoe mchango wangu kwenye eneo hili la mazingira. Utunzaji wa mazingira ni muhimu sana kwa uhai wa binadamu. Utunzaji wa misitu, vyanzo vya maji, usafi wa mazingira ni sehemu ya uhai wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi kwenye utunzaji wa misitu kwa sababu ndiyo chanzo kikubwa kinachovuta mvua, hivyo kupata maji ya mvua kwa ajili ya kilimo na vilevile maji kwenye mito, maziwa kwa ajili ya ustawi wa jamii. Bado Serikali haijawekeza vya kutosha katika

utunzaji wake. Tumeshuhudia misitu ambayo imetunzwa kwa muda mrefu ikikatwa kiholela. Tumeshuhudia makazi yakijengwa au shughuli za kibinadamu katika misitu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wananchi wengi bado wanatumia nishati ya kuni na mkaa kwa matumizi ya nyumbani, ni kweli pia kwamba uchomaji mkaa umekuwa changamoto kubwa katika kuteketeza misitu na watumiaji wengi wa mkaa wanaishi mjini. Ni kwa nini sasa Serikali hii ya Awamu ya Tano isifanye maamuzi magumu kwa kutoa ruzuku kwenye mitungi ya gasi iliyojazana mjini ili kuwezesha watumiaji wengi waweze kununua mitungi hiyo kwa bei nafuu sana na kuachana na matumzi ya mkaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna usambazaji wa gesi asilia kwa baadhi ya makazi na viwanda mbalimbali lakini zoezi hili ni la muda mrefu sana mpaka kuja kusambaa eneo kubwa la nchi. Utatuzi wa haraka wa kuinusuru misitu yetu na vyanzo vya maji ni matumizi ya mitungi ya gesi ya majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba Serikali itachukua hatua ili kunusuru mazingira na uhai wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuunga mkono hutuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naishauri Serikali izingatie ushauri uliotolewa katika hotuba ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala uchafuzi wa mazingira na kukosekana kwa usimamizi mzuri unasababisha uharibifu wa mazingira. Nani asiyejua uidhinishaji/usajili unaofanywa wa viwanda ambavyo ni hatari kwa mazingira yetu? Hivyo basi, pamoja na kauli ya Waziri Mkuu kupiga marufuku utumiaji wa mifuko ya plastiki, je, kauli hiyo imeenda sambamba na ufungaji viwanda vinavyozalisha mifuko hiyo? Je, kauli ya

Waziri Mkuu inaenda sambamba na utoaji wa elimu kwa wananchi hasa vijijini? Nina mashaka makubwa na faini/vifungo watakatavyopata wananchi hasa vijijini. Naishauri Serikali itangaze kufunga viwanda vya utengenezaji mifuko hiyo mara moja na elimu itolewe kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ukataji wa miti unakithiri kila mwaka na hakuna jitihada za upandaji miti hali ambayo inasababisha mabadiliko makubwa ya hali ya hewa. Serikali iweke mkazo katika upatikanaji wa gesi na umeme vijijini na mijini kwa matumizi ya viwanda, magari na majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri Serikali ipeleke miradi ya ufugaji nyuki kwa wananchi vijijini. Ahsante.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia suala la uhifadhi na uendelevu wa mazingira. Dhana hii ni pana na inajumuisha vitu vyote vinavyotuzunguka katika sekta mbalimbali kama vile maji, kilimo, nishati na kadhalika. Bado sekta hii ya utuzaji wa mazingira na uhifadhi haijapewa umuhimu na uzito unaostahili, kwani utekelezaji wake unakumbana na changamoto kadha wa kadha hasa upatikanaji wa rasilimali fedha zinazoendana na Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa hasa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwa sehemu kubwa ni kame kwa sababu ya matumizi mabaya ya mbolea ya chumvichumvi bila kufuata ushauri wa wataalam pamoja na kukata miti hovyoo. Nashauri Wizara itenge fedha kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kupitia luninga, redio vipeperushi na wadau hususan Serikali za Vijiji na Vitongoji pamoja na sekta binafsi kueleza madhara ya uharibifu huo wa mazingira, ikiwemo Operesheni Kata Mti Panda Mti itengewe fedha pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko ya plastiki. Waziri Mkuu alivyokuwa akihitimisha hoja ya Wizara yake, alipiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia miezi miwili ijayo. Hata hivyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri wa Mazingira

anavyohitimisha hoja yake aje na mbinu mbadala kuhusu vifungashio vitakavyotumika katika nchi yetu na namna watakavyoweza kuzibiti mifuko itokayo nje ya nchi yetu. Vilevile ashirikiane na wahusika wa viwanda vilivyokuwa vikitengeza mifuko hiyo ili kuona namna watakavyoshirikiana nao kufanya kazi mbadala kwa sababu ughafila wa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampeni ya upandaji miti. Katika Mkoa wa Iringa kuna ustawi wa miti, matunda na mboga mboga. Nashauri Serikali iweze kutenga fedha ili kusaidia kampeni ya upandaji miti ya matunda ambayo pamoja na kuhifadhi mazingira itasaidia wananchi kupata kipato na kuboresha afya zao. Kwa mfano, wananchi wakipatiwa miti ya miparachichi na *apple* (matufaa) itakuza sana pato kwa wananchi na kuhifadhi mazingira.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Naibu Waziri, viongozi wote katika ofisi kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeze Mheshimiwa Waziri kwa uamuzi wake wa kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya *nylon* ifikapo tarehe 1/6/2019. Kimsingi jambo hili limekuwa ni kubwa kuliko faida ya mapato ya kodi ambayo Serikali imekuwa ikipata kutoka kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uamuzi huu mkubwa wenye manufaa mapana kwa Taifa, binafsi naona kama taarifa ya sitisho la matumizi ya mifuko hii halijatangazwa sana. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri akisema kwamba wamekaa na wadau wa mifuko hii kwa muda mrefu, lakini naamini kutokana na uamuzi huu mzuri wa Serikali, nina ushauri kwamba ofisi yako kupitia vyombo mbalimbali vya habari, kupitia Watendaji mbalimbali Serikalini hususan katika Halmashauri zetu, nao wawe sehemu ya

kusambaza katazo hili kwa sababu siyo wananchi wote wanatazama *TVs*, wanasikiliza *Radio* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani itakuwa ni busara sana kuhakikisha wafanyabiashara wa kada zote pamoja na watumiaji wanapata taarifa hii kwani ni takribani miezi miwili tu imebaki kufikia mwisho wa matumizi ya mifuko ya plasitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha katazo hili muhimu, Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake kwamba, baadhi ya bidhaa zitaendelea kutumia mifuko ya *nylon*, kama vifungashio vya dawa na kadhalika. Nadhani kwa umuhimu siku za usoni kuhakikisha matumizi yote ya plasitiki au *nylon* yanapigwa kabisa marufuku kwa kuzingatia athari za mazingira na hata uzalishaji wa mazao umepungua kwa sababu ya ardhi imeathirika kwa matumizi ya mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeze Serikali kwa jitihada kubwa za ofisi yako kwa namna inavyokabiliana na uharibifu wa mazingira hususan ukataji wa miti ovyo. Naiomba ofisi yako pia itoe katazo la wananchi wote kulima kwenye milima. Kama ambavyo katazo la kufanya shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji, pia kulima kwenye milima kumekuwa na athari za kuleta mabadilikoo ya tabia nchi hususan kwa mvua kupungua, pia tumeshuhudia kuona vyanzo vyote vya maji vinachafuliwa na maji ya mvua yanayochanganyika na udongo kutoka milimani. Naiomba sana Serikali itazame katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la mazingira ni suala mtambuka, napongeza maelezo ya Mheshimiwa Waziri kusema Halmashauri zetu zina wajibu mkubwa wa kusimamia suala la mazingira. Swali hapa ni je, Halmashauri zetu zina watumishi wa kutosha kusimamia mazingira? Je, Serikali inajipangaje kuhakikisha Halmashauri zinapeleka watumishi wenye elimu na weledi wa kutosha juu ya mazingira? Ni vyema tukajipanga katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kushika kalamu na kuchangia hoja hii. Pia napenda kuipongeza Serikali kwa kuja na hoja ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya *plastic* nchini. Kwa hili, pongezi kwanza zimwendee Mheshimiwa Waziri Mkuu kwani yeye ndiye kwa kwanza kuja na tamko hili. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwa kuona umuhimu wa jambo hili na kuamua kuchukua hatua, tena niseme hatua hii imecheleweshwa sana hapa nchini, kwani athari za kimazingira juu ya matumizi ya mifuko hii ya *plastic* ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo cha kuhamahama, biashara ya mazao ya misitu na ujenzi wa miundombinu mbalimbali za kimaendeleo. Mfano, katika Wilaya ya Liwale, Wilaya hii imezungukwa na misitu ya asili; na kwa kuwa huko nyuma hali ya miundombinu ya barabara ilikuwa siyo mizuri, uharibufu wa misitu hii haukuwa mkubwa sana lakini kwa sasa uvunaji wa magogo, mbao na mkaa ni biashara inayokua kwa kasi sana na ni uvunaji usiozingatia sheria na kuwaachia wananchi wa Liwale jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha ushuru Halmashauri inachopata hakiwezi kurudisha uoto wa asili wa misitu hiyo kwani miti imekuwa ikipandwa pembeni mwa majengo ya taasisi za Umma kama shule, hospitali na kadhalika, lakini kule ambako miti hii imekatwa kunabaki kuwa jangwa. Hivyo, napendekeza Wizara ya Maliasili na Wizara ya Mazingira zikafanye kazi kwa pamoja kutafuta namna bora ya kuona misitu au miti inarudishiwa kupandwa pale mti ulipokatwa na lkiwezekana fedha za upandaji miti ziongezwe na zikasimamiwe moja kwa moja na Halmashauri husika. Kiasi cha asilimia tano cha sasa kinachotokana na uvunaji wa mazao ya misitu kifanyiwe marekebisho ili kiendane na aina au kiasi cha uharibifu unaotokea, hivyo Halmashauri iweze kupanda miti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu zaidi inahitajika juu ya utunzaji wa mazingira hasa kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji. Ufugaji wa samaki pembezoni mwa mito ni bora ukapigwa marufuku, kwani mito mingi sasa imeanza kukauka baada ya watu kuchimba mabwawa ya samaki pembezoni mwa mito. Urinaji wa asali kwa njia za kizamani unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa misitu kwa kuchoma moto na kuharibu maisha ya viumbe vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie kidogo kuhusu Muungano wetu. Kwa kuwa Muungano huu ni wa muda mrefu, kizazi cha leo hakina uelewa wa kutosha kwa nini nchi hizi mbili; Tanganyika na Zanzibar ziliamua kuungana na faida za Muungano wetu na hivyo, kutambua dhamira ya Waasisi wetu. Ndiyo maana kizazi hiki kimeishia kuangalia changamoto tu za Muungano bila kuangalia faida zake kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, nazishauri Serikali zote mbili za Muungano kuwekeza zaidi kwenye elimu ya kuelimisha jamii ya leo kuelewa Muungano. Pia pale panapotokea changamoto, basi Serikali zote mbili zichukue hatua za haraka kutatua changamoto hizo kabla hazijaota sugu na kuchafua sura nzuri ya Muungano wetu, tena nyingine zinapaswa zitatuliwe na ngazi za Taasisi za chini kama zile za Uhamiaji, *TRA* na *ZRA*. Hivyo, naiomba Serikali kulinda na kudumisha Muungano huu kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumze juu ya uchafuzi wa mazingira unaofanywa na viwanda vinavyotoa moshi au vumbi mawinguni. Jambo la viwanda vinavyorusha moshi angani na teknolojia iliyopitwa na wakati huchangia kwa kiwango kikubwa uchafuzi wa hali ya hewa ikiwa ni pamoja na magari yanayotoa moshi kupita kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vinavyotoa moshi nashauri viwe vinatozwa tozo za uchafuzi wa mazingira ili iwe kama ni juhudi za kulinda mazingira, kwani sasa nchi za wenzetu viwanda hivi sasa haviko tena na pale vilipo,

teknolojia yake haitoi tena huo moshi. Hivyo basi, imefika wakati sasa kuazima teknolojia hiyo ili kulinda mazingira yetu. Viwanda hivi ni kama vile vya *cement*, chuma na viwanda vya nafaka kama ngano na vile vya kuchakata kokoto na Marumaru.

**MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri na wasaidizi wenu wote kwa kazi nzuri katika masuala ya Muungano na Mazingira. Kipekee, naipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuondoa mifuko ya plastiki sokoni ifikapo tarehe 31 Mei, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo matatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania siyo kisiwa. Kwa kuwa nchi nyingi zilizoendelea zinaratibu matumizi mazuri ya mbegu za *GMO*, nashauri wataalam waendeleo kufanya utafiti wa kitaalam hususan kwenye mbegu za mazao zinazotumia teknolojia ya *GMO* ili kujua faida na madhara yanayotokana na teknolojia hiyo badala ya kuchukua uamuzi wa jumla wa kuikataa teknolojia ya *GMO*. Kwa mfano, utafiti umeonesha kuwa uzalishaji wa pamba kwa kutumia teknolojia ya *GMO* umeongezeka maradufu katika nchi zinazozalisha pamba kwa *GMO* (Wizara ya Kilimo wanazo takwimu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongeza uzalishaji wa pamba tutawezesha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya nguo tunavyoanzisha sasa. Hata hivyo, kutakuwa na haja ya kufanya utafiti wa kina kuhusu matumizi ya mafuta ya kula yanayotokana na pamba itakayozalishwa kwa teknolojia ya *GMO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi makubwa ya maji ni yale ya kilimo cha umwagiliaji kwa sababu *consumptive use* ya mimea inayomwagiliwa ni kubwa kuliko matumizi ya nyumbani (*domestic use*), viwandani na yale ya miradi ya kuzalisha umeme ambayo *consumptive use* ni sawa na



hakuna kwa sababu karibu maji yote yanayotumika kuendesha mitambo yanarudishwa kwenye mto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kushirikiana kwa karibu na Wizara inayohusika na kilimo cha umwagiliaji na Wizara ya Maji, makampuni makubwa ya miwa (sukari) na mashamba makubwa ili wazingatie mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Matumizi sahihi ya maji kwa mazao husika (*crop water requirements*) na *water rights* ili kuepuka matumizi makubwa yanayosababisha vyanzo vya mito kukauka.

(b) Kulinda uharibifu wa ardhi kwa chumvi na kuwa na kilimo endelevu. Kila mradi wa umwagiliaji, hasa ile ya *flooding* iwe na miundombinu ya kutoa maji ya ziada shambani (*drainage systems*) kwa sababu ukosefu wa miundombinu hiyo husababisha chumvi kuongezeka (*salinity*) na ardhi inaharibika. Gharama za kurejesha ardhi inayoharibika kwa *salinity* ni kubwa sana.

(c) Usimamizi wa sheria nyingine zinazoshabihiana na Sheria ya Mazingira, mfano Sheria ya Rasilimali za Maji ya 2009. Wenye viwanda vinavyotumia maji ni lazima waheshimu sheria hii pamoja na sheria nyingine. Katika miaka ya 1990, kulikuwa na mgogoro mkubwa kwenye Kiwanda cha Karatasi Mjini Moshi (*Kibo Pulp and Paper Board*). Tatizo lilianza pale ambapo kiwanda kilipewa *water right* kwa ajili ya kutumia kiwandani kuzalisha karatasi. Katika kiwanda hicho, matumizi mengine yalikuwa ya kemikali ya *aluminium sulphate* ambayo ina sumu (*toxic*).

Sheria ya Rasilimali Maji iliwataka wenye kiwanda kujenga mtambo wa kusafisha maji (*treatment plant*) kabla ya kuyarudisha maji katika Mto Karanga baada ya kuyatumia kiwandani. Kiwanda hakikufanya hivyo badala yake kilichepusha maji katika mfereji na kuwapelekea wakulima wa mpunga. Matokeo yake yalikuwa mawili; moja, wakulima waliwashwa na sumu ya  $Al_2(SO_4)_3$ ; pili, mazao ya mpunga yalipungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana suala hili lilisharekebisha kwa sababu wanamazingira waliingilia. Ushauri wangu ni kwamba sheria zote ambazo zinashabihiana na utunzaji wa mazingira, zisimamiwe vizuri na zieleweke kwa ngazi zote katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kuchangia kwenye Wizara hii nyeti na muhimu ya Muungano na Mazingira. Wilaya yetu ya Kilosa ni Wilaya Kongwe sana hapa nchini; na kwa kweli changamoto kubwa sana tunayoipata kila mwaka ni mafuriko ya mara kwa mara ambayo yanasababisha vifo, uharibifu mkubwa wa mashamba, mali na miundombinu mbalimbali katika Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya mafuriko hayo ni kupasuka kwa bwawa la Kidete ambapo mvua zinaponyesha kidogo tu yanamwagika kwa wananchi lakini pia kupoteza ulekeo wa mto Miyombo ambao ni mto unaopita kwenye kata nyingi za Wilaya ya kilosa yenye Majimbo ya Kilosa kati na Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali itusaidie pesa ili kujenge bwawa hili muhimu la Kidete kwa kuwa Waziri wa Maji alishafanya ziara na kuahidi kuwa pesa zimeshatengwa na wapo kwenye mchakato wa kumalizana na mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mto Miyombo tunaomba sana tujengewe tuta katika Kata ya Masanze iliyopo Jimbo la Mikumi ambapo kwa ujenzi huu wa tuta ni muhimu sana na utasaidia sana kuzuia maji yasiende kwenye makazi ya wananchi na kuepusha maafa ambayo yanatokea mara kwa mara kwenye kata hii pamoja na Kata Magomeni na kuleta maafa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaiomba sana Serikali kuchonga kingo za Mto Miyombo hasa kwenye maeneo ya

Kata ya Kilangali ili kuzuia maji kuingia kwenye maeneo ya wananchi (makazi na mashamba yao) na kuyaharibu vibaya sana kutokana na mto huu kupoteza uelekeo mara kwa mara kwa kuzidiwa na maji mengi ambayo yanatiririka kwa wingi sana hasa kipindi kama hiki cha masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba sana Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii hasa kwenye mfuko wa mazingira ili kuwezesha Wizara hii kutimiza majukumu yake muhimu sana kwa Taifa hili kwenye masuala muhimu yahusyo mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mazingira ni namna Wizara inavyoachia mifugo hasa ng'ombe kuharibu mazingira yetu kwa kiwango kikubwa. Mkoa wa Lindi ni moja ya mhanga mkubwa wa hali hii; mifugo inaingia bila kuzingatia uwezo wa mazingira yaliyopo katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Lindi ipo hatarini kugeuka jangwa. Jimbo langu la Mchinga ni kielelezo cha hoja hii. Wafugaji wanavamia maeneo yote oevu ya Jimbo la Mchinga kama vile bonde la Mbwenkulu na eneo la bonde la Mkoa lililopo katika Kata za Mvuleni na Kitomanga. Wizara lazima ishirikiane na Wizara ya Mifugo katika kupanga maeneo mbalimbali hapa nchini. Uchungaji holela wa mifugo yetu utapelekea kuligeuza Taifa letu kuwa jangwa siku chache zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ni kuhusu miti adimu ya mikoko na mkakati wa nchi wa upandaji mikoko. Kutokana na umuhimu wa miti hii, Serikali inapaswa kuongeza juhudi katika kuilinda na kuongeza miti ya mikoko.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli za wanasiasa zinakua kikwazo katika ustawi wa Mazingira yetu. Sheria ya mita 60 kama ikifanywa kama siasa na kuruhusiwa kuharibu vyanzo vya maji, itakuwa kiam

kwa nchi yetu, kwani itaharibu mazingira, kusababisha upotevu wa mvua na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipi vifungashio vya mikate, ni sehemu ya katazo hilo? Kwa nini tusitoe muda maalum kwa wazalishaji hawa? Naomba ku-*declare interest* kwamba mimi nazalisha mikate na kutumia mifuko hiyo. Bado hakujawa na mbadala sokoni na wafanyabiashara washanunua mizigo na hata kubadilisha mashines.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ije itusaidie kutengeneza kingo za bonde la Mto Msimbazi kwani bonde linazidi kukua na kutafuna majengo na makaazi ya watu. Tunaomba Wizara itoe kipaumbele kwa mto huu. Tunawaombeni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati mbadala kama gesi zishushwe bei hata kupunguza kodi ili wananchi wengi watumie gesi badala ya kuni na mkaa kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi vya akina mama viwe *motivated* na Wizara. Wale wanaozalisha mkaa mbadala binafsi, naikaribisha Wizara kutembelea mradi wa akina mama wa Tabata wanaozalisha mkaa mbadala. Karibu mtunishe mfuko wao waweze kupata mashine ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara isaidie wabunifu kubuni zaidi mashine za kuzalisha mkaa mbadala.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara kuona umuhimu wa mazingira na afya kwa wananchi kwa kutoa tamko la kusitisha matumizi ya mifuko ya plasitikik kuanzia tarehe 1 Juni, 2019. Kama tujuwavyo, mazingira bora na usafi ni kiunganishi kikubwa cha kuondoa umasikini na kukuza uchumi wa nchi na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii ni lazima ihamasishwe kuwa rafiki wa mazingira na waelimishwe kuwa uharibifu wa

mazingira ndiyo unaopelekea kuharibika kwa miundombinu, upungufu wa maji, matatizo ya kiafya, upungufu wa mazao kutokana na uharibifu wa rutuba katika udongo. Vile vile kukosekana kwa mvua na ongezeko la joto vyote hivyo vinachangiwa na uharibifu wa mazingira hayo. Elimu ya kutosha kwa wananchi ni lazima iendeleo kutolewa kwa kasi ili wajue umuhimu wa kutunza mazingira. Maana ukiangalia vijijini suala hili la elimu ya mazingira bado sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingine ya wazoa taka mitaani. Unapomwambia Mtanzania wa kawaida, yaani mwenye maisha duni atoe shilingi 5,000/= ili taka zake zibebwe kila wiki, hapa suala la utunzaji wa mazingira tunaweza kulifanya kuwa gumu. Serikali iangalie inafanya nini katika hili ili kila mtu aweze kumudu kutoa taka kila wiki (gharama za wazoaji taka).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la mitaro katika mitaa yetu; watu wamekuwa wakikamatwa kwa kumwaga maji nje ya nyumba zao na wakati mwingine kutozwa faini hadi shilingi 50,000/= ili mradi tu pakiwa pabichi hata kama ni maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutunza mazingira na kuweka urahisi na amani kwa wananchi ili wawe rafiki na mazingira yao, Serikali iwatengezee mazingira mazuri ya kuyatunza. Kama hilo la kuwa na mitaro mitaani, tozo ya shilingi 5,000/= kwa wanaomwaga maji ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusikiliza hotuba hii, pia nimeona upungufu kwa sehemu kubwa ya hotuba kugusa mazingira kuliko Muungano na hiyo kupelekea kuziacha changamoto nyingi za Muungano bila majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka elimu ya Muungano kwenye vyombo vya habari ili watu wengi wajifunze na kupata majibu ya maswali waliyonayo, ikibidi elimu hii ianzie Shule za Msingi, watoto wakue na uelewa wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia changamoto zinazokua *addressed* zipatiwe ufumbuzi ili tuudumishe Muungano wetu na kuondoa malalamiko yanayokuwa yanajirudia rudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Tumemaliza uchangiaji, sasa tunaanza upande wa Serikali. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, jiandae Naibu Waziri Mazingira na jiandae Mtoa Hoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kuwapongeza sana kaka yangu Mheshimiwa January, Waziri, pamoja na Naibu Waziri kaka yangu Mheshimiwa Sima kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mambo machache sana baada ya pongezi, kwenye hotuba hii na hoja hii iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na jambo la kwanza ambalo limeonekana kwenye vitabu vyote vitatu, kitabu cha Upinzani, kitabu cha Kamati zote mbili za Kudumu za Bunge walipoongelea fedha ambazo zimetolewa, hasa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi hutolewa kulingana na jinsi zinavyopatikana, kwa hiyo zikipatikana *then* mgao unafanyika nani apate nini kulingana na majukumu ya Ofisi husika na kama ilivyooneshwa kwenye vitabu hivi bajeti ilipitishwa na sisi hasa hii sehemu ya kujenga na kufanya ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Luthuli, Tunguu na Wete-Pemba. Tumetoa kiwango hiki cha fedha shilingi milioni 538.4 ndizo ambazo zimetolewa kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi hii, lakini ninachoomba kusema hapa ni pale ambapo vitabu vyote vimesisitiza kwamba fedha hii iliyotolewa ni fedha ya nje hakuna fedha ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kusema tunatoa fedha hizi kulingana na upatikanaji wa fedha husika. Katika hili mkononi mwangu nimebeba kitabu cha hotuba ya bajeti ya Serikali nzima aliyoisoma Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Ndugu zangu tunapojadili jambo hili tusioneshe kwamba kuna mtu ambaye hapewi kwa sababu ya aina fulani ya Wizara yake, hapana. Vyanzo vya mapato vya bajeti kuu wa Serikali vimetajwa kwenye kitabu hiki. Moja ya vyanzo vya mapato kama ilivyoenezwa, tuna mapato ya ndani na tuna mapato ya nje ambayo kwenye mapato ya nje tuna misaada na mikopo nafuu, tuna misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo, tuna misaada na mikopo nafuu ya kisekta kwa hiyo tunapoongelea jambo hili tuijongelee bajeti ya Serikali kama ilivyowasilishwa na vyanzo vyake vya mapato kuliko kusema fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zinapopatikana kwenye kapu, Mfuko Mkuu wa Hazina zinapoingia fedha hizi zinagawiwa kutokana na mgao ambao kwahiyo haingii akilini tunaposema kwamba huyu apewe fedha za ndani wakati tayari ana fedha za nje na Wizara nyingine haina fedha za nje, kwa hiyo kwa kuwa tu tunataka na huyu aonekane ana fedha za ndani basi tulazimishe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliombe Bunge lako Tukufu liweze kuzingatia yanayowasilishwa na tunayoyapitisha ndani ya Bunge lako Tukufu. Hiyo ilikuwa hoja ya kwanza ambayo nilikuwa napenda kusema kuhusu mapato ya Serikali na jinsi gani tunavyoyapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependelea kulitolea maelezo hapa ni kuhusu Akaunti ya Fedha ya Pamoja. Nakumbuka vizuri sana mwaka jana tulitoa ahadi kama Serikali kwamba jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi. Tunafahamu, Serikali ina ngazi zake za kufanya maamuzi, tayari watalaam wetu wameshamaliza kulifanyia kazi jambo hili na sasa tulipo kikao kilifanyika tarehe 9 Februari, 2019 chini ya Mwenyekiti wa Kamati hii ambaye ni Makamu wetu wa Rais anafanya kazi nzuri sana mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli nimpongeze sana Mama Samia amesimama imara kuhakikisha Muungano wetu unakuwa imara na unaendelea kudumu tofauti na inavyowekwa hapa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba Chama cha Mapinduzi, tukumbuke ni Chama cha Mapinduzi ndicho kilichoasisi Muungano huu. Ni viongozi wa vyama hivi viwili kwa dhamira njema ya pande zote mbili za Muungano. Ndiyo maana nataka kumpongeza kwa dhiti ya moyo wangu Mheshimiwa Makamu wa Rais. Angekuwa na moyo kama wa hao wanaotaka kupotosha Watanzania kwenye Bunge lako Tukufu tusingetoka. Serikali ina dhamira njema ya kuhakikisha jambo hili tunafika muafaka ambapo tutakapoanza kuja kwenye migao halisi sasa ya fedha hizi pande zote mbili za Muungano ziwe zimeridhika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza kaka yangu Mheshimiwa Jaku anasema, Zanzibar wakati wanaungana walikuwa wachache, hivyo Watanzania Bara wakati tunaungana tulikuwa milioni 55? Kwa hiyo tuangalie hoja hizi, *base* yetu ni nini ya kuleta hoja hizi. Kwa hiyo tunaposema 4.5 ni ndogo umechukua kigezo gani kusema 4.5 ni ndogo inayopelekwa Zanzibar? Kwa hiyo tarehe 9 Februari, 2019, kikao kilichofanyika hapa Dodoma maamuzi yalifanyika. Kama tulivyokuwa tuna-*report* siku zote kwamba Serikali inayafanyia kazi pale ambapo hatujaelewana na sasa tumeelewana na unaandaliwa Waraka wa Baraza la Mawaziri ili kwenda kufanya maamuzi ya mwisho na jambo hili liweze kufika mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kombo amesema tutoe *commitment*, *commitment* ndiyo hiyo. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kikao hili ameshaelekeza na tayari waraka umeanza kuandaliwa, anataka *commitment* nyingine ipi Mheshimiwa Kombo? Kwa hiyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imedhamiria kuona Muungano huu unaendelea kuwa imara, Muungano huu unaendelea kuwa na faida na pande mbili zote za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limeongelewa ni kuhusu kodi mara mbili. Nimekuwa mimi na



naomba niwe shahidi ndani ya Bunge lako Tukufu, nimekuwa nikisema siku zote hakuna kodi, hakuna bidhaa yoyote inayotozwa mara mbili. Kinachotokea nimesema hapa na jambo hili ni katika mambo ambayo yapo kwenye Waraka ulioandaliwa wa Baraza la Mawaziri kwamba *valuation system* zetu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara siyo moja. Watalaam wetu wamemaliza kuandaa taarifa yao ya kitaalam, wameshaileta tayari inaingia kwenye Waraka huu unaoshughulikia kero za Muungano ili sasa tuweze kulitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye dunia huru ambayo tunafanya boiashara. Haiwezekani jirani yako akaingiza bidhaa kutoka kwa jirani mwingine kwa bei ya chini halafu bidhaa hiyo useme uilete nyumbani kwako ili uweze kufanya biashara. Hiyo haitowezekana, ni ngumu sana, kama kweli sisi ni Taifa moja, ni lazima tuwe na *valuation system* moja yenye manufaa mapana kwa Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kulikumbusha Bunge lako Tukufu hakuna maendeleo bila kodi. Lazima kodi ilipwe na lazima ilipwe katika *rate* zilizokubalika. Tunachikifanya Mamlaka ya Mapato Tanzania tuna-*adopt international system*...

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tume-*adopt international system* ambayo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa jaku kaa chini *please*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tume-*adopt international system*, tuna *international database* sasa huwezi ukajifungia chumbani ukasema mimi siangalii kinachotokea duniani, mimi nataka nilinde watu wangu, unalinda watu wako ukiwa na nini mkononi? Kwa hiyo ni lazima tukubaliane na dunia inakwenda vipi, *global business* inakwenda vipi ili kwa pamoja tuweze kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgao wa Mashirika ya Umma; nilijulishe Bunge lako Tukufu kama ambavyo wamesema Waheshimiwa Wabunge hapa, Benki Kuu tunapeleka na tayari tarehe Mosi Februari, 2019 tumepeleka zaidi ya shilingi bilioni 15 ambazo ulikuwa ni mgao kutoka gawiwo la Benki Kuu. Kwa Mashirika mengine yaliyosalia tunaendelea kuyafanyia kazi na ni moja ya mambo yanayoshughulikiwa kwenye kero za Muungano ili kwa pamoja Mashirika haya yaweze nayo gawiwo waliloanza kutoa, kwanza lazima, tukumbuke Mashirika haya yalikuwa hayafanyi vizuri, Serikali imefanya jitihada kubwa Mashirika haya yameanza kufanya vizuri kwa sasa tunalishughulikia ili kama linavyoingia gawiwo la Benki Kuu, moja kwa moja...

**MWENYEKITI:** Nakuongezea dakika moja malizia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa hiyo tunakwenda kumaliza na mashirika mengine likiingia tu gawiwo lile kwenye Mashirika haya iende moja kwa moja asilimia 4.5 kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki yetu *TPB*; hii huwa tunagawana kulingana na hisa ulizonazo kwenye Benki hii. Kwa hiyo hili halina changamoto yoyote, limekuwa likitendeka miaka yote ya Muungano na tangu *TPB Bank* ilipoanza kutengeneza faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nirejee kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri Wizara hii na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mazingira, ajiandae mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza leo, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa

kuniteua na kuendelea kuniadini kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumshukuru Makamu wa Rais, Mama yetu, Mama Samia Suluhu kwa maelekezo na ushauri mzuri ambao amekuwa akiutoa kwenye Wizara na tumekuwa tukiufanyiakazi. Nichukue fursa hii pia kumshukuru Waziri Mkuu wa ushauri ambao ameendelea kutupatia. Nimshukuru pia Waziri wangu Mheshimiwa Januari, amekuwa ni mstari wa mbele sana kunipa mwongozo mzuri wa kuhakikisha natekeleza majukumu yangu, nimshukuru sana.

Mhshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote katika Wizara yetu, tumefanya kazi kwa pamoja vizuri na hatimaye tunaendelea vuzuri. Vile vile nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Mwenyekiti na Wenyeviti wengine kwa kazi kubwa ambayo tumeendelea kuifanya kwa pamoja. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, niwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Singida Mjini, wamekuwa wavumilivu kwa kipindi chote ambacho nikitekeleza majukumu ya Serikali. Mwisho kabisa niwashukuru pia Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira wametupa ushirikiano mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na wengine wamechangia kwa maandishi, lakini nijikite kwenye maeneo machache hasa yahasuyo mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia hotuba ya bajeti ya Kambi Rasmi ya Upinzani ukurasa wa 10 wamegusia suala la *Stiegler's Gorge* kwamba misitu inafyekwa sawa na ukubwa wa Dar es Salaam nzima. Jambo hili likisemwa hivi kwa Watanzania linaweza kuleta sura tofauti. Mtanzania anayeifahamu Dar es Salaam anaweza akaona eneo lile linalokatwa miti litabaki kuwa jangwa, lakini ni wajibu wetu sasa kufika mahali kueleza faida ya ule mradi wa *Stiegler's Gorge* ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mbuga ya Selou ina kilometa za mraba zaidi ya 50,000 lakini ni asilimia tatu tu ambapo ule mradi unaotarajiwa kujengwa na umekwishanza ndiyo zitatumika kwa ajili ya kuhakikisha tunapata umeme wa *megawatts* 2,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunahitaji umeme na tunahitaji umeme rafiki wa mazingira. Sisi ambao tuko kwenye eneo hili la mazingira, huu umeme kwetu ndiyo umeme rafiki wa mazingira kuliko umeme wa mafuta. Kama umewasikia Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakizungumza kwenye bajeti iliyopita ya TAMISEMI wanataka umeme wa *REA* na mambo mengine yote, lakini umeme ule wanaohitaji wanahitaji wapate umeme rafiki na hapa nilitarajia na mimi kuona Waheshimiwa Wabunge kwanza wanampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na hatua kubwa ya ujasiri ya kuhakikisha kwanza tunapata umeme rafiki wa mazingira ambao tunapata *megawatts* 2,100. Eneo hili linahitaji ushirikiano wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini faida kubwa sana tunaipata. Unapozungumzia tu ile miti ambayo sisi hatukati asilimia 3, ile miti ni kama 1.8 lakini faida ya ule umeme ni kubwa kwa nchi nzima na duniani. Wamezungumzia habari ya mabadiliko ya tabianchi kwamba tuwe na umeme rafiki lakini leo wananchi wetu wanawekewa umeme ama umeme unaofika vijijini unahitaji kuwa wa gharama nafuu ambapo ni lazima tuwe na umeme unaotokana na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la umeme kumekuwa na mambo mengi watu wanayaeleza lakini wanaeleza kwenye eneo la kukata misitu lakini waeleze faida ya kile kinachopatikana pale. Mbali ya faida ya ule mradi kwenye umeme pia kuna ajira, kilimo, ufugaji na mambo mengi ambayo tunahitaji tushirikiane na wenzetu kwa ajili ya kuhakikisha kwanza tunaweza kupata umeme huu ambao utatusaidia kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo mengine wenzetu wamejaribu kuzungumzia lakini nieleze jambo moja

kwenye eneo la taka ngumu na taka hatarishi, wakati nafanya ziara kwenye Mikoa sita ya Nyanda za Juu Kusini moja ya hoja ilikuwa ni hiyo ya vyanzo vya maji lakini nyingine ya taka. Vyanzo vya maji Mto Rufiji wenyewe unaunganishwa ama unalishwa na mito mikuu mitatu: Mto Rwengu, Mto Kilombero na Mto Ruaha Mkuu. Nimeenda kuangalia vyanzo vya maji na namna vinavyohifadhiwa, nataka niwahakikishie Watanzania tunayo maji ya kutosha na Watanzania ni waadilifu wametunza vyanzo vya maji na tunahitaji kuendelea kuwapa elimu waendeleo kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeangalia eneo la taka ngumu na taka hatarishi, Kamati yangu imelizungumza vizuri, moja ya eneo ambalo linaleta changamoto ya taka, nimemsikia Mheshimiwa Hawa Mwaifunga pia amezungumza eneo hili la taka, ni eneo ambalo ni vizuri kwa kweli tukashirikiana kwa pamoja. Nimeendelea kutoa elimu kwenye mikoa yote ambayo nimepitia, nimetembelea madampo na kuona namna ambavyo wanateketeza zile taka zinapotoka majumbani na kupelekwa kwenye madampo, eneo lile tumewaomba wenzetu wa Serikali za Mitaa walioko chini viongozi wale tunashirikiana kwa pamoja japo tunajaua kwenye Sheria yetu ya Mazingira ya mwaka 2004, Ibara ya 6 kwamba jukumu la usafi ama la utunzaji wa mazingira ni la kila Mtanzania ama ni la kila mwananchi ambaye anaishi Tanzania. Eneo hili niwaombe Waheshimiwa Wabunge tushirikiane pamoja, suala la uhifadhi wa mazingira siyo la Wizara moja ama la Serikali peke yake ni suala la kila Mtanzania na kila kiongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Genzabuke amezungumza vizuri na niseme tu kwamba tumepokea ushauri wake juu ya kushirikiana na wenzetu hasa mashirika yale yanayo-*deal* na wakimbizi. Nimefika mpaka Kagera Nkanda nimeona uharibifu mkubwa wa miti na maeneo mengine. Nimuahidi Mheshimiwa Genzabuke jambo hili tumelipokea na tutalifanyia kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mtolea nikuahidi tu kwamba baada ya Bunge hili nadhani nitakapokwenda Jimboni sasa niwasalimie wananchi wangu, nitakwenda kufanya ziara Dar es Salaam. Jambo kubwa hapa siyo tu kutoza faini na hili tuliweke wazi, kwanza tunahitaji watu wale wapewe elimu. Kwa sababu kama Watanzania kwenye gereji na maeneo mengine hawajapewa elimu na tukakimbilia faini, hili kwa kweli hatutakubaliana nalo. Nikuahidi kwamba nitafika mwenyewe nifanye ziara na pia tuwashirikishe wananchi ambao wameamua kuwa wajasiliamali kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza suala la elimu, kwa kweli tunakubaliana nalo, suala la elimu halina mwisho hata kama tunaendelea kutoa inawezekana bado elimu inahitajika sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa Saada Mkuya amesema elimu ya Muungano inayotakiwa sasa ianzie Bungeni. Hili tunakuunga mkono, tutaanza nalo, najua Mheshimiwa Waziri ataeleza vizuri suala la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la elimu ni jambo kubwa sana na siyo jambo la Wizara au Serikali peke yake, kila Mtanzania anayeelewa juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira anapaswa kuwaelimisha na wengine. Pia anayejua umuhimu wa Muungano anapaswa kuwaelimisha na wengine. Sisi tutakuwa mstari wa mbele, tutaendelea na majukumu na mikakati yetu ya kuhakikisha kwamba elimu hii inatolewa kadri inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kadri ambavyo wametupongeza waendeleo kutupa ushirikiano wa dhati na sisi kama ambavyo mnafahamu tunafikika na tuko tayari kufanya kazi wakati wote. Pale tunapobanwa mtu wie radhi inawezekana tusifike kwa wakati lakini tunaweza kushauriana na kusaidiana, majukumu haya yote ni yetu pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nichukue fursa hii kuishukuru sana familia yangu, mke wangu na watoto ambao nao wamenivumilia kwa kipindi chote hiki nimeendelea kutekeleza majukumu yangu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nishukuru kwa fursa uliyonipa ya kuja kuhitimisha hoja hii hapa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru wachangiaji wote, kwanza kwa Kamati zote mbili: Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati ya Katiba na Sheria kwa taarifa nzuri walizozitoa pamoja na ushauri, maoni na mapendekezo ambayo wameyatoa katika taarifa zao. Pia napenda niwashukuru wachangiaji wote waliochangia kwa maandishi walikuwa 25, waliochangia kwa kuzungumza walikuwa 9, jumla watu 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa taarifa yao waliosoma na maneno yao walitueleza na yote tumeyapokea na yote ni ya kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha ambaye ametusaidia kuelezea baadhi ya mambo na kujibu baadhi ya hoja. Pia namshukuru Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mheshimiwa Mwalimu Sima naye kwa mchango wake na majibu aliyoyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye masuala machache ya jumla ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyachangia. Kwanza suala la biashara kati ya Zanzibar na Bara ni jambo ambalo limejitokeza katika michango ya

Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia masuala ya Muungano. Bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ametusaidia kujibu kwamba changamoto za kikodi ndiyo zilizokuwa zinakwamisha biashara kati ya Bara na Zanzibar zilitokana na mfumo tofauti wa ukadiriaji wa kodi kwa bidhaa zinazolingia katika vituo vya forodha vilivyoko upande wa Zanzibar na vituo vya forodha vilivyoko upande wa Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo sasa linashughulikiwa kwa kuweka mfumo mmoja wa ukadiriaji wa kodi kiasi kwamba bidhaa itakayoingia kwenye kituo cha forodha cha Zanzibar ikadiriwe kodi sawa na kituo chochote ambacho bidhaa hiyo imeingia kwa upande wa Bara. Imani yetu ni kwamba hilo litapunguza malalamiko na maelezo kwamba kunakutozwa kodi mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua haja ya kushughulikia masuala ya fedha na biashara kwa wakati wote, Kamati ya Pamoja ya kushughulikia changamoto za masuala ya Muungano iliunda Kamati Ndogo ya Fedha, Biashara na Uchumi ya Mawaziri, Makatibu Wakuu na wataalam ambayo itakuwa inakutana mara mbili kwa mwaka kushughulikia masuala ya fedha, uchumi na biashara yanayojitokeza mara kwa mara. Imani yetu ni kwamba mfumo huu na Kamati hii sasa itasaidia kusukuma mambo haya kwa haraka zaidi na kutatua changamoto za biashara zinazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yetu sisi tuliopo katika Ofisi ya Makamu wa Rais ni kwamba uchumi wa Tanzania Bara ni mkubwa kuliko uchumi wa Zanzibar na Zanzibar lazima ifikie soko la Bara na Bara vilevile lazima iwe na uwezo wa kufikia soko la Zanzibar bila vikwazo vyovyote. Muungano huu ni wa kisiasa, kijamii pia kiuchumi. Kwa hiyo, imani yetu ni kwamba moja ya shabaha za Muungano ni kuleta ustawi wa watu wa pande zote na Muungano usionekane kikwazo cha ustawi wa upande mmoja au mwingine. Sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ni kwamba tufanye jithada zote ili fursa za uchumi, biashara na ustawi na zenyewe ziendele.



Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Bara na Zanzibar wamekuwa wanafanya biashara hata kabla ya Muungano kwa miaka mingi, hata kabla ya Uhuru, hata kabla ya Mapinduzi. Imani yetu ni kwamba kuwepo kwa Serikali kusiwe kikwazo kwa biashara ya asili ambayo imekuwepo kwa miaka mingi kati ya watu wa pande zote mbili. Hiyo ni dhamira yetu kwamba ukubwa wa soko la Bara usaidie kujenga uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Tume ya Pamoja ya Fedha, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha amelijibu lakini nitapenda niongezee machache. Ni kweli Tume ya Pamoja ya Fedha imeundwa kwa mujibu wa Katiba na vilevile Mfuko wa Pamoja na wenyewe umeundwa kwa mujibu wa Katiba. Hili suala linajirudia mara kwa mara hapa Bungeni kuhusu lini Mfuko huo utaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka kwamba kwa mujibu wa Katiba, moja ya kazi za Tume ya Pamoja ya Fedha ni kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili. Hiyo ni moja ya majukumu matatu ya Tume ya Pamoja. Tume hiyo ilifanya kazi kubwa sana kuanzia miaka ya 90 na mwaka 2006 ikawasilisha ripoti Serikalini, nakumbuka ilikuwa tarehe 9 Oktoba, 2006 kwa Waziri wa Fedha wakati huo Mama Zakia Meghji na ripoti ile Tume ilikuwa ni ya mapendekezo ya vigezo vya kuchangia na kugawana mapato ya Muungano. Ni ripoti iliyotokana na *study* muda mrefu kwenye nchi nyingi kuhusu mfumo sahihi, bora na na sawia (*equitable*) wa kugawana mapato na kuchangia mapato ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ripoti ile kupokelewa, Serikali zote mbili ziliahidi kuifanyia kazi na kweli baada ya pale ikapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri wataalam wakaifanyia kazi, Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mara kadhaa mapendekezo yale yalitengeneza *cabinet paper* ili yaweze kupitishwa na tuwe na mfumo bora ikiwemo kuanzisha Akaunti ya Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya hilo halikutokea kwa sababu moja au nyingine hadi tukaanza mchakato wa Katiba ambapo ndiyo ulionekana kwamba utakuwa mfumo bora zaidi wa kushughulikia jambo hili. Kwa hiyo, imani yetu ni kwamba mchakato wa Katiba utakaendelea basi suala hili pia litaendelea kushughulikiwa. Tunashukuru kwamba pia Wizara ya Fedha inaendelea kulishughulikia suala hili. Kwa hiyo, Akaunti ya Pamoja ni takwa la Kikatiba na lazima litekelezwe na lazima litatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vikao vya Kamati ya Pamoja, tumesikia kwenye taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani ikisema kwamba vikao hivi havina maana yoyote kwamba vinakaa, hatuoni matunda na hakuna utekelezaji na kadhalika. Labda niseme tu kwamba mwaka 2006 tulipoanzisha utaratibu mpya wa Kamati ya Pamoja ya Fedha kulikuwa na changamoto 15 za Muungano na kwa kutumia mfumo huu wa vikao zimetatuliwa changamoto 11 zimebaki changamoto tano (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi zimetatuliwa katika vikao na siyo kwa njia nyingine na siku zote mambo yote yanamalizwa kupitia vikao. Kwa hiyo, sisi hatuamini kabisa kwamba vikao hivi havina maana kwa sababu tumeona matunda yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu wanapokuwa na mambo wanayamaliza kupitia vikao. Kwa hiyo, ingependeza kama wenzetu Waheshimiwa wangetueleza zaidi ya vikao ni ipi namna bora zaidi ya kuzungumza mambo ya Muungano. Sisi tunaamini vikao ni namna bora zaidi. Bahati nzuri katika kikao cha tarehe 9 Februari, 2019, hapa Dodoma cha Kamati ya Pamoja tuliamua kurasimisha na kuimarisha mfumo wa vikao hivi ili tuweze kufuatilia maelekezo na maagizo yake na kuhakikisha kwamba yanayoamuliwa yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa kwamba vikao vinakaa na changamoto za Muungano haziiishi.

Naomba niseme hapa kwamba changamoto za Muungano hazitakuja kuisha hata siku moja na dhana kwamba kwa sababu kuna changamoto basi Muungano haufai ni potofu kabisa. Siku ya kwanza Muungano umepitishwa, siku ya pili kulitokea changamoto ya namna ya kuunganisha majeshi, mfumo wa fedha na masuala ya ushirikiano wa kimataifa na mambo mengine, siku ya pili tu ya Muungano. Nakumbuka wakati ule tulikubaliana kwamba masuala ya fedha yatakuwa ya pamoja lakini kukawa na mkanganyiko kuhusu nafasi ya *Peoples Bank of Zanzibar* na *BoT* lakini mambo haya yalimalizwa kwa vikao na leo changamoto ile hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 55 ya Muungano changamoto ambazo leo hatuzizungumzii kwa sababu zimemalizwa ni nyingi. Kwa hiyo, sisi tunaamini kwamba Muungano huu kikubwa ni mfumo na utaratibu ambao tutauweka wa kumaliza changamoto na hilo ndio ambalo tunalifanya sasa. Kudhani kwamba hakutakuwa na changamoto ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeongelewa kuhusu *mainstreaming* ya masuala ya Muungano, utaona ni hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Saada Mkuya. Sisi tunadhani kwamba ni hoja muhimu na ya msingi. Wewe unafahamu na Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kwamba kwenye kila bajeti ya kila Wizara iwe ni ya Maji, Miundombinu au Maliasili kuna mambo huwa hayakosi UKIMWI na rushwa siku zote hata kama hayahusu sekta hizo lakini yamo kwenye bajeti zote za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaamini kwamba tufike mahali kwamba kwenye kila bajeti ya kila Wizara iwe ya Muungano isiwe na Muungano basi suala la Muungano na lenyewe liwepo kama ripoti ambayo inatolewa. Hili tunalizungumza Serikalini kwa sababu kwa Wizara za Muungano kuna ulazima wa kushirikiana na mambo ya kutekeleza lakini kwenye Wizara ambazo siyo za Muungano tunahamasisha ushirikiano. Kwa hiyo, itapendeza hapa kwenye hotuba za bajeti kila Wizara ikasema imeshirikiana vipi na upande wa pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda na wenzetu wa Zanzibar kama tutazungumza na kukubaliana pia katika bajeti zao na wenyewe waseme katika mwaka uliopita wa fedha kama ambavyo kwenye masuala ya rushwa na UKIMWI wanaripoti basi vilevile kwenye masuala ya Muungano kuwa na ripoti. Tunaamini hatua hii itasaidia kuimarisha Muungano na italizimisha wenzetu na wengine waripoti kuhusu masuala ya muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba watu wengi hawajui lakini hakuna Wizara isiyo ya Muungano kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iwe ni Wizara ya Maji ambayo siyo jambo la Muungano au Wizara ya Utalii ambayo siyo jambo la Muungano, Wizara zote ni za Muungano. Mheshimiwa Dkt. Kibwangalla anaitwa Waziri wa Maliasili na Utalii wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu hakuna Wizara ya Bara, Wizara zote ni za Muungano. Kwa hiyo, kila Wizara ina wajibu wa kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba angalau tunashirikiana na upande wa pili kuhusu masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetoka hapa hoja kwamba Serikali ya CCM haina nia na Muungano huu. Mimi huwa sipendi kuingia kwenye mambo ya kushambuliana kwenye vyama na mambo ya siasa za aina hiyo, lakini kauli hii lazima ijibiwe. Katika mambo ambayo yanapaswa kuwa nje ya siasa ni masuala ya Muungano. Kwenye nchi zote kuna baadhi ya mambo ambayo siasa haipaswi kuingizwa. Kwenye nchi za wenzetu kuna mambo ambayo yamemalizwa siyo tena mjadala na kwenye nchi yetu mimi imani yangu ni kwamba Muungano ni jambo ambalo tunapaswa kuwa tumelimaza halipaswi kuwa na u-CCM, u-CUF, u-ACT wala namna nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa nchi ya Marekani, wao ni Muungano wa Kifederali na ule Muungano uliletwa kwa vita, kuna nchi zilikuwa hazitaki kuwa sehemu ya Muungano na vita ikapiganwa na wale ambao hawakutaka kuwa sehemu ya Muungano wakaingizwa kwenye Muungano kwa kushindwa kwenye vita hasa

Majimbo ya Kusini. Tangu wakati ule leo *United States of America*, aidha, iwepo au isiwepo siyo tena hoja ya siasa wala kampeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani tunapaswa kufika hapo kwamba wakati wa uchaguzi haipaswi Muungano wetu kuwa kwenye *referendum*. Kwa sababu kilichopo sasa hivi ni kila uchaguzi unapofanyika Muungano ni kama vile upo kwenye kura ya maoni. Kwa hiyo, kama nchi tunapaswa kuondoka huko. Wenzetu ambao wameungana kila mahali, hata Marekani Muungano wao una miaka zaidi ya 200, lakini kila siku wana kauli yao wanasema, *to strive for a more perfect union*. Kwamba, Muungano wao wa miaka 200 bado hauko *perfect* kwa hiyo, nasi leo tukija hapa Bungeni tukataka leo miaka 55 tuwe na *a perfect union* tutakuwa tunaomba mambo ambayo hayako tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Muungano huu kazi yetu ni kuendelea kuujenga na namna ya kuujenga siyo kuusimanga na kuchukulia changamoto ndogo na kuupaka matope na kuupa jina baya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia zaidi ya 94 ya Watanzania wamezaliwa ndani ya Muungano, hawajui Tanganyika, wanajua wamezaliwa ndani ya Muungano na hawana pengine pa kwenda na utambulisho wao ni wa Muungano. Kwa hiyo, nawaomba na kuwasihi Waheshimiwa Wabunge ambao huwa tunarushiana vijembe na maneno na wale wanasiasa ambao wanatumaini changamoto za Muungano zitasaidia kuwabeba, basi tuache hivyo, wote tufanye kazi pamoja kuuimarisha Muungano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imezungumzia kuhusu muundo wa Muungano na kwamba ndiyo chanzo cha changamoto na kwamba haufai na ndiyo umetuletea matatizo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kwenda kwenye mjadala huu kwa sababu ni mrefu na wote tunajua

mjadala huu tuliufanya wakati tunafanya mchakato wa Katiba. Ambacho naweza kusema ni kwamba, Waasisi wa Muungano, Mwalimu Nyerere na Mzee Karume, kabla hawajaamua Muungano wa aina tuliyonayo leo, walitafakari miundo yote ya kila aina, wakatazama dunia nzima, wakatazama mazingira yetu, wakatazama haiba ya watu wetu, wakatazama ukubwa wa pande zote mbili na wakaamua kuwa na Muungano wa kipekee duniani ambao ndiyo tulionao leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiniuliza mimi sababu ya kudumu kwa Muungano huu, tofauti na Muungano wa Senegal na Gambia, tofauti na Muungano wa Misri, Syria na kwingineko ni kwa sababu ya muundo wake. Tunatofautiana; wengine wanadhani Muungano wetu una shida kwa sababu ya muundo wake, lakini sisi tunaamini Muungano wetu umedumu kwa sababu ya muundo wake. Kwa hiyo, kikubwa ni kuendelea kuimarisha mifumo na taratibu za kushughulikia masuala yanayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna bahati kwamba Muungano wetu una bahati ya kuundwa katika misingi ya kijamii, kwa sababu mahusiano ya kijamii ya watu wa pande zote yamekuwepo kabla ya mapinduzi, yamekuwepo kabla ya uhuru na yamekuwepo kabla ya Muungano. Kikubwa tu ni sisi kuendelea kuimarisha masuala ya kitaasisi na kisheria na kiutaratibu ili tuendelee kuwatendea haki watu ambao ni ndugu wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumziwa hapa suala la vyombo vya moto, kwamba haipendezi ikawa kuna ugumu wa kuingia na gari lako kutoka upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa kwamba ni jambo linalokera, linaloudhi kwamba gari kutoka Zambia au Malawi, linavinjari kwa urahisi katika nchi yetu, lakini gari kutoka Zanzibar linapata bughudha. Hilo jambo halikubaliki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sasa Serikali imeanza kulishughulikia jambo hilo na Mwanasheria Mkuu wa Serikalin anafahamu kwamba kulikuwa tayari na mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Usajili wa Magari na Sheria nadhani ya Polisi na ilishafika kwenye Mkutano wa Kamati ya Baraza la Mawaziri ya Katiba na Bunge ili mabadiliko yafanyike kuhakikisha kwamba jambo hilo linakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya tukashauriwa kwamba ili utaratibu huo udumu na uwe imara, tuhakikishe kwamba zinawekwa taratibu ili wale watu ambao wanaweza kutumia mwanya kuingiza magari na badaye kuyauza kwa upande mwingine, basi wasifanikiwe. Sasa *study* hiyo iliyofanywa na TRA na wengine imekamilika, nasi tunaamini kwamba wachache ambao wanaweza kutumia fursa hiyo vibaya wasiwaharibie watu wengi wema ambao wanataka kusafiri na vyombo vya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu huo utawekwa na ni imani yangu kwamba mabadiliko hayo ya sheria yatafywa mapema kupitia kwa wenzetu ili jambo hilo tulimalize. Ni kero kubwa na ni aibu kusema kweli. Kwa hiyo, imani yetu ni kwamba litakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la mifuko ya *plastic*. Naomba niseme, tumezungumza kwa kirefu kwenye hotuba yetu, lakini naomba niseme tu kwamba dhamira hii ni njema. Kwenye hili tumejipanga vizuri kwa sababu tumeshirikisha wadau mapema zaidi. Tunaamini kwamba suala hili ili tufanikiwe ni lazima twende hatua kwa hatua. Kwa sasa hatuwezi kupiga marufuku kila kitu; kuna baadhi ya vifungashio vinavyotumia *plastic* ambavyo ni lazima vitumie *plastic*, kwa mfano, mikate, maziwa, madawa na vinginevyo. Imani yetu ni kwamba, kwa sasa vitaruhusiwa ili tusilete bughudha na mtikisiko kwenye uchumi na kuongeza bei za bidhaa kwa watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaanza na mifuko hii ambayo ni kero, hata hivyo kwa vifungashio

tutaweka *standards* ili viweze kukusanywa na kurejelezwa. Hiyo, tunaamini tutafanikiwa. Hata wale wenye chupa za *plastick* vile vile imani na mpango wetu ni kuweka ulazima wa wao kushiriki kwenye mipango ya *recycling*, kwamba huwezi kuwa unazalisha chupa za Kilimanjaro halafu huna habari hiyo chupa inaishia wapi? Lazima ushiriki kwenye utaratibu wa kuirejesha na kuirejeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kanuni mpya pia zitatoa mahitaji hayo. Naomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane, kwa sababu tutakapofanikiwa jambo hili tutakuwa tumefanya jambo la kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shaka kuhusu mbadala kwamba, je, mbadala upo na unatosha? Naomba niwaambie kwamba wenzetu Wakenya ambao wamepiga marufuku mifuko ya *plastic*, mifuko yao ya karatasi wanaitoa Tanzania. Wenzetu Warwanda, ukienda kule *Mufindi Paper Mills*, malighafi yote ya mifuko ya karatasi ya Rwanda inatoka Mufindi na Rwanda inasifika, Kigali, kama mji safi kabisa hapa Afrika, sababu ni nini? Sababu ni sisi ndio tunawapa karatasi, wanapata mifuko ya karatasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale wametuhakikishia kwamba uwezo wa ku-*supply* mifuko ya karatasi hapa nchini wanao na kwamba, changamoto yetu kubwa kwa sasa ni kuhakikisha wanaongeza *production* na usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni tunazotoa zitatoa adhabu kwa wanaouza mifuko, wanaoweka na kwa wanaoingiza ndani ya nchi. Kunaweza kukatokea mtikisiko na malalamiko kidogo kwenye zoezi hili, naomba Waheshimiwa Wabunge muiunge mkono Serikali kuhakikisha kwamba, jambo hili linafanikiwa. Kwa sababu, siku zote hakuwezi kukosa malalamiko kwenye masuala makubwa ya mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya mkaa na ukataji wa miti, hii ni changamoto kubwa sana sana. Kila dadika moja inayoenda hapa nchini, misitu inayofyekwa ni



sawa na kiwanja cha mpira. Tangu niongee hapa nadhani ni dakika 15, misitu iliyofyekwa ni sawa na viwanja vya mpira 15. Tena hizi ni takwimu za chini na sehemu kubwa ni ukataji wa mkaa, kilimo kisicho endelevu, uzururaji wa mifugo, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa mazingira hapa, akina Mheshimiwa Dkt. Sware wanafahamu kwamba misitu ina thamani katika mifumo ya kikolojia na utajiri wa nchi unapimwa kwenye mambo mengi; kuna utajiri wa watu wenyewe, utajiri wa vitu na utajiri wa maliasili. Katika nchi zinazoongoza duniani kwa utajiri wa maliasili, wanaita *Natural Resources Wealth Per Capita*. Tanzania ni moja kati ya nchi zinazoongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka 20 iliyopita utajiri wa Tanzania kwa maliasili kwa maana thamani ya mito, maziwa, misitu, na kadhalika, thamani yake *per capita* inashuka kwa asilimia 35 kwa miaka 20 iliyopita, ingawa *GDP per capita* inapanda, lakini *natural resources per capita* inashuka chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili pekee ya kwamba maendeleo siyo *sustainable* ni pale utajiri wenu wa maliasili unaposhuka wakati utajiri mwingine unaenda juu. Kuna wakati hata ule unaenda utashuka utakutana na ule wa chini. Kwa hiyo, tuna wajibu mkubwa kuhakikisha kwamba maendeleo tunayoyatafuta ili yawe endelevu, hatuna budi kulinda maliasili zetu kwa nguvu zetu zote kwa sababu, ndiyo utajiri tulionao. Kwa hiyo, sisi ndani ya Serikali tunazungumza na wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Wizara nyingine husika ili kuwa na makubaliano kuhusu mwenendo wa kulinda rasilimali za nchi zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hili jambo tunazungumza na wenzetu kwamba sisi tunaamini msitu uliosimama na miti iliyosimama ina thamani hata kwenye kilimo kwa sababu hata mahindi ili yazae lazima kuwe na wale wadudu na nyuki wanaofanya *pollination* nao wanatoka kwenye misitu. Ukipewa shamba sasa hivi lenye

msitu, usipokata msitu unanyang'anywa kwa sababu hujaliendeleza, ehee! Nasi tunaamini kwamba msitu vilevile unaposimama na wenyewe una thamani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili tunalizungumza kwamba kuna mwenzetu mmoja akiona mti umesimama anauona ni gogo na lenyewe ni chanzo cha mapato. Kwa upande mwingine ule mti pia unaweza kuuweka nyuki na kuzalisha. Kwa hiyo, ni mambo ambayo tunazungumza ndani ya Serikali ili kuhakikisha kwamba tunatunza nchi yetu; na maelekezo ya viongozi wetu, mmemisia Mheshimiwa Rais alipokuwa Njombe alisema tulinde misitu yetu kwa nguvu zetu zote na mapori yetu yote. Imani yangu ni kwamba tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tumewasikia kilio chenu kuhusu kasi ya ukataji wa miti na kasi ya nchi yetu kuwa jangwa. Ukombozi haupo kwenye kupanda miti, ukombozi upo kwenye kutunza miti iliyopo isikatwe, kwa sababu miti iliyopandwa haifiki asilimia nane ya miti yote iliyopo nchini. Tusipokata miti ni bora zaidi kuliko kuhangaika kupanda miti mingine. Kwa hiyo, huko ndiyo ambako jitihada zitaelekezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa kuhusu utendaji wa *NEMC* na nilizungumza asubuhi kuhusu *reforms* ambazo tunafanya. Tumepokea kabisa malalamiko kuhusu utendaji wa *NEMC* na malalamiko hayo ni ya kweli kwa sababu, kulikuwa na changamoto kubwa za ucheleweshaji wa vibali, gharama za vibali na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwa kirefu asubuhi hatua tunazochukua. Bahati nzuri tumepata uongozi mzuri, tunaye Mwenyekiti wa Bodi ya *NEMC* ambaye tuko naye hapa, Profesa Asnath Chagu, tuna Mkurugenzi Mkuu mpya, anapanga safu yake vizuri. Tumesikia changamoto ya watumishi wachache wa *NEMC*, bahati nzuri wenzetu wa Utumishi wametusaikia, wametupa kibali cha kuajiri watu 30 mwaka huu, lakini zaidi ya hapo tumewaelekeza watu wa *NEMC* kwamba, kuna vijana wengi sana wamesoma

mazingira na jografia kwenye vyuo vikuu na hawana kazi na ni vijana wazuri na wasomi. Tumesema kwa sababu kazi za *NEMC* ni nyingi, wawachukue kwa mkataba kama *interns* na kuwatumia kwenye kazi za kwenda kufuatilia, kusimamia, na kadhalika, wapate posho na uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi tunao 40 na miezi michache tutaongeza 100 na mwaka ujao tutaongeza 100 wengine kuhakikisha kwamba *footprints* ya *NEMC* nchi nzima inakuwa kubwa. Tunafungua Ofisi za Kanda ili kuhakikisha kwamba *NEMC* inatoa huduma kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *NEMC* sasa hivi inabadilisha mtazamo wake kutoka taasisi ya kipolisi na kuwa taasisi ya huduma zaidi kwa wawekezaji na kwa wananchi. Nimewaambia watu wa *NEMC*, nyie mkionekana mnafunga viwanda, mnatoza *fine*, mnakusanya pesa, sawa ni kazi zenu, lakini ukisoma sheria mna kazi kubwa na muhimu zaidi ikiwemo utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sheria inasema *NEMC* inapaswa kuweka orodha ya milima na vilima vyote nchini. Sheria ilisema, ndani ya miaka mitano baada ya sheria kuundwa kuwe na orodha iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali kuhusu milima na vilima vyote nchini na hatari ya mazingira kwa vilima hivyo. Hiyo ni kazi ya *NEMC*. *NEMC* inaruhusiwa kumiliki maeneo yaliyolindwa kwa Sheria ya Mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutabadilisha mwelekeo wa *NEMC* ionekane ni taasisi kubwa na yenye heshima na yenye hadhi, siyo ya kufukuzana na watu na kuchelewesha vibali, na kadhalika. Kwa hiyo, mtaiona *NEMC* tofauti na tutaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba, tunataka uwekezaji na uwekezaji ni muhimu, lakini tunaamini uwekezaji lazima uende sambamba na hifadhi ya mazingira. Sasa nataka kusema, mtu yeyote ambaye anacheleweshewa kibali na *NEMC* au anaamini *NEMC*

inamcheleweshea kibali, aje kwetu sisi moja kwa moja tutamsaidia papo hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho limezungumzwa suala la *UNHCR* Kigoma na madhara ya wakimbizi kwenye uharibifu wa mazingira. Tumeongea na wenzetu wa Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wakimbizi kuhakikisha kwamba kwanza makambi yetu yanafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (*EIA*) na hali ya mazingira inarejeshwa na kwamba wananchi pia wanapata manufaa na huduma ambazo wakimbizi wanazipata ikiwemo maji, na kadhalika. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma hili tunalishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mfumo mzima wa usimamizi wa mazingira. Sheria ya mazingira imetengeneza *architecture*, mfumo wa usimamizi wa mazingira. Sheria ya Mazingira imetoa maelekezo kwa Wizara na Taasisi nyingine za Umma na binafsi, lakini hususan na Serikali za Mitaa kuhusu mambo ya kufanya. Kwa hiyo, Maaflisa wa Mazingira wanaajiriwa na Halmashauri na kamati zinapaswa kuundwa kwenye ngazi ya Halmashauri. Kwa hiyo, kikubwa tunachofanya sisi ni kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kwamba ule mfumo wa usimamizi wa mazingira ambao unahusu Wizara zote unasimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mazingira inasema kila Wizara iwe na mratibu wa mazingira na kila Halmashauri iwe na Afisa Mazingira na kila Sekretarieti ya Mkoa iwe na Mratibu wa Mazingira. Kila kijiji kiwe na Kamati ya Mazingira, kila Kitongoji, kila Mtaa, kila Kata, kila Wilaya. Hapo ndipo mfumo mzima wa usimamizi wa mazingira utakuwa umekamilika na kwamba *NEMC* peke yake haiwezi kuwa kwenye kila Mtaa, kila Kijiji na kila Kitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa tumeifanya katika mwaka uliopita kuhakikisha kwamba mfumo huu unakuwepo, kuna baadhi ya mikoa imefanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba Mitaa yote, Vijiji vyote vina Kamati ya Mazingira na matunda tunayaona katika usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala limezungumzwa la kutotosha fedha. Labda niseme tu kwamba fedha siku zote hazitoshi na hasa kwenye nchi kama yetu. Sasa ambacho nataka kusema ni kwamba kuna Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Mazingira, pia kuna fedha za mazingira zinazokuja nchini katika ujumla wake. Ukiangalia Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais na ukaichukulia kwamba ndiyo fedha za mazingira hapa nchini utakuwa umefanya makosa. Nitatoa mfano kwamba, sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tumewatafutia Wizara ya Maji fedha kwenye Mfuko wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabia-Nchi (*Green Climate Fund*). Tumehakikisha wamezipata. Fedha zile ni shilingi bilioni 250 ambazo zinaenda kuleta maji Simiyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zingekuwa kwenye bajeti yetu, si ajabu kusingekuwa na maneno. Kuna fedha zimepitia kwetu lakini ziko Wizara ya Kilimo; kuna fedha zimepitia kwetu, lakini ziko Wizara ya Mifugo. Kwa hiyo, inawezekana fedha zikaonekana hapa kidogo, sisi kazi yetu wakati mwingine ni kuwatafutia wengine fedha kupitia mikataba ya Kimataifa ambayo sisi ni wanachama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo. Tunaamini kwamba ni kweli rasilimali zinahitajika zaidi na tunaamini pale Mfuko wa Mazingira utakapokuwa umeanza kazi, basi na wenyewe utachangia katika kuhakikisha kwamba fedha zaidi zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala mengine yamezungumziwa ya *GMO*, Mheshimiwa Chiza; masuala ya matumizi ya maji kwenye umwagiliaji, masuala ya matumizi ya gesi na Mheshimiwa Ruth Mollé, ameongea kuhusu suala la nafuu ya kodi kwenye mitungi ya gesi ili kuokoa misitu. Hilo tutazungumza na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba linafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ni kikubwa na cha msingi ni kwamba tunaona na tunafarijika sana na kupanuka kwa nishati mbadala ya mkaa. Kiwango cha gesi ya mitungi kinachotumika mwaka huu ni kikubwa mara mbili

ya kilichotumika mwaka jana 2018 na tunaamini kadiri miaka inavyoenda na tunaona uwekezaji katika eneo hilo, imani yetu ni kwamba tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mita 60 nilizungumzia asubuhi kwamba tunaweka kanuni na utaratibu wa kuweza kuhakikisha kwamba tunafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mambo yale makubwa na ya msingi, suala la elimu ya Muungano ni kweli lazima nikiri kwamba hatujafanya vizuri, wakati mwingine tunafanya mambo makubwa lakini hatuyazungumzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba vikao vya Muungano ni vya siri kwamba hakuna *transparency*, hiyo siyo kweli. Udhaifu wetu ni kwamba labda baada ya kikao tulipaswa kuitisha *press conference* ili watu wajue. Kwa hiyo, tumechukua maoni na ushauri kuhusu namna ya kuelezea wananchi kuhusu nini kinafanyika na ofisi zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nirudi tena kwenye suala la Muungano kwa kifupi kwamba, kuna kazi nyingi sana kwenye Muungano zinafanyika hasa kupitia kwa viongozi wakubwa, hasa kupitia kwa wataalam, miradi, uhusiano na ushirikiano uliopo lakini mjadala wetu kuhusu Muungano umejikita kwenye changamoto. Sisi tunadhani kwamba tunayo kazi ya kuonyesha kwamba *definition* ya Muungano sio vikao vya changamoto bali ni mambo mengine mengi yanayofanyika ambayo hayaonekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nitoe ahadi kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba wale ambao hoja zao sijazigusa na hata wale ambao nimezigusa basi tutaziandika vizuri, tutatoa majibu vizuri na tutawapatia kabla Bunge la bajeti hii halijakwisha ili waweze kusoma majibu yao kwa sababu muda wa kujibu hapa wakati mwingine hautoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Toa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kubwa, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*  
Division.....Sh. 2, 973,514,560/=

**MWENYEKITI:** Haya orodha tayari ipo hapa ya wachangiaji katika mshahara wa Waziri, Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwa mujibu wa sheria mbalimbali za Jamhuri ya Muungano, mambo ya mikopo na misaada kutoka nje ambayo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inataka kukopa kutoka nje ni lazima ipate kibali cha Serikali ya Muungano. Sasa nataka *commitment* ya Serikali kwamba ni lini italeta Bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ambao utairuhusu Zanzibar kukopa kutoka nje bila kutegemea idhini ya Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu kwa sababu kuna miradi mikubwa ambayo ipo Zanzibar imeshindwa kutekelezwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Kwa mfano, upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume, Bandari ya Zanzibar na sasa hivi miradi kama ya gesi inaweza ikakwama ikiwa Serikali ya Zanzibar haikupewa mamlaka ya kukopa yenyewe kutoka nje ya nchi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wakati mwingine inatekeleza miradi yake ambayo iko nje ya ile miradi ambayo sio kipaumbele cha Zanzibar. Kwa mfano, ujenzi wa reli ya kati hata pengine Daraja la Salenda. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe *commitment* ya kuleta mabadiliko ya sheria na iwapo kama sikuridhika na majibu hayo nitatoa shilingi ili tuweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kuhusu hoja ambayo ameileta Mheshimiwa Kubenea, ameuliza ni lini Serikali italeta Muswada, lakini kama ambavyo nimeeleza wakati nachangia hoja hii; yapo mambo mengi ambayo yapo kwenye mchakato wa majadiliano katika ngazi ya wataalam ambayo sasa tumesema yamekamilika kwenye ngazi ya wataalam, sasa tunaandika Waraka wa Baraza la Mawaziri ili mambo hayo yaweze kupatiwa ufumbuzi na kupata tiba ya kudumu. Kwa hiyo, moja ya jambo hilo ambalo lipo kwenye waraka huo ni jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Kubenea avute subira na niliombe Bunge lako Tukufu wavute subira, Serikali ina dhamira njema sana ya kuhakikisha kero zote za Muungano zinaondoka. Kuwekwa kwa mfumo huu jinsi ulivyo upo kisheria, kwa hiyo, hilo nimwombe sana avute subira ili Serikali imalize mchakato huu na Bunge ni hili hili tutakuja kutoa majibu hapa hapa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu aliyoyazungumza



Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanazungumzia mchakato wa kisheria, lakini ni vyema tukakumbushwa kwamba suala la mikopo ni suala la Muungano kwa mujibu wa Katiba yetu na kwa hiyo, tutakapokuwa tukizungumzia mchakato huo wa kisheria lakini tukumbuke kwamba lipo katika Katiba yetu na ni lazima pia tuwe tumelifanyia kazi kwenye katiba vinginevyo pia huo mchakato unaweza usifike mbali.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba kwa mujibu wa Ibara ya (iv) kumeorodheshwa mambo ya Muungano, lakini hili ni moja ya kero ya Muungano ya muda mrefu sana. Sasa ninavyotaka waseme lini huo mchakato wa kubadilisha Katiba na sheria yake unaletwa Bngeni. Sasa hapa Waziri anasema tutaleta, tupo kwenye majadiliano, tupo kwenye Baraza la Mawaziri; ni mambo yale yale ya miaka nenda, rudi. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa hoja ili wenzangu waweze kuniunga mkono tuweze kulijadili jambo hili kwa mapana zaidi na kwa maslahi makubwa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makoff)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Wachangiaji Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Maftaha, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Jaku, Mheshimiwa Komu, Mheshimiwa Almas, Mheshimiwa Rehani na Mheshimiwa Ashatu.

Tunaanza na Mheshimiwa Komu.

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niunge mkono hoja aliyotoa Mheshimiwa Kubenea kwa sababu tunavyozungumza nia njema ya Muungano hapa ndipo tunapoanzia.

Inavyochukua takribani miaka 55, mambo haya yanazungumzwa na tuaahidiwa kwamba yataletwa, halafu hayaletwi, sasa hii inakwenda kutishia huu Muungano ambao kimsingi tunajivunia na hii nia njema haionekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa hapa ni kwa nini tunafikiri kwamba sasa Zanzibar inapaswa ipewe fursa tena haraka sana ya kuweza kujisimamia na kukopa kwa kadri inavyoona ni kwa sababu vipaumbele vya Tanzania Bara au kwa maana ya Serikali ya Muungano sio vipaumbele vya Zanzibar na Zanzibar ina mambo yake ambayo ni ya msingi sana. Wakati Mheshimiwa Jaku anachangia aliorodhesha mambo kibao ambayo Zanzibar inawajibika kufanya kwa ajili ya ustawi wa watu wake, lakini kwa sababu ya vikwazo kama hivi, sababu ya kero kama hizi mambo hayo hayawezi kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea amerejea hapa upanuzi wa Bandari ya Zanzibar na upanuzi wa uwanja wa ndege Zanzibar, sasa haiwezi kufanyika kwa sababu tu ya hiki kikwazo ambacho kipo kwenye Katiba. Kwa hiyo, nafikiri ili huu Muungano wetu uweze kuwa endelevu na uweze kuwa ni Muungano ambao kweli utaendelea kuwepo, ni lazima jambo hili lifanyiwe kazi sasa hivi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kubenea kwamba Serikali itoe *commitment* ya lini italetwa Muswada wa Sheria ya Kufanya Mabadiliko ya Katiba ili kuweza kuiruhusu Zanzibar iweze kuingia mikataba ya mikopo na misaada ya Kimataifa moja kwa moja bila kutegemea dhamana (*guarantee*) au kuruhusiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelezo ambayo Serikali inayatoa kuhusiana na michakato ni maelezo ambayo hayaaminiki na hayaaminiki kwa mifano dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1977, Katiba Ibara ya 134 ilianzisha Tume ya Pamoja ya Fedha, ilichukua mpaka

mwaka 1996, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuleta Muswada wa Tume hiyo ya Pamoja ya Fedha. Ilichukua tena mpaka mwaka 2003 Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuleta Kanuni za kuitekeleza hiyo Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, yaani ililetwa sheria na tume kuundwa na mpaka sasa tume haijaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote, uchambuzi uliofanywa na Tume ya Pamoja ya Fedha unaonesha kwamba mapato ya Muungano ambayo yanapaswa kugawanywa pande zote mbili za Muungano yanatumiwa na Tanzania Bara na Zanzibar haipati hata senti tano, kiasi kwamba kwa makusanyo ya sasa hivi, kama Tume ya Pamoja ingekuwa inafanya kazi na mapato ya idara na wizara za Muungano yakagawanywa sawasawa, wala Zanzibar isingehitaji misaada kwa sababu bajeti yake nzima ingeweza kuendeshwa na wizara na mapato ya fedha za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama jambo hili la kikatiba halitekelezwi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Almas.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nichangie hoja hii, lakini siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Kubenea. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapotaka kukopa nje inatoa taarifa tu kwa Serikali ya Muungano, haijakataliwa hata siku moja. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar narudia, inapotaka kukopa nje, inatoa taarifa kwa Serikali ya Muungano na sababu ni moja kubwa suala la fedha ni la Muungano. Vilevile, wanaokopesha Zanzibar wanataka dhamana ya Serikali ya Muungano, hawataki Serikali ya Zanzibar peke yake... *(Makofi)*

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Na hiyo inafanya Serikali ya Muungano iweze kusajili madeni yanayokopeshwa Zanzibar ndio sababu kubwa. Kwa hiyo, siungi mkono suala la Mheshimiwa Kubenea. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwanza mtoa mada ndugu yangu sasa hivi uliyechangia, Mwanasheria alisema hili suala lipo Katiba ya Jamhuri ya Muungano, sasa nashukuru anasema Zanzibar tunakopa, tutapata wapi fursa hiyo na hili suala lipo kwenye Katiba ya Jamhuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisema siku zote humu tena kwa lugha nyepesi kabisa na kwa uchungu, Zanzibar uchumi wake ni mdogo inategemea zao la karafuu na *competitor* wake mkubwa ni Indonesia na wa pili ni utalii. Sasa Zanzibar inataka kukua kuendelea mbele inalia na upanuzi wa uwanja wa ndege na bandari iliyopo pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la msingi, nawashangaa viongozi *commitment* semeni tu mwaka mmoja, miezi sita; suala la *VAT* limechukua muda gani? Kitu chepesi (*simple*) kabisa hiki mpaka tuvutane? Haileti sura nzuri; nataka *commitment* ni lini miezi sita/mwaka mmoja tunazidi kuumia sisi Zanzibar, hali hairidhishi jamani. Hata mtu mzima akilia kuna jambo wazee, tufikirieni jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kubenea asilimia 95 niwe mkweli. Nitakuwa *masuuli* kwa sababu Mwenyezi Mungu ataenda kuniuliza, nimetoka upande wa Zanzibar mimi, kama sikutetea maslahi ya Zanzibar nitakuwa mnafiki, sio uzuri wala uungwana. Mungu ataenda kuniuliza mie, baada ya siasa kuna... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Maftah hukuomba eeh? *Sorry*, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Mattar *sorry*, nimesema Mheshimiwa Mattar, umeomba wewe?

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Lazima nikatae hoja ya Mheshimiwa Kubenea kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa *commitment*, mchakato unaanza kufanyiwa kazi na unaendelea kufanyiwa kazi na utaletwa kwenye Bunge hili, sijaona sababu ya kuweka msisitizo nini tufanye hili suala liishe. Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri, bado tuna nafasi ya kukopa sisi kama Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tuna nafasi nzuri na tunapata mikopo mizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Kubenea, hiyo shilingi amrejeshee Mheshimiwa Waziri tuendeleo kufanyia kazi, hali ya mikopo ya Zanzibar kupata tunapata kwa wakati ambao tunataka. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene, jiandae Mheshimiwa Rehani.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba yapo mambo na miradi mikubwa ambayo imefanyika katika nchi hii kwa mashirikiano ya Serikali zote mbili na yanafanyika Zanzibar na Tanzania Bara. Kusema kuna tatizo kubwa la mikopo ambalo sasa linahitaji *urgency* mimi naweza nikasema sawa, lakini yapo mambo makubwa hapa yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme tu takwa na sheria inayoombwa na Mheshimiwa Kubenea ya kusema ije sheria hapa si jambo dogo, ni mabadiliko ya Katiba maana Nyongeza ya Kwanza ile namba 8, mikopo na biashara za nje ni mambo ya Muungano. Sasa siyo jambo dogo na ndiyo maana wenzetu hata Uingereza wanazungumzia *Brexit* hawatoki haraka haraka, bado wanakwenda nalo taratibu, mambo yanayohusu *stability* ya

nchi hatuwezi kukurupuka hivi. Serikali inatoa *commitment* kwamba tunalijadili jambo hili litafika *levels* zote na litamalizika, siyo jambo jepesi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ushauri unaotolewa unatolewa na nani? Hawa wasioupenda Muungano ndiyo wanaotupa ushauri juu ya Muungano sisi? Lazima tuwe makini na aina ya ushauri na nani anayetoa ushauri. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rehani ajandae Mheshimiwa Mwigulu.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii. Nami nataka kuchangia katika jambo hili, kinachotakiwa hapa ni *commitment*, siyo jambo lingine lolote, kwa sababu hili jambo kweli linakwaza Zanzibar, lazima tuseme ukweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja, Zanzibar imetoa *proposal* ya kujenga Bandari ya Mpigaduri, sasa hivi ni mwaka wa nane...

**MBUNGE FULANI:** Hamna kitu.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Imekwama na ilipata *support* au mkopo kupitia *EU* lakini bado suala hili ni la Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubali kwamba ni *process* lakini tunataka tuone *progress*, miaka nane imepita bado hatujaona *progress*. Kwa hiyo, Waziri atuambie hapa ni muda gani hili suala tutakuwa na mwelekeo. Au tupewe *alternative* nyingine ya kuhakikisha kwamba hii miradi mikubwa kama hii ya kimkakati basi inaweza kupata ufumbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu.

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo tunaloliongelea ni jambo la Kikatiba lakini pia ni la kiuchumi. Upande mmoja wa Kikatiba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameshaelezea vizuri kwamba marekebisho yake yanahitaji kwanza kushughulikiwa Kikatiba. Kwa maana hiyo pale tu kwenye sehemu ya Kikatiba ni lazima jambo hili lichukue muda kwa maana linatakiwa lifanyiwe kazi kwa uangalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukirudi kwenye upande wa kiuchumi, niwaombe wote wanaochangia hapa waelewe kitu kimoja kwamba hili jambo la kukopa liliwekwa sehemu moja kwa sababu ulipaji nao unafanyika sehemu moja. Kwa maana hiyo, huwezi ukafungulia ukopaji halafu mlipaji akawa mwingine, lazima anayelipa aangalie *space* ya ulipaji na makusanyo yake kama yanaruhusu kuweza kukopa mkopo ambao unafanyika katika Taifa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo taratibu za kisasa za ku-*assess* kama Taifa linaruhusiwa kukopa unatakiwa uangalie kwanza kama kuna fedha zinabaki baada ya kufanya malipo ya lazima ndipo uweze ku-*assess* kwamba unaweza ukaruhusu kukopa mradi A, B, C, D. Kwa maana hiyo, katika mazingira haya tuliyonayo sisi tukishaangalia sehemu ile ya Kikatiba, ni vyema Waheshimiwa Wabunge tukazingatia upande wa uwezo wa kulipa. Hata kama *space* ile ingeruhusiwa, hata kama Zanzibar ingepewa nafasi ya kukopa bado kuna jambo lazima lifanyiwe *analysis* kwamba ulipaji wake utafanyika kwa namna gani. Hata sisi Wabunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Tumewekewa ukomo wa kukopa kufuatana na jinsi ambavyo tunaweza tukalipa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ashatu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza mwanzo, nimwombe sana Mheshimiwa Kubenea aiachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu ya maelezo mazuri ambayo ameanza kuyatoa Mheshimiwa Mwigulu. Dhamira ya Serikali ni njema sana, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema kuhakikisha miradi yote mikubwa inatekelezwa pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Mwanasheria Mkuu wa Serikali hili ni jambo la Kikatiba, ndiyo maana mimi nilianza kusema mchakato wake umeanza, yapo mambo ambayo tunajadiliana na moja kubwa ambalo ameliongea Mheshimiwa Mwigulu ni kwamba tunapoomba Zanzibar iruhusiwe kukopa moja kwa moja, je, nani wa kulipa mkopo huo? Turudi tu kwenye hoja hiyo ya msingi kwamba tunapomruhusu yeye akope ni nani wa kulipa? Hili ni jambo la Muungano lazima hilo liwekwe mezani ndiyo maana nimesema Serikali mbili zinajadiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetolewa mfano wa *Terminal II*, ndiyo maana mambo haya yanachukua muda mrefu aliye-*default* wala siyo upande wa Muungano, walio-*default* ni wasimamizi wa mradi wenyewe. Kwa hiyo, haya mambo ni *sensitive* ndiyo maana tunaomba tuyachukulie hivyo ili tuweze kwenda salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeongelewa mfano hapa wa mkopo wa kujenga Bandari ya Mpigadori, tukumbuke Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliwahi kusimama kwenye Bunge lako Tukufu akasema mkopo huu unapoombwa, amesema Mheshimiwa Almas Maige dhamana inayowekwa ni ya Tanzania Bara lakini wanataka kitu gani? Hicho wanachokitaka ili watoe mkopo huo kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri ni kuweka dhamana Benki Kuu ya Tanzania, hivi tuko tayari kuuza utu wetu Watanzania? *(Makofi)*



(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ya kuangalia. Kamati yetu ya Madeni ya Taifa inayashughulikia moja baada ya lingine na tumeanza mchakato, nimwombe Mheshimiwa Kubenea arudishe shilingi ili kwa dhamira njema tuweze kumaliza suala hili. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa AG una cha kuongeza?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuweke *record* sawa. Nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ameteleza tu ulimi. *Guarantee* au dhamana inayotolewa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, sheria ya mwaka 1974 ambayo majuzi tu tuliifanyia marekebisho hapa, dhamana hiyo inatolewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatuna Serikali ya Bara. Nimeona tulinyooshe hilo kwa sababu ni suala la msingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kubenea, baada ya aliyosema Mheshimiwa Mtemi Chenge bado una hoja?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo hoja na hoja yangu ni kwamba Waziri anapozungumza juu ya dhamana inatolewa na Benki Kuu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina *share* katika Benki Kuu ya

Tanzania. Ndiyo maana inapata gawio kila mwaka pale ambapo Benki Kuu inapata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene anazungumza juu ya jambo hili kubwa liko kwenye Katiba. Yeye alikuja na hoja hapa ya mchuzi wa zabibu ambao ulikuwa tayari umepitishwa kwenye bajeti ya nchi na tukabadilisha, mapato ya nchi yakaondolewa, kwa nini tunataka Zanzibar iwe koloni la Tanganyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nillitegemea Serikali ije hapa iseme baada ya miezi mitatu au minne kwa sababu Serikali imeshasema haina kipaumbele katika mchakato wa Katiba mpya. Kwa hiyo, tunataka mabadiliko katika Katiba tuliyonayo na marekebisho ya sheria ili Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama nchi iweze kukopa nje bila hisani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Bunge hili lihojiwe ili *record* ikae sawasawa. Wangapi wanaunga mkono hoja yangu na wangapi wanataka Zanzibar iendelee kuwa koloni la Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea, futa hilo neno koloni.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wangapi ambao wanataka Zanzibar bado iendelee kutegemea Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**MWENYEKITI:** Hapana, hiyo sio hoja yako, hoja yako ni kubadilisha sheria.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Nataka Bunge lihojiwe lini Serikali italeta sheria hapa Bungeni ya kubadilisha Katiba na hiyo sheria ili Zanzibar iweze kukopa, naomba Wabunge wahojiwe.

**MWENYEKITI:** Hapana, Mheshimiwa Kubenea, mimi ndiyo nitakayehoji na hiyo sio hoja ya Bunge.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Yale ambayo sio hoja yangu nimeyaondoa, nilete hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Umefuta?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Nimeonda yale ambayo siyo hoja yangu yamebaki yale ambayo ni hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Kubenea kwa yale aliyoyasema mwanzo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimwa Mwigulu.

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana, siwarejeshi nyuma...

**MWENYEKITI:** Tumeshafunga hoja.

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala haiathiri.

**MWENYEKITI:** Tumeshafunga hoja, samahani sana. Mheshimiwa Kiteto Zawadi.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa upatikanaji fedha katika masuala ya mazingira ni hafifu, hili liko wazi kabisa. Upo Mfuko ambao ulianzishwa kisheria mwaka 2007 ili kusimamia na kuyalinda mazingira. Kwa bahati mbaya sana

Mfuko huu umekuwa haupati fedha kutoka Serikalini wala katika chanzo chochote kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nisipopata maelezo ya kutosha nitashika shilingi. Nachoomba Serikali inipe maelezo ni msimamo gani iliyonao kuanzisha tozo maalum ambazo zitaweza kuchangia katika Mfuko huu wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tozo ya mazingira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ilianzisha Mfuko wa Mazingira kupitia Sheria ya Mazingira na ulikuwa haujaanza kazi kitambo lakini mwaka juzi Mheshimiwa Rais akateua Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi. Tulifanya utafiti wa aina ya vyanzo ambavyo vinaweza kutumiwa na mfuko huu na kuongeza uwezo wa nchi kusimamia mazingira. Vyanzo hivi vilihusisha tozo za shughuli zinazohusu mazingira ikiwemo mikaa, magogo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kamati ya Serikali inayohusu kodi na tozo na jambo hilo lipo huko ili tukubaliane ndani ya Serikali na wenzetu kuhusu zipi ambazo zinaweza kupitishwa kwa sababu hizi zinahusu sekta nyingine, hatuwezi sisi peke yetu tukaamua kutoza kila mtu ili fedha ziende kwenye mazingira. Ni muhimu tukubaliane na wenzetu na hasa Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba tozo tunazotoa haziongezi gharama za maisha, kufanya biashara lakini vilevile zinatupatia fedha kwa ajili ya hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Kiteto kwamba yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Mazingira, anaelewa na anaumia kuhusu mazingira na kuhusu mfuko huu kutokuwa na fedha. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya kazi, hasa na Wizara ya Fedha, ili mapendekezo yale ya vyanzo yaweze kupita na mabadiliko madogo ya sheria kuhusu mfuko ule yaje hapa Bungeni ili tuweze kuyapitisha

na vyanzo vipitishwe basi mfuko huu na wenyewe uweze kufanya kazi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri na hasa alipozungumzia marekebisho ya Sheria hii ya Mazingira. Nachoomba Serikali itoe tu *commitment* kwamba ni lini mabadiliko ya Sheria hii ya Mazingira yataletwa hapa Bungeni. Hiyo yote ni kuipatia Wizara hii ya Mazingira nguvu za kuweza kusimamia vile vyanzo vya mapato ili viweze kusaidia katika mfuko huu. Sina haja ya kuondoka na shilingi ya Waziri lakini naomba tu *commitment* ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *commitment*, mchakato unaendelea?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alituandikia barua Mawaziri wote ambao wana sheria ambazo wangependa zibadilishwe ili mambo yao yaende vizuri na sisi tulimjibu kwa kumuandikia kuhusu vifungu muhimu kikiwemo hiki ambacho tunataka kibadilishwe. Bahati nzuri alitujibu na akatualika tukajadiliane na watu wake kuhusu lugha ambayo inaweza kutumika kwenye haya mabadiliko. Kwa hiyo, suala hili analo Mwanasheria Mkuu na limefika pazuri, wakati wowote Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali utakapokuja Bunge imani yetu ni kwamba mabadiliko hayo yatakuwepo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto umeridhika?

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja yangu mimi ni mabadiliko ya tabianchi lakini nltazungumzia zaidi kwenye suala la kuongezeka kwa kina cha bahari na hatua zinazochukuliwa na Serikali kuzuia bahari isiendelee kula ama kuchukua sehemu ya miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma maandiko ya waandishi mbalimbali yanathibitishi kwamba ifikapo mwaka 2050 ujazo wa bahari utaongezeka katika eneo la Tanzania kwa futi 0.5 mpaka futi 1.4. Hiki ni kiwango kikubwa na kama Serikali haitachukua hatua madhubuti kuna hatari Miji ya Lindi, Bagamoyo, Mikindani, Pangani na mingineyo ikapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze hatua Serikali iliyochukua la *Barack Obama Drive*, wamefanya kazi nzuri. Kwa nini Serikali isitenge fedha zoezi lile likafanywa nchi nzima kuzuia maji katika Miji ya Tanga, Pangani, Bagamoyo, Dar es Salaam, Lindi na Kilwa? Pale Kilwa Kisiwani kuna Msikiti wa zamani wa enzi hizo sasa hivi unazama na Mheshimiwa Waziri anajua kwa sababu bahari inaendelea kusogea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali, nimesoma kwenye vitabu sioni fedha zilizotengwa kwa ajili ya jambo hili. Mheshimiwa Kiteto kazungumza hapa, hii *National Environmental Program* ambayo ilikuwa *adopted* mwaka 2007 haipati fedha na kama haipati fedha maana yake inashindwa kukabiliana na mambo makubwa kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali, nimeona mmetenga fedha za maendeleo shilingi bilioni 19, shilingi bilioni 1 ya ndani na shilingi bilioni 18 za nje, fedha ambazo hatuna uhakika wa kuzipata. Ni lini Serikali itaweka mkakati madhubuti kuhakikisha kwamba wanalinda maeneo haya ya miji ya pwani isije ikachukuliwa na bahari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiporidhika, nitatoa shilingi ili Bunge liweze kupata fursa ya kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bobali yuko sahihi kabisa kwa kweli. Nchi yetu sisi ina ufukwe wa kilometa 1,400 kutoka kule juu Moa (Tanga) mpaka Msimbati (Mtwara) na karibu kila eneo kwenye ufukwe limeathirika sana na mabadiliko ya tabianchi na bahri kula ardhi. Kuna baadhi ya maeneo walikuwa wanalima mpunga na mazao mengine, siyo tu kwamba bahari imelika hata yale maeneo hawawezi tena kulima. Kuna baadhi ya visima vilikuwa vinatoa maji ya baridi sasa hivi vinatoa maji ya chumvi kwa sababu ya bahari kusogea. Kwa hiyo, athari za mabadiliko ya tabianchi zinaathiri sana maisha ya watu na Mheshimiwa Bobali yuko sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu viwili ambavyo sisi tunadhani ni muhimu kuvifanya. Kwanza, nchi yetu ni sehemu ya Mkataba wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na tunalipa *fee* na una fursa mbalimbali. Moja ya fursa ni *Adaptation Fund*, Mfuko wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi. Ili upate fedha na hata huu mradi wa Barabara ya Barack Obama, Kigamboni, Pangani, Mikoko - Rufiji, tulizipata baada ya kutengeneza andiko ili tuweze kufikia hizo fedha za *Adaptation Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba ndugu yangu, Mheshimiwa Bobali tukae pamoja na tuangalie kwake anaposema na hata Wabunge wengine kwenye maeneo kama hayo, kikubwa ni kuandika mradi, fedha kwa ajili ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi hazitolewi kwa jumla, zinatolewa kwa *specific project*. Kwa mfano, watu wa Simiyu walijenga hoja kwamba kuna ukame sana, hakuna maji kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi, wamepata shilingi bilioni 250 kutoka kwenye *GCF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndugu yangu Mheshimiwa Bobali, ni vizuri umelisema hapa lakini ili tulifanyie kazi tutatuma wataalam waangalie tuone kama tunaweza kuandika mradi kwa ajili ya eneo mahsusi ambalo umelisema

halafu tutaona kama ni *Adaptation Fund* au ni *GCF* au ni kwingine ili tuone kama ni kupanda mikoko au kujenga ukuta ifanyike. Tuko tayari kushirikana nawe na Wabunge katika maeneo ya pwani ambao wameathirika na athari za bahari kula ardhi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali maneno mazito hayo ya Waziri.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kukubali uhalisia na ameona ukubwa wa tatizo. Naomba sasa kile alichokisema kwamba Wabunge wanaotoka kwenye maeneo hayo waweze kumwona ili kumpa taarifa, isiwe sasa ni jambo la sisi kumtafuta. Naomba Mheshimiwa Waziri aandae kikao maalum, atuite twende tukampe uhalisia, kwa sababu jambo hili lina *National interest*, tuweze kuokoa maeneo haya ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namrudishia shilingi yake.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa kupata nafasi hii. Sina nia ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri isipokuwa nataka *commitment* yake. Maelezo yangu ni kwamba kuna haja kubwa sana ya kutoa elimu inayohusu Muungano. Nilimwambia Mheshimiwa Waziri katika mchango wetu kwamba kwa sababu *focus* ilikuwa kwa wanafunzi pamoja na jamii nyingine ambayo siyo katika Bunge letu, lakini kwa maelezo haya yaliyotoka katika mjadala huu, kuna *urgent* kubwa sana ya kuwanza na masomo haya yanayohusu Muungano, *process* zake na sheria zake kuanzia katika Bunge letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka *commitment* ya Mheshimiwa Waziri haya mafunzo yanaanza lini? Maana yake siyo kwamba mtafanya au hamfanyi, hoja hapa



imeonekana dhahiri hata wale ambao wana *authority* hawajui *exactly* hili jambo linaendaje? Tunahitaji Mheshimiwa Waziri atupe *commitment* lini tunaanza mafunzo yanayohusu Muungano katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hasa baada ya kushuhudia na kusikia maneno yaliyokuwa yanatoka kwenye mjadala uliopita. Kweli elimu ya Muungano inabidi ianzie Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuko tayari kufanya mafunzo hayo hata kabla ya Bunge hili la bajeti halijaisha wakati wowote ule. Imani yetu ni kwamba hakutahitajika malipo kwa ajili ya kuja kushiriki hayo mafunzo, kwa sababu utakaposema kwamba ulipwe ili kupata elimu ya Muungano ndipo tutakapoanza changamoto. Kwa sababu Mheshimiwa ameyadai, sisi tuyafanya lakini yatakuwa hayana posho. Kwa hiyo, sisi tuko tayari hata kabla ya Bunge kwisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Saada, una lolote la kuongeza?

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina la kuongeza, namshukuru Mheshimiwa Waziri. Naamini Wabunge wote tutakuwa pamoja kusikiliza, kwa sababu maneno mengine yanayotoka ni maneno ambayo wewe mwenyewe unahisi unataka kutetemeka, yaani sijui una-*fee*/vipi. Sasa watu wanaotusikiliza wanachukua haya maneno na ni maneno ya hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sote tuna wajibu, lazima tupate semina kuhusu Muungano tukubalini bila malipo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Narudia tena, sina nia ya kuzuia shilingi ya ndugu yangu Mheshimiwa January. Katika mchango wangu nilisema kuna baadhi ya mashirika na taasisi ikiwemo *NBC, NMB, POSTA BANK, TTCL, TCRA, TCA*, Zanzibar hayapati mchango. Ni lini atafuatilia angalau Zanzibar ipate kujikwamua kutokana na hali hii? Ni hilo tu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii na kwa hoja hii ya Mheshimiwa Jaku. Kama nilivyosema wakati nachangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri kwamba jambo hili ni katika mambo ambayo tunakamilisha muundo wake wa jinsi gani ambavyo gawio hili ambalo mashirika haya yatakuwa yanatoa, utakwenda moja kwa moja kama ambavyo tumefanya kwa Benki Kuu ya Tanzania na kama ambavyo *TPV* Benki pia inatoa gawio lake kulingana na *shares* ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Jaku, Mashirika yetu yameanza kutoa gawio, mwaka 2018 ndiyo tumeona mashirika mengi na sasa Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Mlipaji Mkuu wa Serikali wanakamilisha mjadala huu na wenzetu wa Zanzibar kuhakikisha kwamba gawio lile linakwenda kama lilivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, maneno mazito hayo.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno nakubali kweli mazito, lakini mdomo unasema, lakini vitendo ndiyo kazi.

**MWENYEKITI:** Vitendo vinakuja. Kwa hiyo, nakushukuru, ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware. (*Makofi*)

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Sera yetu ya Mazingira ya 1997 iliyozaa Sheria yetu ya Mazingira ya 2004

imeweka bayana majukumu ya wadau mbalimbali ambao wanatakiwa watekeleze sheria hii ya kusimamia mazingira ikianza ngazi za Serikali za Mitaa mpaka ngazi ya Taifa. Nikisema hivi, kuanzia Serikali ya Mitaa ina maana nahusisha Wizara ya TAMISEMI na wengine wanakuwa wanasimamiwa *plus* TAMISEMI na Wizara ya Muungano na Mazingira. Usimamizi na utekelezaji huu wa Sheria yetu ya Mazingira inakuwa *reflected* kwenye bajeti ambayo inatakiwa isomeke kwenye kitabu chetu hiki cha bajeti kupitia mafungu au *vote* mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia mbalimbali kutoka Wizara 22, ni Wizara tano tu ambazo zimeweka kifungu mahususi ambacho kinagusa masuala ya Mazingira. Hii ni katika ngazi ya Serikali Kuu. Pia katika ngazi ya Mabaraza ya Mazingira au Vikao au Kamati za Mazingira ngazi ya Serikali za Mitaa, huku pia haijawa *reflected*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa pia Mfuko wetu wa Mazingira sasa kwa ukubwa wake hauna fedha, Wizara husika ambazo zinatakiwa zisimamie mazingira hazijaweka fedha. Cha kushangaza, kuna Wizara; kama Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maji, Wizara ya Viwanda na Biashara ambao Kamati ya Bunge inasimamia Viwanda Biashara na Mazingira, hazina fungu au *vote* ambayo inahusia mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi au mikakati ya Waziri kusima kwamba suala hili linafanyiwaje kazi ili kwamba sasa mazingira yawe kipaumbele cha kweli ambayo ipo *reflected* kwenye bajeti yetu iweze kufanyiwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, basi nakusudia kushika shilingi yake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hata mambo ya kitaalam unataka kushinda shilingi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sheria ya Mazingira ina sehemu kabisa, tena ina vifungu vingi; kuanzia kifungu cha 34 mpaka kifungu cha 42, vifungu vyote vinazungumzia wajibu wa *Local Government* katika usimamizi wa mazingira. Vile vile, nyuma yake inaelezea Wizara za Kisekta kuanzia Kifungu cha 30 mpaka 33 na moja ya mahitaji ni kwamba kila Wizara ya Kisekta lazima iwe na Mratibu wa Mazingira; iwe Wizara ya Afya, Maji, Miundombinu na kadhalika. Ni kweli kwamba katika Wizara zote 22, ni Wizara sita tu ndiyo zina Waratibu wa Kisekta. Kwa hiyo, tumewasiliana na wenzetu na ni imani yetu kwamba watatujibu kwamba kila Wizara itakuwa na Mratibu wa Mazingira. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Makamu wa Rais ameelekeza kwa kuwaandikia Viongozi wa Mikoa wahakikishe kwamba wajibu wa Serikali za Mitaa kwenye Mazingira unazingatiwa ikiwemo kila halmashauri iajiri Afisa Mazingira kila Kijiji, Kata, Mtaa, Kitongoji kiwe na Kamati ya Mazingira kama Sheria inavyoitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wetu Wizara wanaweza kulizungumzia na nyuma lilikuwepo; na Mheshimiwa Ruth Mollel atakuwa shahidi kwamba katika kila bajeti ya kila Wizara na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kulikuwa na *budget code* ya Mazingira, kama ambavyo kuna *budget code* ya UKIMWI hata kama Wizara haihusiki na UKIMWI, lakini vilevile kulikuwa na *budget code* ya Mazingira ili fedha zitengwe kidogo na shughuli za mazingira zifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumezungumza na wenzetu Wizara ya fedha ili ile *budget code* irudi ili kwenye vitabu vyote hivi tunavyopitisha angalau kuwe na shughuli ambayo kila Wizara na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinafanya kuhusu mazingira. Bahati nzuri mazungumzo yamefika pazuri, ni imani yetu kwamba katika mwaka ujao wa fedha itakuwa siyo huu tunaoujadili sasa, ni huo unaokuja, tutakuwa na *budget code* ya Mazingira ili taasisi zote na Wizara zote ziweze kuwa na programme za mazingira,

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Sware kamba maelekezo kwa Wizara za Kisekta na Mamlaka Serikali za Mitaa kuhusu wajibu wao kwenye Sheria za Mazingira wameshaelekezwa na viongozi wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATA S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nimepokea maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, sikusudii tena kutoa shilingi, nimeridhika. Kwa mantiki hiyo sasa tunategemea kitabu hiki kwa bajeti inayokuja ya mwaka 2020/2021 basi hivyo vifungu vitasomeka viwe vina vitengo mahususi ambavyo vitakuwa vinashughulikia masuala ya mazingira. Nashukuru. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – Finance and Accouts Unit.....	Sh. 265,805,000/=
Kif. 1003 – Policy and Planning Division.....	Sh. 639,200,000/=
Kif. 1004 – Government Communication Unit.....	Sh.184,718,000/=
Kif. 1005 – Internal Audit Unit.....	Sh. 200,718,000/=
Kif. 1006 – Procurment Management Unit.....	Sh. 127,344,000/=
Kif. 1007 – Information and Communication Technology Unit.....	Sh.163,934,000/=
Kif. 1008 - Legal Services Unit.....	Sh. 193,354,000/=
Kif. 2001 – Union Secretariat.....	Sh. 608,988,000/=
Kif. 5001 – Environment.....	Sh. 4,489,798,440/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001 – Admin. & Human Resources Mgt.....	Sh.7,855,093,000/=
--	--------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 – *Administration and Human Resource division*.....Sh.1,000,000,000/=

Kif. 5001 – *Environment* .....Sh. 18,218,915,442/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja.

### T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari 2016 kanuni ya 104 (3)(a)na (b) kwamba Bunge lako lililokaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 – Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hongera sana na timu yako nawashukuru Wabunge wote kwa kazi nzuri mliyoifanya. Wale wote ambao mliona umuhimu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri na kurudisha shilingi yake mmeonyesha uungawana sana na majibu mazuri yametoka. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *Very professional answers.*

Baada ya maneno hayo, naaharisha shughuli za Bunge mpaka kesho, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.15 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 17 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*

**(Footnotes)**

<sup>1</sup>Romanus C. Ishengoma - Faculty of Forestry and Nature Conservation Sokoine University of Agriculture Morogoro - National trends in Biomass Energy in Tanzania- Presentation on 26  
– 27 February, 2015 Dar es Salaam.

<sup>3</sup>Intended Nationally Determined Contributions (INDCs) were prepared in consistency with decision 1/CP.20, and will be implemented by 2030.











